


**RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU
ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA MASHIRIKA YA
UMMA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

28 Machi 2019



**JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Barabara ya Samora Machel Na. 16, S.L.P. 9080, 11101 Dar es Salaam. Simu ya Upepo: „Ukaguzi“ D“Salaam, Simu: +255(022)2115157/8, Tarakishi: +255(022)2117527, Barua pepe: ocag@nao.go.tz, tovuti: www.nao.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. FA.27/249/01/2017/2018

28 Machi 2019

Mh. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P 9120
Barabara ya Barack Obama, Na.1
11400, DAR ES SALAAM.

**YAH: KUWASILISHA RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU
WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMU
KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (na mabadiliko ya mwaka 2005) na kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 11(4) ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008, ninawasilisha kwako ripoti ya Mwaka ya Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kuiwasilisha Bungeni kulingana na matakwa ya sheria.

Wako Mwaminifu,

Prof. Mussa Juma Assad

MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,

**Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

(Kama ilivyoanzishwa chini ya Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) Majukumu ya kisheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa) na kufafanuliwa na Sheria ya Ukaguzi ya Umma, Na. 11 ya mwaka 2008 (kama ilivyorekebishwa) na kufafanuliwa na Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009.

Dira ya Ofisi:

Kuwa Taasisi ya Hali ya juu katika ukaguzi wa sekta ya Umma.

Dhamira ya Ofisi:

Kutoa huduma za ukaguzi wa sekta ya Umma zenye ubora wa Hali ya juu zinazoimarisha utendaji, uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa rasilimali za Umma.

Misingi Yetu

Katika kutoa huduma zenye ubora, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inaongozwa na misingi ifuatayo:

Kutopendelea: Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi inayotoa huduma kwa wateja wake kwa haki bila upendeleo.

Ubora: Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi ya kitaalamu inayotoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya ukaguzi.

Uadilifu: Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inazingatia na kudumisha maadili ya kazi ya kiwango cha juu na kuheshimu sheria.

Kujali Watu: Tunajali mahitaji ya wadau kwa kujenga utamaduni mzuri wa kujali wateja na kuwa na watumishi wenye uwezo na kuongeza tija.

Ubunifu: Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi bunifu ambayo wakati wote inaimarisha na kukaribisha mawazo mapya ya kimaendeleo toka ndani na nje ya taasisi.

**Matumizi bora ya
Rasilimali za Umma:**

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi inayozingatia matumizi bora ya rasilimali zilizokabidhiwa kwake.

Tunatimiza haya kwa kufanya yafuatayo:

- Kuchangia matumizi bora ya fedha za Umma kwa kuhakikisha kwamba wakaguliwa wetu wanawajibika kutunza rasilimali walizokabidhiwa;
- Kusaidia kuimarisha ubora wa utoaji huduma kwa kuchangia ubunifu kwa matumizi bora ya rasilimali za Umma;
- Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wadau wetu kuhusu mapungufu katika uendeshaji wa shughuli zao;
- Kuwahusisha wadau wetu katika mfumo wa ukaguzi; na
- Kuwapa wakaguzi nyenzo za kufanyia kazi ambazo zitaimarisha uhuru wa ofisi ya ukaguzi.

YALIYOMO

| | |
|--|-----------|
| MUHTASARI | <i>xi</i> |
| SURA YA KWANZA | 1 |
| UTANGULIZI NA TAARIFA ZA JUMLA | 1 |
| SURA YA PILI | 6 |
| AINA ZA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA | 6 |
| SURA YA TATU | 9 |
| MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MIAKA | 9 |
| ILİYOPITA | 9 |
| SURA YA NNE | 11 |
| TATHMINI YA UTENDAJI KIFEDHA NA HALI YA MUENDELEZO WA UTOAJI HUDUMA KWA TAASISI ZA UMMA | 11 |
| SURA YA TANO | 14 |
| USIMAMIZI WA MAPATO KATIKA TAASISI ZA UMMA | 14 |
| SURA YA SITA | 26 |
| UTAWALA BORA KATIKA MASHIRIKA YA UMMA | 26 |
| SURA YA SABA | 31 |
| MAPITIO YA MIKAKATI NA UENDESHAJI WA KIUFANISI | 31 |
| SURA YA NANE | 62 |
| USIMAMIZI WA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA TAASISI ZA UMMA | 62 |
| SURA YA TISA | 69 |
| UWEKEZAJI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA | 69 |
| SURA YA KUMI | 81 |
| MWENENDO WA BENKI ZINAZOMILIKIWA NA SERIKALI | 81 |
| SURA YA KUMI NA MOJA | 93 |
| UTENDAJI KATIKA MIFUKO YA HIFADHI YA JAMII | 93 |
| SURA YA KUMI NA MBILI | 114 |
| USIMAMIZI WA MIKOPO KWA TAASISI ZA UMMA | 114 |
| SURA YA KUMI NA TATU | 118 |
| UTENDAJI WA MAMLAKA ZA MAJI | 118 |
| SURA YA KUMI NA NNE | 128 |
| USIMAMIZI WA RUZUKU ZA SERIKALI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA | 128 |
| SEHEMU YA KUMI NA TANO | 131 |
| USIMAMIZI WA MALI ZA MASHIRIKA YA UMMA | 131 |
| SEHEMU YA KUMI NA SITA | 137 |

| | |
|---|-----|
| USIMAMIZI WA MANUNUZI NA MIKATABA | 137 |
| SEHEMU YA KUMI NA SABA | 152 |
| UKAGUZI WA KIUCHUNGUZI NA UKAGUZI MAALUM | 152 |
| SURA YA KUMI NA NANE | 178 |
| UKAGUZI WA UFANISI KATIKA SEKTA YA MADINI, GESI NA MAFUTA | 178 |
| SURA YA KUMI NA TISA | 187 |
| UTEKELEZAJI WA SHERIA ZA KODI YA MAPATO | 187 |

Orodha Ya Jedwali

| | |
|---|-----|
| Jedwali Na. 1:Muelekeo wa hati za Ukaguzi | 8 |
| Jedwali Na. 2:Utekelezaji wa mapendekezo kwa kipindi kilichopita | 10 |
| Jedwali Na. 3: Mashirika ya Umma yenye hali mbaya kifedha | 12 |
| Jedwali Na. 4: Mashirika ya Umma yasiyokuwa na Bodi za Wakurugenzi | 27 |
| Jedwali Na. 5: Mchanganuo wa gharama za vikao | 29 |
| Jedwali Na. 6: Leseni Zilizotolewa kwa Bidhaa Zilizoshindwa Majaribio | 42 |
| Jedwali Na. 7: Maombi Yaliyofanyiwa Kazi kwa Bidhaa Zisizoruhusiwa..... | 43 |
| Jedwali Na. 8: Kutorejeshewa Gharama za NICTBB..... | 55 |
| Jedwali Na. 9 :Miradi yenye motisha ambayo haizingatii sheria za kodi | 71 |
| Jedwali Na. 10: Mapato na Madai ya Matibabu | 75 |
| Jedwali Na. 11: Hasara za benki za serikali..... | 82 |
| Jedwali Na. 12:Utoshlevu wa mtaji wa benki za Serikali..... | 83 |
| Jedwali Na. 13:Mikopo chechefu ya benki zinazomilikiwa na Serikali | 87 |
| Jedwali Na. 14: Mikopo iliyopo katika hali ya hatari | 87 |
| Jedwali Na. 15:Kutokutosheleza kwa dhamana na mikopo | 88 |
| Jedwali Na. 16:Kupungua kwa Ukwasi kwa Benki zinazomilikiwa na Serikali . | 89 |
| Jedwali Na. 17:Madeni ya Serikali kwa Mifuko ya Hifadhi ya jamii..... | 94 |
| Jedwali Na. 18: Uwezo wa mifuko iliyounda PSSF | 97 |
| Jedwali Na. 19:Michango na Malipo ya Mafao | 98 |
| Jedwali Na. 20:Kundi la uwekezaji na mipaka ya uwekezaji katika PSPF na NHIF | 108 |
| Jedwali Na. 21:Mtiririko wa Mapato na Madai | 112 |
| Jedwali Na. 22: Hasara itokanayo na upotevu wa maji | 119 |
| Jedwali Na. 23: Madeni ya muda mrefu | 121 |
| Jedwali Na. 24: Mwenendo wa Matatizo ya kifedha katika Mamlaka za Maji | 122 |
| Jedwali Na. 25: kiwango cha watu wanaopata Maji | 126 |
| Jedwali Na. 26: Manunuzi ambayo hayajaidhinishwa na Benki ya Posta..... | 141 |
| Jedwali Na. 27:Mwenendo wa Uzalishaji, Mauzo na Gharama | 179 |
| Jedwali Na. 28: Orodha ya Madeni Yasiyolipwa kwa Muda Mrefu..... | 181 |
| Jedwali Na. 29: Bei za Hisa za Madalali wa Kuuza Taarifa za Mitetemo ya Miamba | 184 |
| Jedwali Na. 30:Posho za Watumishi ambazo hazikukatwa kodi..... | 188 |
| Jedwali Na. 31:Taasisi ambazo hazikukata kodi ya Zuio na Kodi ya Maendeleo ya Ujuzi | 190 |
| Jedwali Na. 32:Taasisi zilizolipa au kuuza bila kutoa au kudai EFD | 195 |

SHUKRANI



Kwa mujibu wa matakwa ya Ibara ya 143 (4)ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sura ya 34 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008; ninayo furaha na heshima kuwasilisha Ripoti Kuu ya ukaguzi kwa mwaka 2017/2018.

Kwa furaha kubwa natumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dk. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa msaada wake mkubwa na juhudi binafsi kuhakikisha Ofisi yangu inatimiza jukumu lake kikatiba.

Pia, natambua mchango wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kamati zake kwa usimamizi mzuri ambao umeleta ufanisi na uwajibikaji katika Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma.

Mafanikio na matokeo ya ripoti hii yametokana na mchango wa wadau mbali mbali. Kwa sababu hiyo basi, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Bodi za Wakurugenzi, Menejimenti na Makampuni binafsi ya ukaguzi ambayo yamekuwa yakifanya ukaguzi wa hesabu za Mashirika ya Umma kwa niaba yangu, ushirikiano wao umechangia ukaguzi ukamilike kwa wakati.

Ninayo furaha kwa kuweza kukamilisha ripoti hii kwa wakati kama ilivyoainishwa katika Katiba. Hata hivyo, ukamilifu wa kazi hii umetokana na ushirikiano wa wafanyakazi wangu ambao wamefanya kazi kwa bidii, hata nje ya muda wa ofisi na kwa weledi wa hali ya juu.

Pia, ninayo faraja kuwa ofisi yangu imeweza kuleta mchango juu ya utawala bora katika Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma.

Prof. Mussa Juma Assad

MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

28 Machi 2019

DIBAJI

Ofisi yangu imeendelea kutekeleza majukumu yake vizuri kwa kufanya ukaguzi katika maeneo ambayo yasipoangaliwa vizuri yanaweza kuathiri ustawi wa nchi. Ripoti hii imekusanya masuala muhimu yaliyojitokeza katika kaguzi za Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018. Pia, imejumuisha mapendekezo yaliyotolewa kwa wasimamizi wa mashirika hayo ili kupunguza mapungufu yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi. Hata hivyo, maelezo zaidi yamo katika ripoti husika za Mashirika.

Ripoti hii ina jumla ya sura 19 ambazo zimekusanya mambo muhimu yaliyojitokeza katika kaguzi za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyingine za Umma ukiwemo mwenendo wa hali ya kifedha, uwezo wa kuendelea kutoa huduma, usimamizi wa mapato na matumizi, utawala bora na ufanisi katika utendaji wa Mashirika.

Kutokana na Serikali ya awamu ya tano kusisitiza umuhimu wa ujenzi wa uchumi wa viwanda kote nchini, nilipitia uwekezaji uliofanywa na Mashirika ya Umma ili kuangalia mapungufu, chanzo cha matatizo pamoja na kutoa mapendekezo ili kutatua mapungufu yaliyopo. Pia, kutokana na mwenendo mbaya wa Benki zinazomilikiwa na Serikali, ripoti hii imejumuisha mwenendo wa Benki hizo na kuonesha maeneo ambayo yanahitaji kuboreshwa.

Pamoja na kupongeza juhudi za Serikali katika kuunganisha Mifuko ya Jamii kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza ufanisi katika utoaji huduma, pia nimetoa mapendekezo katika maeneo ambayo yanapaswa kuboreshwa ili malengo hayo yafanikiwe.

Pia, ripoti hii imejumuisha ukaguzi katika Mamlaka za Maji ili kuangalia mwenendo wake katika kusimamia jukumu la upatikanaji wa maji, hatimaye kusaidia maendeleo ya nchi. Pia, imejumuisha ukaguzi wa manunuzi na usimamizi wa mikataba katika Mashirika ya Umma kwa kuwa ni sehemu ambayo pesa nyingi za Umma hutumika, pamoja na usimamizi wa Mali za serikali.

Nimeendelea kufanya kaguzi maalumu na kaguzi za kiuchunguzi (forensic audit) kwa Mashirika ya Umma, ambapo Muhtasari wa matokeo ya kaguzi hizo na mapendekezo yake nimeyajumuisha katika ripoti hii.

Ninayo matumaini kuwa mapendekezo ambayo nimeyotoa katika ripoti hii yatafanyiwa kazi na Mashirika husika. Pia, Serikali itafuatilia utekelezaji wa mapendekezo hayo.

MUHTASARI

Aina na Muelekeo wa Hati za Ukaguzi

Katika kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia 2017/2018 nilikagua na kukamilisha kaguzi za mashirika 138 ikijumuisha kaguzi 6 za miaka ya nyuma yaliyotakiwa kukaguliwa. Hata hivyo, niliweza kutoa maoni ya ukaguzi kwa mashirika 122 pekee kati ya mashirika yaliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Mashirika 121 yalipata hati zinazoridhisha, wakati ni shirika moja (1) tu lilipata hati isiyoridhisha. Hati yenye mashaka na hati mbaya hazikutolewa kwa shirika lolote au taasisi nyingine za Umma katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha.

Muhtasari wa Mapendekezo ya Kaguzi Zilizopita

Katika kufuatilia utekelezaji wa kaguzi za miaka iliyopita, nilibaini kwamba, kati ya mapendekezo 112, ni mapendekezo 52 (sawa na asilimia 46) ndiyo yametekelezwa. Mapendekezo 18 (sawa na asilimia 16) hayakutekelezwa. Mapendekezo 36 (sawa na asilimia 32) yapo katika hatua za utekelezaji na mapendekezo 6 (sawa na asilimia 6) yamepitwa na wakati. Maelezo ya Mapendekezo haya yameelezwa kwa kina katika sura ya tatu ya ripoti hii. Kati ya mapendekezo 18 ambayo hayakutekelezwa, 14 (sawa na asilimia 78) hayakuwa na majibu ya serikali kuonesha mwenendo wa utekelezaji.

Miongoni mwa mapendekezo ya kaguzi zilizopita ambayo hayakutekelezwa ni: Benki ya Azania kutokuwa chini ya usimamizi wa Msajili wa Hazina, Wizara ya Nishati kutokulipa deni la pango la Sh. bilioni 1.12 kwa Kampuni ya Umeme Tanzania (TANESCO), kukosekana kwa mkataba na dhamana kwa mkopo wa Sh. bilioni 44.29 uliotolewa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF); Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kuchelewa kuanzisha mradi wa utafutaji wa gesi katika vitalu 4/1B na 4/1C, Sheria kutompa mamlaka Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi pamoja na Mamlaka ya Maji Safi na Majitaka Mwanza (MWAUWASA) kuchelewa kukamilisha Mradi wa maji wa Sh. bilioni 6.66.

Mwenendo wa Kifedha na Tathimini ya Uwezo wa Kuendelea kutoa Huduma

Nilibaini Mashirika ya Umma 14 yakiwa na matatizo makubwa ya kifedha pamoja na kupata hasara mpaka kusababisha madeni ya Mashirika hayo kuwa zaidi ya Mali zao. Hali hii ina hatarisha mustakabali wa Mashirika hayo katika kuendelea kutoa huduma siku za baadaye.

Usimamizi wa Mapato katika Mashirika ya Umma

Katika kipindi cha ukaguzi, nimeyabaini Mashirika ya Umma ambayo yana kiasi kikubwa cha madeni wanachodai nje (Receivables) ambayo yamesababisha kuathiri ukwasi wa Mashirika hayo. katika Bohari Kuu ya Dawa (MSD), nilibaini mapungufu katika mauzo na usambazaji wa dawa ambayo yamesababisha kiasi kikubwa cha dawa kurudishwa kutoka kwa wateja. Pia, katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) nilibaini malipo yaliyolipwa kwa huduma iliyotolewa kwa watu ambao hawachangii Sh. bilioni 4.8 na watu ambao hawastahili kupata huduma Sh. bilioni 13.99

Pia, katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), nilibaini deni la Sh. trilioni 1.46 linalotokana na Bodi kushindwa namna ya kuwapata wadaiwa wa mikopo hiyo. Nilibaini Shirika la Simu Tanzania (TTCL) linadai kiasi kikubwa cha madeni wakati madeni hayo hayana uthibitisho. Zaidi, nilibaini kuwa Taasisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) inategemea zaidi wahisani katika kupata fedha za kutekeleza majukumu yake.

Ukaguzi wa Utawala Bora Katika Mashirika ya Umma

Katika baadhi ya Mashirika ya Umma nilibaini mapungufu ya utawala bora kama ifuatavyo: katika Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) sikuweza kuona muhutasari wa vikao vya Bodi ya Shirika, kutokuwapo kwa Menejimenti ya Kampuni Tanzu ya Mkulazi, mapungufu ya wajumbe katika Bodi ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere; kushindwa kwa Kampuni ya TTCL Pesa kufanya vikao vya Bodi ya wadhamini kama ilivyoainishwa katika hati ya wadhamini. Kuongezeka kwa gharama katika matumizi ya Bodi ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA); pamoja na mapungufu katika

ufuatiliaji na Usimamizi wa bajeti ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM). Menejimenti za Mashirika ya Umma zinapaswa kuchukua hatua ili kutatua vyazo vya matatizo haya.

Tathmini ya Ufanisi wa Kimkakati na Uendeshaji wa Mashirika ya Umma

Katika kutathmini ufanisi wa utendaji wa mashirika ya Umma nilibaini mapungufu yafuatayo: Shirika la Simu Tanzania (TTCL) halina umiliki na mamlaka ya kusimamia Mkongo wa Taifa. Sambamba na hayo, TTCL inaidai Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Sh. bilioni 20.63 kama marejesho ya gharama walizotumia katika shughuli za mkongo huo; kutokuwapo kwa mfumo wa kusambaza maji ndani ya mbuga ya Serengeti, Shamba la Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) limekuwa likiendeshwa kwa hasara; Kampuni Tanzu ya Mkulazi kuchelewa utekelezaji wa ujenzi wa kiwanda cha Sukari; Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kushindwa kutumia mfumo unaoitwa Jeeva ambao ungeweza kuisaidia hospitali katika utendaji kazi pamoja kuhifadhi kumbukumbu za dawa na madeni; ambapo nilibaini hospitali ilikuwa na kiasi cha madeni chechefu ya Sh. bilioni 1.39 katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 2018, pamoja na Shirika la viwango Tanzania (TBS) kutoa leseni kwa bidhaa zilizokatazwa.

Usimamizi wa Matumizi wa Mashirika ya Umma

Wakati hatua mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa katika kuboresha mapungufu yaliyojitokeza miaka ya nyuma, nilibaini kuongezeka kwa madai ya wafanyakazi katika Taasisi tano za Elimu ya Juu; ambapo madai yalikuwa ni Sh. bilioni 15.9 na Sh. bilioni 18.5 katika mwaka 2016/2017 na 2017/2018 mtawalia. Zaidi, nilibaini ukiukwaji wa miongozo ya malipo ya posho; ambapo Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASA) wamewalipa posho za nyumba wafanyakazi wao jumla ya Sh. bilioni 1.88 kinyume na mwongozo Na.TYC/T/200/583/18 wa mwaka 2018 uliotolewa na Msajili wa Hazina.

Pia, nilibaini kutokuwapo kwa miongozo ya malipo ya posho nyinginezo; ambapo Taasisi ya Utafiti wa Sukari iliwalipa posho kwa kazi za ziada wakufunzi wa kozi za kilimo bila kuwapo na muongozo

wa malipo hayo. Pia, jumla ya riba ya Sh. bilioni 32.25 inapaswa ilipwe na Mamlaka ya Ukanda wa Kutengeneza Bidhaa za Kuuza Nje ya Nchi (EPZA) na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASA) kutokana na kuchelewa kulipa fidia kwa wamiliki wa maeneo yaliyoathaminiwa.

Uwekezaji katika Mashirika ya Umma

Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025) na Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) vimelenga kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Mipango hiyo inaitaka Tanzania kutoka katika uchumi unaotegemea kilimo duni na kuwa nchi inayotegemea uchumi wa kilimo cha kisasa na viwanda.

Nilibaini Mpango Mkakati wa Muda Mrefu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) una mapungufu katika utekelezaji wa ajenda ya viwanda. Pia, nilibaini ukinzani kati ya Sheria ya Kodi ya mapato na motisha zilizotolewa kwa wawekezaji na Kamati ya Taifa ya Uendeshaji Uwekezaji nchini (NISC) kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya viwanda. Zaidi, nilibaini mwenendo mbaya wa uwekezaji na mapungufu katika ukusanyaji wa mapato ya kodi ya pango kutoka kwa wapangaji wa majengo au maeneo yanayomilikiwa na Mashirika ya Umma.

Mwenendo wa Benki za Serikali

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa kati ya benki 6 za Serikali benki 4 (asilimia 67) zilikuwa zikifanya biashara kwa hasara kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo. Hii ilisababisha Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) na Benki ya Twiga kuwa chini ya usimamizi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kutokana na kuwa na kiwango cha chini cha mtaji kama inavyotakiwa na BoT. Pia, nilibaini uwiano wa mikopo chechefu ya benki tatu dhidi ya mikopo yote ya benki hizo umekuwa ukiongezeka zaidi ya kiwango kilichowekwa cha asilimia 11.7 pamoja na lengo la BoT la asilimia 5. Pia, nilibaini Benki tano za Serikali zilikuwa na uwiano wa chini wa mtaji wa msingi na mtaji wa jumla ikilinganishwa na mali zinazoambatana na vihatarishi na mali zilizo katika hali hatarishi zilizo nje ya urari wa kimahesabu (off-balance sheet exposure) kama ilivyoainishwa katika Sheria za Benki na Taasisi

za Fedha ya mwaka 2014 na mwongozo wa BoT wa tarehe 5 Agosti, 2015.

Utendaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inasimamiwa na Mamlaka ya Udhhibiti ya Hifadhi za Jamii (SSRA). Nimeangalia utendaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) na Mifuko ya Pensheni, ikiwamo Mfuko wa Pensheni wa LAPF (LAPF), Mfuko wa Pensheni wa Sekta ya Umma (PSPF), Mfuko wa Taifa wa Mafao ya Watumishi wa Serikali (GEPF), Mfuko wa Pensheni PPF (PPF), na Mfuko wa Pensheni NSSF (NSSF) pamoja na utendaji wa SSRA.

Serikali ina deni ya jumla ya Sh. bilioni 2,390.08 kwenye Mifuko sita ya Hifadhi ya Jamii, ambapo kiasi cha Sh. bilioni 1,625.25 (sawa na asilimia 68) kilipaswa kiwe kimelipwa katika mwaka wa fedha 2017/2018. Mikopo mingine iliiva tangu mwaka 2014. Kuchelewa kulipwa kwa mikopo hiyo kumeathiri uendeshwaji wa Mifuko husika. Mfuko mpya wa Pensheni (Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Umma (PSSSF)) umebeba madeni ya mifuko iliyoungana ambayo yanaweza kuhatarisha ukwasi wa Mfuko huu. Mapendekezo ya kikokotoo kipya cha pensheni yalisababisha ongezeko la wastaafu wa hiyari kutoka wastaafu 2,562 mwaka 2016/17 mpaka wastaafu 4,730 mwaka 2017/18.

Pia, nilibaini Mifuko iliwekeza kiasi cha Sh. bilioni 55.17 na Sh. bilioni 3.15 katika benki M, na benki ya Covenant mtawalia. Hata hivyo, leseni za benki hizo zimefutwa na Benki Kuu ya Tanzania. Benki ya Azania imechukua mali na madeni ya benki M wakati benki ya Covenant ipo katika hatua ya kufilisiwa. Katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), nilibaini kupungua katika ukuaji wa akiba ya mfuko mwaka hadi mwaka kutokana na ongezeko la gharama za malipo kwa huduma ya afya inayotolewa kwa wanachama wa hiyari ikilinganishwa na mapato yanayokusanywa kutoka kwa wanachama hao. Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) unapaswa kuchukua hatua stahiki kuhakikisha mtaji wa mfuko unaongezeka.

Usimamizi wa Mikopo katika Mashirika ya Umma

Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) haikupata kibali cha kukopa kiasi cha Sh. milioni 372.76 kutoka kwa Bodi ya Usimamizi wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko. Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASA) imeshindwa kukamilisha mradi wa maji uliopo Chalinze kutokana na utata uliopo katika mkopo uliokopwa kutoka katika benki ya Export Import Bank ya India. Nilibaini kuwa DAWASA ilishindwa kulipa mkopo wa Sh. bilioni 47.40 kwa kipindi cha muda mrefu. Pia, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) limeshindwa kufanya marejesho ya mkopo waliokopa katika benki ya East African Development, ambapo NHC imekuwa ikifanya marejesho chini ya kiwango walichokubaliana.

Utendaji wa Mamlaka za Maji Safi

Ukaguzi wangu ulibaini mamlaka za maji zinatatizo kubwa la upotevu wa maji. Uchambuzi wangu katika Mamlaka 15 ulibaini kuwa upotevu wa Sh. bilioni 128.21 ulitokana na upotevu wa maji, ambapo kiasi cha Sh. bilioni 47.18 cha upotevu huo kipo juu ya kiwango kinachovumilika kwa mujibu wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Pia, Mamlaka zinadai jumla ya Sh. bilioni 97.58 za huduma ya maji kutoka katika Taasisi za Serikali, na wateja wengine; ambapo madeni hayo yanaathiri ukwasi na mwenendo wa Mamlaka hizo. Pia, nilibaini Mamlaka 12 zimekuwa zikiendeshwa kwa hasara na kuwa jumla zimepata limbikizo la hasara ya Sh. bilioni 221.66.

Usimamizi wa Ruzuku za Serikali katika Mashirika ya Umma

Ingawa Serikali imeendelea kutoa ruzuku za pembejeo kwa ajili maendeleo ya kilimo kwa ajili ya ustawi jamii, lakini nilibaini mapungufu mbalimbali katika pembejeo zenye thamani za Sh. bilioni 19.9 zilizotolewa kwa wakulima wa pamba katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18; ambapo baadhi ya wakulima walipewa viwatilifu zaidi kuliko ukubwa wa mashamba yao. Sikuweza kuona nyaraka za kupokelea viwatilifu hivyo. Pia sikuweza kuona uthibitisho wa saine za wakulima kupokea viwatilifu hivyo katika wilaya nilizofanya ukaguzi; wakati katika wilaya nyingine, viwatilifu viliuzwa kwa wakulima badala ya kugawiwa bure kama ilivyoelekezwa na Bodi ya Pamba.

Usimamizi wa Mali za Mashirika ya Umma

Katika usimamizi wa mali za Serikali nilibaini mapungufu yafuatayo: kutokuwa na rejista ya mali, kutokuwa na miongozo ya usimamizi wa mali pamoja na kutofuata kanuni na miongozo ya kahasibu katika utunzaji wa kumbukumbu za mali. Nimetoa mapendekezo katika usimamizi wa mali hizo, pamoja na mapendekezo katika utatuzi wa migogoro ya ardhi, matumizi mazuri ya mafuta, kurekodi mali zote zinazotakiwa kurekodiwa katika rejista, ukarabati wa mali hizo, kuweka kumbukumbu sahihi za uchakavu wa mali hizo pamoja na taarifa za mali hizo. Ninayo matumaini kuwa utekelezaji wa mapendekezo yangu utasaidia usimamizi wa mali za Mashirika ya Umma.

Usimamizi wa Manunuzi na Mikataba

Katika ukaguzi wangu nilibaini mapungufu kwenye manunuzi na usimamizi wa mikataba katika Mashirika ya Umma 138 niliyoyakagua. Katika manunuzi niliangalia utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Manunuzi pamoja na kanuni zake na mifumo iliyopo ya manunuzi katika mchakato mzima wa manunuzi na usimamizi wa mikataba.

Nilibaini kutokuwapo kwa usimamizi wa mfumo na utekelezaji Sheria za Manunuzi na kanuni zake katika Mashirika niliyokagua. Mapungufu hayo ni pamoja na kutokufanyika kwa tathmini katika mchakato wa manunuzi, kufanya manunuzi nje ya mpango, tozo za fidia kwa kutokutekeleza matakwa ya mkataba na baadhi ya Mashirika kushindwa kupeleka mipango yao ya manunuzi kwa Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi ya Umma (PPRA).

Matokeo ya Kaguzi Maalumu na Kaguzi za Kiuchunguzi

Katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), nilibaini kuwapo kwa malipo hewa ya kiasi cha Sh. bilioni 2.61. Katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), nilibaini kuwa Chuo hakipokei sehemu ya mapato kutoka kwenye kazi za ushauri zinazopatikana kupitia jina la chuo hicho. Hii ni kuwa kazi hizo hufanywa na makampuni yanayomilikiwa na wafanyakazi. Hii imebainika katika mkataba wenye thamani ya Sh. bilioni 5.49 ulioingiwa kati ya NHC na BICO kupitia Chuo Kikuu, ambapo asilimia 76% ya kazi hiyo ilifanywa na kampuni binafsi.

UDSM pia kilidahili wanafunzi zaidi kwa asilimia 560% ikilinganishwa na mpango wake. Katika Shirika la Bima la Taifa, nilibaini kuwa Shirika lililipa kiasi cha Sh. bilioni 3.59 kwa ajili ya kununua mfumo wa bima lakini mfumo huo haufanyi kazi.

Katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE), nilibaini MUCE iliingia mkataba na MM Engineering kisha M/s. CATIC International Engineering Limited kwa ajili ya ujenzi wa ukumbi wa mihadhara kwa gharama ya Sh. bilioni 3.62, ambapo gharama hizo ziliongezeka mpaka Sh. bilioni 9.10. Ujenzi huu ulikosa ufanisi, kwani kazi ilipaswa ikamilike Septemba 2011; lakini mpaka 10 Mei 2018 ujenzi ulikuwa umekamilika kwa asilimia 80.52. Katika Kampuni Tanzu ya UDA (UDART), nilibaini kuwa kati ya mabasi 305 yaliyohitajika kununuliwa, ni mabasi 165 tu yalinunuliwa na ndiyo yaliyokuwa yanafanya kazi.

Utekelezaji wa Sheria ya Kodi ya Mapato

Nilibaini migogoro ya kodi za mapato kati ya Mashirika ya Umma na TRA. Mashirika ya Umma hayo ni Mamlaka ya Udhhibiti wa Bima Tanzania (TIRA), Kampuni Hodhi ya Kusimamia Rasilimali za Shirika la Reli Tanzania (RAHCO), Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na Shirika la Simu Tanzania (TTCL). TTCL haijalipa kodi ya huduma (excise duty) Sh. milioni 234.41 tangu mwaka 2015 kutokana na kutokukamilika kwa usuluhishi kati ya TRA na TTCL.

Pia, nilibaini Mashirika kumi yamekuwa yakichelewa kutuma taarifa za kodi kwenda TRA. Taarifa hizo ni pamoja na ritani ya Kodi za ongezeko la thamani (VAT), kodi ya kuendeleza ufundi stadi (SDL) na kodi ya zuiu ambapo kuchelewa huko kunasababisha riba na adhabu. Kwa mfano, TBC halijalipa kodi yenye thamani ya Sh. bilioni 2.27. Pia nilibaini RAHCO inadai marejesho ya VAT kutoka TRA kiasi cha Sh. bilioni 84.39. Pia, ingawa Serikali inasisitiza utoaji wa stakabadhi za kielektroniki, Mashirika ya Umma bado yana mwenendo mdogo katika utoaji na uchukuaji wa stakabadhi za kielektroniki katika mauzo na manunuzi yake.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI NA TAARIFA ZA JUMLA

1.0 Uanzishaji wa Ofisi ya Ukaguzi Kisheria

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (kama ilivyorekebisha mara kwa mara). Ibara ya 143 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008 pamoja na kifungu cha 48(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.7 ya Mwaka 2011 vinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma si chini ya mara moja kwa mwaka wa fedha.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ana mamlaka ya kufanya ukaguzi wa hesabu na ukaguzi wa thamani ya fedha au kaguzi nyingine katika Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kama ilivyoainishwa kwenye vifungu Na. 26, 27, 28 na 29 vya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya Mwaka 2008. Kifungu cha 12 cha Sheria hiyo kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kutoa maoni kwa nia ya:

- Kuzuia au kupunguza matumizi ya fedha za Umma yasiyokuwa na tija;
- Kuongeza makusanyo ya maduhuli ya Umma;
- Kuzuia hasara inayoweza kutokea kwa uzembe, wizi, kukosa uaminifu, udanganyifu, au rushwa kuhusiana na fedha na rasilimali za Umma; na
- Kuongeza uchumi, tija na ufanisi katika matumizi ya fedha za umma

Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma nchini zinaandaa taarifa za hesabu kwa kufuata msingi usio wa fedha taslimu wa Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu (Accrual Basis). Hivyo basi, zinalazimika kufuata ama Viwango vya Kimataifa

vya Uandaaji wa Hesabu (IFRSs) au Viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa Hesabu katika Taasisi za Umma (IPSASs). Uandaaji na uwasilishaji wa hesabu kwa ajili ya ukaguzi ni matakwa ya sheria. Miongozo zaidi ya kisheria inayotumika kuandaa hesabu ni pamoja na Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002 au sheria yoyote iliyopitishwa na Bunge ya kuanzishwa kwa Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma na Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya Mwaka 2008.

Sheria namba 418 ya Msajili wa Hazina na kifungu cha 6 cha Sheria ya Mashirika ya Umma namba 16 ya mwaka 1992 kuhusiana na kazi za Mashirika, zinasema kwamba Msajili wa Hazina ana kazi na jukumu la kusimamia vyema uendeshaji wa shughuli za Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa kushirikiana na Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika husika. Vyombo vyote hivyo vinafanya kazi katika kusimamia na kuongoza kwa ukaribu Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa ufanisi na kwa kutoa maelekezo ya kiusimamizi.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kuwasilisha ripoti za mwaka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyoelekezwa katika Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Katika kanuni ya 88 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma, ripoti hizo zinatakiwa kuwasilishwa kwa Rais ifikapo tarehe 31 Machi ya kila mwaka. Baada ya kupokea ripoti hizo, Rais atawataka wahusika kuwasilisha ripoti hizo Bungeni ndani ya siku saba tangu kuanza kwa kikao cha kwanza cha Bunge.

Kama Rais hatachukua hatua zozote za kuwasilisha taarifa hizo Bungeni, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu atawasilisha nakala za ripoti hizo kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano (au Naibu Spika ikiwa kiti cha Spika kiko wazi wakati huo au ikiwa kwa sababu yeyote Spika hawezi kutekeleza majukumu yake) ambaye atawasilisha ripoti hiyo Bungeni. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inayohusu Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma itajadiliwa kwanza na Kamati za

Bunge za Hesabu (PAC) kwa niaba ya Bunge na kuandaa ripoti ambayo itawasilishwa Bungeni.

1.1 Wigo wa Ukaguzi na Viwango vya Ukaguzi Vinavyotumika

1.1.1 Wigo na Madhumuni ya Ukaguzi

Madhumuni ya kufanya ukaguzi ni kumuwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutimiza jukumu la kutoa maoni huru kuhusu hesabu za Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma ili kuona iwapo zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu. Ukaguzi huu unahusiana na hesabu zilizokaguliwa kwa kipindi kinachoishia tarehe 31 Desemba, 2017 na tarehe 30 Juni 2018.

Wigo wa ukaguzi wangu unajumuisha tathmini ya ufanisi wa mifumo ya kihesabu na udhibiti wa ndani katika shughuli za taasisi husika. Pia, unahusisha ukaguzi na uhakiki wa hesabu, ripoti za utekelezaji, na taratibu nyingine za kikaguzi ambazo ni muhimu katika kukamilisha ukaguzi. Ukaguzi huu ulifanyika kwa kuzingatia viashiria vya hatari na kiwango cha juu cha miamala kinachokubalika.

Kwa hiyo, matokeo ya ukaguzi yanatokana na kiwango ambacho kumbukumbu, nyaraka, na taarifa zilizoombwa kwa madhumuni ya ukaguzi na ziliwasilishwa kwangu.

1.1.2 Viwango vya Ukaguzi Vilivyotumika

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ni mwanachama wa Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi Duniani (INTOSAI), Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi za Nchi za Afrika (AFROSAI) na Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi kwa Nchi za Afrika Zinazoongea Kiingereza (AFROSAI-E). Hivyo, Ofisi inatumia Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi vya Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi Duniani (ISSAI) vinavyotolewa na “INTOSAI” na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Hesabu (ISA) vilivyowekwa na Shirikisho la Kimataifa la Wahesibu (IFAC).

1.2 Majukumu ya Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma

Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti za Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma zina jukumu la kutayarisha kwa usahihi hesabu kama inavyotakiwa katika Viwango vya Kimataifa vya Utayarishaji wa Hesabu (IFRSs) au Viwango vya Kimataifa vya Utayarishaji wa Hesabu katika Taasisi za Umma (IPSAS). Majukumu hayo yanajumuisha:

- a) Kuhakikisha taarifa za hesabu zinaandaliwa kwa kiwango cha kimataifa, ikiwa ni pamoja na kubuni, kutekeleza, na kudumisha mifumo thabiti ya ndani itakayoweza kuandaa hesabu zilizo huru, zisizo na makosa, wala mapungufu yatokanayo na udanganyifu;
- b) Kuchagua na kutumia sera sahihi za uandaji wa hesabu; na
- c) Kufanya makadirio ya hesabu yanayoendana na mazingira halisi. Viwango vya Kimataifa cha Uhasibu Na. 1 (IAS 1) na Viwango vya Kimataifa vya Utayarishaji wa Hesabu za Taasisi za Umma Na. 1 (IPSAS 1) vinaainisha aina za hesabu zinazotakiwa kuandaliwa na taasisi hizi.

1.3 Mpangilio na Uteuzi wa Makampuni Binafsi kwa Kazi ya Ukaguzi

Ili Ofisi yangu iweze kutimiza majukumu ya ukaguzi kwa ufanisi katika Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma nchini, kitengo cha ukaguzi wa Mashirika ya Umma kimegawanywa katika vijitengo vinne ambavyo ni Ukaguzi wa Taasisi za Fedha, Ukaguzi wa Taasisi za Elimu ya Juu, Ukaguzi wa Taasisi za Usimamizi na Ukaguzi wa Taasisi za Huduma.

Pia, kaguzi za baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma yamekaguliwa na makampuni binafsi ya ukaguzi kwa niaba yangu. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 33 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, ambacho kinampa mamlaka Mdhibiti na

Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya kumruhusu mtu au kampuni yeyote iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Wakaguzi wa Hesabu na Wahasibu Na. 33 ya Mwaka 1972 iliyorekebishwa mwaka 1995 kufanya ukaguzi kwenye Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa niaba yake.

Wakaguzi watakaoteuliwa watafuata sheria kama inavyotakiwa; pia hawatatoa siri za mashirika wanayoyakagua. Wajibu wa kutoa hati ya ukaguzi unabaki kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kaguzi zitakazofanywa na Makampuni binafsi zitahakikiwa ubora wa kazi zake na Ofisi yangu.

SURA YA PILI

AINA ZA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA

2.0 Utangulizi

Kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi Namba 200 (ISA 200), lengo la kufanya ukaguzi wa hesabu ni kumwezesha Mkaguzi kutoa hati ya ukaguzi inayoeleza iwapo hesabu zinaonesha hali halisi ya kifedha ya Shirika na kama zimeandaliwa kwa kufuata viwango na mfumo unaokubalika. Ukaguzi wa hesabu unafanyika ili kumpa uhakika mtumiaji wa hesabu husika kwamba zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika. Hivyo, kumfanya Mkaguzi kupata sababu za uhakika kwamba hesabu kwa ujumla wake hazina makosa na pia kutoa taarifa ya matokeo ya ukaguzi.

2.1 Aina za Hati za Kaguzi Zilizotolewa

2.1.1 Hati Inayoridhisha

Hati hii inatolewa wakati Mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu au viwango vingine vya utoaji wa taarifa za fedha vinavyokubalika.

2.1.2 Hati zisizoridhisha

i. Hati Yenye Shaka

Aina hii ya hati hutolewa pale;(a) Mkaguzi anapokuwa amepata vielelezo vya kutosha kuhitimisha ukaguzi na kuona athari lakini si za kimsingi katika usahihi wa taarifa za fedha; au (b) mkaguzi anapokuwa ameshindwa kupata uthibitisho wa kutosha kumuwezesha kuhitimisha ukaguzi lakini athari zinazotokana na kukosa uthibitisho kwa ujumla wake si za kimsingi katika usahihi wa taarifa za fedha.

ii. Hati Isiyoridhisha

Hati isiyoridhisha inatolewa pale Mkaguzi anapona kuwa, taarifa za fedha kwa kiasi kikubwa zina makosa; na

zikiangaliwa kwa ujumla wake zinakuwa hazikufuata viwango vinavyokubalika vya uandaaji wa taarifa za fedha.

iii. Hati Mbaya

Hati hii hutolewa pale mkaguzi anaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kuhusu taarifa za fedha zilizoandaliwa kwa ajili ya ukaguzi. Hali hiyo inaathiri taarifa za fedha kiasi cha kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi kuhusiana na taarifa za fedha hizo.

2.1.3 Aya za Msisitizo wa Jambo Kwenye Ripoti ya Mkaguzi

Kama mkaguzi ataona umuhimu wa kuwatanabaisha wasomaji wa taarifa za fedha kuhusu suala ambalo limeoneshwa au kuainishwa kwenye taarifa za fedha, na ambalo limeonekana kuwa ni muhimu na la msingi kwa ajili ya kuleta uelewa wa taarifa hizo kwa ajili ya kufanya maamuzi yenye tija, ataweka Aya za Msisitizo. Aya hii itawekwa tu pale ambapo mkaguzi amepata vielelezo vya kutosha kuwa taarifa za fedha hazijakosewa kwa kiasi kikubwa; na inatakiwa itokane na suala ambalo limeoneshwa au kuainishwa kwenye taarifa za hesabu.

2.1.4 Aya ya Mambo Mengineyo ya Ukaguzi

Kama mkaguzi ataona umuhimu wa kuwasilisha mambo mengineyo zaidi ya yale ambayo yameoneshwa au kuainishwa kwenye taarifa za fedha; na kwa maono ya mkaguzi ni muafaka kwa watumiaji wa taarifa za fedha ili waweze kufahamu ukaguzi, majukumu ya mkaguzi au ripoti ya ukaguzi, ataweka Aya ya Mambo Mengineyo katika ripoti yake.

2.2 Uwasilishaji wa Mambo Muhimu ya Ukaguzi

Katika kipindi cha mwaka 2017/2018, kulikuwa na jumla ya hati za ukaguzi 122. Kati ya hizo, zinazoridhisha ni 121; Pia, hati moja (1) isiyoridhisha ilitolewa; na hapakuwa na hati yoyote mbaya au yenye mashaka. Angalia *Kiambatisho Na. I.*

2.3 Muelekeo wa Hati za Ukaguzi

Uchambuzi wa mielekeo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa Mashirika ya Umma kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2013/2014 mpaka 2017/2018 ni kama ifuatavyo:

Jedwali Na. 1: Muelekeo wa hati za Ukaguzi

| Aina ya Hati ya Ukaguzi | Ukaguzi Ripoti Kuu ya Mwaka | | | | |
|-------------------------|-----------------------------|------------|------------|------------|------------|
| | 2013/2014 | 2014/2015 | 2015/2016 | 2016/2017 | 2017/2018 |
| Mwaka wa fedha | | | | | |
| Zinazoridhisha | 117 | 107 | 108 | 101 | 121 |
| Zenye mashaka | 3 | 5 | 4 | 4 | 0 |
| Zisizoridhisha | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Mbaya | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Jumla | 121 | 112 | 112 | 115 | 122 |

Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa

SURA YA TATU

MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MIAKA ILİYOPITA

3.1 Utangulizi

Sura hii inaainisha kwa ufupi muhtasari wa utekelezaji wa mapendekezo ya Ripoti ya Ukaguzi wa miaka iliyopita. Baadhi ya mapendekezo hayajatekelezwa, na mengine yakiwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji hadi ilipofikia wakati wa kuandaa taarifa hii kama ilivyoainishwa kwenye kifungu namba 40 (4) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya mwaka 2008.

Tarehe 15 Mei, 2018 nilipokea majibu ya Serikali ya ripoti ya mwaka uliopita kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali. Ninapenda kutambua juhudi zilizofanywa na Mlipaji Mkuu wa Serikali katika kujibu na kuandaa mpango wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwa Mashirika ya Umma.

3.2 Tathmini ya hali ya utekelezaji wa mapendekezo kwa kipindi kilichopita

Kati ya mapendekezo 112 ya ripoti yangu ya mwaka iliyopita, mapendekezo 54 (asilimia 46) yametekelezwa, 36 (asilimia 32) yapo kwenye hatua ya utekelezwaji, 18 (asilimia 16) hayajatekelezwa na mapendekezo 6 (asilimia 6) yamepitwa na wakati. Kati ya mapendekezo 18 ambayo hayajatekelezwa na Serikali, 14 (asilimia 78) hayana majibu kabisa kuonesha mwendelezo wa utekelezaji wake. Tathmini ya majibu imeonesha kuwa, mapendekezo mengi bado hayajatekelezwa na mengine yapo kwenye hatua za utekelezaji.

Kwa hali hiyo, hatua za ziada zinahitajika katika utekelezaji wa mapendekezo hayo. Maelezo ya tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo na uchambuzi wa muda

wa miaka yake ni kama inavyooneshwa kwenye kiambatisho namba II na jedwali namba 2.

Jedwali Na. 2: Tathmini ya hali ya utekelezaji wa mapendekezo kwa kipindi kilichopita

| Mwaka wa Fedha | Yametekele zwa | Yanayotekele zwa | Hayajateke lezwa | Yamepit wa na muda | Jumla |
|----------------|----------------|------------------|------------------|--------------------|------------|
| 2012/13 | 9 | 1 | | 1 | 11 |
| 2015/16 | 24 | 9 | 5 | 2 | 40 |
| 2016/17 | 19 | 26 | 13 | 3 | 61 |
| Jumla | 52 | 36 | 18 | 6 | 112 |
| Asilimia | 46 | 32 | 16 | 6 | 100 |

Kuchelewa kutekelezwa kwa mapendekezo kunasababisha kujirudia kwa mapungufu yaliyoainishwa; hivyo kuzorotesha utendaji na ufanisi wa huduma zitolewazo katika taasisi za Umma.

Kwa hiyo napenda kuisisitiza Serikali, kupitia kwa Mlipaji Mkuu, iwahimize maafisa masuuli kujibu kwa wakati mapendekezo yaliyotolewa ili kuboresha ufanisi katika utoaji wa huduma kwenye Mashirika ya Umma na taasisi nyingine.

SURA YA NNE

TATHMINI YA UTENDAJI KIFEDHA NA HALI YA MUENDELEZO WA UTOAJI HUDUMA KWA TAASISI ZA UMMA

4.0 Utangulizi

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali inamiliki jumla ya Mashirika ya Umma 201¹. Mashirika hayo ya Umma yanajumuisha yale yote ambayo yanazalisha faida kulingana na utendaji wao.

Tathmini kwa hali ya utendaji kifedha kwa taasisi za Umma ilifanyika, ikiwamo kuwapo kwa faida iliyopatikana kutoka katika mtaji uliowekezwa. Kwenye mapitio ya tathmini ya utendaji kifedha na hali ya uendelevu katika utoaji huduma kwa taasisi 138, nimekuja na mapungufu na mapendekezo yafuatayo:

4.1 Mashirika Yasiyo na Uhakika Katika Utoaji Huduma kwa Siku za Usoni

Wakati napitia Mashirika ya Umma kwa ajili ya kuangalia uwezo wa kifedha, niligundua kuna mashirika 14 ambayo hayana uhakika katika utoaji wa huduma zake katika siku za usoni kwani uwiano wa madeni na mtaji ni zaidi ya asilimia 100. Mashirika 9 kati ya 14 yana ukwasi hasi kwa maana yanajiendesha kwa hasara kwa zaidi ya miaka 2 sasa (Rejea jedwali namba 3). Uwiano mkubwa wa kutumia mikopo na ruzuku kujiendesha unamaanisha kuwa Taasisi haiwezi kumudu gharama zake za uendeshaji bila kutegemea wahisani. Kufuatia hali ngumu ya kiuchumi kwa baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma, ni dhahiri kuwa hayawezi kujiendesha bila kutegemea msaada kutoka Serikalini. Kuna hatari kwa taasisi hizi kuanguka na kuathiri huduma zitolewazo kwa jamii.

¹ Ripoti ya Msajili wa Hazina

Jedwali Na. 3: Mashirika ya Umma yenye hali mbaya kifedha

| Taasisi | Mwaka wa Fedha | Hasara-Sh. "000" | Mtaji-Sh. "000" | Deni-Sh. "000" | Uwiano wa mkopo na mtaji |
|---|----------------|------------------|-----------------|----------------|--------------------------|
| Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Lindi | 30-Juni-18 | (92,968) | (265,129) | 38,288,041 | (144.41) |
| Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Lindi | 30-Juni-17 | (47,001) | (172,091) | 9,450,293 | (54.91) |
| Shirika la Maendeleo ya Petroli | 30-Juni-18 | (64,543,000) | (375,136,000) | 3,544,892,000 | (9.45) |
| Bodi ya Utalii Tanzania | 30-Juni-18 | (110,417) | (258,298) | 2,023,503 | (7.83) |
| DAWASCO | 30-Juni-18 | (8,528,170) | (32,542,827) | 93,167,173 | (2.86) |
| Baraza la Michezo la Taifa | 30-Juni-18 | (27,510) | (125,098) | 182,711 | (1.46) |
| Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) | 30-Juni-16 | (38,641,049) | (129,981,792) | 166,036,782 | (1.28) |
| Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) | 30-Jun-17 | (16,120,696) | (146,359,685) | 184,758,843 | (1.26) |
| Tanzania Geothermal Development Company Limited | 30-Jun-17 | (3,224,978) | (5,997,399) | 7,159,180 | (1.19) |
| Baraza la Biashara la Taifa | 30-Jun-18 | (297,562) | (922,353) | 1,073,370 | (1.16) |
| DAWASCO | 30-Jun-18 | (8,528,170) | (32,542,827) | 93,167,173 | 2.86 |
| Mamlaka ya Maji Safi na usafi wa Mazingira Mtwara | 30-Jun-18 | (117,976) | 4,875,088 | 7,420,069 | 1.52 |
| Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza | 30-Jun-18 | (378,442) | 38,057,178 | 92,703,879 | 2.44 |
| Electrical Transmission and Distribution Construction and Maintenance Company Limited | 30-Jun-17 | (773,888) | 220,937 | 633,733 | 2.87 |
| Kampuni ya TTCL Pesa | 30-Jun-18 | (360,305) | 139,695 | 577,592 | 4.13 |
| Bodi ya Maziwa Tanzania | 30-Jun-18 | (33,662) | 4,913 | 84,901 | 17.28 |

Chanzo: Taarifa za fedha kwa mwaka 2017/18

Napendekeza Serikali ifanye mapitio ya namna ya uendeshaji wa Mashirika haya na kuongezea mitaji ili yaweze kumudu gharama za uendeshaji.

SURA YA TANO

USIMAMIZI WA MAPATO KATIKA TAASISI ZA UMMA

5.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea matokeo ya kaguzi juu ya usimamizi wa mapato katika taasisi mbalimbali za Umma katika mwaka wa fedha 2017/2018. Usimamizi wa mapato ni kipengele muhimu sana katika Taasisi za Umma, kwani huchangia kiasi kikubwa katika kuzalisha fedha taslimu hivyo kuiwezesha Taasisi kukidhi mahitaji yake ya kifedha pale inapohitajika. Pia, usimamizi wa mapato huchangia kwa kiasi kikubwa katika kufanya vizuri kwa Taasisi za Umma kwa kuwa huathiri faida inayopatikana. Yafuatayo ni masuala niliyoyabaini katika usimamizi wa mapato katika ukaguzi wa taasisi mbalimbali za Umma:

5.2 Kuwapo kwa Wadaiwa Sugu wa Pango

Wapangaji 623 wameendelea kupokea huduma ya upangaji kutoka Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC), huku wakiwa na madeni sugu ya pango yanayofikia Sh. bilioni 3.80, ingawa Sera ya Usimamizi wa Mali ya mwaka 2010 inataka ada ya pango kulipwa miezi miwili kabla.

Shirika la Bima la Taifa (NIC) liliripoti madai ya kibiashara na madai mengine ya muda mrefu yanayofikia Sh. bilioni 53. Upungufu wa thamani unaofikia Sh. bilioni 10 ulifanyika katika madai hayo.

Kuna uwezekano kuwa mapato yaliyorekodiwa hayakuwa halisi. Hii ni kwa kuwa ukusanyaji wa madai hayo umekuwa mgumu, hivyo unaweza kusababisha hasara kutokana na mrundikano wa madai hayo.

Nakishauri kituo cha AICC kutekeleza matakwa ya sera ya upangaji ili kuwa na usimamizi imara wa mapato.

5.3 Udhaifu katika Utaratibu wa Mauzo na Makabidhiano

Katika mapitio ya sampuli za mauzo yanayofikia Sh. bilioni 8.82 kati ya mauzo ya Sh. bilioni 251.38 ya na Bohari Kuu ya Dawa (MSD), nilibaini kukosekana kwa ushahidi kama nakala zilizopigwa muhuri au hati ya mapokezi au ankara zinazonesha kuwa bidhaa hizo zenye thamani ya Sh. bilioni 3.84 zimeuzwa, zimekabidhiwa kwa mteja na mteja husika amezikubali. Hii ni kinyume na Mwongozo wa Uhasibu wa MSD unaotaka mteja aliyeuziwa kuthibitisha kuwa amepokea bidhaa husika. Pia, vifaa tiba vyenye jumla ya thamani ya Sh. bilioni 1.45 vilivyozwa kwa vituo vya tiba 18 vilirudishwa MSD kwa kuwa havikuagizwa na vituo husika.

Pia, MSD hufanya mauzo kwa utaratibu maalum, ambapo vituo vya tiba hutumia mapato waliyozalisha wenyewe kununua vifaa tiba. MSD huainisha mahitaji na manunuzi yanayofanyika katika utaratibu huo kama manunuzi maalum. Nilibaini kuwa, vifaa tiba vya Sh. bilioni 3.55 vilivyonunuliwa kwa mfumo wa manunuzi maalum vilivyorudishwa kutokana na kuzidi kiasi walichoagiza wateja kutokuwa na sifa zilizotakiwa na wateja. Baadhi ya vifaa tiba vilivyorudishwa vilikuwa vikikaribia kikomo cha muda wa matumizi kwa kuwa vilitumia hadi miezi saba (7) kufika MSD. Vifaa hivyo vilipokelewa na MSD kwa kuwa hakukuwa na vigezo na masharti yanayohusiana na urudishaji wa vifaa tiba vilivyozwa.

Kurudisha bidhaa zilizonunuliwa chini ya utaratibu maalum kunaweza kusababisha ufujaji wa fedha za Umma kwani bidhaa zilizorudishwa zinaweza kuwa hazihitajiki na wengine. Pia, kuuza bidhaa bila kuwa na uthibitisho kuwa zimepokelewa na mteja kunaweza kusababisha ubadhirifu katika mauzo, na bidhaa kutomfikia mteja husika.

Napendekeza kuwa MSD ifuate utaratibu wa mauzo na makabidhiano na mteja uliowekwa, na kuzingatia sifa za

bidhaa kama alivyoagiza mteja kuepuka madhara tajwa hapo juu.

5.4 Utumikaji wa Bei Zisizo Sahihi na Malipo kwa ajili ya Wanachama Wasiochangia

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) una bei elekezi zilizopitishwa na kukubalika kwa kila huduma inayotolewa na vituo vya tiba.

Hata hivyo, nilibaini madai kwa mfuko wa NHIF ambayo yametumia bei kubwa zaidi ya zile ambazo zimepitishwa na kukubalika. Kutoka kwenye sampuli ya vituo vya tiba vya Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya TMJ, Kliniki ya Tiba ya Regency na KCMC, nilibaini malipo ya ziada ya Sh. milioni 141.61 kutokana na kuongezwa kwa bei katika madai. Pamoja na hayo, nilibaini malipo ya Sh. bilioni 4.80 yaliyofanywa na NHIF kwa vituo vya tiba kwa ajili ya wateja ambao hawakuchangia katika mfuko, kinyume na taratibu za bima ya afya.

Mapungufu yaliyobainika yanaweza kuwa yameusababishia mfuko hasara kwa kuzingatia idadi ya vituo vya tiba vinavyofanya kazi na mfuko.

Napendekeza Menejimenti ya NHIF kuboresha udhibiti kwenye madai kwa kuhakikisha inatumia mfumo wa komputa. Pia, inaweka utaratibu wa kuhakiki madai pamoja na kuongeza umakini katika suala hilo kwa sasa.

5.4 Madai Makubwa Kutoka kwa Watoto Tegemezi Wasioostahili

Nilibaini malipo yaliyofanyika kwa vituo vya tiba ya Sh. bilioni 13.99 kwa ajili ya watoto tegemezi ambao wamefikia umri wa miaka 18. Hii ni kinyume na Sheria ya NHIF ambayo inaweka kikomo cha watoto tegemezi kuwa chini ya miaka 18. Malipo haya yamesababisha upotevu wa fedha kwa mfuko wa NHIF. Fedha hizo zingeweza kutumika katika shughuli nyingine za maendeleo.

Ninapendekeza menejimenti ya NHIF ihuishe kanzi data yake ili kuwatambua watoto tegemezi waliozidi umri wa kisheria na kuweka udhibiti ambao utahakikisha hawahudumiwi tena na bima.

5.5 Kukinzana kwa Taarifa za Watalii kati ya Idara

Tathmini yangu ya Mamlaka ya Usimamizi wa Eneo la Ngorongoro (NCAA) ilibaini tofauti ya taarifa za watalii kati ya Idara ya Utalii na Idara ya Fedha. Nilibaini kuwa Idara ya Utalii ilirekodi jumla ya watalii 1,040,618 na 787,032 kama jumla ya watalii wa nje na wa ndani mtawalia wakati Idara ya Fedha ilirekodi watalii wa nje na wa ndani 1,016,607 na 791,140, mtawalia. Idara ya Utalii ilirekodi watalii wa nje 24,011 zaidi na wa ndani pungufu kwa 4,108 ikilinganishwa na Idara ya Fedha kati ya mwaka 2015/16 na 2017/18. Idadi ya watalii ilitakiwa kufanana kwa idara zote kwa kuwa ina athari ya moja kwa moja kwenye mapato yaliyorekodiwa.

Pia, nilibaini kuwa ada zilizoingizwa kwenye mfumo wa Safari Portal wa NCAA hazishabihiani na Tangazo la Serikali Na.2017, kwani baadhi ya tozo zilizotumika hazipo katika Muongozo wa Tozo; na baadhi ya nukuu zilizolipwa hazikuonekana katika mfumo wa Taarifa za Fedha wa ADV.

Kuna uwezekano kuwa taarifa za mapato ya utalii zimekosewa; na menejimenti ya NCAA inaweza kupewa taarifa ambazo si sahihi, hivyo kufanya maamuzi ambayo si sahihi pia.

Ninapendekeza menejimenti ya NCAA kuhakikisha kulandana kwa taarifa kupitia kufanya usuluhishi wa taarifa kati ya idara na kuwianisha tozo zilizopo kwenye portal na Tangazo la Serikali. Pia, sababu za tofauti zilizobainika zinahitaji kuchunguzwa ili kuchukua hatua za kusahihisha.

5.6 Ukokotoaji Usio wa Kawaida wa Tozo za Adhabu na Ada ya Utambulisho wa Makundi ya Bidhaa

Kutoka kwenye sampuli ya miamala ya tozo za adhabu 50 na miamala 60 ya ada za utambulisho wa makundi ya bidhaa, nilipata jumla ya miamala 7 na 6, mtawalia. Shirika la Viwango Tanzania (TBS) limetumia thamani za bidhaa tofauti na zile zilizohibitishwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kutoza adhabu ya asilimia 15 kwenye mizigo ambayo haijakaguliwa katika utaratibu wa Uhakiki wa Kukidhi Vigezo kabla ya Kusafirisha na asilimia 0.2 katika Utambulisho wa Makundi ya Bidhaa. Vitendo hivi ni kinyume na matakwa ya Kifungu cha 5.1.5 cha Taratibu za Ukaguzi Bidhaa zilizofika Kutoka Nje.

Nilibaini pia kuwa TBS wakati mwingine imekuwa ikitoza asilimia 15 ya adhabu katika mizigo ambayo haijakaguliwa katika utaratibu wa uhakiki wa Kukidhi Vigezo kabla ya Kusafirisha kwa bidhaa zinazodhibitiwa tu badala ya mzungu wote. Kitendo hiki ni kinyume na matakwa ya Kifungu cha 5.1.5 (c) cha Taratibu za Ukaguzi Bidhaa zilizofika Kutoka Nje.

Kutokana na kutofautiana huko, shirika linapoteza mapato kwa kutumia thamani ndogo zaidi ya zile ambazo zimethibitishwa na TRA. Pia, haki inashindwa kutendeka kwa baadhi ya waagizaji wa bidhaa. Hii ni kutokana na ukweli kwamba misingi tofauti ya tozo imetumika kuadhibu waingizaji tofauti wa mizigo ambayo haijakaguliwa kabla ya kusafirishwa katika bandari ya upakiaji.

Ninapendekeza TBS kutumia thamani ya bidhaa iliyohibitishwa na TRA ili kukidhi matakwa ya Taratibu za Ukaguzi Bidhaa zilizofika Kutoka Nje.

5.7 Kutopatikana kwa Wafaidika wa Mikopo

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ina jumla ya mikopo yenye thamani ya Sh. trilioni 1.46 ambayo imeshindwa kuwapata wakopaji husika. Kiasi hiki cha fedha

ni kikubwa sana kwa kuzingatia muongozo wa Kifungu cha 4(h) cha Sheria ya Bodi ambayo inataka Bodi kutengeneza mtandao na kushirikiana na taasisi na mashirika mbalimbali ili kuwatambua wadaiwa ili kuweza kupata marejesho ya mikopo iliyotolewa.

Kuwa na mikopo mikubwa ambayo wafaidika wameshindwa kupatikana kunapunguza uwezo wa Bodi wa kuendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wapya na wanaoendelea.

Ninapendekeza Bodi ishirikiane na taasisi nyingine na vyanzo vingine vya taarifa ili kuiongeza nguvu kanzidata yake na kuweza kuwatambua wakopaji ambao haijaweza kuwatambua.

5.8 Kutumika kwa Leseni Moja Zaidi ya Gari Moja

Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa nchi Kavu na Majini (SUMATRA) ndiyo yenye jukumu ya kutoa leseni ambazo zina namba ya kipekee kwa kila chombo cha usafiri kinachohitaji leseni. Hata hivyo, baada ya ukaguzi na kufanya marejeo ya leseni 165,230 niligundua leseni 20 zilitolewa kwa gari zaidi ya moja. Hii inaweza kutoa mianya ya uwezekano wa kufanyika udanganyifu ambao utasababisha Serikali ikose mapato.

Napendekeza kuwa SUMATRA warekebishe mapungufu yaliyojitokeza ili kuondoa uwezekano wa Mamlaka kupoteza mapato.

5.9 Udhaifu Katika Ukaguzi na Utoaji wa Leseni kwa Viwanja vya Ndege

Kutokana na ukaguzi niliufanya kwenye viwanja vya ndege 30 kati ya 70 niligundua kuwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania haifanyi kabisa ukaguzi katika viwanja vinne vya ndege ambavyo ni Kasense, Matipwili, Mashado na uwanja wa ndege wa Lila. Pia, katika mapitio yangu ya mafaili na ripoti za ukaguzi nilibaini kuwa kati ya viwanja 30 nilivyotembelea, 6 vinafanya kazi lakini havijasajiliwa, kinyume na kanuni za usafiri wa anga

kifungu namba 15 (1) za mwaka 2017. *Rejea kiambatisho namba III.*

Mamlaka ya Usafiri wa Anga wana wajibu wa kukagua leseni za Minara yakuongozea ndege ili kujiridhisha kama kinafaa kwa matumizi. Hali hii inasababisha kupungua kwa mapato kwa Mamlaka na hata ndege zinazotumia viwanja hivyo kuwa katika hatari.

Napendekeza kuwa, Menejimenti ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege iongeze usimamizi katika ukaguzi na utoaji wa leseni kwa kuhakikisha viwanja vyote vinakaguliwa na vinakuwa na leseni halali.

5.10 Udhaifu katika mifumo ya Ankara

Baad Udhaifu Katika Mifumo ya Ankara Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Ankara za mizigo 39,239 (asilimia 17) kati ya ankara 237,516 hazioneshi taarifa muhimu za malipo kama vile gharama za kuhifadha mzigo tofauti na ankara halisi ambayo ina taarifa zote zinazohusiana na mzigo. Pia, mfumo wa Ankara hauchukui ankara za meli ambazo zimetengenezwa nje ya mfumo. Kwa kipindi kilichoishia mwezi Juni 2018 niligundua pia Mamlaka ya Bandari inatumia viwango tofauti kutoka kwenye kitabu cha tozo katika kukokotoa mapato. *Rejea kiambatisho namba IV* kwa maelezo zaidi.

Udhaifu uliogundulika unaweza kusababisha kunakiliwa kwa taarifa za mapato zilizo tofauti. Hivyo basi, napendekeza Mamlaka ya Bandari iwasiliane na mtaalam aliefunga mfumo ili kuweza kutafuta suluhu katika eneo la ankara.

5.11 Kutofautiana kwa Taarifa za Tozo kwa Ajili ya Maegesho kati ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na Mamlaka ya Bandari Tanzania

Mamlaka ya Mapato Tanzania wanakusanya tozo za maegesho ya meli kwa niaba ya Mamlaka ya Bandari; na kila mwisho wa mwezi Mamlaka ya Bandari inafanya usuluhishi wa kibenki. Hata hivyo,

wakati wa ukaguzi katika eneo la mapato ya maegesho niligundua tofauti ya Sh. bilioni 42.5 katika kumbukumbu za TPA na TRA. Mamlaka ya Bandari inasema haipati maelezo/ushirikiano wa kutosha inapofikia suala la usuluhisho pindi inapotokea tofauti.

Napendekeza Mamlaka ya Bandari iboreshe usuluhishi wa kibenki katika eneo la tozo za maegesho ili kuhakikisha inafanyika kwa ufanisi na usahihi; na tofauti za kimahesabu zinamalizwa kwa wakati.

5.12 Udhaifu katika Usimamizi wa madeni ya Wadaiwa wa Kampuni ya Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTCL)

Wakati wa mapitio ya nyaraka za wadaiwa wa Kampuni ya Mawasiliano ya simu Tanzania (TTCL) niligundua tofauti ya Sh. bilioni 24.71 kati ya taarifa zilizopo kwenye vitabu vya TTCL na taarifa zilizothibitishwa na wateja. Wateja walithibitisha jumla ya Sh. bilioni 100.46, wakati taarifa zilizopo kwenye vitabu zinaonesha kuna deni la Sh. bilioni 125.18. Tofauti hii ilibainika baada ya kugundua kuwa TTCL haifanyi usuluhishi wa kila mwezi kati ya nyaraka walizonazo na zile za uthibitisho kutoka kwa wateja kwa ajili ya kupata usahihi, kinyume na kifungu Namba 3.11.2 (f) cha Mwongozo wa kiuhasibu wa Kampuni.

Pia, niligundua tofauti ya Sh. bilioni 109.59 kati ya mfumo wa utayarishaji hesabu na mfumo wa bili ambapo mfumo wa utayarishaji hesabu umeripoti Sh. bilioni 208.35 na mfumo wa bili; uliripoti Sh. bilioni 98.76. Kati ya Sh. bilioni 208.35 ambazo zimeripotiwa kama deni kwa wadaiwa, Utawala umeshindwa kutoa uthibitisho wa viambatisho vya deni la wadaiwa kiasi cha Sh. bilioni 91.43.

Taarifa za madeni ya wadaiwa inawezekana zikawa zimerekodiwa kimakosa katika vitabu vya uhasibu. Hivyo basi, naishauri Menejimenti ya TTCL ichunguze tofauti nilizobaini na kurekebisha hesabu ili kuripoti deni kwa usahihi.

5.13 Kutotimia kwa Taarifa ya Mapato

Mfuko wa huduma za mawasiliano (UCSAF) ndio uliopewa jukumu la kutoza ushuru kwa watoa huduma za mawasiliano nchini ambao wamesajiliwa ndani ya Tanzania kupitia Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa kiwango cha asilimia 0.7 cha mapato ghafi kama ilivyoainishwa kweye sheria ya Huduma za mawasiliano ya mwaka 2009. Hata hivyo, nilibaini kuwa Mfuko unatumia taarifa zinazokinzana na zile za Mamlaka kwani Mfuko una jumla ya watoa huduma za Mawasiliano 99 tu, wakati Mamlaka ina jumla ya watoa huduma 334.

Kutumia taarifa zisizo sahihi kunasababisha upotevu wa mapato kutoka kwa Mfuko (UCSAF) hivyo basi, naishauri Menejimenti ya Mfuko wa Huduma za Mawasiliano kuhuisha kanzidata yao ili iweze kulingana na ile iliyopo kwenye Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano nchini.

5.14 Kutosimamia kwa Mapato ya Matangazo, Kumbi na Maegesho kutoka kwa Kampuni ya Mlimani Holding Limited

Kifungu namba 10.1 cha mkataba wa upangaji kati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Kampuni ya Mlimani Holding Ltd (MHL) kinakitaka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam au wawakilishi wao kuweza kupitia vitabu vya Kampuni ya MHL kwa ajili ya kuthibitisha kiwango cha upangaji wanachotoza kwa wapangaji waliopo ndani ya majengo na huduma za maegesho zitolewazo. Kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2018 imebainika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hakitimizi majukumu yake ya kimkataba kwa kushindwa kupitia viwango vya tozo; hivyo kutegemea taarifa zitolewazo na Kampuni ya MHL. Jumla ya kiasi cha Dola za Kimarekani 10,869.90 na dola 8,204.73 ziliwasilishwa kwa Chuo Kikuu kama kiwango cha gawio la mwaka kutokana na mgawanyo wa hisa katika mapato ya eneo la matangazo na maegesho ya magari, mtawaliwa. Hata hivyo, nimethibitisha kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hakijafanya uhakiki wowote kujiridhisha na usahihi wa hesabu za mapato hayo.

Pia nilibaini kuwa, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam hakina idadi kamili ya vikao na makongamano yaliyofanyika ndani ya ukumbi wa mikutano wa Mlimani City. Hivyo kutokuwa na uwezo wa kujua kiwango halisi cha mapato yaliyopatikana kutokana na kukodishwa kwa ukumbi huo. Kutokana na kushindwa kumsimamia mpangaji, ni dhahiri Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hakiwezi kuthibitisha thamani halisi ya hisa zilizopo na kiwango cha gawio kinachostahili kulipwa.

Napendekeza kuwa, Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ifanye ufuatiliaji wa karibu na wa mara kwa mara, ikiwamo ukaguzi wa vitabu, ili Chuo kiweze kupata stahiki zake kwa usahihi kutoka kwenye mradi wa Mlimani City.

5.15 Kutegemea zaidi Wahisani wa Maendeleo katika kufanikisha shughuli za msingi za Taasisi

Ofisi ya Taifa ya Takwimu ni taasisi ya Serikali ambayo majukumu yake ni kuhakikisha masuala yote yanayohusu takwimu yanasimamiwa na kuratibiwa na wao kupitia mfumo wa Taifa wa Takwimu (NBS).

Nilibaini kuwa kwa kiwango kikubwa, shughuli kuu zifanywazo na taasisi hii zinafadhiliwa na wahisani. Katika kipindi cha mwaka wa ukaguzi taasisi ilikuwa na bajeti ya Sh. bilioni 1.64 ambayo inawezeshwa na Serikali kwa ajili ya kushughulikia masuala muhimu yahasuyo taasisi; isipokuwa Mishahara. Kiasi cha Sh. bilioni 13.84 kilifadhiliwa na Mradi wa Mpango Mkuu wa Kitakwimu Tanzania (TSMP) kwa ajili ya kutimiza majukumu muhimu ya NBS; ambapo pesa zinatoka kwa wabia wa maendeleo. TSMP ni mradi wa miaka saba (7) ambao ulikomea kuisha tarehe 30 Juni 2018; hivyo, hakutakuwa na fungu la ziada. Matokeo yake, Serikali itapaswa iongeze ruzuku kwa ajili ya kutimiza majukumu ya taasisi, vinginevyo taasisi itashindwa kukamilisha majukumu hayo kwa ufanisi. Napendekeza kuwa Serikali iongeze ruzuku ili taasisi iweze kutimiza majukumu yake kwa ufanisi.

5.16 Kutotambuliwa kwa mapato yatokanayo na riba kutoka kwenye akaunti ya amana

Kampuni Hodhi ya Kusimamia Rasilimali za Shirika la Reli (RAHCO) imefanya uwekezaji wa amana ya Sh. bilioni 7.61 na milioni 962 katika Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) na UTT Microfinance. Kwa pamoja uwekezaji huo ulitarajia kuzalisha riba ya Sh. Milioni 707.90 lakini kiasi hicho cha fedha hakikuweza kuthibitishwa kwenye vitabu vya RAHCO. Pia, RAHCO haiwezi kurudishiwa kianzio wala riba kutoka UTT au TIB.

Kwa msingi huo vitabu vya RAHCO vitakuwa na nakisi ya kiasi hicho cha fedha za riba ambacho hakijarekodiwa kwenye vitabu vya akaunti. Hali hii itaathiri ukwasi na shughuli za uendeshaji za RAHCO kutokana na kushindwa kurejesha kiasi kilichowekezwa.

Napendekeza kuwa Menejimenti ya RAHCO ifanye ufuatiliaji ili kuweza kurejesha kiasi kilichowekezwa. Pia Serikali iingilie kati na kuona ni namna gani inaokoa hali iliyopo na kuchukua hatua stahiki.

5.17 Kutokukusanywa kwa mapato yatokanayo na kodi kutoka Kampuni za Mawasiliano

Mnamo mwezi Juni 2010 Kampuni Hodhi ya kusimamia Rasilimali za Shirika la Reli Tanzania (RAHCO) iliingia makubaliano na Kampuni tatu za mawasiliano ya Simu kwa ajili ya kuweka mitambo ya Mawasiliano kando kando ya miundombinu ya reli. Mkataba ulioingiwa ulikuwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni 1.01. Hata hivyo, kiasi cha Dola za Kimarekani 540,800 ya kiwango hiki hakijapokelewa kwa zaidi ya miaka 8 sasa mpaka mwishoni mwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 2018.

Menejimenti bado haina uhakika kama kiwango hicho cha fedha kitalipwa ama la kutokana na mapungufu ya utunzaji kumbukumbu.

Kutokana na hali hiyo, ni dhahiri kuwa makampuni haya matatu ya simu yanafaidi matumizi ya mali za RAHCO bila kutimiza majukumu yao yaliyopo kwenye masharti ya mkataba. Pia, nina wasiwasi kuwa huenda mapato yatokanayo na makampuni haya ya simu yakawa yanalipwa kwenye akaunti ya mtu binafsi, kwani niligundua akaunti tatu ambazo zinamilikiwa na RAHCO lakini hazikuingizwa kwenye vitabu vya uhasibu vya RAHCO.

Napendekeza kuwa Menejimenti ya RAHCO ifanye ufuatiliaji wa karibu ili kuhakikisha kuwa kiasi cha fedha kilichopaswa kulipwa kinapatikana kutoka kwa wakodishaji.

SURA YA SITA

UTAWALA BORA KATIKA MASHIRIKA YA UMMU

6.1 Utangulizi

Nimepitia masuala ya utawala bora kwenye Mashirika ya Umma, na nimetoa ushauri wa kuhimiza Bodi zinazosimamia mashirika kuweza kuendesha mashirika hayo kwa kufuata misingi ya utawala bora ili kuweza kuleta tija na ufanisi.

Ukaguzi wangu ulilenga kuangalia utekelezaji wa shughuli muhimu za taasisi ili kutathmini malengo yaliyowekwa kwenye mpango mkakati. Pia, ulihusisha tathmini ya utendaji wa Bodi za Wakurugenzi na maelekezo yao kwa Menejimenti. Yafuatayo ni mambo muhimu yaliyojitokeza pamoja na mapendekezo yake:

6.2 Mashirika ya Umma Kutokuwa na Bodi za Wakurugenzi na Bodi za Wadhamini

Katika ripoti zangu za ukaguzi za mwaka 2015/16 na 2016/17, niliripoti Mashirika ya Umma 18 na 20, mtawalia, yaliyokuwa yakijiendesha bila ya kuwa na Bodi za Wakurugenzi. Nilishauri mamlaka za uteuzi kuchukua hatua za makusudi kuteua wakurugenzi ili kuboresha mchakato wa utawala na udhibiti ndani ya taasisi. Hata hivyo, nimeendelea kuona kuongezeka kwa mwenendo wa Mashirika ya Umma kutokuwa na Bodi za Wakurugenzi kutoka 20 yaliyoripotiwa mwaka jana mpaka 27. Kati ya Mashirika 27, nane (8) yanafanya kazi bila ya kuwa na Bodi kwa zaidi ya mwaka mmoja, na Mashirika manne (4) kwa zaidi ya miaka miwili. Kukosekana kwa Bodi za Wakurugenzi kunazorotesha uangalizi wa ndani wa Mashirika hayo ambao unatoa uelekeo wa kimkakati wa Mashirika; hivyo kuchelewesha utekelezaji wa baadhi shughuli ya kiutendaji za mashirika hayo ambazo zinahitaji idhini ya bodi. Jedwali Na.4 linaorodhesha Mashirika ya Umma yasiyokuwa na Bodi za Wakurugenzi.

Napendekeza mamlaka ya uteuzi kuchukua hatua stahiki, ikiwamo kuanza mapema mchakato wa kuteua kabla ya kuisha muda wa Bodi zilizopo, ili kuondoa changamoto ya kuchelewa kuteua.

Jedwali Na. 4: Mashirika ya Umma yasiyokuwa na Bodi za Wakurugenzi na Wadhamini

| Na | Taarifa | 2017/18 | 2016/17 | 2015/16 |
|----|--|---------|---------|---------|
| 1 | Baraza la Walaji la Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (SUMATRA CCC) | ✓ | | |
| 2 | Kampuni ya Uendelezaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KADCO) | ✓ | | |
| 3 | Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) | ✓ | | |
| 4 | Shirika la Usimamizi wa Mali na Huduma kwa Wawekezaji (UTT-AMIS) | ✓ | ✓ | ✓ |
| 5 | Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) | ✓ | | |
| 6 | Chuo cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Nyerere | ✓ | | |
| 7 | Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) | ✓ | | |
| 8 | Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) | ✓ | ✓ | |
| 9 | CARMARTEC | ✓ | | |
| 10 | Shirika Tija la Taifa (NIP) | ✓ | ✓ | |
| 11 | Bodi ya Leseni za Ghala Tanzania (WRRP) | ✓ | | |
| 12 | Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (SUMATRA) | ✓ | | |
| 13 | Baraza la Ujenzi la Taifa (NCC) | ✓ | | |
| 14 | Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) | ✓ | | |
| 15 | Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) | ✓ | ✓ | ✓ |
| 16 | Mamlaka ya Usimamizi wa Fukwe za Bahari (MPRU) | ✓ | | |
| 17 | Bodi ya Pareto Tanzania (TPB) | ✓ | | |
| 18 | Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) | ✓ | | |
| 19 | Mamlaka ya Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii | ✓ | | |
| 20 | Makumbusho ya Taifa (NMT) | ✓ | | |
| 21 | Bodi ya Maziwa (Bodi ilikuwapo lakini haikuwa na mwenyekiti) | ✓ | ✓ | ✓ |
| 22 | Wakala wa Uendelezaji wa Wakulima Wadogo wa Chai | ✓ | ✓ | ✓ |

| Na | Taarifa | 2017/18 | 2016/17 | 2015/16 |
|----|--|---------|---------|---------|
| | (TSHTDA) (Bodi ilikuwapo lakini haikuwa na mwenyekiti) | | | |
| 23 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira | ✓ | | |
| 24 | Bodi ya Tumbaku Tanzania (TTB) | ✓ | ✓ | |
| 25 | Taasisi ya Sukari Taifa | ✓ | | |
| 26 | Shirika la Maendeleo na utafiti wa Viwanda (TIRDO) | ✓ | | |
| 27 | Chama cha Hati Miliki Tanzania (COSOTA) | ✓ | ✓ | |
| | Jumla | 27 | 8 | 4 |

6.3 Ukosefu wa Menejimenti ya Kudumu katika Kampuni ya Mkulazi

Kampuni ya Mkulazi ipo chini ya uongozi wa muda tangu kuanzishwa kwake mwezi Septemba 2016. Menejimenti iliyopo ilipatikana kutoka na maafisa waliopo NSSF na PPF ambao ni wabia waliounda Kampuni hiyo; ambapo nafasi zote katika muundo bado hazijajazwa mpaka leo. Hii inasababisha Bodi kukutana mara kwa mara kwa ajili ya kufanya maamuzi ya kila siku kuhusiana na uendeshaji wa Kampuni.

Kifungu namba D.24 (3) cha Mwongozo wa Utumishi wa Umma wa mwaka 2009 kinaeleza kuwa, Mtumishi wa Umma hapaswi kukaimu nafasi ya uongozi kwa zaidi ya kipindi cha miezi sita (6). Afisa aliyeteuliwa kukaimu nafasi anashindwa kufanya maamuzi kwa kukosa nguvu ya kimamlaka. Pia, vikao vya mara kwa mara kati ya menejimenti na Bodi ya Wakurugenzi vilidhoofisha mgawanyo wa majukumu kati yao kwani kazi ya Bodi ni kutoa maelekezo na kusimamia shughuli zifanywazo na Menejimenti.

Napendekeza kuwa Mamlaka inayohusika na uteuzi kuhakikisha inateua timu ya Menejimenti ya kudumu mapema iwezekanavyo.

6.4 Vikao vya wadhamini havifanyiki kama inavyotakiwa kwenye Mkataba

Kifungu namba 7.2 cha makubaliano kati ya Kampuni ya TTCL Pesa Ltd na Taasisi ya Wadhamini wa TTCL Pesa yaliyofanyika mnamo tarehe 1 Mwezi Julai mwaka 2017 kinataka wadhamini kukaa vikao kila robo ya mwaka. Kinyume na makubaliano hayo bodi ya wadhamini haijawahi kufanya kikao chochote kwa kipindi cha kuanzia tarehe 1 Julai 2017 mpaka tarehe 30 Juni 2018. Kushindwa kufanya vikao kama ilivyoelekezwa kwenye makubaliano kunaweza kusababisha kupunguza umakini kwenye usimamizi wa biashara kama ilivyobainika. Pia, kuna akaunti ya Benki imefunguliwa bila idhini ya Bodi ya Wadhamini.

Napendekeza kuwa Menejimenti ya TTCL Pesa ihakikishe vikao vya Bodi ya Wadhamini vinafanyika kwenye kila robo mwaka kama ilivyoelekezwa kwenye Mkataba.

6.5 Ongezeko la gharama za vikao vya Bodi

Bodi ya Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro ilifanya jumla ya vikao 20 na semina 6 kwa mwaka wa fedha 2017/18, ambapo jumla ya Sh. bilioni 1.10 zilitumika kama ilivyoainishwa kwenye jedwali namba 5 hapa chini:

Jedwali Na. 5: Mchanganuo wa gharama za vikao

| Namba | Maelezo | Gharama (Sh.) |
|--------------|-----------------------------|----------------------|
| 1 | Posho ya kujikimu | 799,906,220 |
| 2 | Hela kwa ajili ya mafuta | 81,225,678 |
| 3 | Gharama za ukumbi | 29,320,800 |
| 4 | Chakula na viburudisho | 34,449,834 |
| 5 | Malazi | 57,459,684 |
| 6 | Gharama nyingine za usafiri | 100,545,386 |
| Jumla | | 1,102,907,602 |

Mahudhurio ya timu ya Menejimenti kwenye vikao vya Bodi ya Wakurugenzi yanapunguza nguvu na ufanisi wa Bodi katika kutimiza majukumu yao ya kuisimamia Menejimenti.

Natoa mapendekezo kwa Menejimenti ya Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro kupunguza gharama za kuendesha vikao kwa kufanya vikao visivyozidi vinne (4), kwa mwaka na wale maafisa wa ngazi za juu tu ndio wahudhurie katika vikao hivyo.

6.6 Udhaifu katika usimamizi na ufuatiliaji wa Bajeti

Kifungu namba C.7.2.3 cha Miongozo ya kiuhasibu ya Chuo Kikuu cha Dodoma kinawataka maafisa masuuli kutekeleza majukumu yao kulingana na Bajeti waliyojiwekea. Ili kuweza kutimiza malengo yote yaliyomo kwenye bajeti waliyojiwekea.

Wakati wa mapitio ya Bajeti na usimamizi wake niligundua yafuatayo:

- a) Kutotumika kwa moduli katika mfumo wa vifungu vya bajeti ambao unaunganisha na matumizi halisi,
- b) Bajeti iliyotengwa kwa kila vifungu husika katika mfumo wa uhasibu hautoi maelekezo ya kila shughuli ambayo imeoanishwa na kasma husika ya malipo.

Kutokuwepo kwa vifungu vya bajeti katika kila kasma kunasababisha ugumu katika kuweka viwango vya matumizi. Kutokuwepo kwa utengwaji wa mafungu katika kasma husika kunasababisha utekelezwaji wa majukumu nje ya bajeti.

Napendekeza kuwa Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Dodoma ihuishe mfumo wake kwa ajili ya kusaidia usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli kama zilivyoainishwa kwenye bajeti.

SURA YA SABA

MAPITIO YA MIKAKATI NA UENDESHAJI WA KIUFANISI

7.1 Utangulizi

Uendeshaji wa kimkakati unajumuisha kupanga, kufuatilia, kuchanganua na kutathmini kuhusu kuendelea kwa shughuli ambazo ni muhimu kwa taasisi/shirika katika kutimiza malengo yake. Uendeshaji wa kimkakati unahusisha kuchanganua nguvu na udhaifu wa ndani na nje ya taasisi, kutengeneza mipango mkakati, kufanyia kazi mipango mkakati, kufanyia tathmini mafanikio na kufanya marekebisho ili kufikia malengo.

Uendeshaji wa kiufanisi ni uwiano kati ya rasilimali zilizowekwa kuendesha biashara na matokeo yaliyopatikana kutokana na rasilimali hizo. Uendeshaji wa kiufanisi unajumuisha mikakati mbalimbali inayotumika kukamilisha malengo ya msingi ya kutoa bidhaa na huduma kwa jamii kwa gharama nafuu zaidi na kwa muda uliokusudiwa.

Tathmini yangu ya mapitio ya mikakati na uendeshaji wa kiufanisi ilijumuisha taasisi zifuatazo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Kampuni ya TTCL Pesa, Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Shirika la TTCL, Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA), Taasisi ya Uhasibu Arusha (IAA) na Kampuni Hodhi ya Mkulazi.

7.2 Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA)

Katika tathmini yangu ya uendeshaji wa TIRA, nilibaini mapungufu yafuatayo:

7.2.1 Kukosekana kwa Utaratibu wa Kuhakikisha Bidhaa zote Zinazolingia Nchini Zinakatiwa Bima na Kampuni za Kitanzania

Kifungu cha 40 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Na. 7 ya mwaka 2017 kama ilivyobatiliwa na Kifungu cha 133 cha Sheria ya Bima ya mwaka 2009 kinataka huduma ya bima ya bidhaa zinazolingia Tanzania kwa njia ya barabara, maji na anga

kufanywa na kampuni za bima za Kitanzania. Hii inamaanisha kuwa, bidhaa zote zinazolingia nchini zinatakiwa kukatiwa bima hapa nchini na makampuni ya hapahapa. Sheria hii imeanza kufanya kazi tarehe 1 Januari 2018; TIRA ina wajibu wa kuhakikisha utekelezaji wa sheria hii.

Katika kuhakikisha utekelezaji wa matakwa haya, TIRA kama msimamizi wa Tasnia ya Bima iliratibu uendelezaji na utumiaji wa Mfumo wa Bima za Uingizaji wa Bidhaa (TIIP) kama mfumo ambao unatoa fursa kwa waingizaji wote wa bidhaa kote duniani kupata taarifa kuhusu kampuni za bima za Tanzania kwa ajili ya bidhaa zao zinazolingia nchini.

Hata hivyo, pamoja kwamba mfumo wa TIIP unatoa jukwaa kwa ajili ya urahisi wa utekelezaji wa sheria, bado hauhakikishi utekelezaji wa matakwa yote ya sheria. Hakuna taratibu na udhibiti uliowekwa kuhakikisha kuwa bidhaa zote zinazolingizwa zinakatiwa bima hapahapa nchini. Bado kuna upenyo kwa waingizaji kukwepa kukatia bima bidhaa zao hapa nchini. Hivyo, faida zitokanazo na mjumuisho wa kifedha na kukua kwa tasnia ya bima kushindwa kupatikana.

Ninapendekeza TIRA ishirikiane na wadau wengine kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC), Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) wenye majukumu mbalimbali katika uingizaji wa bidhaa nchini ili kuwe na utaratibu na nguvu ya pamoja katika kuboresha, kudhibiti na kuhakikisha bidhaa zote zinazolingia nchini zinakatiwa bima na kampuni za bima za Tanzania.

7.2.2 Kutojitosheleza katika Ugawanyaji na Matumizi ya Rasilimali katika Kutekeleza Majukumu ya Msingi ya TIRA

Nilibaini kuwapo kwa kiasi kidogo cha shughuli za upambanaji na magendo, programu za uhamasishaji, tafiti na kukosekana msukumo kwenye bima zisizo za lazima. Pia, ukaguzi umefanyika katika shughuli za makampuni machache ya bima na kwa utaratibu wa sampuli kwa kuangalia viashiria vya

hatari dhaniwa vya makampuni hayo. Hoja hii imekuwa ikijirudia, na hakuna juhudi zinazofanyika kuhakikisha hali hii inasahihishwa.

TIRA inaeleza kuwa haina rasilimali watu na fedha za kutosha kuweza kufanya kazi hizo. Hata hivyo, nilibaini kuwa bajeti ya TIRA imekuwa ikiongezeka kila mwaka, lakini fedha zinazopelekwa kwenye shughuli za msingi zimebakia kuwa zilezile au pungufu kiasi. Hii imesababisha shughuli za msingi zilizokuwa zifanywe na ofisi za kanda kufanyika kwa uchache na yakiguswa maeneo machache. Hii inaonesha kuwa kuna upungufu katika mipango na ugawanyaji wa rasilimali ili kutanua na kuongeza shughuli za msingi za TIRA.

Napendekeza kuwa TIRA ifanye mapitio ya mkakati wake wa ugawanyaji na matumizi ya rasilimali ili kuhakikisha watu na fedha za kutosha zinaelekezwa katika kutekeleza majukumu ya msingi, hivyo kuwa na usimamizi wenye tija kwa tasnia.

7.2.3 Kukosekana kwa Utaratibu Unaoelewika katika Kushughulikia Malalamiko ya Bima

Ufanisi katika utaratibu wa kushughulikia malalamiko unatoa nafasi kwa taasisi kupokea mrejesho na kuchukua hatua kwenye huduma inazotoa kwa wateja, wafanyakazi na wadau wengine. Ni muhimu pawe na muongozo au taratibu ili kuongoza upokeaji, ushughulikiaji na utatuzi wa malalamiko. Pamoja na jitihada zinazofanyika katika kushughulikia malalamiko ya jamii kuhusu kutoridhika na bima, madalali au wakala wa bima, TIRA haina mwongozo wa kushughulikia malalamiko hayo. Hivyo, kusababisha kuwapo kwa mpishano wa malalamiko yanavyopokelewa, yanavyoandikishwa, yanavyoshughulikiwa, yanavyotolewa mrejesho, yanavyofungwa na namna rekodi zinavyowekwa na zinavyohifadhiwa.

Zaidi ya hapo, menejimenti ya TIRA haifanyi tathmini katika utaratibu wa kushughulikia malalamiko. Pia, TIRA haijatanabaisha ni malalamiko yepi yanaweza kushughulikiwa

katika ngazi ya ofisi za kanda, Makao Makuu na yepi yatatakiwa kupelekwa kwa msuluhishi wa masuala ya bima. Hakuna uchambuzi unaofanyika kwenye malalamiko ili kuiwezesha TIRA kuchukua hatua maalum. Hivyo kurudisha nyuma juhudi za kuboresha huduma ya bima kwa jamii, hasa wateja wa bima.

Ili kuleta ufanisi katika kutoa huduma ya bima kwa jamii na kukuza huduma ya bima, TIRA inashauriwa kutengeneza mwongozo wa kushughulikia malalamiko ya bima ambao utahakikisha kunakuwa na utaratibu katika kukusanya, kuandikisha na kushughulikia malalamiko.

7.2.4 Tathmini Hafifu katika Shughuli za Kupambana za Magendo katika Kanda na Ofisi ya Zanzibar

Kifungu cha 7.1 cha Mpango Mkakati wa TIRA kinataka Wakuu wa Kurugenzi, Vitengo na Ofisi za Kanda za TIRA kuandaa na kutuma ripoti za robo mwaka kuelezea namna waliyotekeleza Mpango Mkakati kwa Naibu Kamishna wa Bima ndani ya mwezi mmoja baada ya kumalizika kwa robo husika.

Nilipopitia ripoti za utekelezaji kutoka kwenye Ofisi za Kanda zinazoonisha utekelezaji wa shughuli za msingi ambazo zinajumuisha kupambana na makosa ya uhalifu wa bima, uhamasishaji wa masoko na kutoa leseni, pamoja na mambo mengine, nilibaini kutokufuatwa matakwa ya bima kati ya asilimia 10 na 40 ikiwa ni pamoja na kuwapo kwa stika bandia, bima zisizoandikishwa na Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Bima wa TIRA na kuwapo kwa magari yasiyo na bima. Kwa mfano, katika robo iliyoishia tarehe 30 Juni 2018, katika Mji wa Musoma magari 47 (asilimia 38) kati ya magari 123 yaliyokaguliwa hayakuwa na bima halali. Katika Wilaya ya Kibondo magari 35 (asilimia 24) kati ya 148 yaliyokaguliwa hayakuwa na bima halali; na katika Wilaya ya Kasulu magari 135 (asilimia 47) kati ya 288 yaliyokaguliwa hayakuwa na bima halali. Hakuna shughuli zilizoripotiwa katika kupambana na makosa ya bima katika mikoa ya Morogoro,

Lindi, Mtwara, Katavi, Rukwa, Tabora na Singida. Hivyo, ukubwa wa tatizo umeshindikana kubainika.

Nina mashaka kuwa, kama hakuna shughuli za kupambana na makosa ya bima wakati kumekuwa na asilimia zaidi ya 15 ya ukiukwaji, juhudi za TIRA za kutekeleza mpango mkakati zinaweza zisifanikiwe.

Zaidi ya hayo, kuwapo kwa kiasi kidogo cha shughuli za kupambana na makosa ya bima kunatoa nafasi kwa wahalifu kuendelea kuwapo na kuendeleza matendo ya kiuhalifu, hasa katika mikoa na wilaya ambazo shughuli za kupambana na uhalifu wa bima hazijafanywa.

Ninapendekeza TIRA kufanya tathmini ya ukubwa wa tatizo unaotokana na kutokuwa na shughuli za kutosha za kupambana na makosa ya kibima, kuboresha mipango ya kuongeza uzingatiaji pamoja na kuhakikisha kunakuwa na uwanda mpana wa kupambana na makosa ya bima kwa kuongeza rasilimali zaidi katika eneo hilo.

7.3 Kampuni ya TTCL Pesa

Kampuni ya TTCL Pesa ilianzishwa kama kampuni tanzu ya Shirika la TTCL tarehe 6 Julai 2017 ili kutimiza matakwa ya Kanuni ya 12 ya Kanuni za Mifumo ya Malipo (Fedha za Kielektroniki) za mwaka 2015 ambazo zinataka watoa huduma wenye mfumo wa malipo ambao sio Benki au Taasisi za Fedha kuanzisha kampuni yenye mamlaka ya peke yake ya kisheria kwa ajili ya kutoa huduma za fedha za kielektroniki.

Majukumu ya kampuni ya TTCL Pesa ni kufanya Biashara ya Kuhamisha Fedha Kielektroniki kwa mtandao wa simu kwa niaba ya kampuni ya TTCL. Mgawanyo wa umiliki ni kati ya Shirika la TTCL asilimia 99 na Msajili wa Hazina asilimia 1.

7.3.1 Mapungufu katika Kupitisha na Kutekeleza Makubaliano ya Huduma

Tarehe 20 Aprili 2017, katika kikao chake maalum cha 59, Bodi ya Wakurugenzi ya TTCL iliielekeza kampuni ya TTCL

Pesa kuingia katika Mkataba wa Huduma na Shirika la TTCL kukodisha baadhi ya shughuli zake. Mkataba unaainisha wigo wa msaada na mambo mengine yanayohitaji kutekelezwa. Hata hivyo, mkataba haukufanyika mpaka tarehe 25 Oktoba 2018, miezi 19 baadaye. Kwa maana hiyo, kampuni ya TTCL Pesa iliendelea kupata huduma saidizi kutoka kwa Shirika la TTCL bila ya kuwa na mkataba.

Zaidi ya hayo, kwa mujibu wa sehemu ya 3.1.1 ya Mkataba wa Huduma uliosainiwa ambao utafanya kazi kwa miaka mitatu (3) kutoka tarehe ya kuanza kwa makubaliano hayo, 25 Oktoba 2018, pande zote zilikubaliana kuwa mtoa huduma (Shirika la TTCL) kutoa huduma kwa mteja (kampuni ya TTCL Pesa) kwa mujibu wa muongozo na sera ya mteja. Hata hivyo, nilibaini kuwa hakukuwa na muongozo wala sera yoyote ya mteja kwenye huduma iliyotolewa na Shirika la TTCL kwa Kampuni ya TTCL Pesa.

Pia, kwa mujibu wa Kiambatisho cha IV (ii) cha Mkataba wa Huduma, mfumo wa huduma ya fedha kwa njia ya simu utamilikiwa na Shirika la TTCL, na TTCL Pesa itatumia mfumo huo kuzalisha mapato. TTCL Pesa itatakiwa kulipa ada ya muamala kwa Shirika la TTCL kwa kukodishiwa mfumo wa huduma ya fedha kwa njia ya simu unaomilikiwa na Shirika la TTCL. Ada ya muamala itakayotozwa itakuwa sawa na idadi ya miamala ya kibiashara ambapo chini ya miamala 10,000 kiwango cha Sh. 30 kwa muamala kitatumika; na juu ya miamala 10,000 kiwango cha Sh. 20 kwa muamala kitatumika.

Hata hivyo, nilibaini kuwa Mkataba wa huduma haujaweka bayana muda maalum wa kutoza viwango vya ada. Kwa maana hiyo, ada haiwezi kutozwa kwa usahihi kwa kuwa kiasi cha ada kitatofautiana kutegemeana na muda wa kutoza.

Napendekeza kuwa kampuni ya TTCL Pesa itekeleze maelekezo ya Bodi ya Wakurugenzi ndani ya muda

uliokusudiwa. Pia, mapungufu yaliyoonekana kwenye mkataba wa huduma yanatakiwa kusahihishwa.

7.3.2 Tathmini ya Mpango Mkakati wa Kampuni

Mpango wa kimkakati unahitajika kusimamia na kuzielekeza rasilimali zote kuendana na mkakati wa kibiashara na vipaumbele. Kazi za Kampuni ya TTCL Pesa na wadau wa biashara ni kuhakikisha thamani yenye tija inapatikana kutoka kwenye mradi na mjumuiiko wa huduma. Mpango mkakati huboresha ufahamu wa wadau muhimu juu ya fursa na mapungufu ya kampuni, kupata kujua mwenendo wa sasa wa utendaji, kutambua uwezo na mahitaji ya rasilimali watu pamoja na kubainisha kiasi cha uwekezaji unaohitajika.

Kampuni ya TTCL Pesa ina Mpango Mkakati mpana ambao umewasilishwa Benki Kuu ya Tanzania kama sehemu ya matakwa ya kuomba leseni ya kutoa huduma ya fedha za kielektroniki. Hata hivyo, Mpango Mkakati wa Biashara kwa ujumla unaangazia zaidi masuala ya Shirika la TTCL na kuwa na vitu vichache vinavyohusiana na kampuni ya TTCL Pesa. Kwa maana hiyo, mpango huo hauna maana kwa kampuni ya TTCL Pesa kama kampuni inayojitegemea na inayokusudiwa na mkakati huo.

Ninapendekeza kampuni ya TTCL Pesa ianzishe na kutengeneza mipango ya kutathmini Mpango Mkakati wa Biashara uliopo ambao utaangazia zaidi masuala ya kampuni ya TTCL Pesa kama kampuni iliyokusudiwa na kuhakikisha unaidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya kampuni ya TTCL Pesa.

7.3.3 Kampuni kutokuwa na Sera ya Bei

Kanuni ya 13(t) ya Kanuni za Mifumo ya Malipo (Fedha za Kielektroniki) za mwaka 2015 inataka waombaji wa leseni kuwa na sera za bei ambazo zitajumuisha vigezo vitakavyotumika kupata bei, asili na kiasi cha tozo au ada wanazotozwa wateja.

Tathmini yangu ya kampuni ya TTCL Pesa ilibaini kuwa, kampuni haina sera hizo za bei zenye vigezo. Menejimenti imeeleza kuwa, viwango vya tozo vinategemea viwango vya soko.

Kutokana na kukosekana kwa sera ya bei, vigezo vilivyotumika kupata bei havifahamiki; na msingi wa kutathmini viwango vya tozo vya baadaye unakuwa mgumu.

Napendekeza kuwa kampuni ya TTCL Pesa itengeneze, kutumia na kudumisha sera rasmi ya bei ambayo itajumuisha vigezo vilivyotumika kufikia bei, asili na kiasi cha tozo au ada inayotakiwa kutozwa kwa mteja.

7.3.4 Kukosekana kwa Mkataba wa Ukodishaji wa Mfumo wa Kutuma Fedha kwa Simu za Mkononi

Shirika la TTCL linamiliki mfumo wa malipo kwa njia ya simu ambao unatumia na kampuni ya TTCL Pesa kutoa fedha za kielektroniki. Kiambatisho cha IV (ii) cha Mkataba wa Huduma wa tarehe 25 Oktoba 2018 kati ya Shirika la TTCL na Kampuni ya TTCL Pesa, inatanabaisha kuwa mfumo wa huduma ya fedha kwa njia ya simu utamilikiwa na Shirika la TTCL; na kampuni ya TTCL Pesa itatumia mfumo huo kuzalisha mapato yake, na italipa ada ya muamala kwa Shirika la TTCL kwa kukodisha mfumo.

Utaratibu huo wa ukodishaji utaelezea haki na wajibu wa kila upande pamoja na vigezo na masharti yatakayosimamia mfumo huo.

Kwa kuwa kampuni hizi mbili ni biashara mbili tofauti zinazojitegemea, kukosekana kwa mkataba wa ukodishaji kunaweza kusababisha malumbano kati yao, hasa kunapohusisha mazingira maalum kama malipo kwa ajili ya matumizi ya mfumo, muda wa ukodishaji wa mfumo, kuhuisha kwa kipindi cha kukodisha na huduma za usaidizi zinazohusiana na mfumo wa huduma ya fedha kwa njia ya simu au maeneo mengine yenye shida. Kwa hiyo, ninapendekeza kuwa Shirika la TTCL na kampuni ya TTCL

Pesa waingie katika mkataba wa ukodishaji wa jinsi gani mfumo wa huduma ya fedha kwa njia ya simu utumike.

7.3.5 Kutoandaliwa kwa Bajeti ya Utendaji wa Kampuni ya TTCL Pesa

Kwa tathmini yangu, nilibaini kuwa kampuni ya TTCL Pesa haijaandaa bajeti ambayo ingetumika kama msingi wa kugawanya rasilimali na nyenzo ya uhibitaji wa fedha. Kukosekana kwa bajeti, kutakosesha msingi madhubuti wa kugawanya na kudhibitaji rasilimali fedha za kampuni. Hivyo, ninapendekeza kampuni ya TTCL Pesa ichanganue shughuli zake za kiutendaji katika mfumo wa kifedha.

7.3.6 Hasara Iliyopatikana katika Mwaka wa Kwanza wa Utendaji

Kwa mujibu wa Mpango wa Biashara, kampuni ya TTCL Pesa ilitarajia kupata hasara ya Sh. milioni 28 katika mwaka wa kwanza wa utendaji, kwa makadirio ya mapato ya Sh. milioni 937.

Hata hivyo, nilipofanya tathmini ya mwenendo halisi wa kampuni dhidi ya matarajio, nilibaini kuwa kampuni imepata hasara ghafi ya Sh. milioni 368.8, mapato yakiwa Sh. milioni 85.2 tu.

Pamoja na hayo kampuni ya TTCL Pesa imeweza kumudu gharama zake za uendeshaji kwa kupata msaada kutoka kwa kampuni mama ili kuweza kulinda hitaji la chini la mtaji la Sh. milioni 500 kama inavyotakiwa na Kanuni ya 14(1) ya Kanuni za Mifumo ya Malipo (Fedha za Kielektroniki) za mwaka 2015. Sh. milioni 425.4 zilizogharamiwa na kampuni mama kwa niaba ya Kampuni Tanzu zilibadilishwa kuwa mtaji katika utaratibu wa kugawiwa hisa.

Bila ya kufanya hivyo, hitaji la chini la mtaji lingepungua, hivyo kuleta shaka juu ya uendeleo wa kampuni tanzu.

Mwenendo wa utendaji kwa mwaka wa kwanza kwa kulinganisha na matarajio unatoa tahadhari kuwa kama hatua

hazitachukuliwa, kuna uwezekano mkubwa kuwa kampuni haitaweza kuwa endelevu hapo baadaye.

7.3 Hospitali ya Taifa Muhimbili

7.3.1 Kushindwa kwa Idara ya Rediolojia Kuitumia Vizuri Programu ya Jeeva

Programu ya Jeeva ilinunuliwa na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) mwaka 2005 ili kuongeza ufanisi katika mchakato wa shughuli za kutunza taarifa za kitabibu. Kutokana na gharama kubwa za shajara (stationery), baadhi ya idara zilitakiwa kufanya kazi bila kutumia karatasi kwa kutumia kwa ukamilifu moduli zilizopo katika programu kutoa huduma.

Jeeva ina machaguo ya kuweka maelezo ya kitabibu. Hata hivyo, nilibaini kuwa madaktari hawajazi maelezo kwenye programu; hivyo hali inayosababisha Idara ya Rediolojia kuendelea kutumia karatasi kuandika maelezo ya kitabibu pamoja na kufundishwa jinsi ya kutumia mfumo huo.

Napendekeza kuwa MNH ihakikishe programu husika inatumika kwa ukamilifu na watumiaji wote waliokusudiwa katika idara za watumiaji.

7.3.2 Udhibiti Dhaifu katika Chakula wanachopewa Wanafunzi na Wagonjwa Waliolazwa

Kifungu cha 21.1 (ii) cha Kanuni za Fedha za Hospitali kinasema kuwa kuanzisha na kurekodi taarifa za fedha, kusuluhisha na kutathmini shughuli zinatakiwa kufanywa na watu tofauti ili kuwa na mfumo unaowezesha kazi ya mtu mmoja kutazamwa na mwingine.

Hata hivyo, nilibaini kutokuwapo kwa mgawanyo wa kazi katika kusimamia mkataba wa kutoa chakula kwa wanafunzi na wagonjwa waliolazwa; ambapo mtu mmoja ana jukumu la kuangalia kiasi cha chakula kilichogawiwa na wakati huo huo anaidhinisha bili zilizotolewa.

Udhibiti wa gharama za ugavi wa chakula unaweza kuwa mgumu kwa kukosa mgawanyo wa majukumu katika kuhakiki vyakula na kuidhinisha bili. Hivyo, ninapendekeza MNH iboreshe udhibiti kwa kufanya uangalizi wa ndani kwa ufanisi zaidi.

7.3.3 Kuongezeka sana kwa Makisio ya Madeni Yasiyotarajiwa
Kifungu cha 6.2.1(ii) na (iii) cha Kanuni za Fedha za Hospitali kinasema kuwa mbinu zenye ufanisi na za haraka zitatumika kukusanya madai ambayo yamefika muda wa kulipwa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa kwenye Sera ya Madai ya Hospitali.

Pamoja na juhudi na hatua madhubuti zilizochukuliwa na Hospitali kukusanya madai kutoka kwa wateja mbalimbali, nilibaini kuongezeka kwa madeni yasiyotarajiwa kulipwa (Bad debts) mpaka kufikia Sh. bilioni 1.44 katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2018 kutoka Sh. milioni 941.32 zilizokuwapo mwaka uliopita. Madeni hayo yameongezeka sana kutokana na Hospitali kujishughulisha na taasisi za Serikali ambazo hazijawakatia bima watumishi wao katika makampuni ya bima.

Ninapendekeza Hospitali ya Taifa Muhimbili ichukue hatua ambazo zitahamasisha taasisi za Serikali kujiunga na bima mbalimbali za afya zilizopo.

7.4 Mapitio ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS)
Katika ukaguzi wangu wa mapitio ya mikakati na uendeshaji wa kiufanisi wa TBS nilibaini mapungufu yafuatayo:

7.4.1 Utoaji wa Leseni kwa Ajili ya Kutumia Nembo ya Ubora kwa Bidhaa Zisizofaa
Kifungu cha 4(e) cha Sheria ya Viwango ya mwaka 2009 kinataka Shirika kutoa, kuhuisha, kusitisha, kubadili au kuifuta leseni iliyotolewa kwa ajili ya kutumia nembo yoyote ya viwango. Kuhusu utoaji wa leseni kwa ajili ya kutumia nembo ya ubora ya Shirika, aya ya 4.2.6 ya Mwongozo wa Taratibu za Ithibati ya Bidhaa ya mwaka 2017 inataka

maamuzi ya kutoa au kutotoa leseni ya TBS au Cheti cha Ukaguzi wa Bidhaa kwa mteja yazingatie kuwapo kwa ripoti safi ya maabara, ripoti ya mwanzo ya tathmini ya hali ya kiwanda pamoja matakwa ya kiutawala.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi nilibaini leseni 2 ambazo nimezipitia wakati wa ukaguzi, zilitolewa na TBS kwa wateja ambao bidhaa zao zilishindwa majaribio kama ilivyoonekana kwenye ripoti ya majaribio ya bidhaa kwa sampuli zilizojaribiwa.

Jedwali Na. 6: Leseni Zilizotolewa kwa Bidhaa Zilizoshindwa Majaribio

| Na. | Mteja | Bidhaa | Nambari ya leseni | Kumbukumbu |
|-----|----------------|--------------------------|-------------------|--|
| 1. | Goodwill | Vigae vya sakafu | L. 1868 | Rejea QCA 6943 |
| 2. | Anxifa Limited | Mabati yaliyopigwa chapa | L. 1858 | Rejea <ul style="list-style-type: none"> • QCA 6379 • QCA 6380 • QCA 6381 |

Nilibaini pia kuwa baadhi ya leseni zilitolewa kwa wateja ambao viwanda vyao vilishindwa katika tathmini ya mwanzo. Hakukuwa na ushahidi unaonesha kuwa bidhaa zilizoshindwa zilijaribiwa tena kama ilivyotakiwa na aya ya 4.2.5.7 ya Mwongozo wa Taratibu za Ithibati ya Bidhaa ya mwaka 2017. Udhaifu huu unaonesha kutokuwapo kwa udhibiti katika kusimamia mchakato wa utoaji leseni.

Ninapendekeza kuwa TBS ichunguze na kuchukua hatua kwa leseni ambazo zilitolewa kwa wateja ambao majaribio ya bidhaa zao na tathmini za awali za viwanda vyao zilishindwa na kuhakikisha taratibu za utoaji wa leseni zinafuatwa bila upendeleo.

7.4.2 Kukubali na Kushughulikia Maombi ya Bidhaa Zisizoruhusiwa na Ambazo zipo Chini ya Kiwango

Kifungu cha 4(g) cha Sheria ya Viwango ya mwaka 2009 kinaitaka TBS kuandaa, kutengeneza, kuboresha na kubadili Viwango vya Ubora vya Nchi. Kwa Kuzingatia hilo, Shirika lilitengeneza viwango vya ubora ikiwa ni pamoja na kiwango cha ubora namba SH.1476:2012 kwa ajili ya mabati ya aluminium yasiyo na migongo, na yaliyo na migongo. Kifungu cha 4.7 cha ubora wa viwango kinasema kuwa kiwango cha chini cha unene wa bati ambalo lina mgongo linatakiwa kuwa geji 28.

Hata hivyo TBS imepokea maombi kwa ajili ya kuzalisha mabati yaliyopigwa chapa (IT4 & IT5) ya geji 30 na kuyafanyia majaribio. Haijafahamika kwa nini TBS walipokea na kuyafanyia kazi maombi yaliyohusisha bidhaa ambazo haziruhusiwi kuzalishwa kwa kuwa hazijakidhi viwango vya ubora na kuzifanyia majaribio. Zifuatazo ni sampuli za bidhaa zilizogundulika kuwa haziruhusiwi kuzalishwa:

Jedwali Na. 7: Maombi Yaliyofanyiwa Kazi kwa Bidhaa Ambazo Haziruhusiwi Kuzalishwa

| Na. | Mteja |
|-----|-------------------------------------|
| 1 | Anxifa Limited |
| 2 | Quansheng International Trading Ltd |
| 3 | MM Intergrated Steel Mills Ltd |

Kushughulikia maombi na kufanyia majaribio bidhaa ambazo haziruhusiwi kuzalishwa ni kielelezo cha matumizi mabaya ya alama za TBS kwenye bidhaa ambazo zipo chini ya viwango.

Ninapendekeza kuwa TBS ichunguze maombi yaliyofanyiwa kazi na bidhaa husika kujaribiwa kisha ichukue hatua zinazostahili. Pia, ihakikishe inafanya mchakato wa leseni kwa bidhaa ambazo zimefikia matakwa ya viwango vya ubora.

7.4.3 Kukosekana kwa Hatua Sahihi Dhidi ya Bidhaa ambazo Zimeshindwa Vipimo Muhimu

Kifungu cha 4(d) cha Sheria ya Viwango ya mwaka 2009 kinalitaka Shirika la TBS kutoa idhini, kuandikisha na kudhibiti matumizi ya nembo za ubora kwa mujibu wa sheria.

Kwa mujibu wa aya ya 4.2.7.1 ya Mwongozo wa Taratibu za Ithibati ya Bidhaa wa mwaka 2017, Shirika la TBS linatakiwa kufanya ukaguzi wa kushtukiza wa mara kwa mara si chini ya mara mbili (2) kwa mwaka kwa wateja wenye leseni halali au wenye cheti cha majaribio ya bidhaa.

Katika ukaguzi wa kushtukiza wa mara kwa mara, sampuli zinaposhindwa kufikia matakwa ya viwango vya ubora, mzalishaji hufahamishwa na kutakiwa kuchukua hatua za kusahihisha tatizo na kutoa taarifa kwa Shirika la TBS mara moja. Kama sampuli zitashindwa katika vipimo muhimu, Shirika la TBS litamtaarifu mteja kuacha kusambaza sokoni bidhaa husika; na kumwelekeza mzalishaji kufanya marekebisho na kulitaarifu Shirika la TBS ili liweze kufanya ukaguzi ndani ya siku 30.

Kwa bidhaa ambazo zimethibitishwa na kukutwa na mapungufu huku zikiwa zimeshasambazwa sokoni, mzalishaji ataelekezwa kuomba bidhaa hizo zirudishwe kwa madhumuni ya kuziharibu kwa namna inavyowezekana. Pia, mteja/mzalishaji atatakiwa kuijulisha jamii juu ya hatua zilizochukuliwa kuhusiana na bidhaa husika na Shirika kuthibitisha hilo.

Nilibaini bidhaa zilizoshindwa majaribio ya vipimo muhimu wakati wa ukaguzi wa kushtukiza na hakuna hatua zilizochukuliwa na Shirika la TBS. Pia, kuna bidhaa zilizoshindwa majaribio ya vipimo muhimu ambazo zilikuwa zimeshasambazwa katika masoko, na shirika la TBS halikuchukua hatua zozote.

Zaidi ya hapo, nilibaini matukio kadhaa ambapo rekodi za TBS zilionesha kuwa walisimamisha wazalishaji (Smoke House and Ando Products Ltd Mwanza) lakini bidhaa zao bado zilionekana sokoni.

Shirika la TBS lilijieleza kuwa sio kazi rahisi kudhibiti kila kitu kilichopo sokoni kutokana na kuwa na idadi ndogo ya rasilimali kama vile watu, vifaa na vituo vya kufanyia kazi.

Ukaguzi wa kushtukiza wa mara kwa mara uliofanywa na Shirika haukutosha kuondoa bidhaa zisizo na ubora. Aidha viashiria vya hatari kwa walaji kutumia bidhaa zilizo chini ya kiwango havikuweza kudhibitiwa.

Ninapendekeza Shirika la TBS kuanza kufuata matakwa ya Mwongozo wa Taratibu za Ithibati ya Bidhaa mara moja pale linapogundua bidhaa ambazo zimeshindwa majaribio ya vipimo muhimu.

7.4.4 Kutochukuliwa Hatua Dhidi ya Bidhaa Zilizo Chini ya Kiwango Ambazo Zinaruhusiwa Kutoka kwa Masharti

Kanuni ya 10 ya Kanuni za Viwango vya Ubona (Uthibitisho wa Lazima wa Makundi ya Bidhaa Zilizoingia) za mwaka 2009 zinaruhusu bidhaa zilizoingia kutoka nje ya nchi katika hali fulani kutolewa kwa masharti wakati Kanuni ya 10(2) ya kanuni hizo inakataza bidhaa hizo kusambazwa, kuuzwa, kutumika au kuhamishwa zote au sehemu yake kwa mtu au sehemu yoyote ambaye hajatajwa kwenye anuani iliyopo kwenye Cheti cha Kuruhusu Mzigo Utoke kwa Masharti. Ikitokea mzigo haukufaulu katika vipimo, mzigo huo unatakiwa aidha urudishwe ulipotoka au uharibiwe kwa mujibu wa kifungu cha 5.1.10 cha Mwongozo wa Ukaguzi wa Bidhaa Zinazolingia Nchini wa mwaka 2017.

Hata hivyo, nilibaini bidhaa kadhaa zilizoingia chini ya utaratibu wa kutoka kwa masharti ambazo zilishindwa ukaguzi wa vipimo muhimu lakini hakuna ushahidi kuwa hatua

zilichukuliwa zaidi ya barua za onyo kwa waingizaji wa bidhaa. Kuchelewesha matokeo ya uchunguzi na kushindwa kuwasiliana na mteja kwa wakati kuhusu bidhaa zilizo chini ya utaratibu wa kutoka kwa masharti kunahamasisha ukiukwaji wa matakwa ya kanuni ya 10(2) iliyotajwa hapo juu.

Katika jambo hili, kuna viashiria vya hatari kuwa bidhaa zilizo chini ya viwango zinaweza kupenya na kuifikia jamii kutokana na mianya iliyojitokeza katika kusimamia bidhaa zinazotoka kwa masharti.

Ninapendekeza kuwa TBS itengeneze na kuifanyia kazi mifumo ya ufuatiliaji, utathmini na udhibiti wa bidhaa zilizo kwenye utaratibu wa kutolewa kwa masharti; kuchukua hatua stahiki kwa bidhaa ambazo zimeshindwa ukaguzi wa vipimo muhimu; kuweka ukomo wa kuvumilika kwa mwingizaji wa bidhaa ambaye bidhaa zake zinashindwa mara kwa mara, ambapo hatua zaidi zitatakiwa kuchukuliwa kwa ambaye kushindwa kwake kumezidi ukomo wa kuvumilika uliowekwa; na kuhakikisha ripoti za ukaguzi wa bidhaa ambazo zinatolewa kwa masharti zinatolewa na mteja kujulishwa ndani ya muda.

7.4.5 Kuruhusu Bidhaa za Chakula Zilizomalizika Muda Wake wa Matumizi na Zilizobakiza Muda Mfupi wa Matumizi

Kifungu cha 4(1)(a) cha Sheria ya Viwango ya mwaka 2009 kinataka TBS kuchukua hatua za kudhibiti ubora wa bidhaa, huduma na mazingira ya aina zote na kukuza viwango katika viwanda na biashara. Hii inafanyika kupitia upekuzi na ukaguzi wa bidhaa.

Nilibaini matukio ambayo TBS ilichukua sampuli za chakula ambacho muda wake wa matumizi ulikuwa umeisha au unakaribia kuisha ndani ya siku kadhaa au mwezi baadaye kwa mujibu wa maelezo yaliyobandikwa kwenye bidhaa na kuzikagua. Baadhi ya sampuli hazikuonesha hata muda wa

mwisho wa matumizi. Hata hivyo, ripoti za ukaguzi wa bidhaa zilionesha kuwa sampuli hizo zilifaulu; na hivyo, bidhaa hizo za chakula zilitolewa kwa matumizi ya walaji.

Kuna viashiria kuwa bidhaa za chakula zilizoisha muda wa matumizi zilisambazwa masokoni na zinatumiwa ambapo zinaweza kuathiri afya za walaji.

Ninapendekeza kuwa TBS ihakikishe bidhaa zilizoisha muda haziruhusiwi kwa matumizi ya binadamu na ichunguzwe namna ambavyo bidhaa zilizoisha muda wake zilifaulu ukaguzi na kuruhusiwa kwenda kwenye matumizi ili kuchukua hatua stahiki.

7.4.6 Bidhaa Zilizo Chini ya Kiwango Kuruhusiwa Kuuzwa Nje ya Nchi na Nembo ya Ubona ya TBS

Kifungu cha 4 (1)(a) cha Sheria ya Viwango ya mwaka 2009 kinaitaka TBS kufanya vipimo kwa ajili ya kudhibiti ubora wa bidhaa, huduma na mazingira ya aina zote na kukuza viwango katika viwanda na biashara. Hii inafanyika kwa kufanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye soko na wazalishaji wa ndani Kifungu cha 4.2.7.2 cha Mwongozo wa Bidhaa Zinazolingia Nchini wa mwaka 2017 kinaitaka TBS kuchukua hatua stahiki kwa bidhaa na wazalishaji ambao hawafikii viwango vya ubora.

Nilibaini tukio moja ambalo TBS haikuchukua hatua yoyote dhidi ya bidhaa za mzalishaji wa vigae (Goodwill Tanzania Ceramic Co. Ltd) ambaye bidhaa zake hazikufaulu katika ukaguzi wa vipimo muhimu kwa kila jaribio lililofanyika wakati wa ukaguzi wa kushtukiza. Bidhaa hizi zinauzwa katika masoko ya nje ya nchi; hivyo zinabeba sura ya bidhaa za Tanzania katika soko la kimataifa. Mwezi Septemba 2017 na Mei 2018 bidhaa zilionekana kuwa chini ya kiwango baada ya kwenda kuuzwa nchi jirani; na mzalishaji kupewa barua ya onyo. Bidhaa hizo zilishindwa tena kufaulu na zilikataliwa kuuzwa kwenye soko la nchi hiyo kwa mujibu wa barua ya nchi hiyo yenye kumbukumbu Na. KEBS/HQ/QAS/18 ya

tarehe 18 Julai 2018. Malori 30 kati ya 31 yaliyopatikana na bidhaa zilizokataliwa yalisitishwa, lakini wakati wa ukaguzi wa TBS; hayakuonekana kuwa na nembo ya TBS na yalipatikana katika maeneo tofauti. Lori moja kati ya yale 31 halikupatikana kabisa; na mpaka leo halijajulikana lilipo.

Mapungufu yaliyobainika yanatokana na utaratibu wa TBS kutoa leseni hata kwa wazalishaji ambao wameshindwa katika tathmini ya mwanzo ya kiwanda. Hivyo kushindwa kuchukua hatua kwa mzalishaji aliyeshindwa wakati wa ukaguzi wa kushtukiza sokoni. Hii inasababisha soko la bidhaa za Tanzania kupungua katika soko la kimataifa.

Ninapendekeza TBS kuboresha udhibiti wa viwango vya ubora kwa bidhaa zinazozalishwa nchini ambazo zinatarajiwa kuuzwa nje ili kukuza uaminifu na heshima ya bidhaa za Tanzania katika masoko ya kimataifa. Zaidi ya hapo, mapungufu yaliyobainika yachunguzwe na hatua stahiki kuchukuliwa.

7.4.7 Mapungufu Yaliyobainika katika Uhakiki wa Kukidhi Vigezo Kabla ya Kusafirisha Bidhaa (PVoC)

(i) Utozaji wa Ada ya Ukaguzi wa Magari Zaidi ya Kiasi Kilichokubaliwa

Kwa mujibu wa kifungu cha 20 cha Masharti Maalum ya Makubaliano ya Uhakikisho wa Kukidhi Vigezo Kabla ya Kusafirisha Bidhaa (PVoC) kati ya TBS na watoa huduma wanne (4) kwa magari yaliyotumika kwa kipindi cha mwezi Machi 2018 hadi mwezi Februari 2021, ada ya ukaguzi inayotakiwa kutozwa ni Dola za Kimarekani 150 kwa gari (Machi 2015 hadi Februari 2018 ilikuwa Dola za Kimarekani 140) ambapo Shirika la Viwango linapata asilimia 30% ya kiasi hicho.

Katika mapitio yangu ya biashara ya magari yaliyotumika kwa makampuni matano (5) yajulikanayo kama SBT Japanese Vehicle, Beforward, Autorec

Japan, Tradecarview na Real Motors Japan nilibaini kuwa kwa kipindi cha kati ya tarehe 5 Novemba 2018 na 15 Desemba 2018, wateja walioomba Ankara kifani walitozwa kati ya Dola za Kimarekani 300 mpaka 380 ambazo zimeleta wastani wa Dola za Kimarekani 316 kwa gari moja kiasi ambacho ni zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa cha Dola za Kimarekani 150 kwa wastani wa Dola za Kimarekani 166.

Kwa mujibu wa ripoti ya TBS ya Uhakikisho wa Kukidhi Vigezo Kabla ya Kusafirisha Bidhaa, kutoka kwa mawakala wa PVoC, jumla ya magari 57,031 yalikinguliwa nchini Japan kwa ajili ya kuingizwa nchini Tanzania kati ya tarehe 1 Januari 2017 na 30 Septemba 2018, jumla ya ada ya ukaguzi ya ziada ya Dola za Kimarekani milioni 9.47 (sawa na Sh. bilioni 20.92) zilitozwa kwa Watanzania na taasisi mbalimbali.

Wauzaji wa magari kwa sasa hawaratibiwi na hawajaandikishwa na TBS hivyo kuondoa dhana nzima ya kulinda maslahi ya mteja. Ninapendekeza kuwa TBS ianzishe kampeni ya ufahamu kuelimisha jamii juu ya kiasi wanachostahili kutozwa na wauzaji wa magari ya mtumba.

Pia ninapendekeza Shirika la Viwango kutengeneza mwongozo ambao utatumika na wauzaji wote wa magari yaliyotumika juu ya umuhimu wa kuhakikisha wanafuata sheria na kanuni za Tanzania, pia Shirika la TBS linatakiwa kuhakikisha kuwa wauzaji wote wa magari wanaofanya kazi katika nchi hii wanaandikishwa na Shirika la Viwango na utendaji wao unaangaliwa kwa karibu ili kuhakikisha magari yao yote yanayoingia nchini yanakuwa na vigezo vya kutembea katika barabara zetu. Zaidi ya hayo, hatua kali zinastahili kuchukuliwa ikiwemo tozo za adhabu,

kuwafungia kwa muda na moja kwa moja kutokana na kiwango cha makosa cha wauzaji hao wa magari.

(ii) Kutozingatiwa kwa Taratibu za Utendaji za Uhakikisho wa Kukidhi Vigezo Kabla ya Kusafirisha Bidhaa (PVoC)

Shirika la TBS liliingia katika mikataba tofauti na makampuni ya EAA, QISJ, Auto Terminal Japan Ltd, Jabal Kilimanjaro Auto Elect. Mechanical and National Institute of Transport (NIT) ya kufanya uhakiki wa kukidhi vigezo kabla bidhaa kusafirishwa (PVoC) kwa magari yaliyotumika kati ya tarehe 1 Machi 2018 na 28 Februari 2021.

Tathmini yangu ya utekelezaji wa vigezo na masharti ya mikataba ya PVoC ilibaini kuwa taratibu za utendaji zililenga kuleta ufanisi, ubora wa matokeo na usawa katika utendaji huku zikipunguza kutokuelewana na kushindwa kukidhi vigezo vya mikataba hivyo kurahisisha utekelezaji wa mikataba bado hazijatayarishwa, kusambazwa wala kuanza kutumika na watoa huduma.

Ninapendekeza kuwa Shirika la TBS litengeneze na kusambaza kwa watoa huduma Taratibu za Utendaji ambazo zitaelezea kwa undani hatua muhimu za kufuata wakati wa ukaguzi wa magari.

(iii) Kukosekana kwa Mfumo wa Kuhakiki Wateja Mtandaoni

Kifungu cha 2.2.2 (i) cha mkataba wa PVoC kati ya TBS na Watoa huduma kinataka Cheti cha Kukidhi, ripoti ya ukaguzi na picha za gari kuwekwa kwenye kanzi data ya tovuti ili maafisa wa TBS waweze kuziona wakati wa uhakiki.

Nilibaini kuwa, mfumo wa kuhakiki wateja mtandaoni unapatikana kwa TBS tu na sio kwa Umma kwa ujumla pamoja na umuhimu wa taarifa hizo kwa wateja kwani katika utaratibu wa sasa, magari ambayo yamefaulu ukaguzi yanaweza kubadilishwa kwa urahisi.

Ninapendekeza kuwa TBS itengeneze mfumo wa uhakiki mtandaoni ambao utaweza kutumiwa na Umma kuzuia uwezekano kuyachezea magari baada ya ukaguzi.

(iv) Kukosekana kwa Umakini (Due Diligence) kwa Waombaji wa kutoa Huduma ya PVoC

Kanuni ya 373(1)-(2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 inataka mamlaka inayotoa kandarasi kufanya umakini dhidi ya mshirika binafsi ambaye amependekezwa apewe kandarasi kwa kuangalia sifa zake na uzoefu, kuwasiliana na wadhamini walio kwenye orodha iliyotolewa, kuhakikisha kuwa madai au utata wowote unaohusiana na mshirika binafsi na timu yake hauathiri uwezo wake wa kutekeleza mkataba na kuhakiki mtaji wake wa uendeshaji kupitia kwa benki pendekezwa au mdhamini mwenye kuaminika.

Tathmini yangu ya utaratibu wa zabuni za PVoC uliolenga kupata watoa huduma wenye sifa ilibaini kuwa, jumla ya watoa huduma sita (6) (zikiwemo Taasisi ya Usafirishaji ya Taifa na Kampuni ya Ukaguzi na Ithibati ya China), walipewa zabuni kati ya mwezi Oktoba 2017 na Februari 2018 lakini hakukuwa na umakini uliofanyika kwenye orodha ya wadhamini iliyotolewa na waombaji wa zabuni, kufanya uhakiki na benki na wadhamini wanaoaminika, na madai kutoka mamlaka sahihi.

Pia, hakukuwa na ushahidi wa mawasiliano yaliyofanyika na mamlaka za usajili za nchi ambazo waombaji walitokea. Zaidi ya hapo, nilibaini kuwa hakuna mchakato rasmi wa kufanya umakini ikiwemo taratibu, vigezo muhimu, orodha ya kujazwa na kila timu inayofanya umakini na hitimisho lililofikiwa na kila timu kwenye masuala ya uwezo wa kifedha, ujuzi wa kazi, kisheria, usajili wa muombaji wa zabuni na kuhakikiwa na mamlaka nyingine za ithibati.

Ninapendekeza kuwa TBS ihakikishe mchakato wake wa manunuzi unapangiliwa na kuwekwa kwenye maandishi kwa ajili ya umakini ambao ni mpana unaogusa nyanja zote kama inavyotakiwa na Kanuni ya 373(1)-(2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013.

7.5 Shirika la TTCL

7.5.1 Kutokuwa na Umiliki na Mamlaka Dhidi ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (NICTBB)

Wakati wa tathmini ya uendeshaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (NICTBB) niligundua kuwa Shirika la TTCL linabeba gharama zote za uendeshaji na usimamizi wa Mkongo wa Taifa zikijumuisha mishahara ya wafanyakazi wa Mkongo wakati Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inashikilia na kudhibiti akaunti ya mapato ya NICTBB. Bei za bidhaa za NICTBB pia hupangwa na kuamuliwa na Wizara. Kwa mujibu wa Randama ya Makubaliano kati ya Shirika la TTCL na Wizara Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Shirika la TTCL halina mamlaka juu ya mapato ya NICTBB wakati Wizara haina wajibu juu ya gharama za uendeshaji za NICTBB. Shirika la TTCL linatakiwa kurudishiwa gharama zake mwisho wa mwaka husika.

Utaratibu huu unaweza kupunguza uwajibikaji katika kuutunza Mkongo wa Taifa. Pia unaweza kuleta ombwe la umiliki kati ya taasisi hizi mbili kama inavyoonekana kuwa

Shirika la TTCL halina mpango wa kuhuisha upya Mkongo baada ya kumalizika muda wake.

Ninapendekeza menejimenti ya Shirika la TTCL ikae na Serikali ili kupata ufumbuzi na iweze kumiliki Mkongo huo kwa ajili ya usimamizi mzuri.

7.5.2 Kutokurejeshewa Gharama za Kuendesha NICTBB za Sh. Bilioni 20.63

Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(1)(a) na (e) ya Sheria ya Shirika la Mawasiliano ya Simu Tanzania ya mwaka 2017, Shirika la TTCL lina wajibu wa kuendesha na kudumisha aina zote za miundombinu ya mawasiliano ya simu kama Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (NICTBB) pamoja na mifumo mingine ya TEHAMA na huduma ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sambamba na Sheria hii, tarehe 17 Novemba 2016, Shirika la TTCL na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano walianzisha Randama ya Makubaliano (MoU) kuongoza uendeshaji wa NICTBB ambapo gharama zote za uendeshaji zitabebwa na Shirika la TTCL wakati mapato yatakusanywa na Wizara na baadaye gharama zitarejeshwa mwishoni mwa mwaka na Wizara. Pia, kwa kuwa mradi wa NICTBB hauna namba ya mlipakodi (TIN) na namba ya uandikishwaji ya kodi ya ongezeko la thamani (VRN), ankara zote za kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hupelekwa Shirika la TTCL.

Katika tathmini ya uendeshaji na usimamizi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (NICTBB), nilibaini wigo wa maboresho katika maeneo yafuatayo:

- (i) Randama ya Makubaliano (MoU) kati ya Shirika la TTCL na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano iliyokamilika tarehe 17 Novemba 2017 ilikuwa bado ni rasimu inayosubiri kusainiwa na kuanza kutumika mpaka namaliza ukaguzi huu mwezi Desemba 2018. Kwa hiyo, hakukuwa na makubaliano yoyote ya

kisheria yanayoongoza uendeshaji wa NICTBB. Nashauri Wizara na Shirika la TTCL kusaini Randama ya Makubaliano ili kuwa na uwazi juu ya majukumu ya kila upande unaoendesha mradi wa NICTBB hivyo kupunguza misugvano isiyo na tija.

- (ii) Katika Mzunguko wa Kusini, matumizi ya NICTBB ni asilimia 15 tu ya matumizi yake ya juu; wakati mizunguko mingine ina wastani wa matumizi ya asilimia 75. Matumizi madogo yanatokana na ukosefu wa fedha za kufanyia uhamasishaji/masoko katika nchi ambazo hazipakani na bahari na wateja wa ndani. Kwa ujumla NICTBB unafanya kazi kwa asilimia 10 tu ya uwezo wake na chini zaidi ya ilivyokusudiwa ufanye kazi pamoja na kuwa mwaka 2016 Serikali ilipanua uwezo wake kutoka 40G mpaka 200G ili kuongeza ufanisi. Kwa kuwa Serikali imewekeza jumla ya Sh. bilioni 250 katika NICTBB, matumizi chini ya kiwango yanaweza kusababisha hasara kwa Serikali. Napendekeza kuwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano pamoja na Shirika la TTCL kuanzisha sera na mikakati ya masoko hasa katika Mzunguko wa Kusini ili kupata wateja zaidi kutoka kwa nchi ambazo hazijapakana na bahari ili kuongeza matumizi yake.
- (iii) Jumla ya Sh. bilioni 95.36 zimekipwa na Shirika la TTCL kama gharama za uendeshaji ya NICTBB kutokea mwezi Januari 2010 mpaka tarehe 30 Juni 2018; na hakuna marejesho yoyote yaliyofanyika kutoka kwa Wizara. Kwa kuwa TTCL ni mteja wa NICTBB kwa bidhaa mbalimbali, kuna madai ya Sh. bilioni 74.73 ambayo Wizara inatakiwa kulipwa na Shirika la TTCL. Hivyo, ukitoa bakaa hizo mbili, Wizara itatakiwa kurejesha kwa Shirika la TTCL Sh. bilioni 20.63 kama ilivyoinishwa kwenye jedwali hapa chini

Jedwali Na. 8: Kutorejeshewa Gharama za NICTBB

| Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|--|-----------------------|
| Tozo za kuhifadhi na kuhudumia Mkongo 1 Julai 2017 | 40,502,794,350 |
| Ada za Usimamizi 1 Julai 2017 | 21,189,963,550 |
| Tozo za Pango ya Ofisi 1 Julai 2017 | 556,248,000 |
| Gharama za uendeshaji na matengenezo 1 Julai 2017 | 4,799,548,824 |
| Tozo za Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) 1 Julai 2017 | 11,853,096,845 |
| Tozo za bima 1 Julai 2017 | 323,663,408 |
| Jumla ya Kiasi 1 Julai 2017 (A) | 79,225,314,977 |
| | |
| Tozo za kuhifadhi na kuhudumia Mkongo kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2018 | 10,792,652,701 |
| Ada ya usimamizi kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2018 | 1,986,039,335 |
| Tozo ya pango ya ofisi kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2018 | 106,614,278 |
| Gharama za uendeshaji na matengenezo kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2018 | 753,998,903 |
| Tozo za Kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2018 | 2,492,741,417 |
| Tozo za bima kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2018 | - |
| Jumla ya kiasi kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2018 (B) | 16,132,046,635 |
| Jumla ya kiasi ambacho mradi wa NICTBB unadaiwa na Shirika la TTCL kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2018 (A)+(B) | 95,357,361,612 |
| | |
| Kiasi ambacho Shirika la TTCL linadaiwa na mradi wa NICTBB kwa kutumia huduma ya Mkongo 30 Juni 2018 | |
| | |
| Bakaa ya kufungulia 1 Julai 2017 (C) | 70,322,009,467 |
| Jumla ya ankara zilizotolewa kwa mwaka ulioishi 30 Juni 2018 | |
| Ankara namba 352/NICTBB/2017 | 1,185,945,004 |
| Ankara namba r 363/NICTBB/2017 | 124,280,292 |
| Ankara namba 364/NICTBB/2017 | 1,185,945,004 |
| Ankara namba 365/NICTBB/2017 | 1,185,945,004 |
| Ankara namba 367/NICTBB/2017 | 36,465,392 |
| Ankara namba 380/NICTBB/2018 | 98,233,567 |
| Ankara namba 381/NICTBB/2018 | 571,540,199 |
| Ankara namba 382/NICTBB/2018 | 10,418,667 |
| Ankara namba 383/NICTBB/2018 | 10,418,667 |
| Jumla kiasi cha ankara kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2018 (D) | 4,409,191,795 |

| Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|-----------------------|
| Jumla ya Kiasi mradi wa NICTBB unacholidai Shirika la TTCL kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2018 (C) + (D) | 74,731,201,262 |
| Mpango wa kuoanisha madeni | |
| Jumla ya kiasi mradi wa NICTBB unachodaiwa na Shirika la TTCL 30 Juni 2018 | 95,357,361,612 |
| Jumla ya kiasi Shirika la TTCL linachodaiwa na mradi wa NICTBB 30 Juni 2018 | 74,731,201,262 |
| Malipo kwa Shirika la TTCL | 20,626,160,350 |

Ninapendekeza kuwa Shirika la TTCL lifanye ufuatiliaji Wizarani juu ya kiasi linachodai na lihakikishe kiasi chote kinapatikana.

7.6 Hifadhi za Taifa za Tanzania (TANAPA)

7.6.1 Jitihada Zaidi Zinazohitajika Kuondoa Mimea Vamizi na ya Kigeni Kwenye Hifadhi

Wakati wa ukaguzi wangu, nilibaini madhara ya mimea ya kigeni isiyo ya kawaida katika Hifadhi ya Taifa ya Arusha na Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara. Aina hiyo ya mimea inaharibu mazingira ya hifadhi hizi kwa kasi kubwa kama ilivyoainishwa hapo chini:

i. Hifadhi ya Taifa ya Arusha (ANAPA)

Takribani hekta 143.5 zilizofanyiwa utafiti zimeathiriwa na aina ya vizazi vamizi katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Ngongongare, Seneto ya zamani, Kinandia, Mweka, Rest House, Rydon na Mareu. Miongoni mwa aina nyingi za vizazi vamizi viletavyo maafa ni magugu ya *Caesalpinia Decapetala* ambayo yenye kuonekana sana ambayo yanaenea katika hifadhi hiyo kwa kasi.

ii. Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara (LMNP)

Katika hifadhi hii, niliona magugu ya *Acalypha Fruticosa* (jina la kisayansi) yanatawala eneo kubwa la Hifadhi kiasi cha kutishia kuwapo kwa Flora na Fauna.

Nilibaini kuwa, hakukuwa na fedha zilizotengwa na hifadhi kwa ajili ya kuondoa vizazi vamizi hivyo ndani ya hifadhi. Aidha Sh. milioni 12.49 zilipokelewa na LMNP kutoka makao makuu ya TANAPA zikiwa ni fedha maalum za kupambana na tatizo hilo.

Hifadhi ya ANAPA haina taratibu zozote zinazoendelea ili kukomesha tatizo hili. Hii inasababishwa na ukosefu wa fedha zilizotengwa kutoka makao makuu ya TANAPA kwa ajili ya kutatua tatizo hilo. Vizazi vamizi hivi vinaweza kusababisha kutokuonekana kwa wanyama katika shughuli za kitalii, kuzuia uzungukaji wa askari wakati wa shughuli za doria, kuzuia ukuaji wa baadhi ya mimea au kua aina za mimea ya uoto asili.

Napendekeza ANAPA na LMNP, kwa kushirikiana na TANAPA, kuchukua hatua stahiki za kuondoa magugu ya vizazi vamizi katika hifadhi zake.

7.6.2 Kutotekeleza Hatua Walizokubaliana Juu ya Athari za Aupunguza Ajali za Barabarani

Katika Hifadhi ya Taifa ya Arusha kuna barabara (Momella kwa Ngongongare) iliyo chini ya TANROAD inayounganisha upande mmoja wa hifadhi (Mommella, Kisimiri), na upande mwingine. Kumbukumbu kutoka idara ya utalii zilionesha kwamba jumla ya magari 10,353 na watu 68,534 walivuka hifadhi hiyo kwa kipindi cha miezi 6 kuanzia Julai hadi Desemba, 2017, wakati jumla ya magari 6,530 na wagonjwa 29,909 na magari 5,361 na wagonjwa 23,585 walivuka hifadhi hiyo kwenda kupata huduma za matibabu kwa mwaka 2015/2016 na 2016/2017, mtawalia. Hata hivyo, hakukuwa na malipo yoyote kutoka kwa jamii kwa kutumia barabara ya hifadhi wakati hifadhi hufanya matengenezo ya mara kwa mara kwenye barabara hiyo.

Katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi (MINAPA) kuna barabara kuu ya Tanzania-Zambia inayokatisha Hifadhi. Kwa mujibu wa ripoti ya mazingira na ulinzi hadi kufikia tarehe 30 Machi 2018, wanyama 228 waliuawa; ambapo 216 (asilimia 97) waliuawa kwa njia ya ajali za barabarani. Idadi ya wanyama waliuawa kupitia ajali za barabarani iliongezeka kwa asilimia 41 ikilinganishwa na kipindi cha 2016/2017. Kama ada ya adhabu kutokana na mauaji ya wanyama, MINAPA ilipaswa kukusanya Sh. milioni 59.2, badala yake, ilikusanya Sh. milioni 1.1 tu, sawa na asilimia 2.

Hali hii inaharibu mazingira na usalama wa Hifadhi. Pia hupunguza idadi ya wanyama kupitia mauaji ya ajali za barabarani.

Ninapendekeza TANAPA kuimarisha hatua za ufuatiliaji wa ajali za barabarani. Pia, kutafuta wadau wengine kama TANROAD na kushirikiana nao gharama za matengenezo ya barabara kwa ANAPA.

7.7 Taasisi ya Uhasibu Arusha (IAA)

7.7.1 Upungufu wa walimu katika Chuo Kikuu

Kanuni ya 33 (1) a-g ya Sheria ya Kukubaliwa na kutunuku “accreditation” ya NACTE ya 2001 inahitaji Taasisi za kitaaluma kuwa na wafanyakazi wenye ujuzi na wenye uzoefu ambao wanaajiriwa na kupewa mafunzo sahihi na kudumisha uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi wa wastani wa 1: 8.

Katika Ukaguzi wa mwaka wa fedha wa 2017/2018, nilibaini mapungufu yafuatayo katika Taasisi ya Uhasibu ya Arusha;

- a) Kulikuwa na upungufu wa walimu 88 wa makundi mbalimbali ya kitaaluma.
- b) Idadi ya sasa ya walimu wenye ngazi ya Shahada ya Uzamivu ni ndogo sana sawa na asilimia 11.3 ya walimu wote ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi na shughuli

nyingi zinazohitajika kufanywa na Taasisi zinazohitaji kiwango hicho cha elimu.

Hii inaweza kusababisha mzigo mkubwa wa kazi kwa walimu hao wa sasa, hatimaye unaweza kusababisha kushuka kwa ufanisi katika huduma za kufundisha, utafiti na ushauri. Zaidi itaweza kuharibu ubora wa shughuli hizi za msingi za Taasisi.

Ninapendekeza kuwa Menejimenti ya Taasisi ya Uhasibu ya Arusha ifuatilie haraka kupata kibali cha kuajiri wafanyakazi wanataaluma na kuandaa mpango wa ajira wa wafanyakazi wanataaluma.

7.8 Kampuni hodhi ya Mkulazi

Kampuni hodhi ya Mkulazi ilianzishwa na Mfuko wa Pansheni ya PPF (PPF) na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi wa Jamii (NSSF) mnamo tarehe 6 Septemba, 2016 ili kujenga na kuendesha kiwanda cha sukari chenye uwezo wa kuzalisha tani 200,000 za miwa kwa mwaka katika eneo la Mkulazi mkoani Morogoro.

Mnamo Februari 2017, Kampuni ilisaini Mkataba wa Maelewano na Tanzania Prison Service (TPS) shamba la Mbigiri.

Ukaguzi wangu wa upembuzi yakinifu uliofanywa na Mkulazi ulibainisha dosari zifuatazo:

- (i) Katika matumizi ya shamba la Prison Corporation Sole (PCS), hakuna uwiano wa hisa uliorodheshwa kati ya washiriki (Kampuni hodhi ya Mkulazi na Taasisi ya magereza).
- (ii) Gharama za mradi wa jumla zitakuwa Dola za Kimarekani milioni 49.15 ambazo zimefanywa kwa uwiano wa madeni /na mtaji wa asilimia 70 na asilimia 30, mtawalia. Hata hivyo ripoti haina maelezo ya zaidi ya kuhusiana na deni kama vile

mkopeshaji wa fedha, kiwango cha riba, muda wa kulipa, dhamana ya deni na jinsi gani mkopo utafadhiliwa.

- (iii) Mradi haujaainisha vikwazo mbalimbali vinavyoweza kurudisha nyuma uwezo wa kazi iliyopangwa kana kwamba kiwanda kitafanyia kazi kwa ufanisi bila kikwazo chochote kwa mwaka mzima.
- (iv) Fedha za uwekezaji ni uwiano wa madeni kwa mtaji wa asilimia 70 na 30, lakini taarifa ya mtirirko wa fedha taslim hazielezi jinsi fedha zitakavyopokelewa na kulipa asilimia 70 kwa ajili ya fedha za uwekezaji.
- (v) Hesabu za NPV ya mradi haijajumuisha gharama za riba ambayo ni asilimia 70 ya gharama ya uwekezaji wa mradi. Nina mashaka kwamba kutokana na kuachwa kwa gharama za riba, mradi hauwezi kuwa na uwezo na kuzalisha mapato tarajiwa.
- (vi) Pia mfumo bora juu ya uamuzi wa ufanisi wa mradi lazima ulinganishe viashiria na vigezo vya uwezekano wa mradi dhidi ya viashiria na vigezo vya mradi huo wa kazi. Hii haikufanyika katika mradi huu.

Ninapendekeza kuwa Uongozi wa kampuni ufanye uchambuzi wa kina juu ya jinsi kiwango tozo ya riba (discount rate) kinavyopatikana kutokana dhana husika. Hii ni kwa sababu fedha za mradi zinahusisha uwiano wa madeni kwa mtaji kwa uwiano wa 70:30. Kadhalika Uongozi uzingatie udhaifu uliotajwa na kuandika upya uchunguzi wa ufanisi.

7.9 Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL)

Kampuni ya Ndege ya Tanzania imekuwa ikipata hasara kwa muda wa miaka 10 kwa mfululizo, kutoka mwaka 2006/07 mpaka 2016/17. Hasara imepunguza mtaji wa kampuni

mpaka kufikia mtaji hasi. Kwenye miaka mitatu ya hivi karibuni nimeanza kuona mwenendo mzuri wa kampuni maana hasara imepungua kutoka Sh. bilioni 38.72 ya mwaka 2005/06 mpaka Sh. bilioni 16.21 mwaka 2016/17, kupungua kwa takribani asilimia 58. Kupungua kwa hasara kumetokana na kuongezeka kwa mapato kwa asilimia 20 na kupungua kwa gharama za uendeshaji kwa asilimia 27.

Kampuni imeandaa mpango kazi wa miaka mitano unaotumika kama muongozo wa utekelezaji wa malengo ya Kampuni kuanzia mwaka 2017/18. Mpango unajumuisha mbinu za kuongeza mapato na kupunguza gharama za uendeshaji ili kuendelea kupunguza hasara na baadaye kumaliza kabisa kwenye siku za usoni. Sambamba na haya maboresho, Kampuni inafanya mageuzi kwenye muundo wa Kampuni, mabadiliko kwenye utendaji wa kazi na rasilimali watu ili kufikia utendaji wenye ufanisi.

Kufuatia mwendelezo wa maboresho kwenye rasilimali watu, kuongezeka kwa ndege, utekelezaji wa mpango mkakati wa miaka mitano na mbinu za kupunguza gharama za uendeshaji kunatoa ishara nzuri ya ukuaji wa kampuni. Ili kuharakisha mwenendo mzuri wa utendaji na ukuaji wa kampuni, msaada wa kifedha kutoka Serikalini ni muhimu sana ili kuiwezesha kampuni kulipa madeni yake ya nyuma ambayo yanaibebesha kampuni mzigo mkubwa wa kulipa riba za kila mwaka.

Ninapendekeza kuwa Kampuni ya Ndege ya Tanzania iendeleo kuimarisha utendaji wake wa kazi ili kuweza kupata faida kwa kuongeza mapato na kupunguza gharama za uendeshaji kwa kutoa huduma nzuri kwa wateja, kutumia vizuri ndege zilizopo na kubuni mbinu za kupunguza gharama zaidi. Pia, napendekeza Serikali itoe msaada wa kifedha kwa Kampuni ili kuiwezesha kulipa madeni ya nyuma yanayoiongezeka gharama kampuni kupitia ulipaji wa riba ambayo inachukua nafasi kubwa ya gharama.

SURA YA NANE

USIMAMIZI WA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA TAASISI ZA UMMA

8.1 Utangulizi

Katika tathimini yangu ya udhibiti wa ndani katika usimamizi wa matumizi ya fedha za Umma nilibaini kuwa, Taasisi za Umma ziliendelea kuingia gharama zisizo na tija. Aidha, Taasisi za Umma hazijaboresha udhibiti wa ndani katika matumizi; ambapo baadhi ya gharama hazikuidhinishwa kwa usahihi. Kuwapo kwa idhini ya malipo ya posho kwa wafanyakazi ambayo hayapo kwenye miongozo, hayajaidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi au yanakinzana na miongozo ya Msajili wa Hazina (TR); Pamoja na kuwapo kwa matumizi yaliyozidi bajeti iliyoidhinishwa kunaongeza madeni kwa Taasisi hizi. Nilibaini pia kuwa sehemu kubwa ya matumizi yamefanyika nje ya shughuli za kazi kuu za Taasisi husika.

Sura hii inaonesha mapungufu niliyoyabaini kwenye matumizi ya fedha za Umma na ushauri niliyotoa kuimarisha udhibiti wa ndani kwenye matumizi.

8.2 Tathmini ya Ufanisi katika Udhibiti wa Gharama

8.2.1 Kuripotiwa kwa Tuhuma za Ubadhirifu katika Mamlaka ya Udhibiti wa Chakula na Dawa (TFDA) - Ofisi ya Kanda ya Kaskazini

Matumizi ya Taasisi za Umma yanaongozwa na sheria, kanuni, miongozo na sera zilizotengenezwa na Serikali na taasisi husika. Zote hizi kwa pamoja zinalenga katika kulinda matumizi bora ya rasilimali za Umma ili zitumike katika shughuli zenye manufaa ya kiuchumi. Pamoja na juhudi za kuboresha udhibiti wa matumizi katika taasisi za Umma, nilibaini tuhuma za ubadhirifu katika Ofisi ya Kanda ya Kaskazini ya Mamlaka ya Udhibiti wa Chakula na Dawa (TFDA).

Katika Ofisi za TFDA Kanda ya Kaskazini nilibaini matumizi mabaya ya fedha yaliyofanywa na watumishi wasio waaminifu. Tuhuma hizi za ubadhirifu zimebainika baada ya kufanywa uchunguzi na menejimenti ya TFDA kupitia kwa mkaguzi wa ndani.

Baada ya kupitia ripoti ya mkaguzi wa ndani, nilibaini ubadhirifu wa fedha za Umma unaotokana na mapungufu kwenye mifumo ya udhibiti wa ndani. Ubadhirifu huo unajumuisha matumizi ya kughushi yenye jumla ya Sh. milioni 513.36 kwa mwaka wa fedha 2017/18, Sh. milioni 703.01 kwa miezi ya Julai, Agosti na Septemba 2018 na fedha zilizohamishwa Sh. milioni 423.81 hazikuonekana kwenye taarifa za kibenki.

Pamoja na hatua za kinidhamu ambazo tayari zimechukuliwa, nina mashaka na ufanisi wa udhibiti uliopo kwa kuwa umeshindwa kung'amua/kugundua na kuzuia ubadhirifu huu kabla haujatokea. Hii inaonesha kuwa kuna uwezekano wa matendo mengine ya ubadhirifu ambayo hayajabainika/hayajagundulika.

Ninapendekeza TFDA ihakiki nyenzo zake za kuzuia na kudhibiti ili kulinda mali za Umma ili kupunguza viashiria vya hatari ya kupata hasara itokanayo na ubadhirifu wa fedha na rasilimali nyinginezo.

8.2.2 Gharama Zisizofaa Zilizotokana na Riba ya Kucheleweshwa Malipo ya Fidia - Sh. bilioni 32.25

Uthaminishaji na malipo ya fidia hufanyika kwa mujibu wa Kifungu cha 3(1)(g) cha Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999. Sheria ya Ardhi inataka malipo ya fidia kuwa katika msingi wa haki na kulipwa fedha yote mapema. Kanuni ya 13(2) ya Kanuni za Ardhi za Mwaka 2001 na Kanuni ya 19(1) - (3) ya Kanuni za Ardhi za Vijiji ya mwaka 2001 zinataka fidia kulipwa ndani ya miezi sita (6) baada ya kufanyika tathmini; baada ya hapo, riba itatozwa kwa kuzingatia kiwango cha soko kwa wakati husika.

Mamlaka ya Kanda Maalum ya Kuzalisha Bidhaa za Nje (EPZA) ilichukua ardhi katika eneo la Kituo cha Biashara na Usafirishaji, eneo la Kanda Maalum ya Kiuchumi ya Bagamoyo, Tanga, Ruvuma na Kanda Maalum za Kiuchumi za Manyoni. EPZA iliingiza katika rekodi zake ardhi iliyochukuliwa mara tu baada ya uthamini kufanyika na Mthaminihaji Mkuu wa Serikali. Rekodi za EPZA zilionyesha kiasi cha riba kilichojikusanya kwa kipindi cha zaidi ya miaka 8 kuwa ni Sh. bilioni 31.02 sawa na asilimia 46 ya thamani halisi ya Sh. bilioni 67.24.

Katika shauri jingine linalofanana na hili, nilibaini kuwa uthaminihaji wa ardhi na mali katika eneo la makazi la Kurasini ulifanyika mwezi Machi 2015 kufuatia maelekezo yaliyotolewa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi mwezi Agosti 2013. Fidia zilifanywa na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mkoa wa Dar es Salaam (DAWASA) kwa kuwa ardhi hiyo ilichukuliwa ili kuanzisha bwawa la maji machafu. Thamani halisi kwa mwaka 2015 ilikuwa Sh. bilioni 7.38 ambayo iliongezeka na kuwa Sh. bilioni 8.60 mwaka 2017. Ongezeko la Sh. bilioni 1.23 limetokana na riba iliyojilimbikiza kwa miaka miwili (2) kutokana na kuchelewesha malipo ya fidia.

Ninapendekeza, Serikali na Taasisi zingine za Umma kuchukua ardhi pale tu zinapokuwa na fedha za kulipa fidia ili kuepuka kuongezeka kwa gharama zisizokuwa za lazima.

8.2.3 Posho Zilizolipwa Kinyume na Waraka wa Msajili wa Hazina Sh. Bilioni 1.86

Waraka wa Msajili wa Hazina Na. 1 wa mwaka 2010 uliotolewa tarehe 22 Julai 2010 ukiwa na Kumbukumbu Na. TYC/T/200/538/18 unataka posho za nyumba kulipwa watumishi kama Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na viongozi wenye ngazi ya mshahara ya PUTS/PHTS/PGMS/PRSS 18-21.

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) limeingia gharama za jumla ya Sh. bilioni 1.6 kama posho za nyumba. Hata hivyo, nilibaini kuwa kiasi hicho kimelipwa kwa watumishi wasiostahili, wakiwamo watumishi wa mkataba na wanafunzi, kinyume na waraka wa Msajili wa Hazina na miongozo ya TBS kuhusu posho ya nyumba.

Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mkoa wa Dar es Salaam (DAWASA) imelipa Sh. milioni 276.23 kama posho ya nyumba, ikiwa ni asilimia 15 ya mshahara kwa wafanyakazi wote, bila kujali nafasi zao. Hii ni kinyume na Waraka wa Hazina. Ninapendekeza Msajili wa Hazina ahakikishe kuwa nyaraka za Serikali ambazo zinafanya kazi zinazingatiwa na kama kuna mahitaji maalum yamejitokeza kwa baadhi ya taasisi, atoe muongozo kwa mahitaji hayo.

8.2.4 Kukosekana kwa Miongozo ya Posho Zilizolipwa kwa Watumishi wa Mashirika ya Umma

Pamoja na kuwapo kwa Waraka wa Msajili wa Hazina Na. 1 wa mwaka 2010 wa tarehe 22 Julai 2010 wenye Kumbukumbu Na. TYC/T200/583/18, kila taasisi ya Umma ina sheria zake, kanuni na sera zinazoongoza malipo ya posho kwa watumishi wake.

Nilibaini matukio ambapo posho zililipwa bila ya kuwa na miongozo sahihi au zililipwa kinyume na miongozo. Katika DAWASA, Bodi ya Wakurugenzi iliidhinisha kuwa posho za ziada (Posho ya gari, usafiri, tiba na ya nyumba) zisizidi asilimia 40 ya mshahara wa msingi, hata hivyo, DAWASA ililipa posho hizo kwa kiwango cha asilimia 45 ya mshahara wa msingi ambayo ipo juu ya kiwango kilichoidhinishwa cha asilimia 40. Taasisi ya Sukari ya Taifa (NSI) imelipa Sh. milioni 22 kama posho ya moduli ya ziada kwa wakufunzi wa kozi za kilimo. Hata hivyo, taasisi hiyo haijatengeneza muongozo unaoonesha viwango vitakavyotumika kwenye posho hizo.

Nimaoni yangu kuwa kukosekana kwa miongozo sahihi kwa ajili ya posho kumetoa mwanya katika udhibiti wa matumizi

ya Umma. Hivyo, kila taasisi inakuwa huru kuchagua kiwango ambacho posho inaweza kulipwa. Hii inaweza kusababisha taasisi za Umma kutumia fedha zaidi katika shughuli ambazo si za msingi.

Ninapendekeza Msajili wa Hazina achunguze posho zote zinazolipwa kwenye Taasisi mbalimbali za Umma na kutoa miongozo ambayo itasaidia taasisi hizo katika kulipa posho.

8.2.5 Ongezeko la Madeni ya Wafanyakazi Katika Taasisi za Elimu ya Juu na Vyuo Vikuu

Kila taasisi ya elimu ya juu ina kanuni au sera zake zinazotoa miongozo ya stahiki mbalimbali zinazolipwa kwa wafanyakazi wake kama vile kiinua mgongo. Aidha, Kanuni hizo zinatoa mwongozo juu ya malipo ya kiinua mgongo kwa wafanyakazi wa mikataba baada ya kukamilisha muda wao wa mkataba. Ukaguzi wa shughuli mbalimbali za Taasisi za elimu ya juu, ulibainisha kuwa, madeni ya wafanyakazi yamebakia kuwa makubwa au kuzidi kuongezeka kwa muda.

Madeni haya yanatokana na stahiki mbalimbali za wafanyakazi kama vile posho za majukumu na malipo ya kiinua mgongo. Kuanzia 2016/2017 hadi 2017/2018 madeni hayo yameongezeka kwa zaidi ya asilimia 40 katika vyuo vikuu vyote vilivyokaguliwa.

Kwa mfano, kutoka mwaka 2016/2017 hadi 2017/2018 madeni yanayohusiana na malipo ya posho ya majukumu kwa Chuo Kikuu cha Mzumbe na Ardhi yameongezeka hadi kufikia Sh. bilioni 3.41 na Sh. bilioni 2.26 kutoka Sh. bilioni 1.49 na Sh. bilioni 1.48 mtawalia.

Kadhalika, Chuo Kikuu cha Dar es salaam na Chuo Kikuu cha Mzumbe vilikuwa na madeni ya malipo ya kiinua mgongo ya Sh. bilioni 5.59 na Sh. milioni 525, mtawalia, kwa wafanyakazi ambao wamekamilisha mikataba yao ya

huduma. Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) kilikuwa na Sh. bilioni 6.80 kama madeni ya wafanyakazi tangu Juni 2017, ikiwa ni posho za nyumba na madeni mengineyo. Taasisi ya Uhasibu Arusha (IAA) pia ilikuwa na deni la Sh. milioni 519, ikiwa ni madeni yatokanayo na posho za wafanyakazi. Hata hivyo, limeshuka kwa Sh. milioni 6 tu (2016/17: kutoka Sh. milioni 525).

Madai ya watumishi ambayo hayajalipwa yanaweza kushusha morali wa utendaji kazi kwa wafanyakazi. Kiinua mgongo hutumika kama malipo ya mwisho ya ajira ya wafanyakazi ambao wamekamilisha mikataba yao ya huduma.

Wakati ninakiri jitihada za Serikali kuhakiki madai ya wafanyakazi kabla ya kulipwa, ninaisihi Serikali kuangalia muda wa uhakiki wa madeni hayo, kwani kutumia muda mrefu kuhakiki madeni, kunazidisha ongezeko la madai na kuzidi kuongeza mzigo kwa Serikali.

Ninapendekeza kuwa Serikali ikamilishe mchakato wa uhakiki wa madeni hayo na kuweza kuyalipa madeni husika kwa wakati.

8.2.6 Makosa Katika Usimamizi na Malipo ya Kodi ya Ardhi Sh. Milioni 112.96

Kituo cha stadi za kazi na ufundi tawi la Mwanza kinamiliki viwanja viwili vilivyopo nyakato ambavyo ni kiwanja namba 3 chenye hati namba 13220 ya tarehe 6 Mwezi Novemba mwaka 2000 chenye ukubwa wa ekari 7.24 na kiwanja namba 4 chenye hati namba 13221 ya tarehe 6 Novemba, 2000 chenye ukubwa wa ekari 9.45. Niligundua kwamba kituo hiki hakijawahi kulipa kodi ya ardhi katika ofisi za Halmashauri ya Manispaa ya Mwanza tangu mwaka 2000, na matokeo yake kimelimbikiza deni la Sh. milioni 112.96.

Napendekeza kituo cha stadi za kazi na ufundi tawi la Mwanza wawasiliane na Halmashauri ya Manispaa kwa ajili ya kupata usahihi wa deni la pango la ardhi kwa ajili ya malipo na kuingiza kwenye vitabu vyao vya hesabu.

SURA YA TISA

UWEKEZAJI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA

9.0 Utangulizi

Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025) imelenga kuifanya Tanzania kuwa ni nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Dira inaitaka Tanzania kutoka katika uchumi unaotegemea kilimo duni kuwa nchi inayotegemea uchumi wa kilimo cha kisasa, sambamba na maendeleo ya viwanda vijijini na mijini.

Katika mchakato wa kufikia uchumi wa kati, Tanzania imeandaa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) ambao umeainisha umuhimu wa kutumia kanda maalumu za uwekezaji (SEZ) na vituo vinavyotoa huduma mahala pamoja kwa wawekezaji (One-stop Centers) ili kuchochea uwekezaji na biashara.

Hivyo, Mashirika ya Umma kama vile Mamlaka ya Kanda Maalum ya Kuzalisha Bidhaa za Nje (EPZA), Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) yamepewa jukuma la kuchochea, kuwezesha na kuratibu biashara na uwekezaji ili kufanikisha ajenda ya uwekezaji na maendeleo ya viwanda.

Ukiyaacha mashirika tajwa hapo juu, Mashirika mengine ya Umma pia yanafanya uwekezaji wa namna mbalimbali ili kufanikisha maendeleo ya viwanda au mafao ya baadaye yatakayopatikana kutokana na faida katika uwekezaji. Uwekezaji unaofanywa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Benki zinazomilikiwa na Serikali umeelezewa katika sura ya 10 na 11 mtawalia.

Kwa hiyo, sura hii inaelezea mambo yaliyojiri katika uwekezaji na mapendekezo kwa Mashirika ya Umma ambayo yana jukumu la kufanikisha uwekezaji ili kustawisha uchumi, pamoja na mashirika mengine ya Umma yanayofanya uwekezaji,

isipokuwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Benki zinazomilikiwa na Serikali.

9.1 Mapitio ya Uendeshaji Katika Mashirika ya Umma Yenye Jukumu la Kuchochea, Kuwezesha na Kuratibu Biashara na Uwekezaji

9.1.1 Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)

Katika kipindi cha ukaguzi, nilibaini mambo yafuatayo katika shughuli za TIC:

- i. **Kutokuwapo kwa Mwongozo wa Utendaji katika Ofisi za Kanda**
TIC imefanikiwa kuanzisha ofisi za kanda saba nchi nzima. Ofisi za kanda zinatakiwa kutekeleza majukumu yake vizuri na kwa ufanisi ili ziweze kuwasaidia wawekezaji pamoja na kusaidia kuratibu huduma kati ya wawekezaji na makao makuu ya TIC. Katika mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2018, TIC ilikuwa na jumla ya miradi ya uwekezaji 9,698 yenye jumla ya thamani ya Dola za Kimarekani milioni 187.22, miradi hiyo inasimamiwa na ofisi za kanda za TIC (Mashariki, Kusini, Magharibi, Nyanda za Juu Kusini, Kaskazini, Ziwa na Kati).

Hata hivyo, nilibaini kutokuwapo kwa muongozo wa utendaji unaoonesha mipaka ya utendaji na miongozo kwa meneja wa kanda kuhusu majukumu yao na namna ya kufanya kazi ndani ya wigo wa kanda zao. Aidha, nilibaini shughuli za ofisi za kanda zinatofautiana kati ya kanda moja na nyingine. Kutokuwapo kwa muongozo wa utendaji wa ofisi za kanda kunaweza kusababisha kushindwa kutoa taarifa ya mafanikio ya huduma zinazotelewa na ofisi za kanda.

Ninapendekeza kuwa TIC itengeneze mwongozo wa utendaji wa ofisi za kanda ili ziweze kufanya kazi kwa utaratibu unaofanana.

ii. Motisha kwa Wawekezaji Isiyozingatia Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004

Kifungu cha 20 cha Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 kinaitaka Kamati ya Taifa ya Uendeshaji Uwekezaji nchini (NISC) kuidhinisha nyongeza maalum ya motisha ambayo pia hujadiliwa na Wizara ya Fedha na Mipango baada ya kuidhinishwa na NISC.

Ukaguzi wangu katika Kurugenzi ya Uchocheaji na Uwezeshaji ya TIC ulibaini kwamba, NISC iliidhinisha motisha kwa wawekezaji. Hata hivyo, motisha hizo hazikuweza kutumiwa na wawekezaji kwa kuwa zinakinzana na Sheria ya Kodi ya mapato ya mwaka 2004.

Wawekezaji wengi waliomba kufutiwa kodi ya zuio katika huduma inayotolewa na washauri wa ujenzi wa miradi; ambapo, maombi hayo yaliidhinishwa na NISC. Hata hivyo, motisha hizo zinakinzana na kifungu cha 83 (1) (c) cha Sheria ya Kodi ya mapato ya mwaka 2004 kilichorekebishwa katika sheria ya mwaka 2016 kifungu cha 4 (c) ii. Jedwali hapo chini linaonesha mifano ya miradi na motisha:

Jedwali Na. 9 :Miradi yenye motisha ambayo haizingatii sheria za kodi

| Na | Jina la Mradi | Aina ya Motisha iliyotolewa NISC | Utekelezaji |
|----|---------------------|---|----------------|
| 1 | Mchuchuma & Liganga | Msamaha wa ongezeko la Kodi thamani (VAT) kwenye makaa ya mawe ya kupikia, Kemikali kwa ajili ya kutenganisha chuma, vanadi na titan. | Haijatekelezwa |
| | | Msamaha wa kodi ya zuio ya huduma ya washauri wa ujenzi. | |
| | | Msamaha wa Kodi ya Mafunzo na Maendeleo (SDL) asilimia tatu kwa miaka 15. | |
| 2 | Goodwill Ceramics | Msamaha wa kodi ya zuio ya huduma ya washauri wa ujenzi. | Haijatekelezwa |

Ninapendekeza kuwa Wizara ya Fedha na Mipango na wadau wengine watatue ukinzani huu na waangalie njia iliyo bora ambayo haitakinzana na sheria za kodi.

iii. Kutokuuwezesha Kifedha Mfuko wa Benki ya Ardhi

Kifungu cha 6 cha Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 kinahitaji TIC, kwa kushauriana na Taasisi za Serikali na Mashirika yake, kutambua maeneo ya uwekezaji na viwanja pamoja na maeneo ya vituo vya kutolea huduma kwa ajili ya shughuli za uwekezaji.

TIC imeanzisha Mfumo wa Benki ya Ardhi ambao unalenga kuwa na ardhi kwa ajili ya kuwasaidia wawekezaji. Malengo mengine ni kuwa na fedha katika Mfuko huo ambazo zitaisaidia TIC kusimamia shughuli zake. Hata hivyo, nilibaini kuwa TIC bado haijafungua akaunti ya Mfuko wa Benki ya Ardhi. Kutofanya kazi kwa akaunti hiyo kutasababisha matokeo hasi kwa TIC katika kufikia malengo yake kwa wakati.

Ninapendekeza kuwa TIC ihakikishe Mfuko wa Benki ya Ardhi unafanya kazi ili kuongeza uwezo wa Kituo kwa ajili ya kuendeleza maeneo na kurahisisha shughuli za uwekezaji.

iv. Kukosekana kwa Uhamasishaji na Taarifa ya Kuwapo kwa Ofisi za Kanda za TIC kwa Wawekezaji

Kifungu cha 6 (g) cha Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 kinahitaji TIC kutoa na kusambaza taarifa mpya kuhusu fursa za uwekezaji na motisha zilizopo kwa wawekezaji.

Nilipotembelea vituo 30 vya wawekezaji vilivyopo ndani ya kanda 6 za TIC katika kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2018, nilibaini kwamba wawekezaji hawakuwa na taarifa za kuwapo kwa vituo vya kanda vya TIC katika maeneo yao.

Kukosekana kwa taarifa juu ya kuwapo kwa Ofisi za Kanda kumesababisha wawekezaji kutumia mawakala kupata vibali na leseni. Wakati mwingine, wawekezaji walikuwa wanasafiri kwenda Makao Makuu (Dar es Salaam) kupata huduma ambazo zingeweza kutolewa na Ofisi za Kanda.

Uelewa hafifu wa uwepo wa Ofisi za Kanda unamaanisha kwamba, TIC haijafikia malengo yake ya kuanzisha Ofisi za Kanda.

Ninapendekeza kuwa TIC waandae warsha zaidi kwa ajili ya kusambaza taarifa ya uwepo wa ofisi za kanda na huduma zinazotolewa katika ofisi za kanda.

9.1.2 Mamlaka ya Ukanda wa Kutengeneza Bidhaa za Kuuza Nje ya Nchi (EPZA)

Katika kipindi cha ukaguzi, nilibaini mapungufu yafuatayo katika shughuli za EPZA:

i. Kutojitosheleza katika kuwawezesha wawekezaji wa EPZA

Nilibaini mapungufu katika kuwasaidia wawekezaji ambao wanafanya uzalishaji chini ya leseni ya EPZA. Baadhi ya mapungufu yanasababishwa na kutokutekeleza wajibu. Baadhi ya Taasisi za Serikali kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Shirika la Umeme (TANESCO), Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira Tanzania (NEMC) na Halmashauri.

Nilitembelea wawekezaji 16 na kubaini kuwa, hakuna utaratibu pamoja na vituo vya mikoja vya EPZA kwa ajili ya kuwasaidia wawekezaji. Ukosefu huo wa vituo na utaratibu unasababisha wawekezaji waliopo mikoani kusafiri kwenda Dar es Salaam kupata huduma za EPZA. Pia, baadhi ya wawekezaji, kama vile African Vegetables Limited, Africado Limited na Milama Processing ambao wanazalisha mazao ya kilimo wanatumia bandari ya Mombasa badala ya bandari ya Dar es Salaam kwa sababu ya ucheleweshwaji wa taratibu za TRA na upakiaji wa mizigo. Baadhi ya wawekezaji, kama vile Tanhin

Quality Limited and Huacheng International Limited walilalamika kutozwa kodi au tozo wakati hawapaswi kulipa kodi hizo wakiwa na leseni ya EPZA. Muwekezaji M/s. African Dragon Limited alilalamika kuhusu kukatika kwa umeme wa TANESCO bila taarifa, kwani kumekuwa kunaathiri biashara yake. Pia, wawekezaji Dekker Bruins Limited na Fides Tanzania Limited wanadai marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) toka TRA kwa zaidi ya miaka miwili.

Ninapendekeza kuwa Mashirika ya Serikali yatoe huduma kwa mpangilio na kwa wakati ili huduma hizo ziweze kuwasaidia wawekezaji waliopo chini ya EPZA. Hii ni kwa sababu matatizo tajwa hapo juu yanaweza kuwavunja moyo wawekezaji waliopo na wenye mpango wa kuwekeza.

- ii. **Kuchelewa kuendeleza Kanda Maalumu za Uwekezaji (SEZ) kwa sababu ya Kutokukamilisha Fidia ya Maeneo kwa Walengwa** Majukumu ya msingi ya Mamlaka ya Ukanda wa Kutengeneza Bidhaa za Kuuza Nje ya Nchi (EPZA) ni pamoja na kununua maeneo kwa jina lake na kuyaendeleza kwa ajili ya kuyakodisha kwa wawekezaji. Nilibaini EPZA ilichelewa kulipa fidia kwa walengwa katika maeneo yaliyopangwa kuendeleza ukanda maalum wa uchumi (Special Economic Zone) wa Kurasini Trade and Logistic Centre, Bagamoyo, Tanga, Ruvuma na Manyoni, wakati uhakiki na uthaminishaji wa maeneo hayo ulishafanywa na Mthamini Mkuu wa Mali za Serikali.

Nilibaini jumla ya kiasi cha Sh. bilioni 67.2 kilipaswa kulipwa kwa wanufaika, lakini ni kiasi cha Sh. bilioni 34.2 tu ndicho kilicholipwa katika kipindi cha miaka minane iliyopita.

Ninapendekeza kuwa EPZA ilipe kiasi kilichobaki ili waweze kuendeleza maeneo maalum ya uwekezaji ya kanda.

9.2 Mapungufu yaliyobainika katika uwekezaji wa Mashirika ya Umma

9.2.1 Uwekezaji Usiokuwa na Mwenendo Mzuri

Shirika la Bima la Taifa (NIC) linamiliki mradi wa Matibabu (Medicare Insurance Scheme Product). Mradi huo unatoa huduma ya matibabu ya bima kwa ajili ya kikundi cha watu au mtu mmoja. Hata hivyo, Mradi huu umekuwa ukipata hasara toka mwaka 2013. Jedwali la hapo chini linaonesha hasara hizo:

Jedwali Na. 10: Mapato na Madai ya Matibabu

| Mwaka | Mapato (Sh.) | Madai (Sh.) | Hasara (Sh.) |
|----------------------|----------------|------------------|------------------|
| Januari-Desemba 2013 | 149,619,923.00 | 261,993,363.92 | (112,373,440.92) |
| Januari-Desemba 2014 | 200,925,193.45 | 223,881,810.27 | (22,956,616.82) |
| Januari-Desemba 2015 | 211,136,819.17 | 306,067,330.60 | (94,930,511.43) |
| Januari-Desemba 2016 | 195,082,207.60 | 474,480,129.01 | (279,397,921.41) |
| Januari-Desemba 2017 | 158,088,083.86 | 262,896,291.77 | (104,808,207.91) |
| Jumla | 914,852,227.08 | 1,529,318,925.57 | (614,466,698.49) |

Kutofanya vizuri kwa mradi huu kunasababishwa na kuwapo kwa mikakati duni ya uwekezaji, kukosekana kwa taratibu za kutathmini utendaji pamoja na ukosefu wa uhakiki wa vihatarishi. Mambo haya husaidia katika kufanya maamuzi.

Ninapendekeza kuwa NIC itathimini kama kuna umuhimu wa kuendelea na mradi huo wa matibabu, kisha ifanye maamuzi sahihi.

Pia, Katika Kampuni Hodhi ya kusimamia Rasilimali za Shirika la Reli (RAHCO) nilibaini kwamba, RAHCO ilikuwa imewekeza katika amana za muda mfupi za benki (fixed deposit) kwenye mfuko wa UTT na Benki ya Maendeleo ya TIB kiasi cha Sh. milioni 962 na Sh. bilioni 7.61, mtawalia. Amana hizo za RAHCO katika UTT na TIB ziliiva katika kipindi cha mwezi Novemba na Juni 2018 mtawalia. Ingawa, mpaka muda wa ukaguzi, mwezi

Januari 2019, UTT na TIB hawakuweza kulipa amana hizo pamoja na faida kwasababu ya matatizo ya kifedha.

Ninapendekeza kuwa RAHCO ifuatilie kwa karibu kuhakikisha amana hizo zinalipwa na UTT na TIB.

9.2.2 Mapungufu katika ukusanyaji wa Kodi

Katika Shirika la Bima la Taifa (NIC), nilibaini kuwa kodi ya pango kutoka kwa wapangaji wa majengo ya NIC ilikua hairekodiwi kwa wakati na ulinganisho wa kiasi kilicho kusanywa ulikuwa haufanywi na Meneja wa Majengo. Matokeo yake, kiasi cha kodi Sh. milioni 896 cha kuanzia mwezi Julai 2016 mpaka Desemba 2016 cha majengo ya shirika hakikurekodiwa kwa wakati. Kushindwa kurekodi na kufanya ulinganisho kwa wakati wa kiasi cha kodi ya pango kilichokusanywa kunaongeza hatari ya uwezekano wa kutokukusanya kodi hiyo.

Ninapendekeza Menejimenti ya NIC ihakikishe kodi ya pango inarekodiwa kwa wakati. Pia, ihakikishe ulinganisho wa kiasi kilichokusanywa unafanyika kwa wakati.

Pia, katika Shirika la Bima la Taifa (NIC), sikuweza kuona ushahidi wa juhudi za Shirika za kukusanya madeni ya muda mrefu ya pango kutoka kwa wapangaji wa majengo ya shirika. Katika kipindi cha mwaka wa fedha kilichoishia Juni, 2017, nilibaini baadhi ya wapangaji walikuwa wameondoka bila kulipa madeni yao wanayodaiwa na NIC. Sikuweza kupata ushahidi wa juhudi za Menejimenti au wakala kuhusu kukusanya madeni hayo ya muda mrefu. Mapungufu haya yamesababisha shirika kuwa na kiasi cha madai ya kodi ya pango Sh. bilioni 7.4 kwa mwaka wa fedha ulioshia Juni 2017.

Ninapendekeza kuwa NIC ifuatilie kwa karibu kuhakikisha madeni hayo ya kodi ya pango yanakusanywa kutoka kwa wapangaji.

Shirika la Masoko la Kariakoo (KMC) lilitoa taarifa ya kiasi wanachodai cha kodi ya pango Sh. milioni 219.70 kwa kipindi kilichoishia Juni 2018. Hata hivyo, Sikuweza kupata ushahidi wa juhudi za KMC kuhusu kukusanya madeni ya pango ya muda mrefu. Matokeo yake, baadhi ya wadaiwa kama vile Ms Lumit Co. Ltd (Sh. milioni 25.65) na Ms Mocuba Enterprises (Sh. milioni 26.23) wameshahama ilihali bado wanadaiwa. Pia, nilibaini upungufu wa Sh. milioni 87.65 wa kiasi kilichopokelewa kutoka katika makusanyo ya tozo ya kuegesha magari toka kwa mkusanyaji M/s. General Public Traders. Kwa mujibu wa makubaliano KMC walipaswa kupokea Sh. milioni 21 kwa mwezi kutoka kwa mkusanyaji. Hata hivyo, mkusanyaji aliwapatia KMC kiasi cha Sh. milioni 164.35 badala ya Sh. milioni 252 kwa kipindi cha miezi 12 kuanzia Julai 2017 mpaka Juni 2018, nakusababisha tofauti ya Sh. milioni 87.65. Zaidi ya hayo, nilibaini kutokuwapo kwa ushahidi wa juhudi za KMC za kukusanya deni hilo kutoka kwa mkusanyaji.

Ninapendekeza kuwa KMC wahakikishe mkusanyaji wa tozo za kuegesha magari anawasilisha kiasi walichokubaliana kwa mwezi, na analipa deni la nyuma.

9.2.3 Kuchelewa kumalizika kwa Miradi ya Nyumba za NHC Yenye Thamani ya Sh. Bilioni 245.55

Jukumu kuu la Shirika la Nyumba (NHC) ni ujenzi wa makazi Tanzania bara ili kuyauza kwa jamii.

Aya ya 2.1 ya Sera ya Uwekezaji wa NHC ya 2011 inataka uwekezaji wa NHC uzingatie marejesho ya mtaji uliowekezwa (ROI), muda wa marejesho ya uwekezaji, pamoja na kuangalia sababu nyingine za kiuchumi na kijamii. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa miradi miwili ya NHC imesimama tangu mwaka, 2017 kwa sababu ya ukosefu wa fedha.

i) Mradi wa nyumba (711-1) uliopo Kawe wenye Sh. Bilioni 142.55

Mradi wa Nyumba (711-1) ni mradi wa NHC uliopo katika kitalu Na 711 Kawe, Kinondoni, Dar es Salaam. Mnamo tarehe 04 Aprili 2014, NHC iliingia mkataba na Estim Construction Company Limited wenye thamani ya Sh. bilioni 105.11 pamoja na VAT kwa ajili ya usanifu na ujenzi kupitia zabuni Na. PA/066/2011-2012/HQ/W/03 kwa muda wa wiki 156 toka siku ya kwanza ya ujenzi. Mnamo tarehe, 04 Novemba 2014, NHC na Estim Construction Company Limited waliingia mkataba wa nyongeza kwa ajili ya kuhamisha mradi huo kutoka sehemu ya awali ulipokuwa umepangwa kutekelezwa katika eneo la Ngano kitalu Na. 79-82 na kupelekwa kitalu Na.711-1 Kawe. Upembuzi yakinifu wa mradi huu ulifanywa Juni 2014; miezi miwili badaye baada ya kusaini mkataba. Hii inaonesha kwamba mkataba ulisainiwa kabla hata ya kufanya upembuzi yakinifu kwenye mradi huo.

Matokeo ya upembuzi yakinifu ni pamoja na gharama za ujenzi zilizokisiwa kuwa ni Dola za Kimarekani milioni 69.43, sawa na Sh. bilioni 114.4, muda wa ujenzi ulikadiriwa kuwa ni miaka mitatu mpaka 2017, uliainisha vyanzo vya fedha za mradi, ambapo vyanzo vya ndani vitachangia asilimia 35 na mikopo itachangia asilimia 65. Mnamo mwezi Septemba 2017, NHC walibadili andiko la kibiashara na kuainisha kuwa, gharama za mradi zitaongezeka mpaka Sh. bilioni 142.55, mradi utaisha baada ya miaka miwili mpaka 2019, na vyanzo vya fedha za mradi vitabadilika na kuwa vyanzo vya ndani vitachangia asilimia 37 na mikopo itachangia asilimia 63.

Nilibaini kuwa mradi ulisimama tangu mwanzoni mwa mwaka 2017 kutokana na ukosefu wa fedha. Mpaka wakati huo, mradi ulikuwa umekamilika kwa asilimia 20, na umetumia jumla ya Sh. bilioni 26.31 kutoka katika vyanzo

vya ndani. Kwa mujibu wa upembuzi yakinifu, NHC ilikuwa na uhakika wa kupata fedha kwa ajili ya mradi, lakini mpaka sasa imeshindwa kukopa kwa ajili ya ujenzi huo.

ii) Mradi wa nyumba (711-2) uliopo Kawe wenye Thamani ya Shillingi Bilioni 103

Mradi wa Nyumba (711-2) ni mradi wa NHC uliopo kawe katika kitalu Na 711/2 karibu na ufukwe wa bahari, Kinondoni, Dar es Salaam. Mnamo tarehe 16 Octoba 2013, NHC iliingia mkataba na CRJE (EA) LTD wenye thamani ya Sh. bilioni 64.37 pamoja na VAT kwa ajili ya usanifu na ujenzi kupitia zabuni Na. PA/066/2011-2012/HQ/W/38 kwa kipindi cha muda wa wiki 130 kuanza siku ya kuanza ujenzi. Mnamo tarehe 03 Novemba 2014, NHC na CRJE (EA) LTD waliingia nyongeza ya mkataba ambapo walikubaliana bei mpya ya kazi kuwa ni Sh. billioni 71.17 pamoja na VAT. Upembuzi yakinifu wa mradi huu ulifanywa mnamo mwezi Juni 2014 miezi tisa baada ya kusaini mkataba. Hii inaonesha kwamba, mkataba ulisainiwa kabla hata ya kufanya upembuzi yakinifu wa mradi huo.

Matokeo ya upembuzi yakinifu ni pamoja na gharama za ujenzi zilikisiwa kuwa ni Dola za Kimarekani milioni 43.61 sawa na Sh. bilioni 71.86, muda wa ujenzi ulikadiriwa kuwa ni miaka mitatu mpaka 2017, uliainisha vyanzo vya fedha za mradi, ambapo vyanzo vya ndani vitachangia asilimia 15 wakati mikopo itachangia asilimia 85. Mnamo mwezi Septemba 2017 NHC walibadili andiko la kibiashara na kuainisha kuwa, gharama za mradi zitaongezeka mpaka Sh. bilioni 103, mradi utaisha baada ya miaka miwili mpaka 2019 na vyanzo vya fedha za mradi vitabadilika na kuwa vyanzo vya ndani vitachangia asilimia 29 na mikopo itachangia asilimia 71.

Nilibaini kuwa mradi huo ulisimama tangu mwanzoni mwa mwaka 2017 kutokana na ukosefu wa fedha. Mpaka wakati huo mradi ulikuwa umekamilika kwa asilimia 30 na umetumia jumla ya Sh. bilioni 34.87; ambapo vyanzo vya ndani vilichangia kiasi

cha Sh. bilioni 11.64 na mkopo kutoka benki ya TIB ulikuwa ni Sh. bilioni 23.23. Mkopo wa TIB uliochukuliwa tarehe 6 Julai 2015 na ulitakiwa uanze kulipwa baada ya miezi 36 (Julai 2018). Hii inamaana kwamba, kwa sasa NHC inatumia fedha kutoka vyanzo vingine kwa ajili ya kulipa mkopo huo. Hii ni kwa kuwa, wakati wa kulipwa mkopo huo tayari umeshafika huku ujenzi haujakamilika.

Kupitia mazungumzo yangu na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara kuhusiana na miradi hii miwili, nilibaini kwamba NHC imeshindwa kukopa benki baada ya kufika ukomo wa kukopa wa Sh. bilioni 300, ambapo wameomba kibali cha kuongeza mkopo toka Wizara ya Fedha na Mipango bila ya mafanikio. Gharama za ujenzi zinaweza kuongezeka kutokana na uwezekano wa kupanda kwa vifaa vya ujenzi, ambapo kutaathiri faida ya uwekezaji na muda wa kurudisha gharama za uwekezaji.

Ikiwa NHC haitopata kibali cha kukopa na kushindwa kukamilisha miradi yake itapaswa iwalipe wakandarasi jumla ya Sh. bilioni 99.99 kutokana na uvunjaji wa mkataba. Pia itapaswa kufanya marejesho ya Sh. bilioni 2.6 kwa wateja waliokwishaanza kulipia malipo ya awali ya ununuzi wa nyumba hizo.

Ninapendekeza kuwa Menejimenti ya NHC ifuatilie kwa karibu, na kuhakikisha wanapata kibali cha kukopa toka Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na kueleza hasara itakayopatikana kwa kukosa kibali hicho. Pia, ihakikishe inafanya upembuzi yakinifu kabla hawajaingia mikataba ya ujenzi wa miradi.

SURA YA KUMI

MWENENDO WA BENKI ZINAZOMILIKIWA NA SERIKALI

10.1 Utangulizi

Benki za Serikali ni benki ambazo Serikali inamiliki hisa zaidi ya asilimia 50 katika benki hizo. Hivi karibuni, benki hizi zimekuwa na mwenendo usioridhisha, na kusababisha baadhi ya benki kuwa chini ya usimamizi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT). Kati ya benki 6, benki 4 (asilimia 67) zilikuwa zikifanya biashara kwa hasara kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo, wakati benki zingine mbili zilikuwa chini ya usimamizi wa BoT.

Sura hii inaelezea mapungufu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa benki hizo. Pia inaelezea mapendekezo ili kuboresha maeneo mbalimbali kama vile urejeshwaji wa mikopo, mikopo chechefu, utoshelevu wa mtaji, mikopo iliyo katika hali ya hatari, maamuzi katika utoaji wa mikopo, usimamizi wa miradi na ufuatiliaji wa wateja wanaochelewa kufanya marejesho. Ukaguzi ulipitia utendaji wa benki zifuatazo: Benki ya Wanawake Tanzania (TWB), Benki ya Biashara ya TIB, Benki ya Maendeleo ya TIB, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Benki ya Posta Tanzania (TPB) na Benki ya Twiga na matokeo ya ukaguzi ni kama ifuatavyo:

10.2 Kuendelea kupata hasara kwa Benki za Serikali

Nilibaini kuwa benki nne (asilimia 67) kati ya benki sita zinazomilikiwa na Serikali zilipata hasara kwa miaka miwili mfululizo. Kati ya benki hizo, Benki mbili (Benki ya Wanawake Tanzania (TWB), na Benki ya Twiga) zimepata hasara kwa miaka mitatu mfululizo (Angalia jedwali Na.11). Pia, nilibaini kwamba Benki ya Maendeleo ya TIB ilifuta mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 3.69 katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba 2017. Hasara hizo zinasababishwa zaidi na mapungufu katika kufanya upembuzi wa maombi ya mikopo, dhamana zisizotosheleza kudhamini mikopo na mapungufu ya ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo kwa wateja waliopitisha

muda wa kurejesha mikopo na mapungufu katika maamuzi ya mchakato wa kutoa mikopo.

Ninashaka kuwa hasara inayopatikana inapunguza mtaji wa msingi wa benki na inaziweka benki katika hatari ya kuwa na mitaji iliyo chini ya kiwango cha mtaji kinachohitajika, ambapo huweza kuzifanya benki kushindwa kurejesha amana za wateja. Pia, kuna hatari za kuzifanya benki zipate adhabu, ikiwa ni pamoja na kupokonywa leseni kutokana na mitaji kuwa chini ya kiwango kinachohitajika.

Jedwali Na. 11: Hasara za benki za serikali

| Jina la Benki | 31.12.2017 (Sh) | 31.12.2016 (Sh) | 31.12.2015 (Sh) |
|---------------------------|--------------------|--------------------|--------------------|
| TWB | (5,924,816,323) | 652,805,061) | (268,807,664) |
| Benki ya Biashara ya TIB | (8,668,389,000) | 291,841,000) | 5,302,570,000 |
| Benki ya Maendeleo ya TIB | (29,602,000,000) | (35,620,000,000) | 15,675,000,000 |
| | 31.12.2015 (Sh) | 31.12.2014 (Sh) | 31.12.2013 (Sh) |
| Benki ya Twiga | (3,459,000,000) | (13,081,000,000) | (6,953,232,000) |

Chanzo: Uchambuzi wa mkaguzi

Ninapendekeza kuwa benki ziangalie na ziongeze uwezo wa kukusanya madai ya mikopo kwa wateja, na kuwa na mifumo mizuri ya upembuzi wa maombi ya mikopo. Hii itasaidia kupunguza hatari ya utoaji wa mikopo kwa watu ambao hawarejeshi mikopo na hasara ya mikopo hiyo. Pia, waweke mikakati imara ya kufuatilia marejesho ya mikopo na mikopo chechefu. Zaidi, zihakikishe dhamana za mikopo zina bima ambapo benki zitaweza kupata marejesho yake pindi dhamana hizo zitakapoharibika. Vilevile kupitia mwenendo wa matumizi ya benki ili kupunguza matumizi hayo.

10.3 Uwiano wa Utoshelevu wa mtaji (Capital Adequacy) kuwa chini ya Kiwango cha BoT

Kanuni ya 9 (a) na (b) za benki na Taasisi za Fedha (Utoshelevu wa Mtaji) ya mwaka 2014 na mwongozo Na. FA.43/433/01/vol III wa BoT wa tarehe 5 Agosti, 2015 zinaitaka benki au taasisi

ya fedha wakati wowote kudumisha kiasi cha chini cha mtaji wa msingi na mtaji wa jumla usiopungua asilimia 12.5 na 14.5, mtawalia, wa jumla ya mali zinazoambatana na vihatarishi na mali zilizo katika hali hatarishi zilizo nje ya urari wa kimaheسابu. Kanuni ya 19 (2) za benki na Taasisi za Fedha (Maendeleo ya Uwekezaji) ya mwaka 2011 inataka Taasisi za kifedha za maendeleo wakati wowote kudumisha kiasi cha chini cha mtaji wa msingi na mtaji wa jumla usiopungua asilimia 13 na 15, mtawalia, wa jumla ya mali zinazoambatana na vihatarishi na mali zilizo katika hali hatarishi zilizo nje ya urari wa kimaheسابu.

Katika ukaguzi wa benki 6 za Serikali, nilibaini uwiano wa mtaji wa msingi na mtaji wa jumla wa benki hizo ulikuwa chini ya kiwango cha chini cha mahitaji ya mtaji kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2014 na muongozo wa BoT wa tarehe 5 Agosti, 2015. Uwiano wa mtaji wa msingi na mtaji wa jumla wa benki na mali zinazoambatana na vihatarishi na mali zilizo katika hali hatarishi zilizo nje ya urari wa kimaheسابu umetolewa katika jedwali Na.12 hapo chini:

Jedwali Na. 12: Utoshelevu wa mtaji (Capital Adequacy) wa benki za Serikali

| Maelezo | 31.12.2017 | | 31.12.2016 | |
|---|---------------------------------|-----------------------------|------------------------------|-----------------------------|
| | Mtaji wa Msingi (Sh.Miioni) | Mtaji wa Jumla (Sh.Milioni) | Mtaji wa Msingi(Sh. Milioni) | Mtaji wa Jumla (Sh.Milioni) |
| Benki ya Maendeleo ya TIB | | | | |
| Msingi na mtaji wa Jumla | 74,304 | 75,095 | 76,437 | 77,423 |
| Jumla ya mali zinazoambatana na vihatarishi | 856,702 | | 942,621 | |
| Msingi na mtaji wa Jumla Uwiano | 9% | 9% | 8% | 8% |
| Kiwango cha chini cha Msingi na Mtaji wa Jumla cha BoT uwiano | 13% | 15% | 13% | 15% |
| | Benki ya Biashara ya TIB | | | |

| | | | | |
|---|------------|-----------|------------|-----------|
| Jumla ya mali zinazoambatana na vihatarishi | 235,269 | | 179,958 | |
| Msingi na mtaji wa Jumla uwiano | 6.52% | 6.86% | 11.90% | 12.40% |
| Kiwango cha chini cha Msingi na Mtaji wa Jumla cha BoT uwiano | 12.50% | 14.50% | 12.50% | 14.50% |
| Benki ya Posta Tanzania (TPB) | | | | |
| Msingi na mtaji wa Jumla | 42,200.03 | 45,300.59 | 40,745.81 | 43,597.69 |
| Jumla ya mali zinazoambatana na vihatarishi | 350,734 | | 321,397.35 | |
| Msingi na mtaji wa Jumla uwiano | 12% | 13% | 13% | 14% |
| Kiwango cha chini cha Msingi na Mtaji wa Jumla cha BoT uwiano | 12.50% | 14.50% | 12.50% | 14.50% |
| Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) | | | | |
| Msingi na mtaji wa Jumla | (2,597.45) | (2,540) | (894.07) | (779.98) |
| jumla ya mali zinazoambatana na vihatarishi | 12,571.92 | | 19,749 | |
| Msingi na mtaji wa Jumla uwiano | -21% | -20% | -5% | -4% |
| Kiwango cha chini cha Msingi na Mtaji wa Jumla cha BoT uwiano | 12.50% | 14.50% | 12.50% | 14.50% |
| Mtaji unaotakiwa na BoT | 15,000 | | 15,000 | |
| Benki ya Twiga | | | | |
| | 31.12.2015 | | 31.12.2014 | |
| Msingi na mtaji wa Jumla | -2,597.45 | -2,540.00 | -894.07 | -779.98 |
| Jumla ya mali zinazoambatana na vihatarishi | 12,571.92 | | 19,749 | |
| Msingi na mtaji wa Jumla uwiano | -21% | -20% | -5% | -4% |
| Kiwango cha chini cha Msingi na Mtaji wa Jumla cha BoT uwiano | 12.50% | 14.50% | 12.50% | 14.50% |
| Mtaji unaotakiwa na BoT | 15,000 | | 15,000 | |

Chanzo: Uchambuzi wa mkaguzi

Nilitaarifiwa na Benki ya Biashara ya TIB kuwa Wizara ya Fedha na Mipango imeamua kuongezea benki hiyo mtaji kupitia Tasisi ya Maendeleo ya Mtaji (DFI) ya TIB ili iweze kufikia uwiano wa

kiasi cha mtaji kinachotosheleza. Benki hiyo ilisamehewa kuchukuliwa hatua na BoT, ambapo ilipaswa kuboresha mtaji wake na kufikia kiwango cha mtaji unaotakiwa kufikia mwezi Juni 2018. Pia nilitaarifiwa kuwa, Benki ya Maendeleo ya TIB imepangiwa kuongezewa mtaji wa kiasi cha Sh. bilioni 91 katika bajeti ya mwaka 2017/2018. Kiasi cha Sh. bilioni 50 kilipokelewa na Benki ya maendeleo ya TIB mwishoni mwa mwezi Disemba 2017. Kwa sasa, benki inafuatilia kiasi kilichobaki Sh. bilioni 41 toka Wizara ya Fedha na Mipango.

Kushindwa kwa benki kuzingatia kanuni zilizowekwa na BoT kunaweza kuzisababishia benki adhabu, ikiwa ni pamoja na kupokonywa leseni.

Ninapendekeza kuwa Benki zote za Serikali zipitie viwango vyao vya mitaji kwa malengo ya kuongeza kiasi cha mtaji ili kudumisha kiwango cha chini cha mtaji kinachotakiwa; zifuatilie na kuhakikisha Wizara ya Fedha na Mipango inaongeza mitaji; zifanye uchambuzi ilikujua sababu za mmomonyoko wa mitaji yao na kuweka mikakati ya kurejesha uwiano wa mtaji unaohitajika na BoT. Pia, wafanye mapitio ya mwenendo wa Benki ya Wanawake (TWB), madeni na mali zake kwa malengo ya kusaidia kuiunganisha na TPB.

10.4 Mapungufu ya Ufuatiliaji kikomo cha Mikopo (Overdraft Facility)

Taarifa za mikopo ya Benki ya Biashara ya TIB zilionesha kwamba mikopo sita (Overdraft) ilikuwa imepita muda wake; na kiasi kilichokopeshwa kilikuwa kimezidi kikomo kilichowekwa. Jumla ya kiasi cha mikopo (overdraft) 6 ilikuwa Sh. bilioni 27.54 ikilinganishwa na kikomo kilichoidhinishwa cha Sh. bilioni 24.92. Ninaamini kwamba, mapungufu yaliyobainika yanasababishwa na ukosefu wa ufanisi wa mapitio na ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo hiyo. Benki imejiweka katika hali ya hatari ya kuongezeka kwa madeni chechefu, ambapo mkopaji anaweza kushindwa kulipa kwa kiasi kikubwa na kushindwa

kuhuisha mkopo uliopo (overdraft) na kusababisha kwa benki kufuta au kupunguza thamani ya mkopo huo.

Pia, nilibaini mfumo wa Benki (Core Banking System) ya Posta Tanzania (TPB) ulishindwa kubaini matukio matatu ya wateja kutoa pesa zaidi ya kiwango kilichowekwa. Jumla ya pesa zilizotolewa zilikuwa ni Sh. milioni 576.83 dhidi ya ukomo wa mkopo wa mfumo Sh. milioni 330. Pia, kitabu cha mkopo kinaonesha kiasi cha Sh. milioni 330 cha mkopo (overdraft) kilikua hakijakusanywa tangu mwaka 2009. Menejimenti wanaona kiasi hicho hakitoweza kukusanywa. Hata hivyo walishindwa kuelezea kwanini walishindwa kukusanya kiasi hicho. Kushindwa kukusanya marejesho kunaiweka benki katika hali ya hatari ya kupata hasara.

Ninapendekeza kuwa Benki ya Biashara ya TIB na Benki ya Posta Tanzania zifuatilie kwa ukamilifu mikopo (overdraft) kuhakikisha wananchi wote wanapata mikopo ndani ya kikomo kilichowekwa; wazidishe uhibitaji wa mifumo kuhakikisha mkopo (Overdraft) hauzidi kikomo kilichowekwa, pamoja na kuhakikisha urejeshaji wa mikopo unafanyika kwa wakati.

10.5 Mikopo Chechefu (Non Performing Loan)

Mikopo Chechefu (NPL) ni mikopo ambayo wadaiwa wameshindwa kulipa riba au marejesho ya mkopo ndani ya siku 90. Ukaguzi wa mikopo ya benki zinazomilikiwa na Serikali ulibaini kuongezeka kwa mikopo iliyopo katika hali ya hatari kwenye benki tano kati ya sita. Uwiano wa mikopo chechefu dhidi ya mikopo yote umekuwa ukiongezeka zaidi ya kiwango cha asilimia 11.7 ilivyoainishwa katika sera ya Fedha ya BoT ya mwezi Februari 2018 na lengo la BoT la asilimia 5. Jedwali Na. 13 hapo chini linaonesha mikopo chechefu:

Jedwali Na. 13: Mikopo chechefu ya benki zinazomilikiwa na Serikali

| Jina la Benki | 30.06.2017 | Jumla ya Mikopo | Asilimi a ya Mikopo | 30.06.2016 | Jumla ya mikopo | Asilimi a ya Mikopo |
|----------------------------------|-------------------------------|-----------------|---------------------|-------------------------------|-----------------|---------------------|
| | (Mikopo chechefu Sh. Milioni) | (Sh. Milioni) | | Mikopo chechefu (Sh. Milioni) | | |
| Benki ya Maendeleo ya TIB | 237,345 | 751,572 | 32% | 265,375 | 809,009 | 33% |
| Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) | 8,017 | 22,548 | 36% | 10,504 | 25,774 | 41% |
| Benki ya Biashara ya TIB | 6,672 | 136,231 | 5% | 63 | 104,964 | 0.06% |
| TPB | 21,131 | 344,469 | 6% | 12,420 | 307,238 | 4.04% |
| TADB | 1,135 | 11,621 | 10% | 1,081 | 3,969 | 27% |

Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi kutoka katika mahesabu ya fedha ya mwaka 2016 na 2017

Pia, nilipitia uwiano wa mikopo iliyo katika hali ya hatari ambayo haijakusanywa kati ya kipindi cha siku 30 mpaka 90. Nilibaini kuwa Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) na Benki ya Biashara ya TIB zina kiasi kikubwa cha mikopo iliyo katika hali ya hatari ya asilimi 9 na 22, mtawalia (angalia Jedwali Na.14). Ni maoni yangu kuwa, Serikali inapaswa iandae mpango ambao utasaidia kupunguza kiasi cha mikopo chechefu na mikopo iliyo katika hali ya hatari ya Benki ya Biashara ya TIB na Benki ya Maendeleo ya TIB.

Jedwali Na. 14: Mikopo iliyopo katika hali ya hatari kati ya kipindi cha siku 30 mpaka 90

| Jina la benki | Mikopo iliyozidi siku (>30 mpaka < 90) Milioni | Jumla ya Mikopo (Milioni) | Asilimia | Mikopo iliyozidi siku (>30 mpaka < 90) Milioni | Jumla ya Mikopo (Milioni) | Asilimia |
|--------------------------|--|---------------------------|----------|--|---------------------------|----------|
| TWB | 1,939.02 | 22,548.07 | 9% | 3247.58 | 25,774 | 13% |
| Benki ya Biashara ya TIB | 50,403.09 | 224,171.45 | 22% | 6325.68 | 196,396 | 3% |

Chanzo: Mahesabu ya fedha ya mwaka 2017

Ninapendekeza kuwa benki ziongeze upembuzi kabla ya kutoa mikopo. Aidha, usimamizi, ufuatiliaji na mikakati ya

ukusanyaji wa marejesho uimarishwe zaidi, kumbukumbu za taarifa za mikopo ziboreshe. Pia, Benki ziboreshe mikakati ya kupunguza uwiano wa mikopo chechefu na mikopo iliyo katika hali ya mashaka kupungua zaidi ya 5% iliyowekwa na BoT.

10.6 Kutokutosheleza kwa dhamana za Mikopo

Tarehe 31 Desemba 2017, Benki ya Maendeleo (TIB) ilikuwa na mikopo mikubwa zaidi ya asilimia 25 ya mtaji wa msingi; na ilidhaminiwa kwa dhamana yenye thamani chini ya asilimia 125 ya mkopo. Hii ni kinyume na Kanuni ya 29 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2011 inayotaka dhamana kuwa zaidi ya asilimia 125 ya mkopo endapo mkopo utakuwa zaidi ya asilimia 15 ya mtaji wa msingi. Pia, nilibaini mikopo ambayo haikudhaminiwa kwa wakati ni zaidi ya asilimia 5 ya mtaji wa msingi, kinyume na kanuni iliyotajwa hapo juu.

Menejimenti ilieleza kwamba, baadhi ya dhamana zilikuwa na thamani zinazotosheleza pindi mikopo husika ilipoidhinishwa ila thamani ya dhamana hizo imekuwa ndogo ikilinganishwa na kiasi cha mikopo husika kutokana na kuongezeka kwa riba na adhabu. Jedwali Na.15 hapo chini linaonesha tofauti kati ya mikopo na dhamana. Kutokutosheleza kwa dhamana ya mikopo kunaongeza hatari ya hasara kwa benki ikiwa mkopaji atashindwa kulipa.

Jedwali Na. 15:Kutokutosheleza kwa dhamana na mikopo

| Jina la mteja | Mkopo 31 Desemba 17 Sh. '000 | Dhamana Sh.'000 | Mtaji wa Msingi Sh.' 000 | % Mkopo kwa mtaji wa msingi | % Dhamana kwa Mkopo |
|----------------------|------------------------------|-----------------|--------------------------|-----------------------------|---------------------|
| CATA Mining Co. Ltd | 53,342,466 | 30,405,615 | 74,304,000 | 72 | 57 |
| Parrot Hotel Limited | 27,163,509 | 25,800,615 | 74,304,000 | 37 | 95 |
| Rialma Co. Ltd | 11,303,874 | 13,386,357 | 74,304,000 | 15 | 118 |
| TANESCO | 34,156,846 | - | 74,304,000 | 46 | 0 |

| | | | | | |
|------------------------------|-----------|-----------|------------|----|----|
| Manawa Ginneries Co. Limited | 8,194,393 | 7,260,000 | 74,304,000 | 11 | 89 |
| Nsagali Co. Limited | 6,223,770 | - | | 8 | 0 |

Chanzo: Uchambuzi wa mkaguzi

Ninapendekeza kuwa Benki ianzishe mfumo stahiki ambao utahakikisha thamani ya dhamana iliyowekwa na mteja inathaminishwa mara kwa mara; na nyongeza ya dhamana inaombwa kutoka kwa mteja ili iweze kuendana na kiasi cha mkopo kilichoongezeka kutokana na riba na adhabu.

- 10.7 Kupungua kwa Ukwasi kwa Benki zinazomilikiwa na Serikali**
Katika ukaguzi wangu wa muda wa kuiva kwa amana nilibaini kiasi kikubwa cha amana katika Benki ya Maendeleo ya TIB cha wateja na benki nyiginezo kinachotia mashaka ya kutolipwa pindi amana hizo zitakapoiva kutokana na tatizo la ukwasi linaloikabili benki hiyo. Kwa mfano, nilibaini kati ya amana zenye thamani ya Sh. bilioni 199 ambazo ni za kipindi kisichozidi mwezi mmoja, amana zenye thamani ya Sh. bilioni 88 zilikuwa zimeiva ndani ya mwaka mzima lakini Benki ilishindwa kulipa amana hizo. Muda wa kuiva kwa amana za wateja na benki nyinginezo katika Benki ya Maendeleo ya TIB hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2017 unaelezewa katika Jedwali Na 16:

Jedwali Na. 16:Kupungua kwa Ukwasi kwa Benki zinazomilikiwa na Serikali

| Muda wa amana | Kiasi (Sh. '000) |
|------------------------|------------------|
| Chini ya mwezi mmoja 1 | 199,367,035 |
| Miezi 1 - 3 | 124,619,815 |
| Miezi 4 - 6 | 27,573,042 |
| Miezi 6 - 12 | 49,239,573 |
| Zaidi ya miezi 12 | 41,971,536 |

Chanzo: Taarifa ya Mahesabu ya Fedha ya Benki ya Maendeleo ya 2017

Kuna mashaka kwamba, Benki itashindwa kulipa amana zilizoiva na kusababisha hatari ya kutoaminika.

Ninapendekeza kuwa Benki ya maendeleo TIB iangalie muda na kiasi cha amana ili iandae mkakati wakupata amana za muda mrefu kama inavyohitajika na BoT.

10.8 Mapungufu Katika Utoaji wa Mikopo

10.7.1 Kukosekana kwa Mgawanyo wa kazi wakati wa kutoa mikopo
Katika Benki ya Posta Tanzania (TPB) nilibaini jumla ya mikopo 1270 yenye thamani ya Sh. bilioni 4.82 ilitengenezwa na kutolewa na mtu mmoja katika mwaka wa fedha wa 2017, kinyume na aya 3.2.3 (b) ya Mwongozo wa Ukopeshaji wa Benki ambayo inataka kuwepo kwa mgawanyo wa kazi kati ya mtu anayeandaa mikopo na mtu anayetoa mikopo katika mfumo wa Benki. Kutokuwepo kwa mgawanyo wa kazi katika mchakato wa kutoa mikopo kunaongeza hatari ya wafanyakazi wasio waaminifu kutoa mikopo kwa maslahi binafsi na kusababisha benki kupata hasara.

10.7.2 Mapungufu katika Mabadiliko ya Makubaliano ya Mkopo

Pia, katika Benki ya Posta Tanzania (TPB) nilibaini mikopo ya wateja wawili yenye thamani ya Sh. milioni 206.09 ambapo tarehe zao za marejesho ya mikopo zilibadilishwa bila idhini ya Kitengo cha Tahadhari na Mikopo kama inavyotakiwa na aya ya 7.8.2 ya Mwongozo wa Ukopeshaji wa Benki. Pia, hapakuwapo na mtu wa pili wa kuangalia na kuidhinisha mabadiliko ya tarehe za marejesho ya mikopo katika mfumo wa benki. Zaidi, mikopo ya aina tano yenye thamani ya Sh. milioni 333.34 iliandaliwa katika mfumo wa benki kwa ajili ya mfanyakazi mmoja wa benki kwa siku moja (19 Julai 2017) na hapakuwa na ushahidi wa kuidhinisha mikopo hiyo.

Kushindwa kudhibiti kubadilishwa kwa tarehe za marejesho ya mikopo kunaweza kusababisha kubadilishwa tarehe ya mkopo

kwa ajili ya kumnufaisha mtu. Pia huweka benki katika hatari ya kupata hasara.

Ninapendekeza kuwa TPB kuweka udhibiti wa kimumo kuzuia mtu mmoja kuweza kuandaa na kulipa mkopo. Pia, kuhakikisha kunakuwapo na idhini kabla ya kubadilisha tarehe ya kufanya marejesho na kutoa mikopo.

10.8 Kuungana kwa Benki za Serikali

Katika kipindi cha mapitio, nilibaini benki mbili za Serikali (Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) na Benki ya Twiga) ambazo ziliruhusiwa na BoT kuungana na Benki ya Posta Tanzania (TPB) kutokana na mwenendo usioridhisha wa kifedha na mitaji yao kuwa chini ya kiwango kinachohitajika. Benki hizo mbili (TWB na Benki ya Twiga) zimepata hasara kwa miaka mitatu mfululizo; na kuwa na mtaji wa msingi hasi wa Sh. bilioni 2.56 na hasi Sh. bilioni 20.63, mtawalia, ikilinganishwa na kiasi cha mtaji unaohitajika wa Sh. bilioni 15.00. Kuungana kwa benki kuliidhinishwa ili kusaidia ufanisi, uangalizi na mwenendo mzuri wa benki ya Serikali.

Benki ya Twiga iliidhinishwa kuungana na TPB tarehe 17 Mei 2018; na TWB iliidhinishwa kuungana na TPB tarehe 3 Agosti 2018. Benki ya Twiga ina uwiano hasi wa asilimia 52.74 na hasi 50.69 wa mtaji wa msingi na wa mtaji wa jumla mtawalia, wakati TWB ina uwiano hasi wa asilimia 21 na hasi 20 wa mtaji wa msingi na mtaji wa jumla, mtawalia, kwa jumla ya mali zinazoambatana na vihatarishi na mali zilizo katika hali hatarishi zilizo nje ya urari wa kimahesabu.

Pamoja na makusudio ya kuunganisha benki hizo na TPB kuwa mazuri, changamoto zilizokuwapo kwenye benki hizo zinaweza zisionekane kwa sasa kutokana na mwenendo mzuri wa TPB lakini badaye zinaweza kusambaa na kuathiri mwenendo wa TPB. Pia, ni ukweli kwamba benki hizo zimeungana na TPB wakati zikiwa zinapata hasara hivyo zinaweza kuathiri mtaji na

mwenendo wa benki ya TPB baada ya kuungana, hii ina maana kuwa hatari ya akiba ya wateja kuongezeka.

Ninapendekeza kuwa Serikali ifuatilie kwa ukaribu mwenendo wa benki ya TPB baada ya kuungana na TWB na Benki ya Twiga ili kuepusha kudidimia kwa TPB baada ya kuungana. Serikali inapaswaihakikishe kuwa mapungufu ya TWB na Benki ya Twiga hayaiathiri TPB.

SURA YA KUMI NA MOJA

UTENDAJI KATIKA MIFUKO YA HIFADHI YA JAMII

11.0 Utangulizi

Mifuko ya hifadhi ya jamii ilianzishwa kwa madhumuni ya kutoa mafao kwa wanachama wa mifuko na jamii kwa ujumla. Hapa nchini Mifuko ya hifadhi ya jamii inasimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa mifuko ya hifadhi ya jamii.

Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa mifuko ya hifadhi ya jamii ilianzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi, Sura ya 135 (iliyorekebishwa 2015) kwa lengo la kusimamia sekta ya mifuko ya hifadhi ya jamii na mambo yanayohusiana na hayo. Mamlaka ilianza kazi 2010. Mamlaka ina majukumu muhimu katika kusimamia na kutoa miongozo katika mifuko, ikiwamo mafao ya afya na mafao ya uzeeni.

Fao la afya linatoa nafasi katika eneo zima linalohusiana na afya. Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulianzishwa chini ya sheria namba 8 ya mwaka 1999 Sura ya 395 ili kuhakikisha huduma bora za afya zinapatikana kwa waajiriwa wote wa serikalini, taasisi binafsi na makundi mengineyo.

Mifuko ya jamii ina lengo la kuwawezesha watu kuishi kwenye maisha ya utu na kumudu gharama hata baada ya matukio ya majanga ya kijamii na kiuchumi ambayo yanasababisha kusitishwa kwa kipato. Majanga hayo ni kama vile kifo au ulemavu. Mifuko ya hifadhi ya jamii husaidia pia kwenye kupungua kwa kipato kutokana na kustaafu, uzazi au ugonjwa.

Mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2018, Tanzania ilikuwa na mifuko mitano ya hifadhi ya jamii ambayo ni: Mfuko wa Hifadhi kwa Watumishi wa Umma (PSPF), Mfuko wa Pensheni wa LAPF, Mfuko wa Pensheni wa PPF, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Mfuko wa Pensheni wa GEPF. Hata hivyo, chini ya muundo mpya wa mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Mifuko iliunganishwa chini ya kifungu cha sheria namba 2 ya mwaka

2018 na kutengeneza mfuko mmoja uitwao “Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma” (PSSSF). Mfuko mpya umeanza kazi tarehe 1 mwezi Augosti mwaka 2018.

Sura hii inaonesha mapungufu yaliyomo kwenye mfuko wa fidia kwa wafanyakazi, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na mifuko ya Pensheni. Pia inaonesha mapungufu kwa Mamlaka ya Usimamizi wa mifuko hii (SSRA).

Vile vile inahusisha muhtasari wa mapendekezo kwa ajili ya kuboresha utendaji wa Taasisi. Ni matumaini yangu kuwa, baada ya mifuko kuunganishwa mapendekezo niliyoyatoa yatafanyiwa kazi na mfuko mpya wa PSSSF. Zifuatazo ni hoja na mapendekezo yangu juu ya hali ya uendeshaji wa Mifuko:

11.1 Deni la Serikali wanalodaiwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Sh. bilioni 2,390.08

Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii ina madai makubwa ambayo ni chechefu, mengi ya madeni haya ni ya Serikali na taasisi zake. Mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2018, zaidi ya asilimia 68 ya madeni ya Serikali na taasisi zake yalikuwa bado hayajalipwa kwa Mifuko ya NSSF na NHIF; na tarehe 31 Julai 2018 kwa madeni ya LAPF, PPF, GEPF and PSPF. Baadhi ya mikopo ilikuwa imeiva tangu 2014. Hali hii inasababisha Mifuko kuwa katika hali ya ukata kiasi cha kukwaza utekelezaji wa majukumu yake. Deni ambalo Serikali inadaiwa na mifuko ya hifadhi limefikia Sh. bilioni 2,390.08 kama linavyoainishwa kwenye Jedwali Na.17 hapa chini:

Jedwali Na. 17: Madeni ya Serikali kwa Mifuko ya Hifadhi ya jamii kwa mwaka 2018

| Mifuko ya Hifadhi ya Jamii | Deni la serikali Sh (Bilioni) |
|----------------------------|-------------------------------|
| LAPF | 169.64 |
| NSSF* | 1,253.19 |
| PPF | 292.11 |
| GEPF | 10.04 |
| PSPF | 448.9 |
| NHIF** | 216.20 |

| | |
|-------|----------|
| Jumla | 2,390.08 |
|-------|----------|

*Deni la NSSF pia linajumuisha kiasi cha Sh. bilioni 127.89 ambacho Serikali ilipaswa kuchangia katika ujenzi wa Daraja la Kigamboni.

**Mkopo kutoka Mfuko wa NHIF unajumuisha Sh. billioni 115.11 ambazo waliwapatia Chuo Kikuu cha Dodoma kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya kwa ajili ya mafunzo (Awamu ya kwanza na ya pili). Mkopo huu haukuwa na dhamana kutoka Serikalini wala hapakuwa na makubaliano ya kisheria. Ni muhimu sana kwa mikopo hii kurejeshwa kwa wakati ili mifuko iweze kujiendesha na kutimiza malengo yake, ikiwamo kulipa mafao ya wastaafu.

Kwa ajili ya uhakika na uendelevu wa mifuko, napendekeza Serikali na Taasisi zake kulipa kiasi wanachodaiwa kwa wakati ili kuisaidia mifuko kufikia malengo yake.

11.2 Kuwepo kwa hundi zilizochacha Sh. milioni 836.80

Wakati wa ukaguzi niligundua kuwa, hundi zilizolipwa na wachangiaji kwenye mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja ambazo zilikuwa na jumla ya Sh.milioni 836.80 zilikataliwa na Benki husika kutokana na taasisi husika kutokuwa na fedha za kutosha kwenye akaunti zao.

Hadi kufikia Juni 2018, katika mfuko wa LAPF kulikuwa na hundi zilizochacha za kiasi cha Sh. milioni 74.93 kilichotokana na malimbikizo ya nyuma tangu mwaka 2012. Kwa WCF na GEPF, hundi zilizochacha zilikuwa Sh. milioni 412.84 na Sh. milioni 349.03 ambazo zilikuwa hazijalipwa kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja. Kwa GEPF, hundi zisizolipwa hesabu yake ilibadilishwa na kuwa madeni ya michango kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 2017 na hesabu za mwaka wa fedha ulioishia Juni 2018 deni liliondolewa bila kuwa na maelezo. Kadri madeni haya yalivyokaa kwa muda mrefu bila kulipwa, ndiyo uwezo wa mifuko katika kujiendesha unazidi kudhoofika.

Napendekeza menejimenti za mifuko zichukue hatua za haraka kwenye ukusanyaji wa madeni hayo, na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya watakaoshindwa kulipa.

11.3 Ucheleweshaji wa Urejeshwaji wa Malipo Yaliyofanyika Kimakosa zaidi ya mara moja kwa Wastaafu - Sh.Milioni 218.31

Niligundua kwamba, LAPF ilifanya malipo kimakosa kwa wastaafu 15 kwa kiasi cha Sh.milioni 235.82 kama mafao ya kustaafu huku tayari Hazina ilikuwa imeshafanya malipo kwa wastaafu hao.

LAPF iliamua kuwakata kutoka kwenye mafao yao ya kila mwezi. Mpaka sasa ni kiasi cha Sh. milioni 12.92 (asilimia 6) tu ndicho kimerudishwa kutoka kwenye makato ya mwezi ya wastaafu hao.

Kwa mwendo huu, inaonesha mfuko utatumia miaka 136 ili kuweza kupata salio lililobaki. Napendekeza Mfuko utumie mbinu nyingine ili uweze kupata kiasi chake kilichobaki.

11.4 Watumishi Waliotoka Kazini Bila Kulipa Mikopo yao kwa Mifuko Sh. Milioni 821.82

Mifuko ya hifadhi inatoa mikopo kwa waajiriwa wake, ambapo wanatakiwa kuirejesha mikopo hiyo kabla ya kutoka kazini.

Hata hivyo, niligundua kuwa katika mifuko ya NHIF, LAPF na GEPF kuna watumishi ambao wameondoka kazini bila ya kulipa salio la mikopo yao. Kiasi cha mikopo ambacho hakijarejeshwa katika mifuko hiyo ni Sh. milioni 115.47, milioni 539.22, na milioni 167.13 kwa NHIF, LAPF na GEPF, mtawalia. Kwa LAPF na GEPF tayari kuna hatua zimeshachukuliwa ili kuweza kurejeshwa kwa mikopo hiyo, lakini hakuna uthibitisho wa hatua zilizochukuliwa na NHIF.

Napendekeza mifuko iongeze nguvu na bidii dhidi ya wale wote ambao walikuwa hawajalipa mikopo kipindi wanaondoka ndani

ya mifuko; na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya watakaoshindwa kurejesha mikopo yao.

11.5 Tathmini ya hali Mifuko

Ripoti ya tathmini ya mifuko kuhusu uwezo wa kipato na matumizi kwa baadaye katika mifuko ya PSPF, PPF na LAFI inaonesha hali ya kupungukiwa uwezo wa kujiendesha. Ikifananihwa na mifuko mingine, hali ya mfuko wa PSPF katika kujiendesha upo chini ya kiwango kinachotakiwa.

Kufuatia kuunganishwa kwa mifuko ya hifadhi ya jamii na kuundwa kwa mfuko mpya wa PSSSF uwezo mdogo wa kujiendesha uliobainika utasababisha kuuweka kwenye hatari mfuko mpya kuweza kutimiza majukumu yake kama vile kulipa mafao, kumudu gharama za uendesaji. Zaidi, hata uwekezaji mwingine uliofanyika kuwa hatarini.

Jedwali Na. 18: Uwezo wa mifuko iliyounda PSSSF

| Jina la Mfuko | Tarehe ya tathmini | Mtathmini | Mali za Mfuko (A) | Madeni ya Mfuko (B) | Uhafifu | Uwezo wa kujiendesha (A/B) |
|---------------|--------------------|-------------------------------------|-------------------|---------------------|--------------|----------------------------|
| | | | Sh 'Bilioni' | Sh 'Bilioni' | Sh 'Bilioni' | Sh 'Bilioni' |
| PSPF | 30.6.2014 | Muhana &Co Actuaries | 1,306.71 | 12,460.22 | 11,153.51 | 10.5% |
| PPF | 30.6.2017 | Argen Actuarial Solutions | 2,429.00 | 3,411.00 | 982.00 | 72.2% |
| LAFI | 30.6.2016 | Alexander Forbes Financial Services | 1,169.10 | 2,688.20 | 1,519.10 | 43.5% |
| GEPI | 30.6. 2015 | Muhana &Co Actuaries | 336.27 | 536.15 | 199.88 | 62.7%. |

Chanzo: Taarifa za fedha

Napendekeza PSSSF waangalie namna nyingine za kuweza kutatua changamoto ya kiwango cha kujiendesha.

11.6 Ongezeko la watu wanaojitoa na wanaostaafu mapema

Fao la kujitoa linalipwa kwa mwanachama ambaye atasitisha ajira yake kwa namna yoyote, na ambaye hajafikia kiwango cha kulipwa mafao ya uzeeni. Ustaafu wa mapema ni kwa mwanachama anayeamua kwa hiari katika umri wa miaka 55 kabla ya kufikia umri wa kustaafu kwa lazima wa miaka 60.

Katika mifuko ya LAF, PPF na PSPF niligundua kuna ongezeko la malipo kwa wanufaika la Sh. bilioni 1,951.78 sawa na asilimia 44.31, ndani ya mwaka huu wa ukaguzi kutoka Sh. bilioni 1,352.48 kwa mwaka jana. Ongezeko la malipo limetokana na kuongezeka kwa wanachama wanaojitoa kutoka 2,562 kwa mwaka 2017 mpaka 4,730 kwa mwaka unaoishia Juni 2018. Hii imesababisha kuongezeka kwa malipo ya fao la kujitoa pamoja na wastaafu wa mapema kutoka Sh. bilioni 21.52 na Sh. bilioni 158.05 kwa mwaka 2017 mpaka Sh. bilioni 53.59 na Sh. bilioni 325.55 kwa mwaka 2018, mtawalia.

Kuongezeka kwa idadi ya wastaafu wa mapema na wale wa fao la kujitoa kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuwapo kwa kanuni mpya ya kikokotoo ambayo wanadhani haiwanufaishi. Hili litasababisha kuathirika kwa mtiririko wa ukwasi katika mfuko. Pia niligundua uwiano wa mwaka wa mafao na michango kuwa ni asilimia 123.51 ikilinganishwa na asilimia 92.55 kwa mwaka ulioisha, ambapo inaonesha kupungua kwa mtiririko wa ukwasi katika mifuko.

Jedwali Na 19 linaonesha malipo ya mafao, idadi ya wanufaika na uwiano wa mafao na michango kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia 31 Julai 2018.

Jedwali Na. 19: Michango na Malipo ya Mafao

| Jina la mfuko | Mwaka | Michango (Sh. bilioni) | Mafao- (Sh. bilioni) | Kujit o a (Sh. bilioni) | Kustaafu mapema- (Sh. bilioni) | Mafao/M ichango (%) |
|---------------|-----------|------------------------|----------------------|-------------------------|---------------------------------|---------------------|
| LAF | 31-Jul-18 | 341.1 | 233.25 | 39.43 | 40.43 | 68.38% |
| | 30-Jun-17 | 291.29 | 140.49 | 16.37 | 19.62 | 48.23% |

| | | | | | | |
|------|-----------|--------|----------|-------|--------|------|
| PSPF | 31-Jul-18 | 815.40 | 1,383.19 | 1.78 | 263.10 | 170% |
| | 30-Jun-17 | 771.35 | 988.70 | 1.21 | 118.29 | 128% |
| PPF | 31-Jul-18 | 423.81 | 335.34 | 12.38 | 22.02 | 79% |
| | 30-Jun-17 | 398.78 | 223.29 | 3.94 | 20.14 | 56% |

Chanzo: Taarifa za fedha

Napendekeza PSSF kuja na majibu ya haraka yatakayoelezea masuala yote yanayohusiana na mabadiliko ili kuepusha kujitoa kwa mapema au kustaafu kwa hiari.

11.7 Mgogoro wa Ardhi na ukosefu wa hati ya umiliki

Mifuko ya hifadhi ya Jamii inanunua ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Hata hivyo, mifuko imejikuta ikiingia kwenye migogoro ya ardhi kutokana na kuvamiwa na wenyeji wa eneo husika au kutokana na ukosefu wa hati miliki.

Mfuko wa PSPF ulinunua viwanja 100 kwa ajili ya uwekezaji katika eneo la Mangamba mkoani Mtwara. kati ya hivyo, viwanja 50 vilichukuliwa na wakazi wa eneo lile. Hali hii iliulazimu Mfuko kuomba tena Viwanja kwa uongozi wa halmashauri ya Manispaa ya Mtwara, ambapo Mfuko ulipatiwa viwanja vingine 50 katika eneo la Mitengo na tayari baadhi ya viwanja katika eneo la Mitengo; vimevamiwa. Kwa mujibu wa taarifa ya meneja wa mkoa, suala hili litasuluhishwa mara tu baada ya viwanja kukabidhiwa kwa PSPF.

PSPF pia wamenunua viwanja na baadhi ya viwanja vina majengo katika Mkoa ya Tabora na Shinyanga lakini bado taarifa za umiliki zinaonesha majina ya wamiliki wa awali. Pia PSPF hawana hati miliki za viwanja 277 vilivyonunuliwa mwaka 2008, vilivyopo eneo la Kiseke mkoani Mwanza. Imeelezwa sababu kubwa ya kuchelewa kupatikana kwa hatimiliki ni kubadilishwa kwa uongozi na mamlaka za mipaka ya kiutawala kutoka Mwanza Manispaa kwenda Manispaa ya Ilemela.

Wakati nilipotembelea eneo la Kiseke niligundua mapungufu mengi, yakiwamo kutokuwa na alama za mipaka, usimamizi

hafifu wa wavamizi na hata kuwapo kwa majengo na mashamba ya wavamizi. Kukosekana kwa hati kunasababisha mifuko kuwa katika hatari ya kupoteza umiliki pindi ikitokea mtu atakayejitokeza kuwa na nyaraka zinazomuonesha yeye kuwa mmiliki wa eneo.

Migogoro ya ardhi inarudisha nyuma malengo ya Mfuko. Hivyo basi, napendekeza Menejiment ya Mfuko kuhakikisha inapata hati halali za umiliki. Pia, iwaondoe wavamizi wote kwenye maeneo yake.

11.8 Hati hati ya upatikanaji wa marejesho ya Fedha ya Amana Sh. Bilioni 123.7

Mifuko ya hifadhi inawekeza kwenye mabanki katika mtindo wa Amana ya kudumu kwa lengo la kupata riba. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi nilibaini yafuatayo:

LAPF, GEPF, WCF na Ubungo Plaza wana amana za kudumu ndani ya Benki M ambayo kwa sasa ipo chini ya uangalizi wa Benki Kuu ya Tanzania kutokana na changamoto kubwa ya ukata inayoikabili. Kutokana na changamoto hiyo, ninapendekeza Mifuko iwasiliane na Benki Kuu ya Tanzania ili kuweza kujua namna wanavyoweza kurejesha amana zao.

GEPF na WCF waliwekeza kiasi cha Sh. bilioni 1 na bilioni 2.15 mtawalia kwenye Benki ya Wanawake ya Covenant Tanzania, ambapo leseni ya biashara ya Benki hiyo ilishafungiwa na Benki Kuu ya Tanzania kutokana na changamoto za mtaji wa kujiendesha. Mnamo tarehe 27 Aprili 2018 GEPF walipokea kiasi cha Sh. milioni 1.5 kutoka Bodi ya Bima ya dhamana kama fidia ya Bima ya dhamana ya uwekezaji kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mabanki na Taasisi za Kifedha ya mwaka 2006. Hatima ya pesa iliyowekezwa itategemeana na Sheria ya Ufilisi.

Mpaka kufikia tarehe 31 Julai 2018, PPF na GEPF walikuwa na amana ya kudumu ya Sh. bilioni 65.38 kwenye Benki ya

Uwekezaji. Kulingana na hali ya kifedha ya Benki kushindwa kulipa riba, Mifuko iliamua kukirejesha katika uwekezaji wa amana kiasi cha Sh. bilioni 45.1 ambacho ilikuwa kimeiva ndani ya mwaka wa ukaguzi. Hii inaleta shaka juu ya urejeshwaji wa kiasi hicho cha fedha kutoka kwenye Benki hiyo.

Napendekeza kuwa, Mifuko ichukue hatua stahiki juu ya urejeshwaji wa kiasi hicho cha Fedha.

11.9 Kutofanya Vizuri kwa Kampuni Tanzu Zinazomilikiwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Baadhi ya Kampuni tanzu zinazomilikiwa na mifuko ya hifadhi ya jamii haifanyi vizuri kama ilivyokusudiwa. Kampuni hizo ni kama vile Mkulazi na Mzizima ambapo hata uwekezaji uliopo katika Kampuni ya Ubungo Plaza Ltd imebainika pia kuwa haufanyi vizuri.

Kwa mujibu wa ripoti ya utekelezaji ya Kampuni ya Mkulazi ambayo imeundwa kwa ushirika wa NSSF na PPF, Kampuni ilitegemea kusimika mitambo mwezi Januari 2018 na kumalizika mwezi Juni 2018 na uzalishaji wa sukari uanze mwezi Septemba 2018.

Kampuni ya Mkulazi ilipanda miwa hekta 1000 kati ya hekta 4,856 ndani ya Shamba la Mibigirina. Walitarajia kuvuna mnamo mwezi wa Agosti 2018. Pia, wakulima wadogo, kupitia mikopo waliyoipata kutoka Benki ya Azania walilima jumla ya ekari 645; ambapo walitegemea kuuza miwa hiyo kwa kampuni ya Mkulazi ili kufanya marejesho kwa mikopo waliyoichukua. Mpaka kipindi natembelea shamba hilo kwa ajili ya ukaguzi hakukuwa na mashine zozote zilizosimikwa.

LAPF na Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam waliingia ubia na kuunda kampuni iitwayo Mzizima Properties kwa ajili ya mradi wa stendi ya malori katika eneo la Mbezi Louis kitalu namba 109 'A' chenye ukubwa wa hekta 3.89. LAPF wanamiliki

asilimia 60 za hisa; na tayari wameshatoa kiasi cha Sh. milioni 692.25 kwa ajili ya kuwalipa fidia wamiliki wa eneo hilo.

Baadaye LAPF walijitoa kutoka kwenye ubia huo kwa hoja kuwa, Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam imemuingiza mbia mwingine na kumchagua mshauri mwelekezi wa mradi bila kuishirikisha LAPF. Mwishoni walikubaliana kuivunja Kampuni; hivyo Halamashauri ya Jiji kutakiwa kurejesha Sh. 40,000 kwa kila mita moja ya mraba. Jumla ya Sh. milioni 975.73 zinatakiwa kurejeshwa.

Ubungo Plaza inamilikiwa na NSSF kwa asilimia 35, PSPF asilimia 35 na Shirika la Bima la Taifa kwa asilimia 30. Niligundua kuwa ndani ya jengo kuna maegesho; ambapo malipo yanafanywa kwa mfumo maalum na umefanya kazi kwa hasara ya Sh. milioni 10.63 kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 2018 na hasara ya Sh. milioni 31.91 kwa mwaka 2017. Vifaa mbalimbali ndani ya jengo la Ubungo Plaza, vikiwamo mapambo, urembo na mabomba, havipo katika hali nzuri kutokana na kuathiriwa na chumvi na kutu ambayo itasababisha kuharibika kabisa kama hatua za haraka hazitochukuliwa. Kwa miaka miwili mfululizo (2017 na 2018), Ubungo Plaza Limited ilitumia Sh. milioni 721.95 kwa ajili ya huduma za kisheria. Hii ni kwasababu kampuni haina mwanasheria. Pia, kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 2018, niligundua kuwepo kwa deni toka kwa wadaiwa mbalimbali kiasi cha Sh. bilioni 7.55. Asilimia 86.09 ya deni hilo lilitokana na malimbikizo kutoka hoteli ya Blue Pearl Hotel & Apartments iliyoondolewa ndani ya jengo mnamo tarehe 9 Novemba 2017.

Mapendekezo yangu kwa Mifuko ni kuhakikisha uwekezaji unaendeshwa kama ilivyotarajiwa. Aidha, kiasi cha fedha kutoka kampuni ya Mzizima Properties Limited na zile za kutoka Blue Pearl Hotel & Apartments zinarejeshwa.

11.10 Ufuatiliaji hafifu kutoka kwenye uwekezaji wa Mifuko

Azania Benki iliingia mkataba na PPF kwa ajili ya kuuza nyumba zilizopo eneo la Kiseke. Ilifanikiwa kufanya hivyo mnamo mwezi Julai 2008, ingawa mkataba ulikuja kusainiwa tarehe 15 mwezi Novemba 2011. Kwa mujibu wa mkataba, Benki ilipaswa kuilipa PPF asilimia 80 ya mauzo na kubakiwa na asilimia 20 kama bakaa ambayo itapaswa kuja kulipwa baada ya kumalizika kwa malipo kutoka kwa mnunuzi. Pia, Benki ilipaswa iandae na kuwasilisha ripoti kwenye kila robo mwaka na kuwasiliana na PPF katika kila mwanzo wa mwaka kuhusiana na uwiano wa malipo. Hata hivyo, viwango vya uwiano wa malipo na ripoti za kila robo mwaka hazijawahi kuwasilishwa kwa PPF kutoka Benki; na PPF hawana usuluhishi wa viwango vya uwiano na kiasi cha riba kinachopatikana.

Pia, Azania Benki walishindwa kuwasilisha na hata kuitaarifu Menejimenti ya PPF kiasi cha Sh. milioni 445.25 kutoka kwenye asilimia 20 ya kiwango cha makato ya malipo kwa nyumba 84. Mnamo tarehe 29 Oktoba 2018 Mfuko uliandika barua yenye kumbukumbu Na. PPF/CD.26/97/02/15 kwa uongozi wa Benki kwa ajili ya kukumbushia juu ya malipo; ambapo kiasi cha Sh. milioni 326 kilipokelewa mnamo tarehe 5 Desemba 2018. Kumbukumbu za PPF zinaonesha kuwa, jumla ya nyumba 288 ziliuzwa, wakati kumbukumbu za Benki ya Azania zinaonesha nyumba 251; hivyo kuwa na tofauti ya nyumba 37.

Napendekeza PPF wafanye usuluhishi kwenye hatua zote za mauzo kwa wakati. Pia, Benki iheshimu makubaliano yaliyowekwa. Pia, tofauti za nyumba 37 ipatiwe ufumbuzi.

11.11 Udhaifu katika Mifumo na Usimamizi wa kiutendaji katika Mifuko

Wakati wa mapitio yangu ya ukaguzi nilibaini udhaifu katika mifumo ya kompyuta na kiutendaji ambayo imesababisha hasara, udanganyifu na hata miamala yenye kutia shaka.

Niligundua kuwa katika mfuko wa LAPF mikopo ya wanachama inafanyika nje ya mfumo wa kiuhasibu, ambapo imebainika katika mfumo hakuna kipengele kinachoweza kusimamia uwekaji wa kumbukumbu wala kukokotoa hesabu za riba. Kwa mfano, kwenye mikopo ya nyumba, tarehe ya kustaafu ambayo ni muhimu kwa ajili ya ukokotozi wa riba haijawekwa kwenye mfumo. Hii inasababisha mwanachama anapochelewa kuleta madai bado ataendelea kutozwa riba hata kama mkopo ulishafikia mwisho. Pia, inasababisha kuwapo kwa ongezeko la riba kimakosa katika hesabu za mwisho za taarifa za mwaka. Zaidi, niligundua kuwa kwa mwaka wa fedha ulioishia 2018, kulikuwa na ongezeko la riba iliyorekodiwa kimakosa Sh. milioni 108 wakati mwaka uliopita ilikuwa Sh. milioni 319.

Katika mfumo wa GEPF, niligundua kuwa mfumo wa kiuhasibu unamruhusu mtu mmoja kufanya miamala yote kuanzia mwanzo mpaka mwisho wa mzunguko wa kiuhasibu. Kwa ujumla, malipo ya shughuli mbalimbali kiasi cha Sh. milioni 399.57 yalifanyika bila ya kuwa na idhini. Katika hali hii, ni vigumu kugundua makosa.

Napendekeza mfuko mpya wa PSSSF ulioundwa baada kuunganishwa kwa mifuko mingine kutathimini mifumo yote ili kuhakikisha ukamilifu wa kumbukumbu za mifuko.

Zaidi, kwenye mfuko wa GEPF kuna watumishi watatu katika mikoa ya Tanga, Arusha na Mwanza ambao walitengeneza jumla ya wastaafu hewa 91 katika mfumo mkuu wa Mfuko. Hivyo, walifanikiwa kuingiza michango hewa jumla ya Sh. milioni 809.97 na wakafanya malipo hewa ya Sh. milioni 339.75 kwa wastaafu hewa 35. Pamoja na hatua za kinidhamu zilizochukuliwa bado inaonekana kuna udhaifu katika usimamizi wa mfumo. Baada ya muunganiko wa mifuko, napendekeza PSSSF wafanye uhakiki wa wanachama na wastaafu wake.

Katika mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya niligundua mapungufu yafuatayo: Kuna jumla ya kadi 100,032 ambazo zinafanya kazi na kupokea huduma za afya ambapo jumla ya Sh. bilioni 3.61 zililipwa, wakati ambao wanachama wakuu wa kwenye kadi hizo hawajapeleka michango. Pia niligundua wategemezi waliozidi umri kisheria ni 149,939 wenye jumla ya malipo ya Sh. bilioni 14.81. Zaidi, kuna kadi 156 ambazo zimesajiliwa zaidi ya mara 20 kwa matumizi ndani ya kipindi cha mwezi mmoja, na kadi 132 zimetumika katika maeneo tofauti kijiografia ndani ya siku moja. Vilevile, niligundua kadi 682 za wanachama wakuu ambazo zina wategemezi zaidi ya watano (idadi inaanzia wategemezi saba (7) mpaka 18). Kuna kadi 181,335 zilizoisha muda wake lakini bado zinatumika na jumla ya kadi 1,232 zilizoisha muda wake zimepata huduma za matibabu ambapo jumla ya Sh. milioni 31.06 zilidaiwa kama gharama za matibabu. Hayo yote ni kinyume na sera, kanuni na miongozo ya taasisi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

Napendekeza Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuhakikisha unaweka mifumo imara katika ngazi za mikoa kwa ajili ya utambuzi wa kadi. Pia, kuongeza usimamizi na uhimizaji wa michango kama inavyohitajika kisheria.

11.12 Rufaa za kesi za kodi zinazoendelea

Kuna kesi zinazondelea kutoka kwenye Baraza la Rufaa za kodi la Mamlaka ya Mapato Tanzania na Mahakama ya Rufaa, ambapo PPF wanapinga tathmini ya mapato ya riba kutoka kwenye hati fungani za Serikali kuanzia mwaka 2007 mpaka mwaka 2010. Pia, kesi ipo kwenye Baraza la Rufaa za Kodi ambayo bado imesimama, ambapo Mamlaka ya Mapato Tanzania wamekata rufaa dhidi ya hukumu iliyotolewa na bodi mwaka 2005. Kwa mujibu wa ripoti ya mtathmini wa masuala ya kodi, kuna jumla ya Sh. bilioni 236.90 kama deni kwa mwaka wa fedha 2005 mpaka tarehe 31 Julai 2018. Nimefahamishwa kuwa, kesi za rufaa za kodi zimesimama kufuatia majadiliano yanayoendelea nje ya mahakama kati ya Mamlaka ya Mapato

na Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya usuluhishi wa malipo.

Napendekeza PSSF wafanye ufuatiliaji wa karibu kwenye majadiliano na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa ajili ya kupata ufumbuzi mapema iwezekanavyo.

Pia, nilibaini kuwa Mfuko wa PSPF ulipokea notisi ya malipo ya kodi ya Sh. bilioni 234.3 kwa ajili ya tathmini ya kodi iliyofanywa kwa miaka minne ya kifedha, kutoka mwaka 2011/2012 hadi kufikia mwaka 2014/2015. Wadhamini wa PSPF waliwasilisha shauri hili kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kupata ufumbuzi wa kisheria. Hii ni kwa kuwa Mfuko unaamini kuwa ulipata msamaha wa kodi tangu kuanzishwa kwake tarehe 1 Julai, 1999.

Ninapendekeza PSSF wafuatilie kwa karibu juu ya shauri hili na kufanya mazungumzo na Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) ili kuweza kutatua suala hili kwa wakati.

11.13 Uwekezaji katika Benki ya Azania

Benki ya Azania zamani ilikuwa ikijulikana kama First Adili Bancorp Limited iliyoanzishwa mnamo mwaka 1995; Wabia wake wakuu ni NSSF mwenye hisa asilimia 35.27, PPF mwenye asilimia 30.53, PSPF mwenye asilimia 16.31, LAPF asilimia 15.35, East Africa Development Bank asilimia 1.54 na Wanahisa wengine wadogo wenye asilimia 1. Kama nilivyotangulia kusema kwenye ripoti zingine za huko miaka iliyopita, Benki ya Azania haijawahi kuwasilisha kwa CAG taarifa zake za fedha za mwaka kwa ajili ya ukaguzi. Kwa msingi huo ni vigumu kujua ufanisi wa kiwango cha uwekezaji kilichowekezwa ndani ya Benki. Kufuatia kuunganishwa kwa Mifuko ya hifadhi ya jamii ambayo ni PPF, PSPF, LAPF na GEPF na kuundwa kwa mfuko mpya ujulikanao kama PSSF unaomiliki asilimia 62.16, Benki ya Azania kwa namna nyingine ni dhahiri sasa inamilikiwa na PSSF.

Kwa ujumla, mifuko ya Hifadhi inamiliki asilimia 97.46 ya hisa za Benki ya Azania.

Kwa sababu hiyo, Azania inapaswa kuwa chini ya Msajili wa Hazina na hivyo inapaswa kuwasilisha taarifa zake za fedha kwangu kwa ajili ya Ukaguzi kama ilivyoelezwa kwenye kifungu namba 143 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kifungu cha 9 (a) iii & iv cha Sheria namba 11 ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008.

11.14 Kutokukidhi kwa Mipaka ya Uwekezaji Iliyowekwa na SSRA na BoT

SSRA na BoT walitoa miongozo ya uwekezaji kwa mujibu wa kifungu na 26(2) cha sheria ya mamlaka ya mifuko ya hifadhi ya jamii (2015) ambayo inaweka mipaka kwa maeneo mbalimbali yaliyoainishwa kwa uwekezaji kwenye Mfuko wa Pansheni, Benki na Taasisi za Fedha. Mipaka hiyo ni asilimia 20-70 ya mali ya jumla katika hati fungani za serikali, asilimia 10 ya mikopo na asilimia 30 kwa mali zisizohamishika. Aidha, kifungu Na. 27 cha Sheria ya SSRA kinahitaji Mfuko wa Pansheni kutekeleza usimamizi wa fedha za wanachama kwa faida ya wanachama, na si kinyume chake.

Hata hivyo, nilibaini kuwa PSPF wamewekeza kwenye mikopo ya moja kwa moja kwa Serikali na mali zisizohamishika kwa zaidi ya kikomo kilichowekwa kinyume na masharti niliyoyaeleza. Kwa upande mwingine, nilibaini uwekezaji wa NHIF kwa mikopo ya moja kwa moja kwa Serikali ilikuwa juu ya kikomo kilichowekwa, kinyume na matakwa ya kisheria. Tazama jedwali Na. 20.

Jedwali Na. 20:Kundi la uwekezaji na mipaka ya uwekezaji katika PSPF na NHIF

| | Mipaka | 2018 | 2017 |
|---|------------------|-----------------------------------|-----------------------------------|
| Mfuko wa hifadhi ya jamii kwa watumishi wa umma (PSPF) | | | |
| Kundi la uwekezaji | % ya mali | % ya uwekezaji uliofanyika | % ya uwekezaji uliofanyika |
| Hati fungani za serikali | 20-70 | 0.31 | 1.84 |
| Mikopo ya moja kwa moja | 10 | 34.09 | 26.54 |
| Mali zisizohamishika | 30 | 36.15 | 28.31 |
| Mfuko wa bima ya afya (NHIF) | | | |
| Mikopo ya moja kwa moja | 10 | 18.65 | 15.82 |

Nina shaka kwamba, kutofuatwa kwa vigezo vilivyowekwa kunaweza kuhatarisha fedha za wanachama.

Ninapendekeza PSPF na NHIF kufuata sheria na vigezo vilivyowekwa. Pia, kuepuka mipango ambayo sio mizuri ya fedha za wanachama ili kupunguza athari hasi zinazoweza kutokea.

11.15 Mashaka kwenye kurejesha michango ya kabla ya 1999 kwa PSSF na “Back Purchase” kwa LAPF Sh. bilioni 261.3

Kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Pensheni ya Huduma za Umma, tarehe ya kuanza kwa Mfuko kwa ajili ya kukusanya michango inayolipwa kwa mpango wa lazima ni tarehe 1 Julai, 1999. Michango iliyopatikana kabla ya tarehe 1 Julai, 1999 kwa wastaafu inashugulikiwa na PSPF lakini zinahitajika fedha kutoka Serikalini.

Mnamo mwezi Machi, 2013, Serikali ilitoa utaratibu wa kifedha utakaowezesha ulipaji wa deni la Sh. bilioni 716.6 kama sehemu ya dhima inayohusiana na fedha zilizolipwa na PSPF hadi tarehe 30 Juni, 2010. Chini ya mpangilio huu, Serikali iliahidi kulipa kiasi walichokubaliana kwa kipindi cha miaka 10.

Hata hivyo, nilibaini kuwa kiasi kilichotolewa na Serikali kuhusiana na “Pre-1999” kilikuwa ni Sh. bilioni 186 kwa kuwa, Sh. bilioni 393 tayari zilikwishalipwa kati ya Sh. bilioni 579 zilizopaswa kulipwa hadi Julai 2018. Hii inamaanisha kwamba, mpango wa fedha wa PSPF uliathiriwa kwa kulipa wanachama waliokusanyika kabla ya tarehe 1 Julai, 1999 bila PSPF kurejeshewa fedha zao. Kadhalika, Mfuko wa Pensheni wa LAPF ulitambua deni la Sh. bilioni 107.30 mwaka 2007/2008, wakati Serikali ilikubali kulipa Sh. bilioni 10 kila mwaka kwa kipindi cha miaka 10 kwa kiwango cha riba cha asilimia 11.8 kwa mwaka. Deni la Serikali kwa LAPF lilianzishwa mwezi Juni, 2005 baada ya tathmini iliyofanywa katika mchakato wa kubadilisha LAPF kutoka kuwa “provident” kuja kuwa mfuko wa Pensheni. Kipindi cha ulipaji cha miaka 10 kinatakiwa kukamilika tarehe 30 Juni, 2017. Hata hivyo, hadi mwaka ulioishia tarehe 31 Julai 2018 kiasi kilichotoka Hazina kuhusiana na malipo ya nyuma kilikuwa Sh. bilioni 75.3.

Ulipwaji wa haraka wa madeni haya ni jambo muhimu kwa ajili ya uendeleu wa Mfuko wa (PSSSF) ambao utarithi madeni ya mifuko miwili ya Pensheni.

Ili kuhakikisha uendeleu wa Mfuko ulioanzishwa, napendekeza kwamba Serikali isimamie maamuzi yake kwa Mfuko wa PSPF na Mfuko wa Pensheni wa LAPF kwa kuimarisha majukumu yake.

11.16 Kuchelewa kulipwa Mafao ya Wastaafu

Aya ya 3.3 ya Mfuko wa Pensheni wa NSSF inataka malipo ya mafao kwa wastaafu yalipwe ndani ya siku 14 baada ya maombi ya wastaafu kuwasilishwa. Malipo hayo yanawahusu wanachama waliostaafu kwa lazima au hiyari, malipo kwa wategemezi na malipo kwa wanachama waliositisha mikataba ya kazi. Hata hivyo, nilibaini NSSF ilichelewa kufanya malipo ya mafao yenye thamani ya Sh. milioni 769.42 kwa wastaafu 12 kwa zaidi ya siku 21 mpaka siku 91.

Ninapendekeza kuwa NSSF iboreshe utaratibu wa kulipa mafao; na kuhakikisha mafao yanalipwa kwa wakati.

11.17 Madai ya Michango katika Mfuko wa Penseni wa NSSF na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) Jumla Sh. Bilioni 84.79

Waajiri waliosajiliwa katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wanapaswa kuwasilisha makato ya wafanyakazi wao ndani ya siku 30 za mwezi unaofuata. Mpaka kufikia Juni 2018, NSSF ilikuwa haijakusanya jumla ya Sh.bilioni 61.78 kutoka kwa waajiri kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja. Hata hivyo, sikuweza kuona ushahidi kutoka NSSF unaoenesha ufuatiliaji wa michango hiyo.

Katika Mfuko wa NHIF, nilibaini Mfuko umeshindwa kukusanya jumla ya Sh.bilioni 23.01 na Sh.bilioni 7.16 kutoka kwa waajiri kwa kipindi kinachozidi siku 30 na mwaka mmoja, mtawalia. Kukosekana kwa ufuatiliaji kwa wakati kunaweza kusababisha Mifuko hiyo ikashindwa kukusanya michango hiyo, na kusababisha Mifuko hiyo kupata hasara.

Ninapendekeza kuwa NSSF na NHIF waweke utaratibu wa ufuatiliaji na kuhakikisha michango hiyo inakusanywa haraka.

11.18 Kupungua Kwa Akiba ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

Kupitia ripoti ya Uthamini (Actuarial Report) wa Mfuko wa NHIF ya mwezi Juni 2016 ambayo iliyotolewa mwezi Mei 2018 nilibaini Mfuko una thamani ya Mali mara tano zaidi ya malipo yote yaliyofanywa katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2016. Hivyo, kusababisha Mfuko kuwa na ukwasi katika kipindi cha muda mfupi.

Hata hivyo, kwa mujibu wa ripoti ya uthamini, makisio ya kipindi cha Mfuko kuanza kupata hasara yameshuka kutoka

mwaka 2040 kama ilivyokadiriwa katika uthamini uliofanyika mwaka 2013 mpaka mwaka 2025. Hii inamaanisha kwamba, madai ya huduma za bima ya afya yanaendelea kuongezeka ambapo itafikia kipindi ambacho makusanyo na mapato toka katika uwekezaji hayataweza kukidhi madai, itabidi Mfuko uchukue hatua kama kuuza mali zake ili uweze kulipa madai katika kipindi hicho.

Licha ya ukweli kwamba, makusanyo ya mwaka yanaendelea kuwa zaidi ya malipo ya huduma za bima ya afya, Kwa sasa, uwiano wa malipo ya huduma za afya unakua mwaka hadi mwaka kuliko kiasi cha mapato kinachokusanywa. Hii inaonesha kwamba, ukuaji wa kiwango cha makusanyo upo chini ikilinganishwa na ongezeko la madai ya malipo ya huduma za bima ya afya. Hivyo, makisio ya madai ya huduma za bima ya afya pekee ifikapo mwaka wa fedha utakaoishia Juni 2024 yatakuwa ni asilimia 99.2 ya jumla ya makusanyo yote. Uwiano huu unakisiwa kuongezeka zaidi mpaka asilimia 104.8 katika mwaka unaofuata.

Kupungua kwa ukwasi wa Mfuko kunasababishwa na kuongezeka kwa madai ya huduma za bima ya afya. Hii ni kwa sababu wanachama wa hiyari² wana haki sawa ya kupata huduma kama wachangiaji walio katika mfumo rasmi wa ajira. Ijapokuwa wanachama wa hiyari wanachangia asilimia 2 ya jumla ya michango, lakini madai yao ya huduma za afya ni asilimia 20 ya jumla ya madai yote.

Katika kipindi kilichoishia Juni 2018, uchambuzi wa mapato dhidi ya malipo ya madai ya huduma za bima ya afya zilizotolewa kwa makundi manne ya wachangiaji wa hiyari ambo ni watoto (Tota Afya), Watumishi wa Madhehebu ya Kidini (clerics), Vikundi vya Wajasiriamali (Kikoa) na wanafunzi

² Wanachama wa hiyari ni wanachama ya Mfuko ambao hawapo katika mfumo rasmi ya ajira kama watoto walio chini ya miaka (Tota Afya), Watumishi wa Madhehebu ya Kidini (clerics), Vikundi vya Wajasiriamali (Kikoa) na wanafunzi.

nilibaini nakisi ya Sh. bilioni 27.23 kama inavyoainishwa kwenye jedwali Na. 21 hapo chini.

Jedwali Na. 21: Mtiririko wa Mapato na Madai

| Name | Mwaka | Jumla ya Michango (A) | Jumla ya madai (B) | Ziada ya madai (B-A) |
|-----------|------------|-----------------------|--------------------|----------------------|
| Toto Afya | 30-Juni-18 | 2,278,065,631 | 8,123,611,169 | 5,845,545,538 |
| | 30-Juni-17 | 573,780,970 | 2,117,204,867 | 1,543,423,897 |
| Clerics | 30-Juni-18 | 687,059,973 | 2,243,878,100 | 1,556,818,127 |
| | 30-Juni-17 | 783,446,270 | 1,051,620,455 | 268,174,185 |
| Kikoa | 30-Juni-18 | 2,355,627,403 | 12,649,172,607 | 10,293,545,204 |
| | 30-Juni-17 | 1,335,023,958 | 5,361,853,498 | 4,026,829,540 |
| Wanafunzi | 30-Juni-18 | 6,139,391,901 | 9,830,262,440 | 3,690,870,539 |
| | 30-Juni-17 | 14,152,396,106 | 41,377,603,136 | 27,225,207,030 |

Ili kuhakikisha kunakuwa na mwenendo mzuri wa Mfuko, inapaswa pawe na udhibiti na ufuatiliaji kuhusu kukuwa kwa kiwango cha madai ya huduma za bima ya afya. Kama hali hii itaendelea, huduma ya bima ya afya kwa wanachama wa hiyari itaondoa ukwasi wa mfuko kama ilivyoielezwa na Mthamini.

11.19 Huduma ya Bima ya Afya kwa Wastaafu

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umeanza kutoa huduma ya matibabu ya bima ya afya kwa wastaafu tangu tarehe 1 Julai 2009. Mafao hayo yanahusu wastaafu waliokuwa wanachama wa Mfuko huu kupewa matibabu ya afya yeye na mkewe katika kipindi chao chote cha maisha. Mwanachama huyu anapaswa awe amefikia miaka ya kustaafu kuazia miaka 55 ya kustaafu kwa hiyari au miaka 60 ya kustaafu kwa mujibu wa sheria. Kwasasa, Mstaafu aliyechangia jumla ya miezi kuanzia 120 (miaka 10) hachangii katika kupata matibabu hayo. Kama mstaafu hakufikisha miaka 10 katika kuchangia anatakiwa alipe asilimia 1 ya mshahara wake katika kipindi chote cha maisha yake.

Uthamini uliofanywa tarehe 30 Juni 2016 ulionesha gharama za matibabu kwa wastaafu ni sawa na 80% ya michango yao katika kipindi cha miaka 10 kabla ya kustaafu. Hata hivyo, ongezeko la wastaafu wa hiyari kwasasa (rejea aya na 11.6 ya ripoti hii)

linahatarisha ukata wa mfuko, kwa kuwa wastaafu watakuwa wanapata matibabu bila kuchangia.

Ninapendekeza kuwa NHIF wawekeza asilimia fulani ya michango ya wanachama ili uwekezaji huo uje kusaidia malipo ya huduma za afya za wanachama hao pindi watakapostaafu.

SURA YA KUMI NA MBILI

USIMAMIZI WA MIKOPO KWA TAASISI ZA UMMA

12.1 Utangulizi

Katika kutimiza majukumu yake, Taasisi na Mashirika ya Umma kuna wakati huchukua mikopo kwa ajili ya kufadhili baadhi ya shughuli zao. Mikopo hiyo hutoka sehemu tofauti tofauti, nje na ndani ya nchi yetu. Hivyo kuna aina tofauti ya ukubwa, uasili na hata viashiria vya hatari kwenye mikopo hiyo. Usimamizi wa mikopo hiyo ni jambo linalohitaji umakini mkubwa kwa sababu mikopo hii inahusisha mali za umma kama dhamana.

Ukaguzi wangu kuhusu namna ya usimamizi wa mikopo kwa Taasisi za Umma uligundua na kupendekeza yafuatayo:

12.2 Mkopo uliokosa maelezo kutoka Azania Bank Sh. Milioni 372.76

Mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2018, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko iliripoti deni la Sh. milioni 372.76 kutoka Benki ya Azania. Mkopo huu haukuwahi kuridhiwa na Bodi ya Wakurugenzi, kwani kipindi unachukuliwa hakukuwa na Bodi kwa ajili ya kuidhinishwa. Pia, hata malengo ya mkopo hayakuainishwa wazi, kwani hata nilipohitaji viambatisho kwa ajili ya ukaguzi ili kujua kama kuna vikao vilifanyika pamoja na malengo ya mkopo, hakukuwa na ushahidi. Kuna hatari kwamba, mkopo uliochukuliwa umetumika nje ya malengo, kwani hakuna ushahidi unaothibitisha malengo ya mkopo.

Napendekeza Menejimenti ya Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kuonesha malengo, masharti na matumizi ya mkopo. Pia, kuwajibika kwa kuchukua mkopo bila idhini ya Bodi.

12.3 Kusuasua kwa Utekelezwaji wa Mradi wa Maji kutokana na Masharti Magumu ya Mkataba

Mnamo mwezi Oktoba 2012, Wizara ya Fedha ilikopa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 178.13 kutoka kwa Benki ya India

ijulikanayo kwa jina la Export-Import Bank of India kwa ajili ya kuiwezesha DAWASA kutekeleza miradi ya maji katika maeneo mbalimbali ndani ya mkoa wa Dar es Salaam na Chalinze. Sharti mojawapo la Mkataba wa mkopo huo linataka asilimia 75 ya bidhaa zinazonunuliwa na huduma zitoke nchini India. Maana yake, kuanzia vifaa, Mkandarasi, mashine na vifaa muhimu vipatikane kutoka India. Nimeona pia jumla ya Dola za Kimarekani milioni 41.36 zikitengwa kwa ajili ya mradi wa Chalinze ili kuweza kumlipa Mkandarasi kutoka India wa kampuni iitwayo M/s. Overseas Infrastructure Alliance (India) Pvt Ltd - Pratibha Industries Ltd. Hata hivyo, mradi umesimama ukiwa umefikia asilimia 75 ya utekelezaji kwa sababu Mkandarasi mshiriki/msaidizi kwenye mradi huo hajalipwa fedha zake. Pia, niligundua kuwa DAWASA hawajapokea kiasi chochote cha fedha kwa ajili ya usimamizi wa mradi. Masharti magumu ya mkopo huu yamesababisha miradi kutokuisha kwa wakati.

Napendekeza Serikali ifuatilie kwa ukaribu kutoka Serikali ya India ili kuweza kutafuta ufumbuzi juu ya mkopo huu na usimamizi wake na kumtaka Mkandarasi amalize kazi yake.

12.4 Bakaa ya Muda Mrefu ya Deni Linalodaiwa Sh.Bilioni 47.40

Mnamo mwaka 2003, Serikali ya Tanzania ilikopa kiasi cha Sh. bilioni 77.03 kutoka kwa Mashirika matatu (3) ya kimataifa, na ikaikopesha DAWASA kwa riba ya asilimia 11.5 kwa mwaka kwa ajili ya kufanya marekebisho ya miundombinu ya maji katika Mkoa wa Dar es Salaam. Marejesho ya mkopo yalitakiwa kuanza kufanyika kuanzia mwaka 2010, lakini mpaka kufikia mwaka 2014 DAWASA walikuwa hawajarejesha kiasi chochote. Kulimbikizwa kwa mkopo kumesababisha riba kufikia Sh. bilioni 100.87 hadi mwaka 2014.

Serikali imeamua kubeba mzigo wa riba kutoka DAWASA, na ikaamua kuwapunguzia marejesho ya mkopo mpaka kufikia Sh. bilioni 47.40, ambapo awamu ya kwanza ilipaswa kulipwa mwezi Julai 2018. Hata hivyo, Menejimenti ya DAWASA inaona bado

kuna ugumu wa kulipa awamu hizo za malipo kwa sababu hata makusanyo yatoanayo na ankara za maji hayafikii gharama za uendeshaji. Deni linaonekana kuelemea DAWASA, na huenda ikasababisha kuathiri hata shughuli za uendeshaji wakati wa urejeshwaji wa mkopo.

Ninapendekeza kuwa Serikali iangalie uwezekano wa kuliondoa deni hili kutoka kwa DAWASA ili kampuni iweze kujiendesha bila tatizo.

12.5 Kutokuzingatia Makubaliano ya Mkopo

Kifungu cha 20.2 cha mkataba kati ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na East African Development Bank (EADB) kinaitaka NHC kuhakikisha kudumisha uwiano wa 1:5:1 wa kulipa mkopo. Mkataba umeelezea kwamba, uwiano wa kulipa mkopo unamaanisha faida kabla ya kulipa kodi, kutoa gharama za uchakavu na malipo ya mkopo kutoka EADB.

Nilibaini katika kipindi cha mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2018, kuwa NHC imekuwa na uwiano wa kulipa mkopo wa 0:63:1 ambao upo chini ya uwiano wa mkataba. Kutokuzingatia mashariti ya mkataba kunaweza kusababisha NHC kushindwa kupata mikopo katika kipindi kijacho.

Ninapendekeza kuwa NHC ihakikishe inazingatia makubaliano ya mkataba na ikitokea inataka kwenda kinyume na makubaliano ya mkataba iombe idhini ya mkopeshaji.

12.6 Kuhitajika Kubadilisha Kifungu cha Mkataba ili Kuridhia Ucheleweshwaji wa Malipo ya Mkopo

Mnamo tarehe 29 Desemba 2017 Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU) kilikopa jumla ya Sh. milioni 601.73 kutoka kwa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA). Kifungu cha XI (i) cha mkataba wa mkopo kinaitaka ARU ianze malipo ya mkopo tarehe 30 Novemba 2017 ambayo ni tarehe ya nyuma ikilinganishwa na tarehe ya mkopo. Malipo mengine yanapaswa yafanyike kila mwaka kwenye tarehe

ya malipo ya mkopo wa kwanza. Kuchelewa kutolewa kwa mkopo kumeongeza riba na kupunguza muda wa kulipa mkopo.

Ninapendekeza ARU ifanye mawasiliano na TEA ili kuweza kubadilisha muda wa kulipa mkopo huo.

12.7 Mapungufu ya Mamlaka ya Elimu Tanzania katika Kusimamia Mikopo

Moja ya jukumu la Mamlaka ya Elimu Tanzania ni kutoa msaada wa kifedha kwa kutoa mikopo katika Taasisi za Elimu mbalimbali katika miradi tofauti tofauti ili kuhakikisha elimu inayotolewa ni ya ubora. Katika mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2018, nimebaini madai mbalimbali ya mikopo kutoka taasisi mbalimbali za elimu yanayofikia Sh. bilioni 4.17 ambayo malipo yake yalitakiwa kupokelewa na Mamlaka ya Elimu Tanzania. Hata hivyo, ni marejesho ya Shilingi milioni 197.30 tu (sawa na asilimia 4.7) yalipokelewa kutoka kwa wakopaji katika mwaka huo. Taarifa zaidi zinazohusiana na taasisi na bakaa za mikopo yao zimeripotwa kwenye *kiambatisho Na.V*

Kuzorota kwa marejesho kutoka kwenye taasisi za elimu kunapunguza ukwasi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania hivyo kuathiri uwezo wake wa kutimiza majukumu yake ya msingi hasa ukopeshaji kwenye taasisi nyingine za elimu zenye uhitaji.

Ninapendekeza Mamlaka ya Elimu Tanzania iboreshe mbinu zake za kukusanya marejesho na kutumia juhudi zaidi kuongeza kasi ya marejesho.

SURA YA KUMI NA TATU

UTENDAJI WA MAMLAKA ZA MAJI

13.0 Utangulizi

Utendaji kazi wa Mamlaka za maji unapimwa kwa vigezo vilivyowekwa katika makubaliano waliyosainiana kati ya Mamlaka za Maji na Wizara ya Maji chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Maji na Nishati (EWURA). Viashiria vya ubora katika utendaji ni kama vile ubora katika huduma, ustawi wa Mamlaka za maji, uwiano wa idadi za mita, ufanisi katika ukusanyaji mapato ubora wa miundombinu na utunzaji endelevu wa mazingira.

Sura hii inaangazia mapungufu ya utendaji kazi wa Mamlaka za Maji na maeneo mengine yote yanayohusiana na utoaji wa huduma za maji.

13.1 Upotevu wa maji usiovumilika wa kiasi cha Sh. bilioni 47.18

Maji yanayopotea (NRW) ni kiasi cha maji ambacho kimezalishwa ila hakijafika kwa wateja. Hivyo, hukokotolewa kwa kuchukua tofauti kati ya maji yaliyozalishwa na maji yaliyowafikia wateja kwa kipindi husika. Kigezo kimojawapo cha upimaji wa ufanisi wa taasisi za maji ni jinsi taasisi za maji zinavyoweza kupunguza au kudhibiti upotevu huo ili uendane na viwango vinavyokubalika na EWURA, ambacho ni sawa na asilimia 20. Hili ni lengo lililotakiwa kufikiwa ifikapo 2018. Pia, Wizara ya Maji na Mamlaka za maji zinaingia randama ya makubaliano kila mwaka kwa ajili ya kupima utendaji na ufanisi wa mamlaka hizo, ikiwamo kufikia lengo la asilimia inayokubalika kwenye upotevu wa maji.

Ukaguzi wangu uligundua upotevu wa maji katika Mamlaka za maji bado ni changamoto. Sababu kubwa ni kuchakaa kwa miundombinu inayosababisha kuwapo na uvujaji, uunganishaji haramu, upatikanaji hafifu wa umeme, kupitisha bomba nje ya mita, idadi kubwa ya wateja wasio na mita na kuwapo kwa

kanzidata isiyo sahihi inayoweka ugumu katika ufuatiliaji wa wateja.

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kwa Mamlaka za Maji 15 dhidi ya upotevu wa maji, niligundua kuwa lengo halikufikiwa kutokana na hasara ya upotevu wa maji kiasi cha Sh. bilioni 128.21 (Kiwango cha uvumilivu wa upotevu kikiwa ni Sh. bilioni 81.03 wakati kiwango kisichovumilika cha upotevu kikiwa ni Sh. bilioni 47.18) kulingana na taarifa zilizopo za kiwango cha maji kinachozalishwa na idadi ya wateja waliounganishwa. Jedwali Na. 22 linaainisha zaidi:

Jedwali Na. 22: Hasara itokanayo na upotevu wa maji

| Na | Jina la Mamlaka | Asilimia ya Maji yasiyo Mapatoto | Asilimia ya upotevu unaokubalika | Jumla ya Kiasi cha upotevu katika (Sh. milioni) | Kiasi cha upotevu kinachokubalika (Sh. Milioni) | Kiasi cha upotevu kisichokubalika - (Sh. Milioni) |
|--------------|-----------------|----------------------------------|----------------------------------|---|---|---|
| 1 | Njombe | 35 | 20 | 457.84 | 261.63 | 196.22 |
| 2 | Mwanza | 38 | 30 | 3,218.23 | 2,540.71 | 677.52 |
| 3 | DAWASA | 46 | 25 | 24,763.65 | 13,458.51 | 11,305.14 |
| 4 | Arusha | 47 | 39 | 10,690.88 | 8,863.61 | 1,827.27 |
| 5 | Dodoma | 28 | 27 | 6,226.31 | 5,919.38 | 306.93 |
| 6 | Lindi | 34 | 30 | 186.65 | 163.25 | 23.4 |
| 7 | Iringa | 27 | 25 | 2,637.18 | 2,423.88 | 213.3 |
| 8 | DAWASCO | 45 | 25 | 60,020.44 | 33,344.69 | 26,675.75 |
| 9 | Tabora | 36 | 30 | 1,989.90 | 1,658.25 | 331.65 |
| 10 | Bukoba | 49 | 30 | 2,104.01 | 1,288.17 | 815.84 |
| 11 | Chalinze | 32 | 30 | 842.27 | 789.63 | 52.64 |
| 12 | Moshi | 22 | 20 | 2,552.91 | 2,352.92 | 200 |
| 13 | Babati | 48 | 32 | 1,578.44 | 1,052.30 | 526.15 |
| 14 | Morogoro | 39.4 | 30 | 5,945.12 | 4,526.74 | 1,418.38 |
| 15 | Musoma | 62.89 | 30 | 4,997.51 | 2,383.93 | 2,613.58 |
| Jumla | | | | 128,211.34 | 81,027.60 | 47,183.77 |

Napendekeza Mamlaka za Maji Mijini kupunguza kiwango pendekezwa kilichowekwa cha upotevu wa Maji kwa kusimika mita kwa wateja wote, kuhimili msukumo wa maji kwenye

eneo la usambazaji, pamoja na kubadilisha mifumo chakavu na kuweka miundombinu na vifaa vipya.

13.2 Ucheleweshwaji wa Makusanyo ya Madeni Katika Mamlaka za Maji Sh. Bilioni 97.58

Ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka ya Maji safi na Maji taka (UWSSAs), Sera ya mikopo ya UWSSA ni kurejesha malipo ya ankara zilizoiva kwa mwezi unaofata kwa kila mteja. Pia, kuondolea huduma za maji kwa mteja yeyote anayedaiwa Ankara ya maji kwa siku zaidi ya tisini (90) bila kulipa. Katika kupima utekelezaji wa sera hii, nilibaini kuwa bado kuna kiwango cha chini cha urejeshaji wa madeni katika Mamlaka za Maji kwa kuwa nilibaini mapato makubwa ambayo hayajarejeshwa yalikuwa yamezidi muda uliowekwa kwenye sera ya mikopo.

Katika mkusanyiko huo wa madeni, nilibaini kuwa kati ya Sh. bilioni 97.58, Sh. bilioni 39.59 (sawa na asilimia 41) ni madeni ya Serikali; na Sh. bilioni 57.99 (sawa na asilimia 59) ni madeni kutoka kwa wateja wengine kama vile wateja wa kibiashara, wateja wa majumbani, wateja wa viwanda na wateja wa taasisi za kidini. Ongezeko la madeni husababishwa na kutokuwa na ufatiliaji wa karibu wa ukusanyaji wa wadeni na kutokufuata sera ya UWSSA kwa kushindwa kukata huduma za maji kwa wateja wanaokiuka taratibu kama inavyotakiwa na sera ya mikopo.

Kushindwa kukusanya madeni kwa ufanisi hupunguza uwezo wa kifedha wa Mamlaka hizo za Maji na kusababisha vikwazo vya lazima vya kifedha. Mchanganuo wa kiasi kinachodaiwa na mamalaka husika umeainishwa katika jedwali la 23 chini:

Jedwali Na. 23: Madeni ya muda mrefu

| Na | Mamlaka za Maji | Deni serikali-Milioni | Madeni sehemu ya biashara, majumbani, viwandani n.k-Milioni | Jumla-Milioni |
|----|------------------|-----------------------|---|------------------|
| 1 | DAWASA & DAWASCO | 26,958.61 | 41,941.39 | 68,900.00 |
| 2 | Kigoma | 420.66 | 796.42 | 1,217.08 |
| 3 | Bukoba | 364.00 | 429.19 | 793.19 |
| 4 | Morogoro | 578.13 | 1,682.92 | 2,261.05 |
| 5 | Moshi | 1,525.00 | 305.28 | 1,830.28 |
| 6 | Singida | 275.00 | 231.11 | 506.11 |
| 7 | Tanga | 1,996.00 | 2,601.83 | 4,597.83 |
| 8 | Mwanza | 2,212.81 | 3,689.59 | 5,902.40 |
| 9 | Chalinze | 111.00 | 556.70 | 667.70 |
| 10 | Dodoma | 1,634.00 | 2,300.64 | 3,934.64 |
| 11 | Lindi | 86.51 | 374.13 | 460.64 |
| 12 | Kashuwasa | 1,212.60 | 442.67 | 1,655.27 |
| 13 | Mtwara | | 1,517.56 | 1,517.56 |
| 14 | Arusha | 1,354.01 | 230.49 | 1,584.50 |
| 15 | Iringa | 864.31 | 890.77 | 1,755.08 |
| | Jumla | 39,592.64 | 57,990.69 | 97,583.33 |

Kiasi hicho kinachodaiwa ni kikubwa sana, na kinaweza kuathiri shughuli za Mamlaka za Maji husika kama fedha hizo hazitakusanywa kutoka kwa wateja na kutumika katika kutekeleza shughuli za mamlaka hizo za maji.

Menejimenti za UWSSA zinahitaji kuainisha mipango ya ukusanyaji wa madeni na kuisimamia kwa ukaribu mipango hiyo.

13.3 Kutofikia Malengo ya Wateja DAWASA na AUWASA

Sababu kuu ya ukuaji wa mahitaji ya maji katika maeneo ya huduma ya UWSSA ni ongezeko la idadi ya watu. Kwa hiyo, mtu anaweza kutarajia mahitaji ya maji kuongezeka kwa kiwango ambacho ni sawa na kiwango cha ongezeko la idadi ya watu. Hivyo, huduma ya maji imechambuliwa kwa kuzingatia

viashiria viwili ambavyo ni idadi ya watu wanaohudumiwa na idadi ya watu wanaoishi eneo la mtandao wa maji. Mapitio ya AUWASA na DAWASA yalibaini kuwa, hawajafikia malengo ya mteja waliojiwekea. Idadi ya watu na upatikanaji wa moja kwa moja kwa takwimu za maji viko chini kuliko lengo.

Nilitambua kwamba, idadi ya watu iliyofikiwa na Mamlaka ya Maji safi AUWASA ni wateja 49,107 sawa na asilimia 44 ya idadi ya watu wa mji huo. Pia, nilibaini kuwa idadi ya wateja wa DAWASA iliyunganishwa na maji ni 222,913 ambayo ni asilimia 49 ya lengo lililowekwa ambalo ni 450,000 hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018. Kushindwa kukidhi mkakati wa kufikia wateja 450,000 kunaashiria kuwa kuna asilimia kubwa ya watu wanaoishi bila maji ya moja kwa moja. Pia huathiri Mamlaka kwa kutokupata mapato yaliyokusudiwa.

Ninapendekeza Menejimenti za DAWASA na AUWASA kuchunguza upya na kutekeleza mikakati kama ilivyoielezwa katika mpango mkakati.

13.4 Matatizo ya Kifedha Yanayozikumba Mamlaka za Maji

Nilibaini kuwa jumla ya mamlaka za maji 11 kati ya 20 nilizozipitia wakati wa Ukaguzi wangu wa mwaka zinaendelea kushuka kifedha na kupata hasara kila mwaka. Hali hii inaashiria kuwa mamlaka hazitoweza kujikidhi kifedha katika kipindi kifupi kijacho; hivyo kuzifanya mamlaka hizi kushindwa kulipa madeni yake kadri yanavyotokea. Jedwali 24 hapa chini linaonesha uchambuzi wa baadhi ya Mamlaka za Maji zinazokabiliwa na tatizo la kupungua kwa mtaji wa uendeshaji:

Jedwali Na. 24: Mwenendo wa Matatizo ya kifedha katika Mamlaka za Maji

| UWSSAs | Hasara iliyopatikana (Sh.) | Malimbikizo ya hasara (Sh.) | Uwiano wa madeni ya muda mfupi na mali za muda mfupi (uwiano unaopendekezwa 1:1) |
|---------|----------------------------|-----------------------------|--|
| | Mwaka 2017/2018 | | |
| DAWASCO | 8,769,933,000 | 86,418,819,000 | 0.58:1 |

| | | | |
|---------|---------------|----------------|--------|
| Iringa | 1,233,783,388 | 613,937,228 | |
| DAWASA | - | 99,065,752,000 | 0.85:1 |
| Lindi | 47,000,987 | 1,190,343,424 | 0.29:1 |
| Masasi | 414,926,075 | 2,306,068,294 | |
| Moshi | | | 0.97:1 |
| Mtwara | 117,976,132 | 2,783,219,933 | 0.93:1 |
| Mwanza | 378,442,392 | 141,440,413 | 0.95 |
| Njombe | | 383,170,813 | 0.57:1 |
| Singida | | 1,093,695,417 | 0.91:1 |
| Tabora | 471,675,799 | | |

Uwiano wa hapo juu unaonesha kutokuwepo na uhakika wa Mamlaka hizi kujiendeleza. Hii inaweza kusababisha shaka kubwa juu ya uwezo wa kuendelea kama Serikali isipochukua hatua za haraka za kuboresha uwezo wao wa kifedha.

Ninapendekeza kuwa, UWSSAs ziendeleze mikakati ya kujiokoa kutoka katika tatizo la kifedha lililopo.

13.5 Kukosekana kwa Sheria na Sera ya Majitaka

Ukaguzi wangu katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dodoma ulibaini kuwa Mamlaka haina utaratibu wa kuratibu mifumo ya maji taka ya wateja wao. Kupitia majadiliano yangu na Menejimenti ya Mamlaka, nilibaini kuwa kwa sasa hakuna Sheria na Sera ya Majitaka Tanzania. Tatizo hili lipo katika Mamlaka zote za maji Tanzania.

Ninapendekeza Serikali kuanzisha Sheria na Sera ya Majitaka Tanzania ambayo itasaidia kuratibu masuala ya majitaka Tanzania. Kwa sasa, napendekeza Mamlaka zote za maji zitengeneze utaratibu wa kuratibu mifumo ya maji taka ya wateja.

13.6 Mapungufu Katika Miundominu ya Maji Taka

Nilibaini kiwango cha miundombinu cha maji taka ni kidogo ikilinganishwa na mahitaji ya miundombinu hiyo katika jamii. Uhaba wa miundombinu unasababishwa na gharama kubwa za

kutengeneza miundombinu hiyo pamoja na gharama kubwa ya kutengeneza mabwawa ya kuhifadhia maji taka.

Katika Jiji la Tanga nilibaini karibu kilomita 10 kati ya jumla ya kilomita 30 zimeharibika na kusababisha Mamlaka kuingia gharama kubwa kwa ajili ya matengenezo ili kuepusha madhara ya kiafya katika jamii. Miundominu ya Majitaka taka katika Jiji la Tanga ni asilimia 9.7 ya mahitaji. Nilibaini kuwa majitaka katika Jiji la Tanga hutupwa baharini kabla ya uchafu huo haujatibiwa. Hii inaweza kusababisha uchafuzi wa mazingira. Hali hii inasababishwa na ukosefu wa vifaa vya kupunguza madhara kabla ya kutupwa kwa majitaka hayo.

Pia, Miundominu ya Maji taka katika Jiji la Dodoma ni asilimia 20 ya mahitaji ya wakazi ambao ni takribani 500,000. Hii inasababishwa na ukosefu wa mifereji ya kupitishia maji taka katika makazi ya watu. Pia, mabwawa ya kuhifadhia maji taka hayakidhi mahitaji ya sasa. Hali hii pia imesababisha Mamlaka kupoteza mapato kutokana na uhaba wa mifumo ya maji taka. Mamlaka iliweza kukusanya kiasi cha Sh. bilioni 1.32 kwa kutoa huduma ya maji taka. Hii ni kinyume na matakwa ya kiwango kilichowekwa na EWURA cha asilimia 40 ya jumla ya mapato ambapo mamlaka ilipaswa kukusanya Sh. bilioni 4.99 ambazo ni sawa na asilimia 40 ya mapato ya Sh. bilioni 12.49 yaliyokusanywa kutokana na mauzo ya maji safi kwa mwaka. Pia nilibaini bwawa la kuhifadhia maji taka lililopo katika eneo la Swaswa lipo karibu sana na makazi ya watu na mashamba ya wakazi wa maeneo hayo. Pia, bwawa hilo limejaa sana ambapo maji taka yaliyohifadhiwa yanaweza kutawanyika hasusani kipindi cha mvua. Miundombinu ya maji taka sasa katika jiji la Dodoma haikidhi mahitaji kutokana na ongezeko la watu.

Ninapendekeza Mamlaka za Maji za jiji la Tanga na Dodoma kuhakikisha zinaongeza huduma ya mifumo ya maji taka ili kutekeleza agizo la Serikali la kuhakikisha mfumo wa maji taka

unafika asilimia 30 ifikapo mwaka 2025. Pia, ziongeze mabwawa ya kuhifadha maji taka.

13.7 Mapungufu katika miundombinu ya usambazaji Maji Safi
Randama ya Makubaliano (MoU) kati ya Wizara ya Maji na Mamlakaza Maji Safi na Maji Taka (UWSSAs) inataka kuendeleza kufanyamatengenezo ya mtandao wa maji uliotengenezwa kwa kutoa huduma ya maji. Pia, miongozo ya utendaji ya taratibu za kiufundi zinataka UWSSA kuhakikisha kuwa, nyenzo na miundombinu ya kusambaza maji inatengenezwa ili kuwa na mpango kabambe wa matengenezo.

Ukaguzi wangu ulibaini baadhi ya Mamlaka za Maji kama za Dodoma, Dar es Salaam, Tanga, Lindi, Mwanza, Njombe, Chalinze, Musoma, na Morogoro zina changamoto za mtandao wa maji kuwa wa zamani na mfumo wa usambazaji usiokidhi mahitaji. Kuchakaa kwa miundombinu kunasababisha upotevu wa maji (kuvuja) na kupunguza kiwango cha maji yanayosambazwa kwa wateja.

Nilibaini kuwa Mamlaka hizi zimekuwa zikipambana kupata pesa kwa ajili ya kuondoa miundombinu hiyo inayoonekana kuchakaa. Hata hivyo, kasi ya utekelezaji wa lengo hili kwa kutumia vyanzo vya fedha vya ndani haiendani na kasi ya ongezeko kubwa la idadi ya watu. Hivyo, baadhi ya mamlaka hulazimika kutuma maombi ya fedha toka Wizara ya Maji.

Uhaba wa miundombinu ya usambazaji maji kwa sababu ya uchakavu wa miundombinu na mtandao usiokidhi mahitaji vinaathiri idadi ya watu wanaopata huduma za mamlaka kama inavyooneshwa katika jedwali Na. 25.

Jedwali Na. 25: kiwango cha watu wanaopata Maji

| Na. | Mamlaka za Maji Safi na usafi wa Mazingira | Kiwango cha Watu wanaopata Maji |
|-----|--|---------------------------------|
| 1 | Babati | 67% |
| 2 | Masasi Nachingwea | 44% |
| 3 | Arusha | 55% |
| 4 | Dodoma | 52% |
| 5 | Singida | 74% |
| 6 | Shinyanga | 62% |
| 7 | Njombe | 53% |
| 8 | Chalinze | 60% |

Chanzo: Taarifa za Wakurugenzi 2017-18

Mamlaka (UWSSA) zinatakiwa kufanya utafiti wa kujua idadi ya sasa ya watu kulinganisha na mahitaji ya maji.

Hivyo mamlaka zitafute fedha za kuendeleza na kuongeza mtandao wa maji ili kukidhi kasi cha ukuaji wa miji na ongezeko la watu.

13.8 Mapungufu katika Ankara za Wateja

Randama ya Makubalino kati ya Mamlaka za Maji na Wizara ya Maji inazitaka mamlaka za maji kuwa na usimamizi endelevu katika kuzalisha na kusambaza maji kwa kiwango na ubora. Pia, kulingana na Sheria, Mamlaka zinatakiwa kuweka mita za kusoma kiwango cha maji yaliyozalishwa na kupelekwa kwa wateja.

Nilibaini kuwa baadhi ya mamlaka hazijaweza kuweka mita hizo kwa wateja wote. Hivyo, ankara kwa wateja hao zinafanyika kwa makadirio yanayoweza kusababisha makosa, hatimaye kusababisha hasara kwa mamlaka. Wateja wasio na mita walikuwa zaidi katika mamlaka za maji za Dar es salaam, Musoma, Morogoro, Lindi, Namtumbo, Babati, Njombe na Arusha. Ilibainika pia kuwa, wateja wasio na mita wanalipa kiwango sawa kutegemeana na makadirio ya matumizi ya mwezi. Vile vile kulikuwa na baadhi ya mamlaka ambazo

zilikuwa na wateja ambao hawakupewa ankara za matumizi ya maji ingawa wapo kwenye kanzidata za wateja. Kwa mfano, DAWASA ilikuwa na wastani wa wateja 22,319 (10% ya wateja wote) waliopewa ankara kwa kutumia makadirio, wateja 16,336 (7.6% ya wateja wote) wasio na mita kwa miaka 10, na wateja 53,202 (26% ya wateja wote) wasio na ankara.

Makadirio katika kutoa ankara ni hatari kwa mapato ya mamlaka kwa kuwa matumizi halisi yanaweza kuwa makubwa kuliko makadirio, wakati wateja ambao hawakupewa ankara wanasababisha hatari ya wizi maana watumishi wanaweza kushirikiana na wateja kwa nia ovu ya kujipatia faida binafsi.

Ninapendekeza kuwa Mamlaka zishughulikie mapungufu yaliyobainika kwa kuweka mipango ili kuhakikisha mita zinawekwa kwa wateja wasiokuwa nazo, na ankara zinatolewa kwa kila mteja. Wateja wote wawekewe mita na zisomwe kila mwezi ili kutoa ankara sahihi kulingana na matumizi halisi ya mteja.

SURA YA KUMI NA NNE

USIMAMIZI WA RUZUKU ZA SERIKALI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA

14.1 Utangulizi

Serikali imeweka nguvu na msisitizo katika sekta ya kilimo kwa kuweka ruzuku kwenye pembejeo za kilimo kwa lengo la kuimarisha na kuongeza tija katika uzalishaji na kuimarisha hali ya maisha ya raia na familia zao. Niligundua mapungufu katika usambazaji wa pembejeo za wakulima kama nilivyoainisha hapa chini:

14.1 Udhaifu Katika Ugawaji wa Viwatilifu na Vinyunyizi vya Pamba

Serikali kupitia Bodi ya Pamba iliamua kugawa pembejeo za pamba kwa wakulima bila malipo. Ili kurahisisha zoezi la ugawaji, taarifa muhimu kama vile hati ya mapokezi na fomu namba 4 zilitumika. Hati za mapokezi zilitumika wakati wa pembejeo zikiingizwa kwenye maghala, na fomu namba 4 zilitumika wakati pembejeo zikifikishwa kwa wakulima. Kwa mwaka 2017/2018, pembejeo za jumla ya Sh. bilioni 19.9 zilinunuliwa na kusambazwa kwa wakulima.

Wakati napitia ripoti maalum ya Mkaguzi wa ndani, kwenye mchakato wa ugawaji niligundua yafuatayo:

- i. Kwenye fomu namba 4 ilionekana kuwa baadhi ya wakulima walipewa viwatilifu zaidi ya kiwango cha ekari wanazolima, hasusani kwa wasambazaji na watumishi wa serikali za mitaa.
- ii. Mtu mmoja anasaini upokeaji wa viwatilifu kwa niaba ya wakulima wengine kwa kutumia saini tofauti au saini moja.
- iii. Wakulima wengine waliochukua viwatilifu hawajasaini fomu namba 4 na baadhi ya maeneo fomu namba 4 zimeambatana na hati batili za mapokezi ambazo

hazijasainiwa na maafisa wa Serikali (Mwenyekiti wa kata) ili kuthibitisha kama ugawaji ulifanyika.

- iv. Zaidi ya asilimia 90 za viwatilifu vilivyokuwa vinagaiwa na Kampuni ya ICK vilipokelewa na Mwenyekiti wa Kata lakini hakuna ushahidi wa mapokezi ya viuatilifu hivyo kwa wakulima.
- v. Katika Wilaya nyingine baadhi ya wakulima walikuwa wakiuziwa pembejeo, badala ya kukopeshwa kama ilivyoelekezwa na Bodi. Suala hili lilionekana wakati ukaguzi ukifanyika katika kampuni ya KCCL ambapo viambatisho vya malipo aliyotoa na kupokea yenye jumla ya Sh. milioni 2.84 viliwasilishwa kwa wakaguzi.
- vi. Katika maeneo mengi ambapo Kampuni ya KOM ilikuwa inahusika, fomu moja tu ilitumika katika ugawaji wa viwatilifu na vinyunyizi. Hivyo, kuweka ugumu katika kugundua ni nini hasa kiligawiwa kati ya viuatilifu au vinyunyizi. Fomu namba 4 haionyeshi sana kama vinyunyizi viligawiwa kwa wingi.
- vii. Fomu namba 4 ina majina ya wakulima ambayo mengine ni tofauti na ya kwenye vitabu vya risiti.
- viii. Udhaifu katika uhifadhi wa kumbukumbu kwa Kampuni ya S&C Ginning; hivyo kuzorotesha mwenendo wa ukaguzi, ambapo nyaraka zilizotumika katika ugawaji hazikupatikana. Aidha, Kampuni ya Simiyu Commodities walishindwa kuipatia timu ya ukaguzi kumbukumbu za orodha ya wakulima waliopokea viwatilifu.
- ix. Upotevu wa makasha 2 ya DUDUALL 450 EC yenye jumla ya chupa 40 za viwatilifu kutoka kampuni ya S&C Ginning, ambapo Meneja uendeshaji alieleza kuwa makasha mawili (2) yaliibiwa. Hata hivyo, hakuna viambatisho vya kuthibitisha jambo hilo.

Kulingana na dosari hizi nilizozibaini, inaonekana dhahiri kulikuwa na mapungufu katika usimamizi wa zoezi la ugawaji wa viwatilifu na vinyunyizi lililoratibiwa na Bodi ya Pamba Tanzania kupitia vikosi kazi vya wilaya na mawakala wa usambazaji.

Napendekeza Bodi ya Pamba itengeneze namna nzuri ya usimamizi na ufuatiliaji wa mgawanyo wa pembejeo za kilimo cha pamba. Pia, iboreshe fomu namba 4, ikiwamo kuongeza taarifa zaidi kama vile aina za pembejeo zinazosambazwa, kiasi cha pembejeo na ugawaji wake, pamoja na kubuni fomu maalum kwa ajili ya ugawaji wa vinyunyizi.

14.2 Ucheleweshwaji wa ugawaji wa Pembejeo za Kilimo kwa wakulima

Bodi ya Korosho Tanzania iliingia mkataba na kampuni ya Bajuta International Ltd kwa ajili ya kusambaza dawa ya Sulphur yenye tani za ujazo 15,000 kwa mkataba wenye thamani ya Sh. bilioni 18.9. Kulingana na ratiba ya mapokezi, tani za ujazo 7500 zilitakiwa ziwe zimepokelewa kabla ya tarehe 30 Mei, 2018 na kiasi kilichobaki cha tani za ujazo 7500 ziwe zimeshapokelewa kabla ya tarehe 30 Juni, 2018. Hata hivyo, mzigo wote umepokelewa mwezi Agosti 2018 (uchelewaji wa miezi miwili) kinyume na muda uliowekwa kwenye makubaliano. Hakukuwa na makato wala faini iliyotozwa kutokana na ucheleweshwaji huo. Kuchelewa kwa pembejeo hizo kutasababisha kuathiriwa kwa zao husika na hata uzalishaji kushuka, kwani ugawaji utaenda kinyume na msimu.

Napendekeza Bodi ya Korosho Tanzania wahakikishe vigezo na masharti yaliyowekwa kwenye makubaliano yanafuatwa, ikiwamo muda sahihi wa ugawaji wa pembejeo, ili kuepuka kwenda kinyume na msimu wa kilimo.

SEHEMU YA KUMI NA TANO

USIMAMIZI WA MALI ZA MASHIRIKA YA UMMA

15.1 Utangulizi

Mali, Samani na Vifaa ni mali zinazotumiwa na taasisi ili kuwezesha utoaji wa huduma zake au katika uzalishaji wa bidhaa zake.

Mashirika mengi ya Umma yanakabiliwa na changamoto ya kutambua maeneo mali zilipo, thamani yake, hali ya mali husika, matengenezo, kushuka kwa thamani na utunzaji wa rekodi kwenye rejista ya mali zao zilivyo kwa sasa.

Mapitio yangu ya usimamizi wa mali katika Mashirika ya Umma yalibainisha yafuatayo:

15.2 Uhamisho wa Mali Kutoka TANESCO kwenda ETDCO Bila Nyaraka za Kuhamisha Sh. Milion 844.74

Katika uhakiki wa mali za kampuni ya ETDCO, nilibaini kuwa kampuni hiyo ina Mali mbalimbali kama vile majengo, magari, na vifaa vya ofisi vyenye thamani ya jumla ya Sh. milioni 844.74. Mali hizo zilihamishwa kutoka TANESCO kama kampuni mama kwenda ETDCO. Hata hivyo, hakukuwa na hati yoyote ya kisheria inayothibitisha uhamisho na umiliki kwa ETDCO, hivyo kuniwia vigumu kuthibitisha umiliki wa mali hizo kwa ETDCO.

Ninapendekeza TANESCO ikamilishe taratibu za kisheria kuhalalisha umiliki wa mali hizo kwa ETDCO.

15.3 Ukosefu wa Hati ya Uwekezaji wa TANESCO kwa ETDCO Sh. Bilioni 1

Wakati wa mapitio ya muundo wa hisa za ETDCO, nilibaini kuwa TANESCO iliwekeza kiasi cha Sh. bilioni 1 kuwa mtaji wa hisa kwa ETDCO. Hata hivyo, hati ya uwekezaji haikutolewa kwa TANESCO ili kutambua umiliki wake wa hisa. Hali hii

inasababisha ugumu wa kuthibitisha uwekezaji uliofanywa na TANESCO kwa ETDCO.

Ninapendekeza TANESCO kuhakikisha inapata hati ya mtaji wa hisa kwa uwekezaji waliofanya kwenye kampuni ya ETDCO.

15.3 Ukosefu wa Idhini ya Bodi kwenye Thamani Mpya ya Mali za BUWASA Sh. Bilioni 34.13

BUWASA ilithaminisha mali zake mwezi Aprili 2018 kwa Sh. bilioni 34.13 kutoka Sh. bilioni 12.4 hadi Sh. bilioni 46.53 na kuingiza thamani mpya ya mali katika Taarifa za Fedha mnamo tarehe 30 Juni 2018. Hata hivyo, Uongozi ulikubali ripoti bila kupitiwa wala kupitishwa na Bodi. Hii ni kinyume na taratibu za uongozi bora ambao unataka baada ya ripoti kukamilika, ripoti inapaswa kuwasilishwa kwa Bodi ya Wakurugenzi kwa ajili ya mapitio na idhini yake.

Ninapendekeza kuwa, uongozi utafute idhini ya Bodi, kisha kurekebisha taarifa za kifedha ipasavyo.

15.4 Mabwawa ya Taka ya DAWASA Kutotumiwa kwa Ufanisi Sh. Bilioni 2.02

Ukaguzi wa mali za DAWASA katika eneo la Mikocheni kuanzia tarehe 18 Juni 2018 hadi Juni 22, 2018 ulibaini kuwa kuna mabwawa ya taka ya jumla ya gharama za Sh. bilioni 2.02 ambayo yalikuwa hayatumiki kwa kiwango cha uwezo wake. Mhandisi wa DAWASA alielezea kwamba, mabwawa hayo yaliacha kutumika kwa muda mrefu sana kwa sababu zisizojulikana, na hakuna mipango mbadala ya kuendeleza matumizi yake.

Ninapendekeza Mamlaka itumie mabwawa hayo kikamilifu kama ilikusudiwa.

15.5 Malipo ya Fidia ya Ardhi kwa Wakazi wa Kurasini Yaliyofanywa na DAWASA Sh. Bilioni 2.22

Kifungu Na. 13 (2) cha Kanuni za Ardhi ya mwaka 2001 na Kifungu cha 19 (1) - (3) ya Kanuni za Ardhi za Kijiji ya mwaka 2001 vinaainisha kuwa, malipo ya fidia ya ardhi yanatakiwa kufanywa ndani ya miezi sita baada ya kumaliza zoezi la uthaminishaji na upimaji wa ardhi husika. Kushindwa kufanya malipo hayo kutasababisha fidia hiyo kulipwa katika kiwango kinachotumika katika soko kwa wakati huo.

Hata hivyo, Sehemu ya 22 (1) (k) ya udhibiti wa ardhi ya mwaka 2001 inasisitiza kwamba, malipo ya fidia yanapaswa kufanywa endapo kuna haja ya ununuzi wa lazima wa ardhi kwa madhumuni ya Umma.

Kinyume na masharti yaliyotajwa hapo juu, DAWASA ilifanya tathmini ya ardhi mnamo tarehe 16 Agosti, 2013 kwa wamiliki 136 katika eneo la Kurasini Dar es Salaam kwa lengo la kutengeneza mabwawa ya maji taka. Jumla ya walengwa 95 walilipwa fidia ya Sh. bilioni 6.39. Walengwa 41 waliobaki wanaodai fidia ya jumla ya Sh. bilioni 2.22 hawakulipwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018. Kuchelewa kwa malipo ya fidia kwa wahusika husababisha kuchelewa kuanza kwa mradi. Zaidi ya hayo, huweza kufanya malipo yawe juu zaidi kwa mujibu wa kanuni nilizozitaja.

Napendekeza DAWASA kulipa fidia ili kuepuka malipo kuwa makubwa zaidi. Pia, kuhakikisha kwamba, mradi unatekelezwa kama ulivyopangwa.

15.6 Ukosefu wa Hati ya Ardhi na Kushindwa Kufufua Mpango wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Ofisi ya HESLB- Mikocheni B

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) bado haijapata hati ya ardhi kwa jina lake kwa Viwanja Na. 496-509, 492-495, 436, 464, 478 na 480 vilivyopo Mikocheni B. Ardhi ilitolewa na Taasisi ya Elimu ya Tanzania (TIE) kama

ilivyoainishwa katika mkataba wa kukodisha kati ya HESLB na TIE wa tarehe 18 Oktoba 2010 ambapo TIE imelipwa fidia ya Sh. milioni 769.23. Mpaka sasa hati ya ardhi bado ina jina la Taasisi ya Elimu ya Tanzania (TIE).

Ukaguzi wangu pia ulibaini HESLB ilianza ujenzi wa ofisi ya Makao makuu kutoka mwaka wa fedha 2016-17, na kiasi cha Sh. bilioni 2.27 kimekwishatumika. Hata hivyo, mpaka leo ujenzi haujakamilika, ukiwa katika hatua ya msingi. Nilibaini kuwa, ujenzi huo umezuiwa na Msajili wa Hazina kwa barua yenye Kumbukumbu Namba CEA.170 / 344/01 ya tarehe 14 Juni 2016.

Ninapendekeza HESLB kutafuta ufafanuzi kuhusiana na amri hiyo ya kusitisha ujenzi iliyotolewa. Pia, kuendelea kufatilia hati ya ardhi yao kutoka sehemu husika.

15.7 Kutoendelezwa kwa 90% ya Ekari 265 za Ardhi kwenye Kituo cha Ufundishaji cha Kizumbi (MOCU)

Chuo cha Ushirika cha Moshi (MOCU) kinamiliki ardhi yenye ekari 265 katika Kituo cha Mafunzo cha Kizumbi (KTC). Ardhi imekaa kwa muda mrefu bila kuendelezwa.

Ukaguzi niliofanya ulibainisha mapungufu kadhaa, yakiwamo kutotumika kwa asilimia 90 ya ardhi, na pia, ardhi kuvamiwa na wakulima na wachungaji. Hii inatokana na kutowekwa uzio katika eneo la ardhi ya kituo hicho. Ikiwa hatua madhubuti hazitachuliwa, wavamizi wa ardhi wanaweza kuongezeka.

Napendekeza MOCU iendeleze ardhi hiyo ili kuepuka uwezekano wa migogoro ya ardhi ambayo inaweza kusababisha kupoteza ardhi yake.

15.8 Kuchelewa Kukamilisha Ujenzi wa “Campus-Cum-Lecture theaters” Katika Chuo Kikuu cha Mzumbe Sh. Bilioni 2.8

Chuo Kikuu cha Mzumbe kiliingia mkataba No. PA / 013 / 2015-16 / GWND / 22 na “M/s. Afriq Engineering & Construction Co Ltd” kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa- “cum-lecture theaters” katika ndaki ya Mbeya. Ujenzi ulianza mnamo tarehe 1 Septemba 2016 na ulipaswa kukamilika tarehe 1 Julai 2017.

Wakati wa ukaguzi wa mali za Chuo, Oktoba 2018, nilibaini kuwa ujenzi bado haujakamilika. Cheti cha maendeleo ya kazi kilibainisha kuwa, malipo ya Sh. bilioni 1.42 yalikuwa yamekwishafanyika sawa na asilimia 50 ya jumla ya gharama za ujenzi wa Sh. bilioni 2.8.

Ninapendekeza Chuo Kikuu cha Mzumbe kifanye uangalizi wa karibu ili kuhakikisha ujenzi unakamilishwa bila kuchelewa zaidi ili kupata manufaa yaliyotarajiwa.

15.9 Kazi ya Muda Mrefu Katika Majengo na Mashine

Mapitio ya mali zisizohamishika za SIDO yalibaini kuwa, mwaka 2008 SIDO iliingia mkataba na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Korea (KOICA) ili kujenga uwezo wa usindikaji wa kilimo nchini Tanzania kupitia ujenzi wa vituo viwili vya uzalishaji vya kilimo mkoani Dar es Salaam na Morogoro.

Hata hivyo, hadi kufikia Desemba, 2018 ujenzi huo ulikuwa haujamalizika. Nilibaini kuwa KOICA haikuendelea na ujenzi kama ilivyokuwa kwenye makubaliano, lakini ilitoa jumla ya Dola za Kimarekani 400,000 sawa na Sh. milioni 639.98 kwa SIDO ili iweze kuendelea na mradi. SIDO haijakamilisha mradi huo mpaka sasa kwa kuwa Sh. bilioni 1.06 zinahitajika kuukamilisha.

Ninapendekeza SIDO ifanye mazungumzo na KOICA ili kuona uwezekano wa kukamilisha mradi huo.

15.10 SIDO Kutokuwa na Usimamizi wa Kutosha Katika Mpango wa Ujenzi, Utendaji na Uhamisho

Kujenga, kutumia na kuhamisha ni mpango ambao SIDO na wawekezaji walikubaliana juu ya ujenzi wa majengo mbalimbali; na baadaye mwekezaji anahamisha majengo hayo kwa SIDO baada ya kipindi cha miaka 15. Katika mpangilio huu, SIDO huwapa wawekezaji kipande cha ardhi kwa ajili ya ujenzi wa majengo kama ilivyoelezwa katika makubaliano.

Nilibaini kuwa, SIDO haijabainisha viwango vinavyopaswa kutumika katika ujenzi. Kadhalika, hakuna masharti (ya jumla au maalum) yaliyomo katika mkataba kwa ajili ya ufafanuzi wa mahitaji ya mkataba, majukumu, pamoja na dhima na majukumu kwa kushindwa kuzingatia masharti ya mkataba. Aidha, SIDO haina Meneja wa usimamizi mali ambaye angeweza kusimamia mchakato wote wa ujenzi. Zaidi ya hayo, SIDO haifanyi usimamizi na kufuatilia miradi ipasavyo.

Ninapendekeza kuwa SIDO iandae mpango mkakati ya kushughulikia dosari zote zilizobainishwa hapo juu katika usimamizi wa mradi huo.

SEHEMU YA KUMI NA SITA

USIMAMIZI WA MANUNUZI NA MIKATABA

16.1 Utangulizi

Usimamizi wa manunuzi na Mikataba katika Sekta ya Umma unaongozwa na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013.

Manunuzi ya Umma yamekuwa hayaleti matokeo chanya kama yanavyotarajiwa kulingana na mahitaji na kwa wakati unaotarajiwa. Hali hii husababishwa na urasimu wa mchakato wa manunuzi ambao huathiri vibaya utendaji wa manunuzi na utekelezaji wa mikataba.

Mamlaka ya Udhhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) inasisitiza na kufuatilia kwa karibu mambo yafuatayo: kuhakikisha shughuli za manunuzi zinafanyika kwa kiwango kikubwa, na kwa ufanisi ili kupata tija za kiuchumi, kijamii na kimazingira; kufuata Sheria ya Manunuzi wa Umma, 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013 kama zilivyorekebisha mwaka 2016.

Katika mapitio ya michakato ya manunuzi katika mwaka wa fedha 2017/18 nilibaini mapungufu yafuatayo:

16.2 Bohari ya Dawa Ilitoa Zabuni Bila Kupewa Dhamana ya Utendaji Kazi

Kifungu Na. 29 (1) cha Kanuni za Manunuzi ya Umma (2013) inamtaka mtoa huduma aliyefanikiwa kuwasilisha dhamana ya utendaji kazi kuhakikisha ufanisi katika utendaji kazi kwa kadri ya makubaliano ya mkataba. Kadhalika, masharti maalum Na. 8 na masharti ya jumla Na. 10.1 ya mkataba yanahitaji mtoa huduma kuwasilisha dhamana ya utendaji kazi wenye thamani sawa na asilimia 10 ya kiasi cha fedha kilichokubalika katika mkataba.

Katika ukaguzi wa “call of order” 31, nilibaini kuwa, watoa huduma sita (6) (19.4%) hawakuwasilisha dhamana ya utendaji kazi yenye thamani ya jumla ya Dola za Kimarekani 291,323. Mtoa huduma moja (1) alitoa dhamana iliyokuwa chini ya asilimia 10 (alitoa kiasi cha Dola za Kimarekani 71,630 kati ya Dola 102,247 zizokua zikihitajika, sawa na asilimia 3.2). Aidha, watoa huduma 24 waliobaki (77.4 %) waliwasilisha dhamana za utendaji sawa na asilimia 10 ya kiasi kilichopangwa cha “Call of order”.

Pia, nilibaini kuwa hakuna ufuatiliaji wa karibu wa dhamana za benki pale muda wa dhamana unapokuwa umeisha wakati huduma tarajiwa haijakamilishwa na mtoa huduma husika.

Ninapendekeza MSD ihakikishe kuwa watoa huduma wake wanazingatia masharti yaliyotajwa, ikiwa ni pamoja na kuwasilisha dhamana ya utendaji kazi benki. Kadhalika, kufuatilia kwa karibu ili kuhakikisha kuwa dhamana zote za kazi zinanzoendelea haziishi muda wake kabla ya kazi kukamilika.

16.3 Malipo ya fidia ya Uharibifu “Liquidated damages” Sh. milioni 420.82

Bohari ya Dawa iliingia mkataba Na. MSD / 003 / 2011-2012 / HQ / W / 03 tarehe 13 Mei 2013 na M/s. China Railway Jianchang Engineering Co (T) Ltd kwa ajili ya ukarabati wa Makao makuu ya MSD Dar es Salaam kwa jumla ya Sh. bilioni 7.39. Mkataba ulipangwa kuanza tarehe 22 Juni 2013 na kukamilika tarehe 21 Juni 2015, lakini tarehe ya kumalizika iliongezwa hadi 30 Julai 2016.

Tarehe 23 Machi 2018 Mkandarasi aliwasilisha ankara Na. 1465 ya thamani ya Sh. bilioni 1.83 kama gharama ya kazi ya ziada. Hata hivyo, ankara ilionesha kuwa Sh. milioni 420.82 ni kiasi kilichodaiwa kuwa fidia kutokana na hasara aliyopata mkandarasi kutokana na:

- i. Kucheleweshwa kwa siku 43 katika utoaji wa kibali cha kubomoa jengo;
- ii. Kucheleweshwa kwa siku 63 katika kutoa kibali cha ujenzi;
- iii. Kucheleweshwa kwa siku 20 kusubiri idhini ya mhandisi wa miundo na;
- iv. Kucheleweshwa kwa Siku 180 zilizotumiwa na MSD kukamilisha mchakato na kuidhinisha mabadiliko na tofauti za muundo wa jingo.

Hakukuwa na faida yoyote iliyopatikana kwa malipo ya Sh. milioni 420.82. Ninapendekeza MSD ifanye mipango thabiti kabla ya kuingia katika mikataba yoyote.

16.4 Usimamizi wa Mikataba Usioridhisha kwa TANAPA

TANAPA ilifanya miradi miwili mnamo tarehe 06 Mei, 2017 na mkandarasi JECCS Construction & Supplies Ltd na tarehe 09 Februari, 2017 na Secao Builder Co Ltd. Gharama ya mikataba yote miwili ilikuwa ni Sh. milioni 961. Kipindi cha mkataba kwa miradi hii miwili kilimalizika tarehe 17 Februari, 2018 na 10 Oktoba 2017, mtawalia. Hata hivyo, hadi wakati wa kuandika ripoti yangu (Februari 2019) yapata mwaka mmoja (1) kutoka tarehe iliyopangwa kukamilisha miradi hiyo, miradi hiyo haikuwa imekamilika. Miradi iliyopaswa kutekelezwa na wakandarasi hao ilijumuishwa katika mpango wa kimkakati wa shirika la TANAPA wa mwaka 2013 /2014-2017/2018.

Miradi hiyo ni:Ujenzi wa jengo la utawala katika hifadhi ya Tarangire unaofanywa na M/s. Jeccs kwa gharama ya Sh. milioni 569. Pamoja na ujenzi wa lango kuu katika sehemu ya Mto wa Mbu iliyo eneo la Ziwa Manyara unaofanywa na M/s. Secao kwa Sh. milioni 392. Ujenzi wa sehemu zote mbili haujakamilika. Kadhalika, muda wa nyongeza pia ulikuwa umekwisha tangu tarehe 05 Novemba 2018. Hakukuwa na juhudi zozote zilizofanywa na TANAPA ili kuhakikisha miradi hii inakamilika.

Napendekeza TANAPA ifuatilie mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa miradi inatekelezwa na kukamilishwa kwa mujibu wa mikataba.

16.5 Kutokufanyika kwa Tathmini iliyo Bora ya Zabuni ya Kuchapa Nembo ya TPB Bank PLC Sh. Milioni 495.75

Kanuni ya 203 (1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 (marekebisho ya 2016) inataka kufanyika kwa tathmini ya zabuni kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa katika nyaraka za zabuni; na tathmini hiyo itafanywa kwa kutumia vigezo vilivyotajwa wazi katika nyaraka za zabuni na Kanuni ya 213 hutoa vigezo vya mzabuni wa chini.

Benki ya Posta (TPB) ilihusika na manunuzi ya kuchapa nembo mpya ya Benki. Timu ya Tathmini ya Zabuni ilipendekeza M/s. CI Group Marketing Solution kwa bei ya Sh. milioni 224 kama mtoa zabuni. Hata hivyo, Bodi ya Zabuni kupitia azimio lake (Circular resolution) iliazimia kazi hiyo asipewe M/s.CI Group Marketing Solution kwa kigezo kuwa alichelewa kukamilisha kazi ya tawi la Kijitonyama lililotumika kama tawi la mfano. Bodi ya zabuni iliamua kumpa kazi hiyo mzabuni aliyeshika nafasi ya pili, M/s. Jupiter Company Limited, kwa gharama ya Sh. milioni 495.

Maamuzi yaliyofanywa na Bodi ya zabuni yaliongeza gharama kwa Sh. milioni 271 ambayo ni asilimia 120 ya bei ya mzabuni aliyependekezwa awali, ambaye pia alikuwa na uzoefu wa kazi hiyo. Kwa hiyo, benki iliingia gharama kubwa ili tu kutochewa kwa kuchapa nembo ambayo haiwezi kuzuia shughuli za Benki. Huu ni uamuzi unaotia shaka sababu gharama na ongezeko la Sh. milioni 271 haliwezi kuwa sahihi kwa kutengeneza nembo.

Ninapendekeza kuwa Bodi ya Zabuni ya TPB na Menejimenti wafanye upembuzi yakinifu katika kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia taratibu za manunuzi.

16.6 Manunuzi Ambayo Hayajaidhinishwa kwa Benki ya Posta Sh. Milioni 247

Kanuni ya 69 (7) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (2013) inahitaji shirika kuandaa mpango wa manunuzi kwa mahitaji yote ambayo yamepangwa na kubajetiwa. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2017/2018, nilibaini malipo ya ziada yaliyofikia Sh. milioni 247 yaliyofanywa kwenye shughuli zilizopangwa kama ilivyooneshwa kwenye jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 26: Manunuzi ambayo hayajaidhinishwa na Benki ya Posta

| Maelezo ya Manunuzi | Kiasi kilichopangwa (Sh.) | Jumla ya kiasi kilicholipwa (Sh.) | Tofauti (Sh.) |
|---|---------------------------|-----------------------------------|--------------------|
| Ununuzi wa “severs database” ya Rubicon | 345,540,000 | 548,848,256 | 203,308,256 |
| Ukarabati wa Tawi la Temeke | 350,000,000 | 394,609,051 | 44,609,051 |
| Jumla | 695,540,000 | 943,457,307 | 247,917,307 |

Ninapendekeza TPB ifanye mgawanyo mzuri wa fedha na kupanga manunuzi kwa ufanisi kulingana na fedha ambazo wanatarajia kuzitumia katika kipindi cha mwaka husika.

16.7 Kufanya Mabadiliko ya Bei ya Mkataba bila kibali Sh. Milioni 685.33

Kanuni ya 61 (4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (2013) inakataza kufanya mabadiliko ya bei ya mkataba kwa kiasi kinachozidi asilimia kumi na tano ya bei ya awali bila kwanza kupata idhini ya mamlaka inayoidhinisha bajeti.

Ukaguzi wa mikataba ya TBS ulibaini kuwa, katika kutekeleza mkataba Na. PA/044/2017-18/HQ/W/03 kwa ajili ya ujenzi wa uzio na nyumba za walinzi Sh. milioni 498.26 zilitumika. Hata hivyo fedha zilizokuwa zimeidhinishwa ni Sh. milioni 162; hivyo, kufanya ongezeko la Sh. milioni 336.26 bila idhini ya awali ya mamlaka tajwa hapo juu.

Ninapendekeza TBS izingatie bajeti iliyoidhinishwa katika utekelezaji wa utoaji wa fedha, na ikiwa inahitaji kuongeza fedha za ziada ihakikishe inatafuta idhini inayohitajika.

16.8 Kutokufuata Kanuni ya 232 (1) ya Manunuzi Sh. bilioni 20.37

Kanuni ya 232 (1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (2013) inasema kuwa "Afisa Masuuli wa Shirika husika anatakiwa kutuma nakala ya barua ya tuzo ya mzabuni kwa Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Mamlaka, Mdhiniti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mwanasheria Mkuu na Mkaguzi Mkuu wa Ndani. "

Hata hivyo, Bodi ya Nafaka Tanzania (CBT) haikupeleka nakala za barua za tuzo ya mzabuni kwa Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Mamlaka, Mdhiniti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mkaguzi Mkuu wa Ndani kwa mkataba iliyoingia na M/s. Mocrops Tanzania Limited kwa ununuzi wa lita 105 za Hexaconazole 5g/l zenye thamani ya Sh. bilioni 1.47 na M/s. Bajuta International Limited kwa ununuzi wa MT 15,000 ya sulphur (99.5%) kwa gharama ya Sh. bilioni 18.90.

Ninapendekeza CBT ihakikishe kuwa nakala za mikataba yote iliyotolewa zinawasilishwa kwa ofisi tajwa kama inavyotakiwa na Kanuni ya 232 (1) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma (2013).

16.9 Kushindwa kutoza Malipo ya Fidia ya Uharibifu Sh. Bilioni 1.98

DAWASA iliingia mkataba Na. DAWASA/CW/2012-2013/10 na M/s Serengeti ambayo pia iliingia Ubia na NSPT Limited kwa ajili ya kuchimba visima ishirini (20) katika eneo la Kimbiji na Mpera kwa bei ya mkataba ya Sh. bilioni 19.82.

Kifungu namba 8.7 cha mkataba kinabainisha kwamba, endapo mkandarasi hawezi kukamilisha kazi ndani ya muda uliokubaliwa, mkandarasi anapaswa kutozwa fidia kwa kuchelewa kukamilisha kazi kwa kiwango cha asilimia 0.05 ya

bei ya mkataba, lakini isizidi asilimia 10 ya bei ya mwisho ya mkataba.

Tarehe ya kukamilisha kazi iliyokubalika ilikuwa 31 Desemba, 2015. Hivyo basi, fidia ya kuchelewa kukamilisha kazi ilipaswa kuombwa kuanzia Januari 1, 2016 kufikia kiwango cha juu cha asilimia 10, tarehe 18 Julai, 2016 ikiwa ni siku 200 ambazo ni jumla ya Sh. bilioni 1.98.

DAWASA ilipaswa kudai Sh. bilioni 1.98 ikiwa ni fidia inayotokana na kuchelewa kukamilisha mradi. Hata hivyo, DAWASA haikudai pesa hizo.

Napendekeza DAWASA idai fidia hiyo kutoka kwa mkandarasi.

16.10 SUMATRA Kugawana Mapato ya Makusanyo yake na Mamlaka za Serikali za Mitaa Bila Kuzingatia Makubaliano Sh. Milioni 381.62

Kifungu cha 7.1 cha Mkataba wa Maelewano kinabainisha kuwa, ada zinazokusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka kwenye mizunguko yote ya pikipiki na pikipiki zenye magurudumu matatu (tricycles) zinapaswa kugawanywa kwa usawa na SUMATRA.

Ukaguzi wangu ulibainisha kuwa SUMATRA inatoa asilimia 50% ya makusanyo yake kutoka kwenye mizunguko ya pikipiki na pikipiki zenye magurudumu matatu zilizofanywa na ofisi za kanda za SUMATRA kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hii ni kinyume na matakwa ya kifungu cha 7.1 cha makubaliano ambayo yanayotaka kugawanywa kwa makusanyo yaliyokusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na sio makusanyo yaliyofanywa na SUMATRA.

Napendekeza SUMATRA kugawana makusanyo yaliyokusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa tu kama ilivyobainishwa kwenye makubaliano yao.

16.11 Kuchelewa Kukamilika kwa Miradi kwa Mujibu wa Mkataba kati ya CPB na TANFAS Enterprises Limited

Bodi ya Nafaka na Mazao mengine Tanzania (CPB) na TANFAS Enterprises Limited waliingia mkataba tarehe 22 Februari 2017 kwamba TANFAS itatoa huduma za ushauri wa kubuni, kusimamia na kufunga mashine katika viwanda vya mafuta ya alizeti na usagaji wa unga wa mahindi eneo la CPB Kizota Complex Dodoma kwa jumla ya Sh. milioni 270.41.

Pia, tarehe 7 Machi 2017, Bodi ya Wadhamini ya NSSF na CPB zilisaini makubaliano yaliyoeleza kwamba CPB ingepata mkopo wa Sh. bilioni 3.67 kwa ajili ya ufungaji wa mashine katika kiwanda cha kusaga mahindi Dodoma, ujenzi wa kiwanda cha kusindika mafuta ya alizeti na ununuzi wa mbegu za mahindi na alizeti.

Masharti maalum ya mkataba huu yalitaka TANFAS kuhakikisha mradi huu unakuwa tayari ndani ya miezi 6 (yaani 22 Agosti 2017) tokea tarehe ya kusaini makubaliano hayo, yaani 22 Februari 2017. Hata hivyo, mpaka kufikia Novemba 2018, ikiwa ni zaidi ya miezi 15 tokea tarehe iliyokubaliwa ya kumaliza mradi, TANFAS haikuwa imemaliza wala kuanza mradi kama makubaliano yalivyokuwa. Hakukuwa pia na maelezo yoyote yaliyoandikwa na mhandisi mshauri kwa CPB yakieleza sababu za kuchelewa kama inavyotakiwa na Kanuni 12 (21.2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013.

Ninapendekeza CPB itafute ushauri wa kisheria na hatua stahiki zichukuliwe kwa TANFAS kwa kuchelewesha utekelezaji wa mradi na kwa kutokufuata masharti ya mkataba.

16.12 Mapungufu Katika Mkataba wa Kuleta na Kufunga Mashine na Vifaa vya Maabara ya Sayansi Katika Chuo Kikuu cha Dodoma Ikiwa na Pamoja na Kutoa Mafunzo

Chuo Kikuu cha Dodoma kiliingia mkataba wenye namba RFQ/PA/041/2017-2018/G/14 LOT 2 na M/s. Technotrade Investment Ltd kwa ajili ya kuleta, kufunga, kuanza na kufundisha utumiaji wa vifaa na mitambo ya maabara za sayansi kwa Sh. bilioni 2.33.

Kanuni ya 59(1) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inataka mkataba wowote ulio rasmi utokanao na zabuni ambayo thamani yake ni Sh. bilioni 1 au zaidi uhakikiwe na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kusainiwa na pande mbili.

Nilibaini kuwa mkataba huu ulisainiwa kabla ya kuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia mkataba hauoneshi wajibu wa pande zote mbili.

Ninapendekeza Chuo Kikuu cha Dodoma kihakikishe kuwa, wajibu wa kila upande unaelezwa bayana kwenye mkataba na ujulikane kwa pande zote.

16.13 Kuchelewa Kupokea Bidhaa na Huduma Zilizonunuliwa na Chuo Kikuu Dodoma (UDOM)

Chuo Kikuu cha Dodoma kilifanya manunuzi ya kiasi cha Sh. Milioni 201.32 kwa bidhaa za maabara (Dialysis Supplies) kupitia mkataba Na. RFQ/PA/041/2017-2018/G/11 LOT 2-3 wa M/s. Anudha Limited wenye kiasi cha Sh. milioni 151.32; na mkataba wa pili wenye Na.RFQ/PA/041/2017-2018/G/11 LOT 2-3 na M/s. Hasafa Health Sciences Ltd kwa Sh. milioni 50.

Bidhaa hizo zilitakiwa kuletwa chuoni tarehe 11 Julai 2018. Hata hivyo, mpaka kufikia tarehe 31 Desemba 2018, bidhaa hizo zilikuwa bado hazijaletwa chuoni na hakuna gharama za ucheleweshaji zilizokuwa zimetoza kwa mzabuni. Hii ni

kinyume na kifungu 77(4) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 inayotaka kutoza gharama za uchelewaji katika kutekeleza mkataba kwa mkandarasi au mzabuni wa huduma au bidhaa.

Napendekeza UDOM ifuatilie kwa karibu na kuhahakisha bidhaa zilizoununuliwa zinaletwa, na ziwe na ubora ulioelekezwa wakati manunuzi yanafanyika.

16.14 Malipo ya Awali kwa Huduma ambazo Zilikuwa Hazijapokelewa kwa Zaidi ya Miaka Mitatu Sh. Bilioni 1.07

RAHCO ilifanya malipo ya awali ya kiasi cha Dola za Kimarekani 500,000 ikiwa ni sawa na Sh. bilioni 1.07 mwaka 2015 kwa mhandisi mshauri Advisor STG South Africa kwa kazi ya kutoa huduma ya ushauri ya ujenzi wa reli ya Standard Gauge.

Hata hivyo, huduma hiyo haikutolewa kwa RAHCO mpaka kufikia Februari 2019, ikiwa ni miaka mitatu sasa tokea malipo hayo yalipofanyika. Mkataba ulikuwa wa miezi kumi na miwili tangu tarehe ya kusaini mkataba, tarehe 20 Mei, 2015.

Nilitaarifiwa na menejimenti ya RAHCO kuwa suala hili lilikuwa mahakamani kwa hatua za kisheria.

16.15 Kutokutumika kwa OCS 121 System katika Kampasi ya MAMC Mloganzila

Tarehe 16 Desemba 2014 MUHAS iliingia mkataba na SUMSANG C&T Corporation ya Korea Kusini kwa ajili ya kuleta na kufunga vitu mbalimbali, ukiwemo mfumo unaojulikana kama “OCS 121 System Viewer”. Mfumo huo ulifungwa tarehe 26 Julai 2017 kwa mkataba wa Dola za Kimarekani milioni 1.42.

Nilipotembelea kuangalia ufanisi wa mfumo huo, nilibaini kuwa ulikuwa haujaanza kutumika kwa kuwa ulikuwa haujakidhi matakwa na vigezo vilivyokuwa vimebainishwa kwenye mkataba. Niliona pia kuwa, mfumo huo haukuwa unaendana na

matakwa ya watumiaji kwa kuwa ulikosa moduli zilizokuwa zimebanishwa kwenye mkataba, na hivyo haukuwa tayari kutumika kama ilivyotarajiwa. Haya yalibainika wakati wa kufanya majaribio (User Acceptance Test).

Ninapendekeza MUHAS kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa mzabuni ili kuhakikisha vitu vinavyokosekana katika mfumo huo vinapatikana ili ufanye kazi.

16.16 Kuchelewa Kukamilika kwa Mradi wa Victoria Place wa NHC Sh. Bilioni 34.14

Victoria Place ni mradi wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) uliopo vitalu Na. 36 na 37 pembezoni mwa barabara ya Bagamoyo Manispaa ya Kinondoni Dar es Salaam. Mtaji wa uwekezaji uliotarajiwa kwa mradi ilikuwa Sh. bilioni 34.14 ambapo ungechangiwa kwa mgawanyo wa asilimia 70 kutoka NHC na asilimia 30 ikiwa ni mkopo toka taasisi za kifedha. Tarehe 23 Desemba, 2013 NHC ilichukua mkopo wa Sh. bilioni 15 kutoka benki M kwa ajili ya mradi huo. Tarehe 23 Desemba 2013 NHC iliingia mkataba na Group Six International Ltd kupitia mkataba Na. PA/066/2012-2013/HQ/W/12 wa Sh. bilioni 30.28 (ikiwa na VAT) uliotakiwa kukamilika katika miezi 24 (hadi Desemba 2015) tangu tarehe ya kuanza.

Katika ukaguzi wa utekelezaji wa mkataba huo nilibaini kuwa kulikuwa na gharama za ziada zilizoiingiwa bila ya kuwa na sababu za msingi. Mwanzoni upembuzi yakinifu ulipendekeza ujenzi wa nyumba (units) 200 katika majengo 17 kwa gharama ya Sh. bilioni 34.14. Hata hivyo, wakati wa utekelezaji nilibaini kupunguzwa kwa mawanda ya mradi hadi kufikia nyumba 88 katika majengo 14 kwa gharama ya Sh. bilioni 41, ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni 6.86 ikilinganishwa na gharama ya mwanzo. Ongezeko hilo lisilo la kawaida la Sh. bilioni 6.86 litokanalo na kupungua kwa kazi halikutolewa maelezo ya msingi. Pia, nilibaini kuwa, tathmini ya mazingira iliyofanywa

na NEMC ilikuwa ya majengo 10 tofauti na kilichokuwa kimetekelezwa.

Aidha, nilibaini hakukuwa na mkataba wa nyongeza kwa mabadiliko ya kazi katika mradi ambao ungeweza kuonesha mabadiliko yaliyofanyika katika usanifu wa jengo na ujenzi kwa jumla ikilinganishwa na mkataba wa awali. Hii ni kinyume na matakwa ya Kifungu 60(11) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 (iliyorekebisha mwaka 2016) ambacho kinaeleza kuwa, mkataba wowote au marekebisho yake lazima yasainiwe na pande zote ili mikataba hiyo iwe ya kisheria. Mabadiliko yaliyofanyika yalipaswa kuendana na mkataba wa awali ili kulinda maslahi ya shirika kama kungetokea masuala ya kisheria.

Ninapendekeza menejimenti ya NHC kufuatilia utekelezaji wa mradi ili kuhakikisha unakamilika pamoja na changamoto zilizopo. NHC inashauriwa kuhakikisha mabadiliko yote ya kazi yaliyofanywa yanakuwa katika mkataba wa nyongeza.

16.17 Gharama za Mapungufu (defect liability) Ambazo Hazijarejeshwa Baada ya NHC Kuvunja Mikataba

Tarehe 13 Julai 2017 NHC ilivunja mkataba na M/s. Herkin Builders kupitia mkataba Na. PA/066/2012-2013/HQ/W/07 Lots 3,4, 6 na 7. Pia, NHC ilivunja mkataba Na. PA/066/2013-2014/HQ/W/89 na M/s. Afrem Contractors wa uchimbaji visima virefu vya maji na mfumo wa kuyakusanya, kuyatibu na kuyasambaza. Mikataba hii ilivunjwa kwa sababu za kuchelewa kukamilika kwa kipindi cha miaka 3 na 2, mtawalia.

Nilibaini kuwa, kufuatia kuvunjwa kwa mikataba hii, NHC haijaweza kurejeshewa gharama za mapungufu za Sh. milioni 810.86 (ikiwa ni asilimia 10 ya kiasi cha mkataba) kutoka kwa M/s. Herkin Builders. Dhamana ya zabuni hiyo ilikuwa imeisha muda wake. Hii ilikuwa kinyume na kifungu cha 51.1 cha masharti ya jumla na vifungu vya 40 na 41 vya masharti

mahususi ya mkataba ambayo yanataka kukata gharama za mapungufu.

Tarehe 20 Julai 2017 NHC ilikipa kitengo cha Mali na Maendeleo (Directorate of Property and Development (DPD) cha NHC mkataba wa kukamilisha kazi zilizokuwa zimebaki katika zabuni Na. PA/066/2012-2013/HQ/W/07 Lots 3.4,6 na 7 na mkataba Na. PA/066/2013-2014/HQ/W/89 kwa siku 56 kwa gharama nyingine tena ya Sh. milioni 162.73. Hata hivyo, mpaka kufikia Desemba 2018 kazi hiyo ilikuwa haijakamilika.

Ninapendekeza Menejimenti ya NHC itoze gharama za ucheleweshaji kazi kwa mikataba iliyoivunjwa kama inavyotakiwa na kifungu cha 51.1 cha masharti ya mkataba. Pia, iongeze usimamizi wa miradi na kuhakikisha katika mikataba mingine dhamana za zabuni ziko hai muda wote mpaka mkataba unapokamilika.

16.18 Kukataliwa kwa Zabuni Bila ya Sababu za Msingi Kulikosababisha Gharama ya Nyongeza ya Sh. Milioni 563.32
TANESCO iliingia mkataba na M/s. Agro Vision Limited kwa zabuni Na. PA/001/2016-17/HQ/G/01 wa Hand-held X-ray Spectrometer kwa gharama ya Sh. bilioni 1.89. Katika ukaguzi wangu, nilibaini M/s. Infratech Limited ndiye alitakiwa kushinda zabuni hiyo kwa bei ya Sh. Bilioni 1.33 ikilinganishwa na aliyepewa zabuni. Sababu zilizotolewa na menejimenti za kutokumpa zabuni M/s. Infratech Limited ni kwamba, mzabuni hakukidhi muda ulitolewa na zabuni. Pia, alishindwa kuleta dhamana ya zabuni (bid security) kwa muda. Vilevile, hakuweka kiambatisho cha nguvu ya kisheria (power of attorney). Hata hivyo, sababu zote zilizotolewa na TANESCO hazikuwa za kweli mzabuni alileta nyaraka zote na dhamana toka benki ya Biashara ya Afrika (Commercial Bank of Africa (Tanzania) Limited) ikiwa na Namba ya Rejea CBAT/469/2016 ambayo ilikuwa halali kuanzia 20 Januari, 2017 hadi 20 Mei, 2017. Kuhusiana na nguvu ya kisheria, nyaraka hiyo ilikuwa

imeambatishwa kwenye nyaraka za zabuni kama zilivyooneshwa kwenya fomu 9A ya ufunguzi wa zabuni.

Ilionekana pia kuwa, mzabuni aliyepewa zabuni M/s. Agro Vision Limited hakuwa amekidhi matakwa ya zabuni (not responsive bidder) kwa kuwa hakuwa ameonesha namba ya aina ya spectrometers na asilimia (%) ya unyevu kama ilivyotakiwa kwenye vigezo vya kiufundi (technical specifications) katika zabuni. Hii ni kinyume na kanuni ya 206 (2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (kama zilivyorekebisha mwaka 2016) ambayo inataka mzabuni anayeshindwa kukidhi vigezo kukataliwa na taasisi inayonunua; na haiwezekani kukubaliwa baadaye kwa kurekebisha mapungufu yanayokuwa yametolewa au kuondoa masharti hayo kwenye zabuni. Fedha hizo ya ziada kiasi cha Sh. milioni 563.32 ni hasara ambayo ingeweza kuepukwa na TANESCO kwa kuipa zabuni kampuni ya Infratech kwa bei ya Sh. bilioni 1.33.

Kwa mtazamo wangu, sababu zilizotolewa na kamati ya tathmini kumkataa mzabuni mwenye thamani ndogo hazikuwa sahihi kwa kuwa nyaraka zote zilikuwepo katika zabuni iliyowasilishwa.

Ninapendekeza hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa watu waliohusika katika kutathmini. Pia, kuhakikisha kampuni haiingii katika harasa kubwa kwa uzembe.

16.19 Kutokuwapo kwa Ulazima wa Kurudia Mchakato wa Zabuni ya Sh. Milioni 689.19

TANESCO waliingia mkataba namba PA/001/2015/HQ/G/120 na M/s. Interbest Investment Co.Ltd kwa ajili ya usambazaji wa “Toughened Glass Disc Insulator” kwa ajili ya usafirishaji wa umeme njia kubwa ya (Shinyanga-Bulyanhulu 220 KV) ambayo ni zabuni namba 1 na zabuni namba 2 kwa njia ya Chalinze-Hale-Iyungi (132 KV) kwa Sh. Milioni 689.19.

Katika mapitio ya nyaraka za mikataba, niligunda kuwa M/s. Interbest Investment Co.Ltd alipewa mkataba baada ya kurudiwa kwa mchakato wa zabuni. Kabla ya marudio Bodi ya Zabuni ilimpa zabuni mshindani M/s. Peak Traders ambaye alikuwa na bei ndogo ya Sh. milioni 582.32. Hata hivyo, alikataliwa kwa kigezo kwamba bei aliyoomba ilikuwa kubwa sana ikilinganishwa na bajeti ya Sh. milioni 30 iliyotengwa. Taarifa ya uhakiki wa kiasi kilichokuwa kimetengwa kwa ajili ya mchakato huo ambayo imetumwa kwa mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni kwa waraka Na. SMP/MP/PMU/15/31/26 kwa ajili ya kuidhinisha tangazo la zabuni ilionesha kuwa Sh. milioni 710 zilikuwa zimetengwa kwa shughuli hiyo. Kwa hiyo, kurudia mchakato wa zabuni kwa kigezo cha ufinyu wa bajeti na kumpa mshindani mwingine ambaye ana bei ya juu kwa zaidi ya Sh. milioni 106.87 hakukuwa na sababu zinazoeleweka.

Ninapendekeza Menejimenti ya TANESCO ifanye uchunguzi kwenye suala hili na hatua stahiki zichukuliwe kwa wote waliohusika na jambo hili. Aidha, kwa siku za usoni, suala la kurudia mchakato wa zabuni liwe na maelezo yanayoeleweka na yenye tija kwa shirika.

SEHEMU YA KUMI NA SABA

UKAGUZI WA KIUCHUNGUZI NA UKAGUZI MAALUM

17.1 Utangulizi

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amepewa mamlaka chini ya kifungu cha 29 (2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma namba 11 ya 2008 aweze kufanya ukaguzi maalum atakapopokea maombi kutoka kwa Mtu, Taasisi, Wizara, Idara, Mashirika, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mamlaka mbali mbali ambazo yeye ataona inafaa na kuamua kufanya ukaguzi maalum. Kwa kuzingatia Sheria tajwa hapo juu, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilifanya kaguzi maalum zipatazo tisa (9) kwa baadhi ya Mashirika ya Umma katika mwaka wa ukaguzi.

Mashirika ya Umma ambayo kaguzi hizi zilifanywa ni Shirika la Bima la Taifa (NIC), Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA / UDART), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa (NHIF), Shirika la Posta Tanzania (TPC), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Elimu cha Mkwawa (MUCE) na Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Tanzania (COSTECH).

Matokeo ya kaguzi maalum hizi yaliyotolewa katika ripoti hii ni ya muhtasari tu, matokeo ya kina yanapatikana katika ripoti husika na yanaweza kupatikana kutoka kwa Mamlaka iliyoomba Ukaguzi husika.

17.2 Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa (NHIF)

Mnamo tarehe 08 Machi 2013 Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa katika Mkoa wa Mara, ulifungua akaunti ya benki yenye Na. 30310004066, iitwayo NHIF Faida Akaunti Mara, kwenye tawi la NMB Musoma. Madhumuni ya akaunti hii yalikuwa kulipia watoa huduma wa afya walioingia mkataba na kusajiliwa na Ofisi za NHIF katika Mkoa wa Mara. Ukaguzi huu ulifanyika ili kutambua watu ambao walishiriki katika kuwezesha malipo yenye mashaka kwa kipindi cha kuanzia Mei 2013 hadi Machi 2016 kutoka kwenye akaunti. Ukaguzi ulibainisha yafatayo: -

17.2.1 Malipo Hewa kwa Mzabuni ya Sh. Billion 2.61

Uchunguzi wangu ulibaini kuwa, kiasi cha Sh. bilioni 3 kilikua ni malipo hewa. Malipo haya yalitakiwa kulipwa kwa watoa huduma za afya kwa kutumia hundi zilizofungwa. Hata hivyo, malipo yalifanywa kwa fedha taslimu kinyume na Kanuni za NHIF.

Vifungu vyenye kuhusiana na kitabu cha fedha taslimu “cash book” vinaonesha kuwa, malipo yalifanywa kupitia hundi, lakini taarifa za benki zinaonesha kuwa fedha hizi zilitolewa taslim.

Uchunguzi kutoka Benki ya NMB ulionesha kwamba, wateja walilipwa kulingana na mahitaji yao, na hundi zilizowasilishwa benki zilikuwa za wazi. Ni wazi kwamba wahalifu hawa walifanikiwa kutekeleza azma yao kutokana na udhaifu katika uhibititi wa mifumo ya ndani ya uhasibu wa shirika la NHIF.

Uchunguzi wa vitabu vya fedha, taarifa za benki na hati za malipo ulidhihirisha kwamba, kati ya Sh. bilioni 3, Sh. bilioni 2.61 zilikuwa ni za malipo hewa. Kwenye bakaa ya Sh. milioni 393.47, Sh. milioni 350.87 ni za malipo ambayo hayakuweza kubainika yalipofanyika. Aidha, Sh. milioni 42.6 hazikuweza kuthibitika kupokelewa na walipwaji. Wafanyakazi wanne wa NHIF walihusika na kupokea malipo hayo kutoka benki.

Ninapendekeza Mamlaka husika ichukue hatua zinazofaa dhidi ya wafanyakazi wanaohusika katika ubadhirifu uliobainishwa.

Kadhalika, Ofisi ya NHIF inatakiwa ichukuwe hatua za kinidhamu kwa wafanyakazi wote ambao wameshiriki kwenye ubadhirifu wa fedha. Pia, wafanyakazi husika wanapaswa kuwajibika kwa kiasi cha Sh. milioni 42.6 ambazo hazikuweza kuthibitishwa matumizi yake. Pia, Ofisi inapaswa kuwajibika kutoa majina ya watoa huduma waliolipwa jumla ya Sh. milioni 350.87.

17.2.2 Malipo Yaliyofanywa Kinyume na Kanuni za TISS, Sh. Milioni 404.93

Kifungu cha 6.5 (d) cha Taratibu za Hesabu na Fedha za NHIF (2011) kinaainisha malipo yote yanayozidi Sh. milioni 10 yatumwe kwa kutumia TISS. Aidha, maagizo yote kuhusu kuanzisha na kuidhinisha TISS yanapaswa kufuatiliwa kama ilivyoelezwa kwenye Waraka wa malipo ya TISS.

Mapitio yangu ya taarifa za benki, kitabu cha fedha na hati za malipo yanaonyesha kuwa, jumla ya Sh. milioni 404.93 zililipwa kwa watoa huduma kwa fedha taslimu kinyume na kanuni za TISS.

Hatua stahiki zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya maafisa waliohusika kwa kutokufuata Kanuni za TISS.

17.2.3 Ukosefu wa Hati za Malipo kwa Kiasi cha Fedha Taslimu Sh. Bilioni 1.26

Kifungu cha 5.1 cha Mwongozo wa Uhasibu wa Hesabu za NHIF (2011) kinabainisha malipo yote kufanywa kwenye hati ya malipo iliyoambatana na vielelezo vya kuhalalisha malipo hayo. Kadhalika kuwe na idhini kutoka kwa watu wenye mamlaka ya kuidhinisha malipo hayo.

Viambatisho vya nyaraka za malipo ya Sh. bilioni 1.26 zilizotolewa kwa fedha taslimu kwa watoa huduma mbalimbali za afya havikuweza kuonekana wakati wa zoezi la Ukaguzi huu maalum.

Hii inaashiria kwamba hundi ziliandikwa na kupelekwa moja kwa moja benki bila hati za malipo. Kadhalika, ripoti za benki hazikufafanua majina husika ya watoa huduma wa afya waliolipwa. Ukosefu wa nyaraka za viambatisho kwenye hati za malipo huleta mashaka juu ya huduma zilizotolewa na watoa huduma wa afya husika.

Ninapendekeza menejimenti ya NHIF kwa mkoa wa Mara itoe maelezo kwa malipo haya. Aidha, majina ya walipwaji yafahamike. Zaidi ya hayo, hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watunzaji wa hati za malipo.

17.2 Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam (UDSM)

Nilifanya uchunguzi kuona kama chuo kinapata mapato yatokanayo na shughuli za ushauri zinazofanywa na wafanyakazi wake kwa kutumia jina na miundominu ya Chuo Kikuu. Kutokana na tathmini na uchambuzi wa mkataba kati ya BICO na NHC wa gharama ya Sh. bilioni 5.49, nilibaini usimamizi mbovu wa BICO kwa manufaa binafsi kama inavyoelezwa hapa chini:-

17.2.1 Mgongano wa Kimasilahi kati ya Meneja wa BICO na Wamiliki wa Kampuni ya Uhandishi Ushauri Iliyopewa Kazi (Sub contracted)

BICO ni kampuni ya Uhandisi Ushauri iliyosajiliwa na Bodi ya Usajili ya Wahandisi, ikiwa na namba ya usajili 035 kwa kazi za uhandisi mshauri kwa niaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Tarehe 9 Desemba 2013 Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) liliingia mkataba na BICO kutekeleza mkataba wa gharama ya Sh. bilioni 2.60. Baadaye, tarehe 20 Oktoba 2016 BICO na NHC walisaini mkataba wa nyongeza kwa kazi zilizoongezeka zenye gharama ya Sh. bilioni 1.79 (50%) ukiondoa kodi za ndani na huduma zitolewazo na watu wengine kwa gharama ya Sh. milioni 100 na kufanya jumla ya gharama za mkataba kuwa Sh. bilioni 5.49.

Hata hivyo, nilibaini kuwa wakati mchakato wa manunuzi ukiendelea, BICO na kampuni binafsi ya uhandisi ushauri zilisaini mkataba mdogo tarehe 27 Agosti 2013 ikiwa ni sehemu ya mkataba mkuu uliotajwa hapo juu wa kuchangia mapato yatokanayo na ushauri kwa kuzingatia uwiano wa utaalim wa watumishi. BICO iliwakilishwa na watu wawili, mmoja akiwa na nguvu ya kisheria (power of attorney), na wakati huo huo akiwa ni kiongozi wa majadiliano; na mwingine akiwa ni mtaalam.

Katika kufuatilia umiliki wa kampuni iliyoingia mkataba mdogo wa mhandisi mshauri, ilibainika kuwa wawakilishi wa kampuni ya BICO walikuwa wamiliki wa kampuni hiyo binafsi; ambapo mwakilishi mtaalam alimiliki hisa asilimia 40 wakati mwakilishi kiongozi wa majadiliano alimiliki hisa kwa asilimia 20. Hili lilifanyika makusudi ili kiasi kikubwa cha mapato kiende kwa kampuni binafsi ambayo inamilikiwa na wawakilishi hao wa BICO; hivyo BICO kama taasisi ya Umma ifaidike na mapato ya

kiasi cha asilimia 24.4 tu. Pia, wawakilishi hao wa BICO waliitumia BICO kama kampuni iliyo mstari wa mbele ili kukwepa kodi za serikali kama kodi ya zuio kwa kuwa malipo yalitoka NHC kwenda BICO.

Kutokana na makubaliano yaliyosainiwa, BICO ilikuwa na haki ya asilimia 24.4 tu ya jumla yote ya mkataba. Kiasi kilichobaki (cha asilimia 75.6) kilikuwa haki ya kampuni binafsi ambayo ni ya wawakilishi wa BICO. Kuhusiana na mgongano wa kimasilahi, mtaalam kutoka BICO alipokea kiasi cha Dola za Kimarekani 340,000 kama ada za kitaaluma katika mkataba mdogo wa mhandisi mshauri na si kama mtaalam kutoka BICO.

Napendekeza chuo cha Dar es salaam kuhusisha vyombo vya kusimamia sheria kufanya uchunguzi zaidi na hatua stahiki kuchukuliwa.

17.2.2 Malipo Zaidi Katika Mfuko wa Utafiti wa Wanafunzi Sh. Milioni 225.18

Utoaji wa udhamini wa Kitivo cha Mabadiliko ya Hali ya Hewa (Centre for Climate Change (CCCS)) unataka posho za utafiti zilipwe kama inavyokuwa imeidhinishwa na Makamu Mkuu wa Chuo, ambapo ni kati ya Sh. milioni 4 na milioni 10 kwa wanafunzi wa shahada ya uzamili na kati ya Sh. milioni 12 mpaka Sh. milioni 20 kwa wanafunzi wa Uzamivu. Nilibaini kuwa, viwango vilivyolipwa kwa wanafunzi wa uzamili na Uzamivu vilikuwa juu ya vile vinavyokubalika, hivyo kusababisha malipo zaidi katika mfuko kwa kiasi cha Sh. milioni 225.18 kwa wanafunzi.

Ninapendekeza kuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam aelekeze Menejimenti ya mfuko wa Utafiti wa Wanafunzi (CCCS) kuzingatia viwango vilivyopitishwa na Baraza la Chuo katika Mwongozo Mkuu wa Chuo (Prospectus) na miongozo mingine; badala ya kutumia maamuzi na busara binafsi. Pia uchunguzi zaidi ufanywe na hatua stahiki zichukuliwe kwa maafisa watakaobainika kuhusika na mapungufu yaliyosababisha chuo kupoteza rasilimali.

17.2.3 Manunuzi Yasiyo na Ushindani ya Dola za Kimarekani 112,757

Programu ya Ushirikiano Tanzania (Tanzania Partnership Programme- TPP) inatakiwa kuzingatia Kanuni za Manunuzi za Umma kwa kuitisha nukuu za bei kutoka kwa wazabuni wengine ili kupata ushindani wa bei.

Nilibaini kuwa, TPP ilifanya manunuzi ya kiasi cha Dola za Kimarekani 112,757 (sawa na Sh. milioni 235.44) bila ya kuwa na ushindani wa nukuu za bei ili kupata bei zilizo nafuu zaidi. Menejimenti ya TPP ilieleza kuwa mchakato wa manunuzi ulikuwa ghali na mgumu sana kutokana na muda ambao ungetumika kumpata mkandarasi. Naona kuwa kukosekana kwa ushindani, thamani ya fedha haikuweza kupatikana.

Ninapendekeza kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kihakikishe kinafuata matakwa ya Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake ili kupata thamani ya fedha katika manunuzi.

17.2.4 Ada za Taasisi Ambazo Hazikuchagwa Sh. Bilioni 2.97

Miradi ya tafiti inatakiwa kuchangia kwenye taasisi si chini ya asilimia 12 ya jumla ya gharama za mradi wa utafiti kama gharama za uendeshaji wa taasisi. Nilibaini kuwa, kulikuwa na miradi 83 kutokea Desemba 2013 hadi Machi 2018 ikiwa na jumla ya gharama ya Sh. bilioni 25.91. Hivyo miradi hiyo ilipaswa kuchangia jumla ya Sh. bilioni 3.11. Hata hivyo, kiasi kilichochangiwa na miradi hiyo kilikuwa Sh. milioni 141.12 ikiwa ni sawa na asilimia 4.5 ya michango iliyotakiwa. Huu ni ushahidi kwamba, miradi ya utafiti katika Chuo Kikuu haijasimamiwa vya kutosha na hivyo Chuo Kikuu hakifaidi ipasavyo kutokana na miradi hiyo kama inavyopaswa kuwa.

Ninapendekeza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kihakikishe kuwa, sera ya utafiti inazingatiwa katika kuchangia uendeshaji wa taasisi na kubuni utaratibu wenye ufanisi na madhubuti katika kukusanya michango kutoka kwa miradi yote.

17.2.5 Usimamizi Duni wa Mali-Akili (Intellectual Properties) na Maendeleo ya Teknolojia

Sera ya umiliki wa Mali-Akili ya mwaka 2008 inataka Chuo Kikuu kupata kinga ya kisheria katika kutangaza na kuuza kibiashara bidhaa zinazohusiana na Mali-Akili kadri itakavyokuwainafaa kwa maslahi ya Chuo, mtafiti na umma kwa jumla.

Kuanzia 2007 hadi 2018, Chuo Kikuu kilitunza uvumbuzi mmoja kuhusu uchakataji wa juisi ya ndizi na utafiti huo ulihifadhiwa mnamo Septemba 16, 2009. Chuo Kikuu kwa miaka mingi kiliweza kuchapisha tafiti 2,983. Tangu mwaka 1981 hadi Januari 2018, Chuo Kikuu kupitia Technology Development and Transfer Centre (TDTC) kiliweza kubuni, kutengeneza na kuhamisha mashine 66 za aina tofauti pamoja na vipengele 35769 vya mashine. Hata hivyo, ni mvumbuzi mmoja tu alikuwa na haki miliki. Hii ni dalili ya kuwa, Mali-Akili hazitangazwi vya kutosha na Chuo Kikuu.

Hakuna namna nzuri na imara za kutathmini vumbuzi zenye matokeo yanayostahili kupewa Haki Miliki. Hali hii inasababisha kushindwa kuweka wazi vumbuzi kwa ajili ya kupata haki miliki.

Ninapendekeza UDSM itengeneze mfumo madhubuti (database) ili kurahisisha ufuatiliaji na tathmini ya vumbuzi zinazofaa kupata haki miliki. Pia, kutengeneza mifumo imara ya kuchunguza vumbuzi zinazokidhi kupata haki miliki na kufikiria kutoa motisha kwa wavumbuzi bora katika eneo hili.

17.2.6 Udahili wa Wanafunzi kwa Idadi Zaidi ya Matarajio kwa Asilimia 560

Mnamo 2016/2017, UDSM ilidahili wanafunzi kwa zaidi ya asilimia 560 ikilinganishwa na mpango wake. Hii inamaana kuwa, idadi ya wanafunzi waliodahiliwa ilipita uwezo wa Chuo hicho. Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa udahili haukuwa umetolewa taarifa kwa kiwango ambacho kila kitivo kilielewa idadi ya wanafunzi waliotakiwa kudahiliwa. Majadiliano na baadhi ya maafisa yalionesha kuwa, kiwango cha juu cha udahili huo hakikuwa na uwiano na rasilimali nyingine za Chuo kama vile rasilimali watu na miundombinu, ili kukidhi bila shida

ongezeko hilo. Ongezeko hilo kubwa la udahili linahatarisha ubora wa elimu watakaopata wahitimu; hivyo kuwa na athari ya muda mrefu kwa maendeleo ya kitaifa.

Ninapendekeza UDSM itayarishe na kutekeleza mpango wa udahili ambao utatokana na tathmini ya mahitaji na uwezo wa Chuo Kikuu.

17.3 Shirika la Bima la Taifa Tanzania (NIC)

Nilifanya ukaguzi maalum juu ya uzingatiaji wa sheria za manunuzi kwenye mfumo wa compyuta wa kutoa bima za maisha na zisizo za maisha katika Shirika la Bima la Taifa (NIC) na yafuatayo yalibainika:-

17.3.1 Kutokutumika Kikamilifu kwa Mfumo wa GC Ulionunuliwa kwa Dola za Kimarekani Milioni 3.59

Mkataba husika ulisainiwa tarehe 18 Juni 2012 kati ya NIC na muuzaji huduma kwa muda wa miezi saba (7). Menejimenti ya NIC ilikubali mfumo huo wa Bima ya Maisha na Bima zisizo za maisha (Gnisys Configurator System) kwa kusaini taarifa ya majaribio na kulipa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 3.59 kwa muuzaji huduma wa mfumo wakati mfumo huo ulikuwa haufanyi kazi kikamilifu.

Mfumo huo ulitarajiwa kuunganisha maeneo makuu matatu ya kazi za NIC ambazo ni bima ya maisha, bima nyingine na uhasibu. Wakati nikikagua mfumo huo katika eneo la uhasibu, nilibaini kuwa sehemu inayofanya kazi kikamilifu ni kukiri mapokezi ya fedha tu kwa kutoa risiti. Zaidi, nilibaini kuwa mfumo huu hauwezi kutumika kutoa taarifa za kifedha kwa kuwa moduli nyingine hazikuwa zinafanya kazi; hivyo NIC ililazimika kutumia mfumo mwingine wa legacy (UNISYS).

Menejimenti ilikubali kuwa Mfumo huo wa GC ulikuwa unatumika kwa sehemu ndogo, na hauruhusu kuingiza bidhaa nyingine za bima, kiasi na muda wa bima. Pia, mfumo wa bima ya maisha hauwezi kugawanywa katika makundi ya wateja au kwenye kuandaa madai. Aidha, nilibaini kukosekana kwa Viashiria Muhimu vya Utendaji (KPIs) kwa utendaji kazi wa mfumo kama ilijidhihirisha, ambapo maeneo yote yaliyokuwa

hayafanyi kazi yalikuwa yameoneshwa kwa ujumbe uliosomeka 'error encountered'.

Thamani ya fedha iliyotumika kununua mfumo huo haikupatikana kama ilivyotarajiwa kwa sababu haukuwa unafanya kazi kwa ukamilifu.

Zaidi ya hayo, nilibaini tofauti katika mapato ya mwaka yatokanayo na malipo ya bima ya kiasi cha Sh. bilioni 67.03 kati ya taarifa zilizotunzwa kwenye excel (Sh. bilioni 81.94) na mfumo wa GC system (Sh. bilioni 14.91) kuanzia mwaka 2015 hadi 2017. Taarifa zilizotayarishwa nje ya mfumo zinasababisha kuwa na taarifa za mapato zisizo sahihi ambazo zingeweza kuepukwa kwa kutumia mfumo kama ungetekelezwa kwa ukamilifu.

Ninapendekeza NIC iwasiliane na muuza huduma ili kuhakikisha masuala yote yaliyobaki kama ilivyooneshwa katika Hati ya Mahitaji ya Kazi za Mfumo yanatatuliwa; na kwamba, mfumo unafanya kazi kikamilifu kama ulivyotarajiwa.

17.4 Chuo Kikuu cha Elimu Mkwawa (MUCE)

Tathmini hii ya ukaguzi maalum ilizingatia mikataba iliyoingiwa kati ya Chuo Kikuu cha Elimu cha Mkwawa (MUCE) na M/s. MNM Engineering Services Ltd, CATIC, International Engineering Ltd, Epitome Architects Ltd (ilijulikana awali kama Land Plan Icon Limited) kwa ajili ya ushauri na ujenzi wa majengo pacha ya mihadhara ambayo yangeweza kubeba wanafunzi 1000 kila moja na kuongeza wanafunzi hadi 2000. Wakati wa utekelezaji wa mradi, yafuatayo yalibainishwa: -

17.4.1 Kuongezeka kwa Gharama za Mradi Sh. Bilioni 5.48

Mnamo Julai 2010, MUCE iliingia mkataba wa ujenzi wa Mradi na M/s. MNM Engineering Services Limited wa jumla ya Sh. bilioni 3.62. Ujenzi huo ulitarajiwa kuanza tarehe 4 Julai 2010 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 30 Septemba 2011. Wakati wa utekelezaji, kiwango cha kazi kilibadilika kutokana na jiografia ya eneo na kusababisha nyongeza ya Sh. bilioni 1.08, ikiwa ni pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT). Hivyo, ongezeko hilo ni sawa na asilimia 30 ya bei ya awali ya mkataba na

kufanya jumla ya gharama ya mkataba kuwa Sh. bilioni 4.71. Kiwango hiki cha nyongeza hakikuidhinishwa na Bodi ya Chuo.

Tofauti hizi zingeweza kuepukika endapo tu suala hili la taarifa ya Kijiografia ya eneo hilo iliyotolewa na mhandisi mshauri lingeshughulikiwa kama lilivyokuwa limewasilishwa katika mapendekezo yake na ilivyoenezwa katika Mkataba wa Ushauri. Tarehe 28 Novemba 2012, mkataba ulivunjwa kwa sababu ya kushindwa kwa mkandarasi. Baada ya mkataba kuvunjwa, mkandarasi alistahili kulipwa Sh. bilioni 2.67 kulingana na kazi halisi iliyofanyika.

Tarehe 9 Mei 2013, mkandarasi mpya M/s. CATIC International Engineering Limited aliingia mkataba kwa bei ya Sh. bilioni 4.74. Wakati wa utekelezaji kulikuwa na kusimamishwa kwa kazi kwa muda wa siku 582 ambazo ziliongeza gharama ya jumla ya Sh. milioni 991.70 ambazo zingeweza kuepukwa kinyume na kifungu 22.1 cha Mkataba wa Ushauri. Gharama ya kazi chini ya kiwango zilizofanywa na mkandarasi aliyepita pia zilisababisha ongezeko la Sh. milioni 259.67 na riba ya Sh. milioni 178.64 kwa kuchelewesha malipo. Jumla ya bajeti ya mradi huu kwa CATIC ilikuwa Sh. bilioni 6.17. Gharama zote hizi zingeweza kuepukika kwa kuwa kwa kiasi kikubwa kilitokana na makosa ya mkandarasi.

Kazi ya mhandisi mshauri pia ilibadilika mara mbili na kuongeza gharama kutoka bei ya awali ya Sh. milioni 122.84 mpaka Sh. milioni 263.07. Nyongeza za gharama ya mradi zilifanya uwe wa jumla ya Sh. bilioni 9.10. Gharama hii iko juu kwa Sh. bilioni 4.10 (sawa 82%) ikilinganishwa na makadirio ya mhandisi mshauri ya Sh. bilioni 4.99. Pia gharama ziko juu kwa Sh. bilioni 5.36 (sawa na 151%) dhidi ya bei ya mkataba wa awali ya Sh. bilioni 3.75 kati ya MUCE na MNM Engineering & EPITOME Architects Limited.

Ninapendekeza Serikali ifuatilie kwa karibu miradi yake ikiwa ni pamoja na utoaji wa fedha za utekelezaji wa miradi kwa wakati ili kuepuka gharama zisizo za lazima zitokanazo na kusimamishwa kwa miradi na kusababisha gharama za riba na faini.

17.4.2 Kushindwa Kutekeleza Hukumu ya Mahakama Kuokoa Uharibifu / Hasara

Kuvunjwa kwa mkataba kulisababisha kuchelewa kukamilika kwa mradi kwa zaidi ya miaka saba. Hii imesababisha kuongezeka kwa bei kwa sababu ya muda kupita. Hivyo, kazi ambazo hazikukamilika gharama zake zilizoongezeka kwa Sh. bilioni 2.04 hadi Sh. bilioni 4.74 kwenye mkataba mpya.

Baada ya kukoma kwa mkataba na M/s. MNM Engineering Services Limited, MUCE iliwasilisha kesi ya madai katika Idara ya Biashara ya Mahakama Kuu Dar es Salaam dhidi ya M/s. MNM Engineering Services Limited akiwa mshtakiwa wa kwanza.

Mnamo Machi 16, 2016, Mahakama ilitoa hukumu ya kesi Na. 165 ya 2014 dhidi ya mshitakiwa wa kwanza (M/s. MNM Engineering Services Ltd) Mahakama iliamuru mshitakiwa huyo kulipa jumla ya Sh. bilioni 6.99 ikiwa ni fedha zilizolipwa kimkataba na gharama za uvunjaji makubaliano. Pia, iliamuriwa alipe riba kwa kiwango cha biashara na gharama zote za mashtaka. Hata hivyo mshitakiwa huyo hajatekeleza agizo la mahakama.

Ninapendekeza MUCE iwasiliane na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Wizara ya Elimu sayansi na Teknolojia ili kuweza kutambua mali za M/s. MM Engineering limited; na kutafuta njia bora za kukusanya deni hilo kwa mujibu wa mahakama.

17.4.3 Malipo ya Awali bila Dhamana Sh. Milioni 543.53

Kifungu cha 53.1 cha Mkataba kinataka MUCE kumlipa mkandarasi malipo ya awali ya asilimia 15 ya mkataba baada ya kusaini mkataba. Kifungu cha 54.1 kinamtaka mkandarasi kutoa dhamana kwa mteja siku 30 baada ya kusaini mkataba kwa kiasi cha hadi 10% ya gharama ya mkataba.

Nilibaini kuwa, tarehe 01 Julai 2010 MUCE ililipa malipo ya awali ya Sh. milioni 543.53 kabla ya kuwasilishwa kwa dhamana na mkandarasi, kinyume na masharti ya mkataba yaliyotajwa hapo juu. Hata hivyo, tarehe 5 Julai 2010, siku nne baada ya malipo hayo ya awali, mkandarasi aliwasilisha dhamana kutoka benki ya KCB.

Hata hivyo, mahojiano yangu ya kutaka kuthibitisha kama dhamana ya benki iliwekwa bayana, EPITOME Arch Ltd alikiri kuwa, uthibitisho kwa benki ya KCB ulifanywa kwa mdomo.

Idara ya Mahakama ya Biashara ilimwelekeza mshtakiwa kumlipa mdai (MUCE) deni la Sh. milioni 362.35. Benki ya KCB ilijibu kuwa haikutoa dhamana kwa M/s. MNM Engineering Services Ltd kwa ajili ya ujenzi wa jengo la mihadhara (Lecture Theatre). Kwa hiyo hii ilikuwa hasara kwa MUCE.

Dosari zilizobainika hapo juu ni ushahidi kwamba, juhudi za kutosha hazikufanyika hivyo, kusababisha kutokufuatwa kwa masharti ya mkataba.

Kwa mantiki hiyo hapo juu, mhandisi mshauri (EPITOME Architects Limited) hakutimiza majukumu yake, hivyo anawajibika kwa hasara iliyotokea.

17.5 Shirika la Posta Tanzania (TPC)

Nilifanya ukaguzi maalum juu ya vipengele vya mizania ya hesabu ambavyo vilikuwa havikubaliani katika Shirika la Posta (TPC). Yafuatayo yalibainika:-

17.5.1 Kuondolewa kwa Miamala Isiyosuluhishika kwenye Usuluhishi wa Benki Sh. Bilioni 3.62 na Dola za Kimarekani 103,474.96

Nilibaini kuwa, Shirika la Posta Tanzania (TPC) liliondoa miamala isiyosuluhishika bila kufanya uchunguzi na kuitolea maelezo. Kiasi cha Sh. bilioni 1.45 kiliwekwa benki lakini hakikuingizwa katika vitabu vya hesabu/fedha na kiliondolewa katika orodha ya miamala isiyosuluhishika bila kuwa na viambatisho vya kutosha kuthibitisha usuluhisho uliofanyika. Miamala ambayo haikusuluhishwa kwenye vitabu vya hesabu na upande wa mapato ilikuwa ni kiasi cha Sh. bilioni 2.17 na Dola za Kimarekani 103,474.96. Miamala hii ilirekebishwa na kuondolewa kwenye taarifa ya usuluhisho wa benki bila maelezo.

Menejimenti ilielezea kwamba, ufuatiliaji wa kiasi kilichokuwa kikiingizwa katika kitabu cha fedha dhidi ya taarifa ya benki

ulikuwa mgumu kwa kuwa fedha zilizokusanywa ziliingizwa benki kwa ujumla, wakati miamala hiyo iliingizwa katika kitabu cha fedha kwa kipengele kimoja kimoja kama mapato. Hivyo kusababisha mapato mengi kuingizwa mara mbili, kitu ambacho hakikuwa sahihi.

Uondoaji wa miamala ya benki isiyosuluhishwa au amana za fedha katika taarifa ya usuluhishi wa benki bila kufuata utaratibu wa kihisabu husababisha uwezekano wa udanganyifu. Kwa hiyo, napendekeza kuwa TPC irejeshe miamala yote iliyoondolewa katika taarifa ya usuluhisho bila kuwa na viambatisho. Kisha, itafute vyanzo vya miamala hiyo na amana ya fedha kwa kushauriana na mabenki husika.

17.5.2 Akaunti 31 za TPC Zisizotumika kwa Muda Mrefu

Kutokana na wingi wa kazi, Shirika la Posta Tanzania lina akaunti za benki 202 katika mabenki mbalimbali. Kutokana na ukaguzi wa uendeshaji na usimamizi wa akaunti za benki, nilibaini kuwa akaunti za benki 31 zinazomilikiwa na makao makuu ya taasisi zilikuwa hazitumiki kwa muda mrefu (akaunti 28 ziko benki ya CRDB na 3 ni akaunti za benki NBC). Hali hii inakaribisha mazingira ya hatari ya kutumika kwa matumizi mabaya kama wizi. Pia, huongeza gharama za kila mwezi za kutunza akaunti.

Ninapendekeza menejimenti ya shirika ipate idhini ya Mkurugenzi Mkuu kwa ajili ya kufunga akaunti zisizotumika.

17.6 Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) na Usafiri wa Mwendu Kasi (UDART)

Mlipaji Mkuu wa Serikali alimwomba Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalum wa UDA na UDART. Yafuatayo yalibainika:-

17.6.1 Hisa za UDA Ziliuzwa Bila Kuidhinishwa na Msajili wa Hazina

Tarehe 4 Juni 1974, UDA ilikuwa na idadi ya hisa zipatazo 15,000,000 zilizokuwa zimetolewa na kulipiwa zilikuwa hisa 7,119,679 ikiwa ni sawa na 47.5%; na ambazo zilikuwa bado kutolewa zilikuwa hisa 7,880,303 sawa na 42.5% ya hisa zote. Mnamo tarehe 22 Februari 2011, Bodi ya wakurugenzi ya UDA iliingia mkataba na M/s. Simon Group limited (SGL) kuuza hisa

7,880,303 zilizokuwa bado kutolewa kwa bei ya Sh. 145 kwa kila hisa, ikiwa ni Sh. bilioni 1.14 kwa hisa zote.

Kampuni ya SGL ililipa kiasi cha Sh. milioni 285 tu na kubakisha Sh. milioni 857.64. Hii ilikuwa kinyume na Sheria ya Mashirika ya Umma na Sheria ya Msajili wa Hazina kwa kuwa Bodi ya Wakurugenzi haikuwa na mamlaka ya kuiuza UDA ambayo ilikuwa inamilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali kabla ya kuuza hisa zake zilizokuwa bado kutolewa Februari 2011.

Mnamo Februari 2016 kampuni ya SGL ilirejesha hisa hizo kwa Msajili wa Hazina. Hata hivyo, Hesabu za UDA hazikuonesha hisa hizo zilizorejeshwa; hivyo, kusababisha taarifa zisisizo sahihi kwa watumiaji wa hesabu hizo.

Serikali ilipoteza faida yake kama mwanahisa kutokana na maamuzi yasiyo ya kisheria ya Bodi ya Wakurugenzi wa UDA kwa kipindi cha miaka 3 tokea 22 Agosti 2013 mpaka Februari 2016 kwa kuuza bila faida yoyote hisa ambazo hazikuwa zimetolewa.

Ninapendekeza maamuzi yoyote yanayoathiri mtaji na utendaji wa kampuni yoyote inayomilikiwa na Serikali yahusishe Mamlaka kama inavyotakiwa na sheria. Hisa zilizorejeshwa kwa Msajili wa Hazina zitolewe kwa Serikali ili iweze kuwa mwanahisa mwenye hisa nyingi.

17.6.2 Kuongezeka kwa Mtaji wa UDART bila Kuidhinishwa na Msajili wa Hazina

Kampuni ya UDART ilianzishwa 19 Desemba 2014 ukiwa na mtaji wa Sh. bilioni 1.5 (hisa 15,000 kwa Sh. 100,000 kwa kila moja). Kati ya hisa hizo, 14,850 zinamilikiwa na UDA ambayo ni sawa na asilimia 99 na Simon Group Limited inamiliki hisa 150 sawa na asilimia 1.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi nilibaini kuongezeka kwa mtaji kutoka Sh. bilioni 1.5 mpaka Sh. bilioni 225 (yaani kutoka hisa 15,000 zenye thamani ya Sh. 100,000 kila moja mpaka hisa 2,250,000,000 zenye thamani ya Sh.100 kila moja). Mabadiliko haya ya hisa na mtaji hayakuwa pia yamesajiliwa na Msajili wa Biashara na Wakala wa Leseni (BRELA).

Zaidi ya hayo, nilibaini pia kuwa mmiliki wa pili, yaani Msajili wa Hazina hakuhusishwa katika mchakato wa kuongeza mtaji na idadi ya hisa.

Ninapendekeza Serikali, UDART na wanahisa wote wjadiliane na kukubaliana kuhusu uhitaji wa kuongeza mtaji na idadi ya hisa za UDART.

17.6.3 UDART Kujiendesha kwa Hasara ya Sh. Bilioni 6.78

Mradi wa mabasi ya Mwendo Kasi Dar es Salaam ulianza tarehe 10 Mei 2016. Katika tathmini ya miezi minane kuanzia tarehe ya kuanza kwa mradi mpaka tarehe 30 Desemba 2016 nilibaini kuwa, kampuni ya UDART imekuwa ikifanya kazi kwa hasara kwa kuwa jumla ya matumizi ilikuwa kubwa zaidi ya mapato kwa kiasi cha Sh. bilioni 6.78. Jumla ya matumizi ilikuwa Sh. bilioni 26.57 wakati mapato yalikuwa Sh. bilioni 19.78. Pia nilibaini kuwa hasara hii ilitokana na kutunza vibaya taarifa za matumizi kama inavyoonekana hapa chini:-

- i. UDART ilitoa taarifa za gharama za mafuta kuwa Sh. bilioni 6.02, wakati leja ya mafuta ilionesha kiasi cha mafuta ni Sh. bilioni 4.79. Taarifa hii ilikuwa zaidi kwa kiasi cha Sh. bilioni 1.25.
- ii. UDART ililipa Sh. milioni 750 kwa M/s. Longway Engineering Services kwa kujenga uzio katika kituo cha mabasi Kimara, Kivukoni, Ubungo na Morocco. Hata hivyo, uzio ulijengwa Kimara tu kwa Sh. milioni 241.69 wakati hakukuwa na ujenzi wa fensi katika vituo vingine vitatu vilivyotajwa. Kiasi kilicholipwa cha Sh. milioni 508.31 kwa ajili ya fensi katika vituo vitatu hakikuthibitika kama kilirejeshwa; hivyo kuwa na uwezekano mkubwa kuwa kilitumika vibaya.

Napendekeza UDART ihakikishe kiasi kilichoizidishwa kinarekebishwa kwenye taarifa. Pia, kiasi kilicholipwa kwa kazi ambayo haikufanyika cha Sh. milioni 508.31 kirudishwe; na hatua za kisheria zichukuliwe kwa wote waliohusika.

17.6.4 Uwekezaji wa Serikali Usio na Tija

Serikali kupitia kwa Msajili wa Hazina inamiliki hisa 3,488,651 katika kampuni ya UDA ikiwa ni sawa na 49% ya hisa zilizotolewa na kulipiwa. Hisa za serikali zina thamani kati ya Sh. bilioni 2 na Sh. bilioni 4.32 kufuatana na taarifa ya tathmini ya mali iliyofanyika mwaka 2012. Hata hivyo, Serikali haijawahi kupata gawio lolote kutokana na uwekezaji huu katika UDA tokea kuanzishwa kwake. Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi kwa mwaka 2015/2016 na 2016/2017 ilionesha mwendelezo wa hasara kuwa sababu ya kutolipa gawio. Hivyo, uwekezaji wa Serikali katika UDA umekuwa si wa tija tokea ulipofanywa. Hivyo, napendekeza Serikali kufuatilia kwa ukaribu shughuli za UDA.

17.6.5 Idadi ya Mabasi ya Mwendo Kasi Isiyotosheleza

Katika awamu ya kwanza ya utekelezaji, mradi ulitakiwa kununua mabasi 305. Hata hivyo, mabasi yaliyopo ni mabasi 140 sawa na 45.9% ya mabasi 305 yaliyotakiwa kuwapo. Upungufu wa mabasi 165 ambao ni sawa na 54.1% unaleta changamoto ya mrundikano wa abiria. Mabasi yanajaa sana, na hivyo uchakavu wake unatarajiwa kuwa juu, tofauti na ilivyotarajiwa. Hii ni kwa sababu ya kubeba abiria wengi zaidi ya uwezo wa mabasi hayo.

Napendekeza UDART iongeze kasi ya kutekeleza makubaliano ya kuongeza mabasi ili kukidhi mahitaji ya sasa kwa kutoa huduma nzuri.

17.6.6 Kusimamishwa Uuzaji wa Kadi kwa Abiria kwa Sababu ya Gharama Kubwa ya Manunuzi

Kutolewa kwa Kadi za kulipia kulisitishwa kwa sababu ya gharama kubwa ya uzalishaji wa kadi hizo. Gharama hiyo ni kubwa kuliko mauzo yake kwa abiria. Nilibaini kuwa, gharama ya kuzalisha kadi moja ni Sh. 4,500 ikiwa ni pamoja na kodi za serikali na gharama za uagizaji, wakati serikali ilitangaza kadi moja kuuzwa kwa Sh. 500

Ninapendekeza, UDART iwasiliane na Serikali kutafuta ufumbuzi juu ya suala hili kwa kuwa matumizi ya kadi yanasaidia sana kupunguza upotevu wa mapato yanayoweza kutokea kwa kutumia tiketi za kawaida.

17.6.7 Deni la TRA ambalo Halijaripotiwa katika Hesabu za UDA Sh. Bilioni 5.35

Nilibaini kuwa Sh. bilioni 5.35 za TRA hazikuripotiwa kwenye taarifa za fedha za UDA kama sehemu ya deni lake. Deni hili lilithibitishwa na TRA kupitia barua yenye Kumb. Na. TRA/CCE/C/1 ya 31/1/2018. Kati ya deni hilo, Sh. bilioni 2.11 zilikuwa adhabu ya kuchelewesha kulipa kwa wakati.

Ninapendekeza UDA itambue deni la TRA la Sh. bilioni 5.35 katika taarifa zake za hesabu.

17.7 Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH)

Wakati wa ukaguzi maalum katika Tume hii, yafuatayo yalibainika:-

17.7.1 Kutokuwepo kwa Kanuni za Kuongoza Shughuli za COSTECH/NFAST

Mfuko wa Taifa kwa Utangazaji wa Sayansi na Teknolojia (NFAST) ulianzishwa na kifungu cha 23 (i) cha Sheria ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania Na. 7 ya mwaka 1986. Kifungu cha 25 (4) cha sheria hiyo pia kinaeleza kuwa Waziri anaweza, kwa kanuni zilizochapishwa gazetini, kutayarisha/kutoa Kanuni na miongozo ya Mfuko huo. Hata hivyo, mpaka kufikia Juni 2018 hakukuwa na kanuni zinazohusiana na sheria hiyo ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania.

Menejimenti ilinitaarifu kuwa suala hili lilikuwa tayari limewasilishwa kwa Waziri anayehusika mara kadhaa hivyo, zilikuwa katika mchakato wa kuandikwa; lakini kasi ya kulifanyia kazi jambo hilo ilionekana kuwa ndogo. Ukosefu wa kanuni kwa Sheria ya COSTECH unasababisha mkanganyiko katika kuitafsiri na kuitekeleza Sheria hiyo.

Ninapendekeza kuwa Tume, kwa kushirikiana na Wizara ipendekeze marekebisho ya sheria ya COSTECH ya mwaka 1986 na kutengeneza kanuni ili kuongeza ufanisi katika kutekeleza shughuli za Tume.

17.7.2 Matumizi Mabaya ya Kibali cha Kuajiri

Tarehe 25 Julai 2012, Katibu Mkuu Utumishi PO-PSM aliiruhusu COSTECH kutafuta watu kujaza nafasi mbili zilizokuwa wazi kwa kuwa Tume ya Ajira ya Serikali (PSRS) haikuweza kupata watu wenye sifa, yaani Mkurugenzi wa Sayansi ya Jamii na Afisa Mkuu wa Tafiti.

Hata hivyo, tarehe 18 na 19 Desemba 2012 COSTECH ilitafuta nafasi za watu wengine kumi ambao hawakuwa sehemu ya kibali cha ajira kilichotolewa. Hii ni kinyume na taratibu za ajira.

Menejimenti ilielezea kuwa walipewa kibali cha kuajiri; lakini, kibali cha kuajiri kilichosemwa kilitolewa tarehe 25 Aprili 2013 wakati nafasi hizo zilikuwa tayari zimeshajazwa.

17.7.3 Matumizi Mabaya ya Madaraka

COSTECH ilitoa kiasi cha Sh. milioni 800 kwa Taasisi ya Afya Ifakara (IHI) katika vipindi tofauti bila kuwa na mamlaka sahihi ya Bodi ya Makamishina wa COSTECH. Taasisi ya Afya Ifakara ilikiri kupata fedha hizo na kuzitumia, lakini sikuweza kutambua fedha hizo zilitumika kwa matumizi gani. Hii ni kwa kuwa, fedha hizo zilichanganywa na fedha nyingine. Zaidi ya hayo, COSTECH iliipatia Dar Techno Hama Business Incubator (DTBi) kiasi cha Sh. bilioni 1.1 kwa vipindi tofauti bila ya kuwa na makubaliano yoyote. Pia, DTBi inahudumiwa na COSTECH, na wamepewa ofisi bure, ikiwa ni pamoja na kulipiwa gharama nyingine kama umeme na maji. Gharama hizi zinalipwa na COSTECH ingawa DTBi ni taasisi binafsi tokea mwaka 2011.

Ninapendekeza COSTECH kufuata taratibu zilizopo katika kutoa ruzuku. Pia, ihakikishe kuwa taasisi hizi mbili (IHI na DTBi) zilizopewa fedha zinatumia fedha hizo kwa malengo yaliyokusudiwa. Aidha, pawe na uwajibikaji wa fedha hizo, ikiwa ni pamoja na kuzitolea taarifa kwa COSTECH.

17.7.4 COSTECH Ilitoa Ruzuku Bila kuwa na Mkataba Sh. Bilioni 1.73

Kifungu cha 4.1.5 cha Mwongozo wa Ruzuku kinataka kuwa, mara baada ya maombi ya ruzuku kukubaliwa, mwombaji atasaini mkataba kabla ya kupewa fedha. Hata hivyo, nilibaini

katika kipindi cha 2011/2012 mpaka 2016/2017 COSTECH ilitoa ruzuku ya Sh. bilioni 1.73 kwa watafiti 10 bila mikataba. Hivyo, ninapendekeza menejimenti ya COSTECH ihakikishe inazingatia taratibu zilizopo za kutoa ruzuku, na kuhakikisha kiasi cha Sh. bilioni 1.73 zilizotolewa zinatumiwa kama ilivyokusudiwa. Aidha, matumizi yake yatolewe taarifa kwa COSTECH kwa ajili ya uwajibikaji.

17.7.5 Fedha Zilizorejeshwa Benki ya Dunia kwa sababu ya Kutozingatia Sheria za Manunuzi Sh. Bilioni 1.15 na Dola za Kimarekani 716.21

Nilibaini kuwa, Benki ya Dunia ilitoa fedha kiasi cha Sh. bilioni 1.15 kupitia Mradi wa Sayansi na Teknolojia Elimu ya Juu Tanzania (Tanzania Science and Technology Higher Education Project (STHEP)) ili kuongeza uwezo wa mtandao (bandwidth) mpaka kufikia STM 1. Mradi huu ulichukuliwa na Benki ya Dunia kuwa mradi wenye manunuzi yasiyofaa. Hii ni kutokana na kutozingatiwa kwa sheria na kanuni za manunuzi, ikiwa ni pamoja na kushindwa kufuatilia ruhusa (no objection) toka benki hiyo wakati wa kutathmini zabuni. COSTECH ililazimika kutumia kiasi cha Sh. bilioni 1.17 kutoka vyanzo vingine kilichokuwa kimepangwa kutekeleza miradi mingine. Zaidi ya hayo, Dola za Kimarekani 716,207 zilirejeshwa Benki ya Dunia moja kwa moja kutoka FDR kutokana na matatizo katika manunuzi.

Ninapendekeza kuwa COSTECH ihakikishe inazingatia kikamilifu masharti ya fedha za wafadhili ili kuwahamasisha kuendelea kufadhili miradi ya Tume.

17.7.6 Kushindwa Kutumia Fedha za Wafadhili kwa Wakati Sh. Bilioni 1.31

Tume ilishindwa kutekeleza shughuli za kujenga uwezo zilizokuwa nimefadhiliwa na Benki ya Dunia katika kipindi kilichokuwa kimepangwa. Matokeo yake, kiasi cha Dola za Kimarekani 530,440 na 64,035 ikiwa sawa na Sh. bilioni 1.17 na Sh. milion 140.88, mtawalia, zilirejeshwa Benki ya Dunia na SIDA. Ni maoni yangu kuwa haya yalisababishwa na mipango mibovu na uzembe katika kuzingatia matakwa ya makubaliano

na wafadhili. Hivyo, napendekeza COSTECH izingatie masharti ya fedha za wafadhali.

17.7.7 Kuingia katika Miradi Isiyo na Tija ya Sh. Milioni 874

Nilibaini kuwa, COSTECH haifanyi tathmini ya umuhimu wa miradi na uwezo wa kuitekeleza kabla ya kutoa fedha. Nilifanya mapitio katika miradi mitano yenye thamani ya Sh. milioni 874 nakubaini kuwa ilikuwa imekamilika bila kuwa na tathmini ya tija kwa miradi hiyo. Matokeo yake, miradi hiyo ilikosa uendelevu na haikuweza kufikia malengo yaliyotarajiwa. Miradi hiyo ni mradi wa viazi vitamu, kuongeza uzalishaji wa kuku kupitia chanjo ya kuthibiti magojwa ya mfumo wa hewa, utafiti wa kuboresha uzalishaji wa zao la muhogo, utafiti wa kusaidia utumiaji wa njia mbadala ya kutunza misitu ili kuhuisha bustani za majumbani na kuzijaribu njia zilizobuniwa za kufanya ufugaji wa kijadi kuwa wa kibiashara katika miradi ya Tanzania.

Ninapendekeza Tume ihakikishe inafanya tathmini ya tija ya miradi na uendelevu wake kabla ya kuitekeleza ili kupata thamani ya fedha na faida kwa wananchi.

17.7.8 Kutokuwapo kwa Kanzidata (Database) za Kina za Tafiti na Miradi

Nilibaini kuwa COSTECH haikuwa na kanzidata kwa aina za tafiti na miradi iliyofanywa, matokeo yaliyopatikana, mafundisho yaliyotokana na tafiti/miradi hiyo na kinachotakiwa kufanyika kwa kila utafiti au mradi uliotekelwa ili kuwa na rejea imara kwa maamuzi na ushauri. Ninashauri COSTECH ianzishe na kutekeleza kanzidata kama nyenzo ya kupata na kutunza vizuri taarifa.

17.7.9 Mapungufu Katika Kutekeleza Mradi wa ICT Park

Serikali ilipanga kutengeneza mradi wa ICT Park village ili kuongeza chachu ya kukua kwa teknolojia. ICT Park ililenga kutengenezwa na miundombinu inayofaa ambayo ingesaidia kuvuta uwekezaji mkubwa katika makampuni ya ICT. COSTECH ilionekana kuwa ndiyo ingekuwa taasisi inayofaa kutekeleza wazo la mradi huu. Katika mwaka wa fedha 2012/2013; kiasi cha Sh. bilioni 5 zilitolewa na Serikali kama mtaji wa kuanzia.

Hata hivyo, utekelezaji wa mradi huu ulikutana na changamoto kama zilivyoenezwa hapa chini:

- (i) **Masharti Yasiyofaa katika Randama ya Makubaliano (MoU)**
COSTECH na Export Processing Zone Authority (EPZA) ziliingia kwenye Randama ya Makubaliano (MoU) na makubaliano ya pamoja ya kutekeleza mradi wa ICT Park tarehe 26 Mei 2014. Masharti yaliyowekwa katika makubaliano hayakuwa ya haki kwa COSTECH kwa misingi hii: makubaliano hayo yalitaka pande zote mbili kuchangia kiasi sawa cha mtaji kwa mradi, masharti ya uchangiaji yalikuwa tofauti. Mchango wa EPZA ulikuwa kodi ya pango ya eneo la heka 300 ambayo ingekusanywa kwa miaka 10 iliyokadiriwa kuwa bilioni 3.94. Hata hivyo, nilibaini kuwa COSTECH ililipa fidia ya Sh. bilioni 1.17 kwa eneo hilo. Zaidi ya hayo, makubaliano hayo yaliitaka COSTECH kutoa fidia kwa wakazi wa eneo hilo la mradi la ekari 438 badala ya ekari 300 zilizotajwa awali. COSTECH ilitakiwa kulipa EPZA fedha ambazo zingetumika kulipa fidia hiyo ya eneo la mradi. Kiwango cha fidia kwa ekari kilikuwa Sh. milioni 3.4. Kwa mantiki hii, gharama ya fidia kwa ardhi yote ya ekari 300 ilipaswa kuwa Sh. bilioni 1.02 (ekari 300 x Sh. milioni 3.4) ukiondoa tozo za kuchelewa kulipa fidia hiyo na gharama nyinginezo za uendelezaji wa ardhi.

Nilibaini kuwa jumla ya eneo lililotolewa fidia na COSTECH lilikuwa zaidi ya ekari 383.307 lililogharimu Sh. bilioni 1.71 badala ya Sh. bilioni 1.02 zilizotakiwa. Hii inamaanisha kuwa, COSTECH ililipa zaidi kwa kiasi cha Sh. milioni 693.2, kinyume na randama ya makubaliano na makubaliano ya pamoja. Malipo zaidi yalitokana na kuongezeka kwa eneo lililotolewa fidia ikiwa ni pamoja na tozo kwa kuchelewa kulipa fidia hizo. Yote haya yalikuwa kinyume na makubaliano yaliyomo kwenye randama ya makubaliano na makubaliano ya pamoja.

Ninapendekeza COSTECH kupitia nyaraka za makubaliano na masharti yaliyomo ili kufanya majadiliano yenye tija kwa pande zote mbili kama makubaliano yataendelea kuwepo.

17.7.10 Kutokuandaa Taarifa za Utendaji kwa Fedha za TTMS Sh. Bilioni 8.42

TCRA imekuwa ikitoa fedha za Mfumo wa ufuatiliaji wa mawasiliano ya Simu (TTMS) kwenda COSTECH tangu Septemba 2015. Jumla ya Sh. bilioni 8.42 zilipokelewa na COSTECH kutoka TCRA kwa kipindi cha Septemba 2015 mpaka Juni, 2017. Kwa mujibu wa kifungu cha 4 (i) cha Mwongozo wa matumizi ya fedha za TTMS katika mfuko wa NFAST, COSTECH inatakiwa kupeleka taarifa za utekelezaji wa fedha za TTMS wizarani kwa kila robo mwaka na taarifa za mwaka.

Hata hivyo, nilibaini kuwa taarifa za utekelezaji hazikuandaliwa na kupelekwa katika Wizara husika, kinyume na makubaliano yaliyooneshwa katika mwongozo. Matokeo yake, Serikali (Wizara) haina taarifa sahihi juu ya fedha za TTMS zinazoweza kusaidia katika maamuzi.

Ninapendekeza kuwa Menejimenti ya COSTECH itoe taarifa za utekelezaji wa fedha za TTMS kwa Wizara husika na wadau wengine kama inavyotakiwa.

17.7.11 Mikopo Ambayo Haijarejeshwa Sh. Milioni 469.25

Katika kipindi cha mwaka 2011/2012, COSTECH ilianzisha mpango ya kutoa mikopo. Mpango huo ulikuwa na kiasi cha Sh. milioni 648.5 zilizotolewa kwa taasisi 3 ambazo hata hivyo zilishindwa kurejesha kiasi cha Sh. milioni 469.25. Ukaguzi ulibaini kuwa mpango huo ulishindwa na hakukuwa na mkopo mpya uliotolewa tangu hapo. Taasisi zilizoshindwa kurejesha mikopo yao ni: CARMATEC kiasi cha Sh. milioni 255), Tanzania Engineering & manufacturing Design (kiasi cha Sh. milioni 147.5) na Tanzania Automotive Technology Centre (Sh. milioni 66.75). Mpango huo ulioanzishwa na COSTECH yawezekana haukuwa umefanyiwa utafiti. Pia ulikosa usimamizi, ufuatiliaji na tathmini wakati wa utekelezaji.

Ninapendekeza COSTECH iangalie hatua stahiki za kuchukua kwa taasisi zilizoshindwa kurejesha fedha za mkopo na kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa.

17.8 Mfuko wa Pesheni wa NSSF

Katika kipindi cha Julai 2018 nilianzisha uchunguzi uliolenga kuangalia madai ya taasisi kwa miaka 2015/2016 na 2016/2017, uwekezaji katika dhamana na majengo, utumiaji wa mfumo wa ERP, na usimamizi wa rasilimali watu. Ukaguzi huo maalum ulibaini yafuatayo:

17.8.1 Hasara katika Kununua Ardhi ya Sh. Bilion 4.17

Mfuko wa NSSF uliingia mikataba tarehe 16 Septemba 2010 na 12 Oktoba 2010 wa kununua ekari 277 (Muuzaji wa kwanza) na ekari 180 (Muuzaji wa pili) eneo la Kiluvya kwa Sh. bilioni 3.32 na Sh. bilioni 1.62, mtawalia. Kufuatia mapitio ya taarifa ya tathmini ya ekari 277 nilibaini kuwa thamani ya ardhi hiyo kwa kipindi cha mwezi Oktoba 2010 ilikuwa Sh. milioni 416.40; wakati makadirio ya thamani ya soko kwa ekari 180 ilikuwa Sh. milioni 720. Kwa hiyo, gharama ya ardhi iliyonunuliwa ilizidishwa kwa kiasi cha Sh. bilioni 2.90 na Sh. milioni 900 mtawalia na hivyo, kusababisha jumla ya hasara kuwa Sh. bilioni 3.80. Nilibaini pia kuwa, muuzaji wa kwanza aliripoti mauzo yake kwa TRA kwa Sh. milioni 900 badala ya Sh. bilioni 3.32, kwa sababu hiyo kodi (stamp duty) ya Sh. milioni 24.24 haikulipwa.

Zaidi ya hayo, nilibaini hasara nyingine ya Sh. milioni 370 iliyotokana na NSSF kununua ekari 67.4 kwa muuzaji bandia eneo la Nunge, Bagamoyo. Mahakama ya wilaya katika shauri la madai shauri Na. 7 la 2003 na Mahakama Kuu katika Rufani ya Madai ya shauri Na. 7 la 2006 ilibaini kwamba, muuzaji hakuwa mmiliki wa ardhi ambayo iliuzwa kwa NSSF. Kwa ujumla, NSSF ilipata hasara ya Sh. bilioni 4.17 katika kununua ardhi na ililipa kiasi kidogo cha kodi (stamp duty) kwa Sh. milioni 24.24.

Ninapendekeza kuwa Bodi ya Mfuko na Menejimenti ichukue hatua stahiki kwa wale waliohusika katika mchakato mzima wa kununua ardhi iliyosababisha hasara hiyo ya Sh. bilioni 4.17 kwa NSSF.

17.8.2 Uwekezaji katika Hisa za Vodacom Unaotoa Faida Ndogo kuliko Dhamana za Serikali Sh. Bilioni 47.5

Kifungu cha 9(1) na (2) cha Mwongozo wa Uwekezaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2015 kinataka Bodi ya Wadhamini wa kila mfuko kuwekeza katika vitega uchumi ambavyo faida zake ni zaidi ya ile ya hati fungani (dhamana) za Serikali. Aidha, kama mfuko unahitaji kuwekeza katika uwekezaji ambao faida yake ni chini ya ile ya dhamana za serikali, unatakiwa kupata idhini ya Benki Kuu ya Tanzania.

NSSF iliwekeza kiasi cha Sh. bilioni 47.5 kwa kununua hisa 64,000,000 za Vodacom zikiwa na faida iliyo chini ya faida kutoka dhamana za Serikali, kinyume na mwongozo wa uwekezaji. Faida iliyotarajiwa kutoka hisa za Vodacom kama gawio ni 2% kwa mwaka 2017. Dhamana za Serikali za muda mrefu (bond) kwa miaka 5 mpaka tarehe 12 Aprili 2017 ingetoa faida ya 17.92%; na zile za muda mfupi (Treasury bill) zingetoa faida ya 15% ambazo ziko juu zaidi ya zile za hisa za Vodacom. Tarehe 5 Aprili 2017 NSSF iliomba BoT iwaruhusu kuwekeza kwenye hisa za Vodacom. Hata hivyo, tarehe 10 Aprili 2017 Bodi ya Wadhamini ya NSSF iliidhinisha mfuko kutumia kiasi cha Sh. bilioni 40 katika kuwekeza Vodacom kabla ya kupokea idhini kutoka BoT.

Tarehe 20 Aprili 2017 BoT ilikataa kuidhinisha uwekezaji huo kwa msingi kwamba, faida inayoachwa (opportunity cost) na kuwekeza katika hisa za Vodacom ilikuwa kubwa sana, na kwamba, hakukuwa na taarifa za kutosha zinazoonesha kwamba kulikuwa na mategemeo ya kuwa faida ya uwekezaji katika hisa za Vodacom ingepanda na kuwa juu ya ile ya dhamana za Serikali. Hivyo, uwekezaji katika hisa za Vodacom ulikuwa na athari zaidi kwa mfuko. Pamoja na kushauriwa kitaalam na BoT kwamba mfuko usiwekeze Vodacom, tarehe 28 Aprili 2017 mfuko ulinunua hisa 47,058,820 kwa kiasi cha Sh. bilioni 39.99; na baadaye tena uliongeza, Sh. bilioni 7.59.

Kutokuzingatiwa kwa mwongozo wa Mifuko ya Hifadhi za Jamii ya mwaka 2015 kwa kuwekeza katika hisa za Vodacom ambazo zinatoa faida chini ya faida ya dhamana za serikali bila kuwa na idhini ya BoT kuweka fedha za Mfuko katika athari ya kupata faida ndogo ikilinganishwa na fursa nyingine zilizokuwapo.

Ninapendekeza kuwa hatua za kiutawala zichukuliwe ili kuhakikisha fedha za mfuko zinazalisha faida stahiki. Vivyo hivyo, hatua stahiki zinatakiwa kuchukuliwa kwa maofisa waliohusika kusukuma uwekezaji katika hisa za Vodacom, kinyume na mwongozo na ushauri wa BoT.

17.8.3 Mapungufu katika Utoaji Mikopo kwa Watumishi na Wachangiaji wa NSSF ili Kununua Hisa za Vodacom Sh. Bilioni 1.86

Mfuko ulitoa mkopo bila riba wa Sh. bilioni 1.65 kwa watumishi na Sh. milioni 206 kwa wachangiaji (Members) wengine ili kununua hisa za Vodacom. Hata hivyo, hakukuwa na mikataba kati ya Mfuko na wanufaika hao. Pia, namna ya urejeshwaji wa mikopo iliyotolewa kwa wachangiaji wengine imebaki kuwa mashakani. Mkopo uliotolewa kwa wachangiaji wengine ulikuwa kinyume na mafao yaliyoelezwa katika sehemu ya Sheria ya Pesheni ya NSSF ya mwaka 2015.

Kukosekana kwa mikataba kwa fedha zilizolipwa kwa ununuzi wa hisa za Vodacom kati ya Mfuko na wanufaika wa mkopo kunaweka mazingira ya wakopaji kutokurejesha mikopo hiyo.

Hivyo naushauri Mfuko uweke rasmi utaratibu wa mikopo iliyotolewa na uweke masharti mahususi kuhusiana na mikopo hiyo. Aidha, uanzishe hatua thabiti za kurejeshwa kwa mikopo hiyo ili kukwepa kupata hasara ya fedha hizo.

17.9 Taasisi ya Elimu Tanzania

Nilifanya ukaguzi maalum kuhakiki usahihi wa gharama zilizotumika kuchapisha aina za vitabu 44 vya kiada kwa darasa la kwanza (I) mpaka darasa la tatu (III) kidato cha kwanza (I) mpaka kidato cha sita (6) katika taasisi ya Elimu Tanzania (TIE). Ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo:

17.9.1 Uchambuzi wa Dosari katika Aina 44 ya Vitabu vya Kiada Haukufuata Muongozo wa Tathmini ya Vitabu

Mwaka 2014 Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE), miongoni mwa vitu vingine, ilipewa mamlaka ya kuzalisha, kuchapisha na kusambaza vitabu vya kiada vya shule ya msingi (darasa la I mpaka darasa la III) na vya shule ya Sekondari (kidato cha

I mpaka kidato cha VI). Katika mwaka 2014/15 TIE ilizalisha na kuchapisha aina 44 tofauti za vitabu vya kiada kwa ajili ya elimu ya msingi kwa Sh. bilioni 25.59.

Mwaka 2017 TIE ilisimamisha usambazaji wa vitabu hivyo kufuatia viashiria kuwa vitabu hivyo vina makosa ya kiufundi. Tathmini ya kiasi cha makosa iliyofanywa na jopo la walimu ilibaini kuwa aina za vitabu vya kiada 21 vilikuwa na makosa makubwa ya kiufundi, wakati vitabu vya kiada 23 vilikuwa na makosa madogo ya kiufundi. Hata hivyo, tathmini hiyo haikuwa na muongozo, hivyo matokeo yake hayawezi kuaminika. Hii ni kwa kuwa haikuzingatia Muongozo wa Tathmini ya Vitabu wa mwaka 2015.

Kutotumia muongozo kwenye tathmini kunabatilisha matokeo. Hii ni kwa kuwa unakosekana uhakika wa kuwepo kwa makosa ya kiufundi katika vitabu. Wizara ya Elimu na Taasisi ya Elimu wanashauriwa kufanya tathmini ya ubora wa maudhui wa aina 44 za vitabu kwa kutumia Muongozo wa Tathmini ya Vitabu wa mwaka 2015.

SURA YA KUMI NA NANE
UKAGUZI WA UFANISI KATIKA SEKTA YA MADINI, GESI NA
MAFUTA

18.1 Utangulizi

Sekta ya uchimbaji madini, gesi na mafuta inahusisha utafutaji na uchimbaji mali ghafi kutoka ardhini ili kutumiwa na watu. Sekta ya uchimbaji inajihusisha na kutafuta chuma, madini na kokoto kutoka ardhini. Mchakato wa uchimbaji unaweza kuwa ni pamoja na uchimbaji wa mafuta na gesi, madini na ukataji miamba. Nchi inajulikana kwa kuwa na rasilimali za madini na amana ya gesi lakini bado udhaifu uliobainika unaweza kuzuia kupata thamani ya mali asili hizi kwa uchumi wa nchi.

Ukaguzi wangu ulihusisha mapitio ya ufanisi wa udhibiti uliofanywa na wadau muhimu wa Serikali katika sekta kama vile Wizara ya Madini, Tume ya Madini, TANSORT, Shirika la Madini la Serikali (STAMICO), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Udhibiti wa Petroli (PURA) na Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC).

18.2 Mapitio ya Utendaji wa STAMIGOLD - Biharamulo

Nilifanya ukaguzi maalum katika kampuni ya STAMIGOLD nikiwa na lengo la kuhakiki mali na madeni yake kabla ya kutekelezwa kwa mpango wa ufilisi wa hiari baada kampuni kuwa inapata hasara kwa miaka mitatu mfululizo. Pia, ukaguzi ulilenga kuchunguza kama kampuni ilikuwa na uwezo wa kulipa madeni yake. Mawanda ya ukaguzi huu yalikusishwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 1 Julai 2015 hadi 30 Agosti 2018. Ufuatao ni muhtasari wa yaliyoonekana:

18.1.1 Kushuka kwa Uzalishaji wa Dhahabu na Kusababisha Mwendelezo wa Hasara

STAMIGOLD ni kampuni tanzu ya State Corporation (STAMICO). Ni kampuni inayomilikiwa kwa asilimia 99 na STAMICO, asilimia 1 ilimilikiwa na Msajili wa Hazina. Huu ni Mgodi wa dhahabu uliochukua shughuli za African Barrick Gold Mines baada ya kuwa umenunuliwa na STAMICO.

Mapitio ya taarifa za uzalishaji, taarifa za fedha na nyaraka nyinginezo muhimu kwa miaka mitatu zilionesha mwendelezo

wa kupungua kwa uzalishaji wa dhahabu kutoka wakia (ounces) 14,286 mwaka 2015/16 mpaka wakia 6,011 mwaka 2017/18 ikiwa ni kushuka kwa asilimia 58. Kushuka kwa uzalishaji kulisababisha kushuka kwa mauzo ya dhahabu katika miaka husika, ambapo mauzo yalikuwa Sh. bilioni 60.11; Sh. bilioni 39.02 na Sh. bilioni 17.93 kwa mwaka 2015/16; 2016/17 na 2017/18 mtawalia (Tazama jedwali 27). Kushuka huku ni kwa kiasi cha Sh. bilioni 42.19 ikilinganishwa na mauzo ya mwaka 2015/16 na 2017/2018 ikiwa ni sawa na asilimia 70.

Jedwali Na. 27: Mwenendo wa Uzalishaji, Mauzo na Gharama kwa Miaka Mitatu

| Mwaka | Uzalishaji (Ounce) | Mauzo (Bilioni) | Gharama za Uzalishaji (A) (Bilioni) | Matumizi Mengine (B) (Bilioni) | Jumla ya Gharama (A+B) (Bilioni) | Gharama kwa mwaka (Bilioni) |
|---------|--------------------|-----------------|-------------------------------------|--------------------------------|----------------------------------|-----------------------------|
| 2015/16 | 24,073 | 60.112 | 44.286 | 27.538 | 71.824 | 12.306 |
| 2016/17 | 12,774 | 39.017 | 33.085 | 25.433 | 58.518 | 19.496 |
| 2017/18 | 6,011 | 17.925 | 14.669 | 11.715 | 26.384 | 8.457 |

Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi Maalum

Nilibaini kuwa, baadhi ya sababu za mwendelezo wa hasara ni gharama kubwa za kukodi mitambo na mashine ambazo ziliongeza gharama za uzalishaji. Pia, ni kushuka kwa ufanisi katika kuzalisha dhahabu ambapo STAMIGOLD ilizalisha kati ya gram 0.7 mpaka gram 2 kwa kila tani ikilinganishwa na uzalishaji uliokuwa ukifanywa na Barrick Gold Mine wa gram 10 mpaka 25 kwa kila tani. Nilibaini pia, kuchakaa kwa mitambo iliyokuwa ikitumika kutenganisha chembechembe kubwa na ndogo za madini. Hali hiyo ilisababisha Stamigold kupoteza mapato ya kiasi cha Sh. bilioni 10.5 kutokana na upotevu wa matope susu (tailings).

Zaidi ya sababu hizo, nilibaini kuwapo kwa vitendo vya ubadhirifu vilivyofanywa na aliyekuwa Meneja Mkuu na watumishi 11 ambao walituhumiwa kufanya vitendo vya ubadhirifu kwa kushirikiana na wazabuni na wakandarasi. Kukosekana kwa ulinzi madhubuti kuzunguka mgodi pia kulisababisha matukio ya wizi wa mchanga wa dhahabu. Kulikuwa pia na matumizi yasiyodhibitiwa kiasi cha kusababisha kuwa na gharama kubwa za uendesaji.

Ingawa kumekuwa na kushuka kwa uzalishaji na hasara zilizoripotiwa kwa miaka mitatu, nilibaini kuwa kumekuwa na

ufanisi katika uzalishaji kwa kipindi cha nusu ya mwisho ya 2017/2018 (Januari hadi Juni 2018). Hii ni kufuatia mabadiliko ya uongozi, ambapo Meneja Mkuu alibadilishwa Desemba 2018. Katika kipindi hiki kampuni iliweza kulipa madeni yote yahusianayo na mishahara ya watumishi ambayo haikuwa imelipwa kwa miezi mitano. Pia, taarifa za ufanisi katika kipindi hiki zilionesha kuwa, Kampuni ilikuwa na mapato yanayozidi matumizi/gharama za uzalishaji kwa Sh. bilioni 2.21 (Mapato yakiwa Sh. bilioni 15.03 na matumizi ya Sh. bilioni 12.82). Hii inamaanisha kuwa, Kampuni ina fursa ya kufanya vizuri mbeleni kama Menejimenti itazingatia malengo na kuongeza bidii.

Kwa kuzingatia matokeo hayo hapo juu, ninachukulia kuwa mwenendo mbaya wa utendaji kwa kiwango kikubwa ulisababishwa na uongozi mbovu na usimamizi na ufuatiliaji usioridhisha wa wamiliki wa mgodi, yaani STAMICO na Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango. Pia, naona muda wa miaka mitatu ulikuwa unatosha kwa STAMICO kuchunguza sababu za mwendelezo wa hasara za mgodi, hivyo ingeweza kuchukua hatua haraka za kurekebisha mapungufu kabla hali haijawa mbaya.

Ninapendekeza Serikali kupitia STAMICO na Msajili wa Hazina iimarisha usimamizi wa mara kwa mara na kufanya tathmini ambayo zitasaidia kugundua dalili zote za kushuka kwa utendaji hivyo kutoa miongozo kwa muda na kuelekeza kabla mambo hayajaharibika.

18.1.2 Madeni ya Muda Mrefu ya Kampuni ya Stamigold

Pamoja na kushuka kwa utendaji na uzalishaji wa dhahabu, madeni ya kampuni yalikuwa mpaka kufikia kiasi cha Sh. bilioni 95.09 tarehe 30 Juni 2018. Madeni haya yalikuwa ni pamoja na madeni ya kibiashara, madeni ya watumishi, madeni kwa tasisisi za Umma, na madeni ya kisheria kama inavyo elezwa zaidi kwenye jedwali 28 hapa chini:

Jedwali Na. 28: Orodha ya Madeni Yasiyolipwa kwa Muda Mrefu

| Na | Aina ya Madai | Kiasi cha Madai (Sh.) |
|----|----------------------------------|--------------------------|
| 1 | Madeni ya Kibiashara | 46,918,391,799.76 |
| 2 | Madeni ya Kisheria | 16,586,395,644.74 |
| 3 | Madeni yatokanayo na Kodi | 1,983,029,952.82 |
| 4 | Madeni ya Wafanyakazi | 165,370,336.67 |
| 5 | Madeni ya Kerekebishia Mazingira | 29,417,713,000.00 |
| 6 | Madeni Mengineyo | 17,591,969.89 |
| | Jumla | 95,088,492,703.88 |

Nilibaini kuwa, kuongezeka kwa madeni kulitokana na sababu tofauti. Baadhi yake ni kubadilika kwa bei halisi ikilinganishwa na bei zilizokuwa kwenye mikataba ya kutoa huduma na bidhaa; kushuka kwa ufanisi wa kampuni kulikosababisha kushuka kwa uzalishaji, hivyo kushuka uwezo wa kuwalipa wazabuni na wakandarasi; zabuni zilizotolewa kinyume na makubaliano katika mikataba ya huduma na vitu na kusababisha kuongeza matumizi; kutokuzingatia sheria za kodi ambapo kodi hazikulipwa ndani ya muda kama PAYE na SDL kwa kiasi cha Sh. milioni 5.376 na sh. milioni 1.26, mtawalia.

Sehemu ya deni hilo inatokana na Mkataba wa ulinzi kati ya SUMA JKT Sh. milioni 97 kwa mwezi kuanzia Januari 2016 mpaka Januari 2017, ambapo deni la mkataba huu lilifikia kiasi cha Sh. bilioni 2.03 ilipofika tarehe 30 Juni 2018. Deni hili lilihusisha madeni ya kipindi ambacho SUMA JKT alitoa huduma bila kuwa na mkataba ambacho ni kati ya Januari 2014 mpaka Januari 2016 na Januari 2017 hadi Juni 2018. Katika mkataba wa kununua viatilifu (Reagents) mbalimbali kati ya Stamifold na Waja General Co. Ltd, nilibaini kulikuwa na ongezeko la bei la Dola za Kimarekani 173,629 kutoka Dola za Kimarekani milioni 1.24 zilizokuwa zimetajwa kwenye mkataba mpaka Dola za Kimarekani milioni 1.42. Mkataba kati ya STAMIGOLD na Alpha Choice Company Ltd kuuza vyakula ulionesha samaki halisi waliouzwa kwa kampuni kwa mwaka ni kilo 37,660 wakati mahitaji yalikuwa ni kilo 7,200 sawa na ongezeko la zaidi ya mara nne ya mahitaji. Muuzaji pia alileta nyama kilo 32,868

totauti na mahitaji yaliyoko kwenye mkataba ya kilo 8,400 ambalo pia ni sawa na ongezeko la mara nne ya mahitaji.

Hata hivyo, pamoja na madeni yaliyokuwa hayajalipwa ya Sh. bilioni 95.08, Stamigold ilikuwa na jumla ya mali za thamani ya Sh. bilioni 387.89 mpaka Januari 2016 ambazo ni mara nne ya madeni. Hata hivyo, uthamini wa mali hizi ulifanyika mwaka 2016; kwa hiyo, thamani ya mali ya sasa ingeweza kuwa imebadilika sana na hivyo kubadili uwiano wa madeni na mali.

Ni maoni yangu kuwa, matukio hayo yaliyotolewa hapo juu yalisababishwa na udhaifu wa kusimamia mikataba na kukosekana kwa makadirio halisi ya mahitaji wakati wa kuandaa zabuni za kutoa huduma na bidhaa. Pia, menejimenti ina wajibu mkubwa kama inavyoweza kushuhudiwa kwa mabadiliko ya uongozi kutoka matumizi mabaya ya fedha kwa Meneja Mkuu aliyepita na kuonesha kuimarika kwa ufanisi baada ya mabadiliko ya Menejimenti.

Ninapendekeza STAMIGOLD na STAMICO ziimarishe usimamizi wa mikataba na kuhakikisha makubaliano katika mikataba yanazingatiwa. Pia, STAMIGOLD iendelee kupanga na kuweka vipaumbele katika kulipa madeni yaliyobaki na yale yanayofikia muda wa kulipwa. Mwisho, STAMIGOLD ifanye uthamini wa mali zake kujua thamani halisi ya mali za kampuni kwa sasa.

18.2 Tathmini ya Ufanisi wa Utendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

Nimepitia mikakati na uendeshaji wa kiufanisi wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC). Ukaguzi ulilenga kutathmini ufanisi wa shirika katika kusimamia Taarifa za Mauzo ya Gesi Asilia na Vitalu vya Gesi Asilia (4/1B na 4/1C) katika kutoa mchango unaotakiwa katika nchi.

Yafuatayo ni baadhi ya mapungufu yaliyobainika:

18.2.1 Msukumo Mdogo katika Kutekeleza Maelekezo ya Iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini

TPDC kama Kampuni ya Mafuta ya Taifa imekuwa ikiomba leseni ya utafiti wa mafuta na gesi katika vitalu Na. 4/1B na 4/1C. Wakati inajibu maombi ya TPDC kupitia barua yenye kumbukumbu Na. CBE.144/369/01/3 ya tarehe 15 Oktoba 2015, Wizara ilieleza kuwa Serikali ilikuwa na mpango wa kuvitunza vitalu hivyo kwa maslahi ya Umma. Aidha, ilikuwa na mpango wa kuandaa mazingira mazuri ya kulipa Shirika la TPDC vitalu hivyo. Hivyo, Shirika la TPDC lilielekezwa: (i) Kuongeza thamani ya vitalu Na. 4/1B na 4/1C kwa kununua taarifa za kijiolojia na miamba; na kuandaa taarifa za tathmini za kijiolojia na matarajio; na (ii) kufanya tathmini ya kitakwimu na kiuchumi kwenye umuhimu wa modeli ya mshirika wa kimkakati na makubaliano ya ushirika ya kawaida na kuishauri Wizara. Matokeo ya maelekezo haya yatamwezesha Waziri kutoa ruhusa ya kumtafuta mshirika wa kimkakati.

Nimepitia maendeleo ya utekelezaji wa maelekezo ya Wizara na kubaini kuwa, Shirika la TPDC limeongeza thamani kwenye vitalu tajwa kwa kufanya tathmini ya madhara ya kimazingira (Cheti chenye usajili Na. EC/EIS/2317 cha mwezi Machi 2016), tathmini ya viashiria vya hatari, uwezekano wa kiuchumi na kifedha wakati ukusanyaji wa taarifa za mtetemo kwa mfumo wa 2D ulipofanywa na Kampuni ya WesternGeco na ION GXT kati ya miaka ya 1999 na miaka ya 2000, na tafsiri husika kufanyika mwaka 2017. Hata hivyo, hakukuwa na ushahidi kuwa, TPDC walipeleka ripoti walizoagizwa kwa iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini ili kumwezesha Waziri kutoa maamuzi ya wao kuendelea. Badala yake, TPDC iliendelea kuomba leseni ya uchunguzi wa mafuta na gesi. Ombi la karibuni zaidi lilifanyika tarehe 18 Februari 2018. Hata hivyo, Wizara ya Nishati imeendelea kuisisitiza kutolewa kwa ripoti/nyaraka kama inavyoelekezwa na Kifungu cha 44(4) cha Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015 kuhusiana na Waziri kutoa idhini.

Maoni yangu ni kuwa, kukosekana kwa ripoti na nyaraka zilizotajwa kwenye maelekezo kunamchelewesha Waziri kutoa idhini na utaratibu unaofuatia wa kuwapa TPDC vitalu husika. Zaidi ya hayo, nalihusisha suala hili na kushindwa kutoa ripoti na

kutokuwa na muda maalum wa kutekeleza maagizo yaliyotolewa na Wizara na TPDC kukamilisha shughuli za kuongeza thamani.

Ninapendekeza TPDC iongeze kasi ya taratibu za kuongeza thamani ya vitalu 4/1B na 4/1C kama kigezo muhimu kwa Serikali katika kukuza sekta ya gesi nchini. Aidha, ninapendekeza TPDC kutoa ripoti inayohusiana na uongezaji wa thamani kwenye vitalu na uchambuzi wa kitakwimu na kiuchumi kwenye umuhimu wa kuwa na mshirika wa kimkakati dhidi ya makubaliano ya ushirika na kuifikisha Wizara ya Nishati.

18.2.2 Kukosekana kwa Mpango Mbadala wa Kushughulikia Kushuka kwa Uwezo wa Kifedha wa Madalali

Shirika la TPDC limeingia mkataba na madalali kwa ajili ya kuuza taarifa zake za mitetemo ya miamba. Nimepitia ufanisi wa mikataba katika kufikia malengo yaliyowekwa. Nilibaini kuwa, katika mwaka wa ukaguzi ulioishia 30 Juni 2018 ni dalali mmoja tu kati ya watano ambaye alifanya mauzo ya Dola za Kimarekani 174,000, wakati wanne wengine hawakufanya mauzo kabisa. Zaidi, nilibaini kuwa kushuka kwa mauzo kunaweza kuwa kulisababishwa na kushuka sana kwa bei za hisa za madalali watatu (WesternGeco kama kampuni tanzu ya Schlumberger Ltd, ION GXT naCGG Robertson) zilishuka kwa asilimia 62, 89 na 99, mtawalia, kwa kipindi cha miaka mitano mpaka kufikia tarehe 10 Disemba 2018 (Tazama jedwali la 29). Changamoto zilizotajwa na matatizo ya kifedha kutokana na kushuka kwa thamani ya hisa imesababishwa kwa kiasi kikubwa na kutetereka kwa sekta ya Mafuta na Gesi Duniani.

Jedwali Na. 29: Bei za Hisa za Madalali wa Kuuza Taarifa za Mitetemo ya Miamba

| Jina la Kampuni | Muda uliozingatiwa (Kwa Miaka) | Bei za juu katika muda uliozingatiwa | Bei za sasa | Asilimia zilizoshuka |
|------------------|--------------------------------|--------------------------------------|-------------|----------------------|
| Schlumberger Ltd | 5 | USD 117.50 | USD 45.10 | 61.62% |
| ION GXT | 5 | USD 69.45 | USD 7.53 | 89.16% |
| CGG Robertson | 5 | €240.63 | €1.41* | 99.41% |

Chanzo: Tovuti ya CGG na Yahoo finance tarehe 10 Desemba 2018. * CGG iliongeza mtaji kwa kuuza hisa kwa wanahisa wake katika bei ya punguzo mwaka 2016 ambayo ilisababisha kushuka zaidi kwa thamani ya hisa zake.

Katika ripoti yangu ya mauzo ya taarifa za mtetemo wa miamba ya mwaka uliopita (Juni 2017) nilibaini kuwepo kwa umuhimu wa kutoa majukumu kwa baadhi ya watendaji wa TPDC katika ukusanyaji wa taarifa za kiintelijensia za viashiria vya hatari katika soko la mafuta ili kuchukua hatua za kiintelijensia kwenye athari hasi dhidi ya soko.

Hata hivyo, TPDC bado haijaanzisha utaratibu wa kukusanya taarifa za kiintelijensia za soko ambao utahusisha kuanzisha kitengo cha intelijensia ya viashiria vya hatari vya masoko chenye watumishi wenye ujuzi. Hivyo, TPDC haijaweza kujua changamoto ambazo zimetajwa na hali ngumu ya kiuchumi inayowapata madalali katika utendaji wao. Matokeo yake, Shirika halina mpango wowote mbadala wa kuweza kupambana na changamoto zinazolikabili, ikiwamo mauzo ya taarifa za mitetemo ya miamba.

Kutokana na kukosekana kwa utaratibu wa kukusanya intelijensia ya masoko na mpango mbadala kwa changamoto za mauzo ya taarifa zinazowakabili madalali, ni maoni yangu kuwa changamoto hizi zinaathiri uwezo wa TPDC kuchangamsha na kukuza uchunguzi na uzalishaji wa Sekta ya Mafuta na Gesi.

Ninarudia mapendekezo yangu yaliyopita kuwa TPDC ianzishe kitengo cha intelijensia ya viashiria vya hatari vya masoko na kuishauri menejimenti katika sintofahamu ya soko la kimataifa. Zaidi ya hayo, ninapendekeza TPDC kuwapa majukumu watu wenye kiwango kinachostahiki cha ujuzi kufanya kazi hiyo na pia, iwe na mpango mbadala ili kuweza kupunguza athari za kushuka uwezo wa madalali. Pia, TPDC ikuze uchunguzi ili kuongeza uzalishaji wa mafuta na gesi.

18.2.3 Kutokununua Data za Mtetemo wa Miamba za 3D ili Kuvutia Washirika wa Uchunguzi wa Mafuta na Gesi

Katika ripoti yake ya Ushirika wa Kimkakati ya mwezi Novemba 2016 na Bajeti ya 2017/18, TPDC ilielezea umuhimu wa kununua taarifa za mtetemo wa miamba zinazohusu kitalu 4/1B na 4/1C kwa ajili ya fikra za ushirika wa kimkakati. Taarifa za TPDC kwa sasa ni eneo la Kilomita 598.1 la taarifa mbili za mtetemo wa miamba za mfumo wa 2D zilizonunuliwa na TPDC, WesternGeco

na ION GXT katika miaka ya 1999 na 2000. Mnamo tarehe 15 Desemba 2015, Shirika la TPDC lilianzisha mchakato wa kuboresha taarifa hizi kwa kuingia mkataba na Kampuni ya ION GX Technology. Mchakato huo ni wa kufanya utafiti wa mitetemo ya miamba baharini kwenye maeneo yenye leseni kwa mfumo wa 2D (2D infill non-exclusive multi-client marine seismic survey) katika vitalu vya bahari kuu vya 4/1B na 4/1C. Hata hivyo, mkataba ulivunjwa mwaka 2017.

Kutokana na mabadiliko katika teknolojia na kuvunjika kwa mkataba uliotajwa hapo juu, TPDC ilianza kufanya mchakato wa kununua taarifa za mitetemo ya miamba katika mfumo wa 3D, ambapo tarehe 29 Januari 2018 walituma barua ya pendekezo Wizara ya Nishati yenye Kumbukumbu Na. CBE.144/369/01/25 ikielezea manufaa itakayopata kwa kutumia meli ya uchunguzi iliyopo Zanzibar ya BGP kutafiti mafuta na gesi katika vitalu 4/1B na 4/1C ili kuziboresha taarifa za sasa zilizopo kwenye mfumo wa 3D. Hata hivyo, tarehe 30 Juni 2018 kulikuwa na Sh. milioni 24.79 (0.6%) tu ambazo zilitolewa na Serikali. Hivyo shughuli hiyo haikuweza kufanyika. Menejimenti ilieleza kuwa, katika mwaka wa fedha wa 2018/19 wameweka kiasi cha kutosha cha fedha katika bajeti ili kununua taarifa za mitetemo ya miamba katika mfumo wa 3D. Hata hivyo, hakuna pesa ambayo imekwishapokelewa mpaka inafikia nusu ya mwaka wa fedha wa 2018/19.

Ni maoni yangu kuwa, ununuzi wa taarifa za mitetemo ya miamba za 3D ni muhimu kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uchunguzi katika mafuta na gesi ambayo hujumuisha; tafsiri ya taarifa na kuonesha muundo na matabaka ya miamba; na muhimu zaidi, kuvutia washirika kwa ajili ya uchunguzi na uendelezaji wa vitalu vya mafuta na gesi.

Ninapendekeza TPDC na Serikali kupitia Wizara ya Nishati ipange namna ya kupata fedha kwa ajili ya kupata taarifa za mitetemo wa miamba za 3D kwa ajili ya maendeleo zaidi ya vitalu hivyo viwili vya gesi.

SURA YA KUMI NA TISA

UTEKELEZAJI WA SHERIA ZA KODI YA MAPATO

19.1 Utangulizi

Taasisi za Umma zinatakiwa kuzingatia sheria za kodi, ikiwa ni pamoja na kuwasilisha ritani za kodi kwa wakati. Hata hivyo, kama ilivyoripotiwa katika taarifa zangu za miaka iliyopita, nilibaini kuwa taasisi za Umma ziliendelea kuchelewesha au kutokupeleka kabisa makato ya kodi kutoka kwenye mishahara ya wafanyakazi na kodi ya zuio, hivyo kusababisha faini na riba. Pia, ziliendelea kutokuandaa nyaraka na taarifa za kodi ya ongezeko la thamani (VAT) inayosababisha kuleta ugumu katika kudai marejesho ya kodi (input tax).

Pamoja na msisitizo unaoelezwa kwa kila Taasisi kutumia mashine za kielektroniki kutoa risiti, nilibaini kuwa baadhi ya taasisi hazina mashine za kielektroniki, hasa taasisi zenye mauzo. Nilibaini pia kuwa, kutokufuata sheria za kodi ya zuio kunatokana na kutokuelewa sheria hiyo na kutoa tafsiri tofauti. kwa kina nilibaini mapungufu yafuatayo:-

19.2 Kuwepo kwa Makadirio ya Kodi Yenye Pingamizi Kutokana na Tafsiri Tofauti za Sheria za Kodi.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (1) na (2) cha Sheria ya Mapato ya mwaka 2014, mapato yatokanayo na ajira yanajumuisha malipo ya posho, mishahara, malipo ya likizo, ada, kamisheni, marupurupu na kiinua mgongo au malipo ya kujikimu wakati wa safari au posho nyingine zinazopokelewa kutokana na ajira au huduma iliyotolewa. Pia, kifungu cha 7(3) cha Sheria ya Mapato ya mwaka 2014 kiliondoa posho ya nyumba, posho ya usafiri, posho ya madaraka, posho ya kufanya kazi masaa ya ziada, posho kufanya kazi katika mazingira magumu, na honoraria kwa mtumishi wa Serikali au taasisi ambayo bajeti yake hulipwa yote au kwa kiwango kikubwa na ruzuku za Serikali.

Nilibaini kuwa, SUMATRA, Mamlaka ya Bima (TIRA) na Mamlaka ya Maji (SHUWASA) hazikuwa zimeingiza posho (posho za nyumba, madaraka na likizo) zilizolipwa kwa watumishi katika kukokotoa kodi ya mapato (PAYE). Hivyo, kulikuwa hakuna kodi

ya mapato iliyokusanywa na kuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kutokana na posho hizi. Taasisi hizo zilikokotoa mapato kutoka kwenye mshahara tu na siyo jumla ya mshahara na posho zilizolipwa. Kwa upande mwingine, Mamlaka ya Anga (TCAA) imekuwa ikikata kodi ya zuio kutoka katika mapato yake kwa asilimia mbili (2%) na kulipa Kodi ya Kuendeleza Ufundi Stadi (SDL). Zaidi ya hayo, TCAA ilikata kodi ya mapato kutoka kwenye mishahara na posho (PAYE) badala ya mishahara pekee kwa kuwa ni taasisi ambayo bajeti yake yote hulipwa na Serikali, hivyo kutokana na sheria ya mapato haipaswi kukata kodi kwenye posho. Hata hivyo, TCAA haijaomba mwongozo au maelezo kutoka TRA.

Katika Mamlaka ya Bima (TIRA), kulikuwa na kutokukubaliana juu ya kukata kodi kwenye posho wanazolipwa watumishi. Menejimenti ya TIRA ilieleza kuwa, Sheria ya mapato inatoa msamaha kwa Taasisi za serikali. Hivyo, TIRA ilichukua fursa hiyo kuomba ufafanuzi kutoka mamlaka ya mapato na Wizara ya Fedha na Mipango kama ilitakiwa kukata kodi katika posho iliyokuwa ikilipa watumishi wake. Hata hivyo, hakukuwa na jibu lililokuwa limepokelewa. Jedwali Na. 30 hapo chini linaonesha orodha ya Taasisi na posho ambazo hazikukatwa kodi.

Jedwali Na. 30:Posho za Watumishi ambazo hazikukatwa kodi

| Na | Jina la Taasisi | Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|----|--|---|-------------|
| 1 | Mamlaka ya Bima Tanzania (TIRA) | Posho ya nyumba, Posho ya safari, Posho ya kukaimu na posho ya huduma | 755,229,227 |
| 2 | Mamlaka ya Maji Safi na Taka Shinyanga (SHUWASA) | Posho ya nyumba, Posho ya chakula na posho ya madaraka. | 205,645,000 |
| 3 | SUMATRA | Posho ya likizo | 684,418,835 |

Kwa namna ya kufanana, mfuko wa pesheni wa PSPF haukulipa makadirio ya kodi ya kiasi cha Sh. bilioni 199.76 ikiwa ni kodi itokanayo na mapato ya uwekezaji kwa miaka ya 2011/12, 2012/13 na 2013/14. Sababu ya kutolipa kodi iliyokadiriwa ni msamaha uliotolewa chini ya kifungu cha 47 cha Sheria ya Mafao ya Kustaafu (Public Service Retirement Benefits Act No. 2 of 1999). Msamaha ulitegemeana na historia ya Mfuko, ambapo ulianza na uhaba mkubwa kifedha; hivyo kuwa na haja ya kuongeza fedha za kutosha kulipa mafao.

Ni maoni yangu kuwa, TIRA na Taasisi nyingine zina nafasi ya kupata ufafanuzi wa sheria za kodi ambazo ndizo zinazoanzisha makadirio ya kodi. Kujirudia kwa matukio ya kutokuzingatia sheria ya mapato kwa taasisi za Umma kunaonesha uelewa tofauti wa sheria hiyo katika Taasisi hizo. Hii husababisha kufanya majadiliano yasiyo ya lazima. Hivyo, kuzifanya Taasisi hizo kuwa na mzigo wa kodi zilizolipwa. Fedha hizo huchukua sehemu ya fedha ambazo zingefanya shughuli nyingine katika miaka inayofuata.

Ninapendekeza kuwa mamlaka ya mapato, kama Taasisi ambayo imekasimiwa kusimamia utekelezaji wa sheria za kodi, itoe ufafanuzi wa mara kwa mara wa sheria hizo kwa Taasisi za Umma ili kuzisaidia kuzingatia sheria hizo.

19.3 Kutokutayarisha au Kuchelewa Kupeleka Ritani za Kodi (tax returns)

za Ongezeko la thamani (VAT), Kodi ya Mshahara (PAYE), Kodi ya Kuendeleza Ufundi Stadi (SDL) na Kodi ya Zuo Mamlaka ya Mapato Tanzania

Kifungu cha 15 na 66 cha Sheria ya VAT ya mwaka 2014 na Kanuni ya 20 ya Kanuni za kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya mwaka 2015, zinataka VAT kulipwa siku ya 20 au kabla ya kila mwezi unaofuata mwezi wa biashara ambao ndio tarehe ya kupeleka taarifa ya kodi mamlaka ya mapato. Pia, Kifungu 83 (l) na (A) cha Sheria ya Mapato ya mwaka 2008 iliyorekebisha na Kifungu cha 28(3) cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 kinataka kuzuia kodi ya zuio kwenye malipo yanayohusiana na utoaji huduma kwa kiwango cha asilimia 15 kwa kampuni za kigeni na asilimia 2 na 5 kwa bidhaa na huduma kwa kampuni za Tanzania.

Pamoja na kuripotiwa katika taarifa zangu za miaka iliyopita, nilibaini kuwa taasisi za Umma bado hazijaweza kuboresha utunzaji kumbukumbu za kodi na utoaji taarifa sahihi za kodi ili kuendana na matakwa ya sheria na kanuni za kodi. Kwa mfano, Baraza na Ujenzi la Taifa (NCC) na Shirika la Bima la Taifa (NIC) hazikupeleka taarifa za kodi ya ongezeko la

thamani (VAT) kwa kiasi cha Sh. milioni 38.7 kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2018.

Mamlaka ya Uhifadhi Ngorongoro (NCAA) haikutoza kiasi cha Sh. milioni 63.5 katika mauzo ya mali zake. Pia, NCAA ilipunguza makadirio ya jumla ya mauzo yake katika taarifa ya kodi ya ongezeko la thamani kwa kiasi cha Sh. bilioni 1.6 (ikiwa ni Sh. 125.1 bilioni badala ya Sh. bilioni 126.7) na kusababisha kupunguza kodi itokanayo na mauzo (output tax) kwa kiasi cha Sh. milioni 285.

Nilibaini pia kuwa, Shirika la Bima la Taifa lilichelewesha kupeleka taarifa za VAT zilizokuwa zikitakiwa tangu mwanzoni mwa mwaka na zilipelekwa mwezi Februari 2018. Nilibaini kuwa taasisi kumi (10) za Umma zilikuwa na matukio ya kutokukata kodi ya zuio kwenye malipo ziliyofanya, ikiwa ni pamoja na Kodi ya Kuendeleza Ufundi Stadi (SDL); hivyo, hazikupelekwa Mamlaka ya Mapato (Jedwali Na. 31). Kutokuzingatia sheria za kodi kunaweza kusababisha adhabu za tozo na riba kwa taasisi na hivyo kusababisha kutumika kwa rasilimali za taasisi katika mambo ambayo hayakuwa kwenye bajeti. Hivyo, kuathiri shughuli nyingine. Pia, kwa kutozingatia sheria hizi za kodi, taasisi za Umma zinajikuta zimechangia ukwepaji wa kodi kwa wazabuni na wakandarasi.

Ninapendekeza kuwa Taasisi za Umma zihakikishe zinazingatia sheria za kodi kwa kuhakikisha kuwa Taarifa za kodi zinaandaliwa mapema na kuzipelekwa Mamlaka ya Mapato kwa wakati.

Jedwali Na. 31: Taasisi ambazo hazikukata kodi ya Zuio na Kodi ya Maendeleo ya Ujuzi

| Na | Jina la Taasisi | Maelezo |
|----|---|--|
| 1 | TPDC | Malipo yaliyofanywa kwa gazeti la Tanzania Standard Newspapers (TSN) kwa ajili ya matangazo ya Sh. milioni 3.7 |
| 2 | Mamlaka ya Maji Safi na Taka Dodoma (DUWASA), | DUWASA haikupeleka TRA taarifa ya nusu mwaka kwa kodi za PAYE, SDL na kodi ya zuio. |

| Na | Jina la Taasisi | Maelezo |
|----|--|---|
| 3 | Shirika la Bima la Taifa (NIC) | Shirika halikukusanya kwa muda vyeti vya kodi ya zuio kutoka kwa wapangaji wake. Matokeo yake, Shirika lilijikuta likiwa na kiasi kikubwa cha madai ya kodi bila kuwa na nyaraka za vyeti. Hii ilisababisha Shirika kuyaweka kwenye madeni yenye shaka kukusanya kwa kiasi cha Sh. milioni 451 mpaka tarehe 30 June 2017. |
| 4 | Taasisi ya Teknolojia Dar es salaam (DIT) | DIT haikukata kodi ya zuio kwenye malipo ya Sh. milioni 10.41 ya huduma za ulinzi. |
| 5 | Mamlaka ya Maji Safi Dar es salaam (DAWASA) | Malipo 16 ikiwa sawa na 44% ya malipo yaliyofanywa kwa watoa huduma mbalimbali, hayakukatwa kodi ya zuio kwa kiasi cha Sh. Milioni 60.24. |
| 6 | Chuo Huria cha Tanzania (OUT). | Kwa sababu ya viwango vidogo vilivyotumika, kiasi cha Sh. Milioni 10.44 hakikupelekwa mamlaka ya mapato. |
| 7 | Mamlaka ya Maji Safi na Taka Shinyanga (SHUWASA) | Mamlaka haikukata kodi ya zuio na kuipeleka TRA kutoka kwenye malipo yaliyofanywa kwa wazabuni juu ya malipo tofautitofauti ya Sh. Milioni 5.30 yaliyofanywa kwa wazabuni mbalimbali. |
| 8 | Bank ya Uwekezaji Tanzania (TIB) | <ul style="list-style-type: none"> • Haikuandaa taarifa za kodi ya maendeleo ya Ujuzi (SDL). • Benki inatoa mikopo katika riba ndogo kwa watumishi wake ya 4% kwa mwaka. Riba ya Benki kuu katika kipindi hicho ilikuwa 16% ambayo inaonesha kulikuwa na faida itokanayo na tofauti hiyo ya riba. Hata hivyo, benki haikukata kodi kwenye faida hiyo katika miezi, ambapo riba ya benki ilikuwa chini yaani 12% kutokea mwezi Machi 2017 mpaka Julai 2017 na 9% kutoka mwezi Agosti 2017 mpaka mwisho wa fedha. • Benki ilichelewa kupeleka kodi ya zuio iliyokatwa kwenye mapato ya amana za benki. |
| 9 | Mamlaka ya Bandari Tanzania | <ul style="list-style-type: none"> • Usuluhishi wa kodi ya ongezeko la thamani kati ya vitabu vya kiuhasibu (General ledger) na ritani za kodi za kila mwezi |

| Na | Jina la Taasisi | Maelezo |
|----|---|---|
| | | <p>haufanyiki, na hii ni kwa kila mwezi.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kodi ya ongezeko la thamani kwenye tozo ya maegesho ya meli zinazokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania hazikuonyeshwa kwenye ritani za kodi za kila mwezi za Mamlaka ya Bandari ila deni limerekodiwa kwenye vitabu vya Mamlaka ya Bandari. • Mamlaka ya Bandari Tanzania haitoi marekebisho ya ankara kwa wateja wake pale inapotokea wamefuta hizo ankara za mwanzo. Hii ni kinyume cha Kifungu namba 71 cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 2014. |
| 10 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira. | <ul style="list-style-type: none"> • Mamlaka haijawsilisha ritani za kodi za nusu mwaka na mwaka mzima kwenye kodi zifuatazo: kodi ya zuio, kodi ya mshahara (PAYE), kodi ya kuendeleza ufundi stadi, na makato ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi. • Kutokana na kutowasilisha ritani za kodi, Mamlaka ilitakiwa kulipa tozo isiyopungua Sh. milioni 20. • Kodi ya zuio yenye jumla ya Sh. milioni 4.28 iliyokwishakatwa haikupelekwa Mamlaka ya Mapato Tanzania. |
| 11 | Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) | <ul style="list-style-type: none"> • Kuchelewa kupeleka makato ya kisheria kwenye Mamlaka ya Mapato Tanzania na Mamlaka zingine. Makato hayo ni kama kodi, makato ya pensheni, na makato ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi |
| 12 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Arusha | <ul style="list-style-type: none"> • Mamlaka haijawsilisha ritani za kodi za nusu mwaka na mwaka mzima kwenye kodi zifuatazo: kodi ya zuio, kodi ya mshahara (PAYE), kodi ya kuendeleza ufundi stadi, na makato ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi. |
| 13 | Kampuni ya Umeme Tanzania (TANESCO) | <ul style="list-style-type: none"> • Kutopeleka makato ya kisheria kwenye Mamlaka ya Mapato Tanzania na Mamlaka zingine. Makato hayo ni kama kodi, makato |

| Na | Jina la Taasisi | Maelezo |
|----|-----------------|---|
| | | ya pensheni, na makato ya Mfuko wa Fidya kwa Wafanyakazi. |

19.3 Kodi Zinazodaiwa Kwenye Taasisi za Umma

Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) linadaiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kodi ya ongezeko la thamani lenye jumla ya Sh. bilioni 2.27, ukiondoa adhabu. Hii ni kinyume na Kifungu 66(1) cha Sheria ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 2014. Uongozi wa Shirika la Utangazaji Tanzania umeeleza kuwa, wapo kwenye majadiliano na Mamlaka ya Mapato Tanzania jinsi ya kulipa deni hilo wakati wakisubiri majibu yao ya maombi ya msamaha kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Pia, Shirika limeomba punguzo la faini na adhabu kutoka Wizara ya Fedha tarehe 25 Septemba 2018.

Pia, Shirika la Simu Tanzania linadaiwa kodi ya bidhaa na Mamlaka ya Mapato yenye jumla ya Sh. 234.41 milioni kutoka mwaka 2015. Nilitaarifiwa kuwa, malipo yanasubiria zoezi la usuluhishi linaloendelea kati ya Shirika na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Ninapendekeza kuwa Taasisi za Umma zilipe kodi kwa wakati ili kuondokana na malipo ya adhabu yanayotokana na ucheleweshaji.

19.4 Mapungufu Kwenye Uwasilishaji wa Ritani za Kodi ya Ongezeko la Thamani

Kifungu 69 (1) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kinataka taasisi yenye usajili wa kulipa kodi ya ongezeko la thamani lenye salio hasi la kodi hiyo kuidai Mamlaka ya Mapato ndani ya miezi sita. Pia, Kifungu cha 16 (1) (b) cha Sheria ya Ongezeko la Thamani kinataka taasisi yenye usajili wa kodi ya ongezeko la thamani kudai kodi ya ongezeko la thamani kwenye manunuzi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kila mwezi.

Niligundua kuwa Kampuni Hodhi ya Mali za Shirika la Reli (RAHCO) ilikuwa na kodi ya ongezeko la thamani jumla ya Sh. bilioni 31.09 kwenye manunuzi yake kwa kipindi kinachoanzia Juni 2016 mpaka Juni 2018. Pia, niligundua kuwa RAHCO ililipa malipo ya awali kwa YAPI MARKEZI yenye ongezeko la thamani

la Sh. bilioni 53.3. Hata hivyo, ongezeko la thamani la kiasi hicho halikuoneshwa kwenye vitabu vya RAHCO. Pia, RAHCO ilikuwa haipeleki ritani za ongezeko la thamani kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kila mwezi. Kwa ujumla wake, niligundua kuwa RAHCO inaidai Mamlaka ya Mapato Tanzania jumla ya Sh. bilioni 84.39, lakini haijaomba kurejeshewa fedha hizo na Mamlaka ya Mapato.

Pia, niligundua kuwa RAHCO inadaiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kodi ya ongezeko la thamani lenye jumla ya Sh. bilioni 3.11 kwa mwaka wa fedha 2017/18. Hata hivyo, RAHCO haijapeleka ritani za ongezeko la thamani kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kama inavyotakiwa na sheria ya ongezeko la thamani. Hii itasababisha RAHCO kulipa adhabu ya ucheleweshaji wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye mauzo.

Ninapendekeza kuwa RAHCO ihakikishe kuwa kodi ya ongezeko la thamani kwenye manunuzi na mauzo inarekodiwa kwenye vitabu vya kijasibu. Pia, RAHCO iimarisha uwasilishaji wa ritani za kodi ya ongezeko la thamani kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kama inavyotakiwa na Sheria ya Ongezeko la Thamani.

19.5 Madeni ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa Mkongo wa Taifa - Sh. bilioni 10.83

Nilibaini kuwa, Mkongo wa Taifa unatumia namba ya mlipa kodi ya Shirika la Simu. Hivyo basi, ritani za kodi za Mkongo wa Taifa zinawasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kupitia Shirika la Simu.

Nilibaini kuwa, Shirika la Simu ndio msimamizi wa mkongo wa taifa, na linapokea gharama za usimamizi kutoka Mkongo wa Taifa. Kwa mwaka wa fedha 2017/18, Shirika la Simu limerekodi kodi ya ongezeko la thamani ya jumla ya Sh. bilioni 10.83 yatokanayo na mauzo kwa Mkongo wa taifa. Hii kodi iliyorekodiwa ya ongezeko la thamani kwenye mauzo haina kodi yake ya upande wa manunuzi. Kwa mantiki hii, shirika linaonekana linadaiwa na Mamlaka ya Mapato kwa niaba ya Mkongo wa taifa.

Ninapendekeza Shirika la Simu na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wamalize hili suala la kodi ya ongezeko la thamani la Mkongo wa taifa.

19.6 Taasisi za Umma Zimeshindwa Kupokea/Kutoa Stakabadhi za Kielektroniki (EFD)

Nilibaini Taasisi 11 za umma ambazo zilinunua bidhaa na huduma bila kudai stakabadhi za kielektroniki (EFD), na nyingine ziliuza bila kutoa stakabadhi za kielektroniki (EFD). Hii ni kinyume na kanuni za 24 na 28 (1) za Kanuni za Stakabadhi za Kielektroniki (EFD) za mwaka 2010 kama zilivyorekebshwa mwaka 2012. Maelezo zaidi yapo kwenye jedwali namba 32.

Jedwali Na. 32: Taasisi zilizolipa au kuuza bila kutoa au kudai EFD

| Na. | Jina la Taasisi | Maelezo |
|-----|--|---|
| 1 | Shirika la Posta Tanzania | Malipo kwa watoa huduma ambayo hayakuwa na stakabadhi za kielektroniki Sh. milioni 515.96. |
| 2 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Babati (BAWASA) | Malipo kwa watoa huduma ambayo hayakuwa na stakabadhi za kielektroniki ya Sh. milioni 16. |
| 3 | Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) | Malipo kwa watoa huduma ambayo hayakuwa na stakabadhi za kielektroniki ya Sh. milioni 35.34. |
| 4 | Mfuko wa Taifa wa Bima Ya Afya | Malipo kwa watoa huduma ambayo hayakuwa na stakabadhi za kielektroniki ya Sh. milioni 2.2. |
| 5 | Shirika la Masoko Kariakoo (KMC) | Manunuzi yaliyofanyika bila kudai stakabadhi za kielektroniki (EFD) ya Sh. milioni 56.16. |
| 6 | Kampuni Hodhi ya Mkulazi | Manunuzi yaliyofanyika bila kudai stakabadhi za kielektroniki (EFD) ya Sh. milioni 15.76. |
| 7 | Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) | Baraza halijatoa stakabadhi za kielektroniki kwa wateja kwa mwaka mzima unaoishia 30 Juni 2016 kinyume na muongozo uliotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania Na. TRA/CDR/T.30/222/Vol.III/142. |
| 8 | Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) | Malipo kwa wauza bidhaa ambayo hayakuwa na stakabadhi za kielektroniki Sh. milioni 431.45. |
| 9 | Taasisi ya Mipango ya Maendeleo Vijijini | Taasisi hii haina mashine za kutolea stakabadhi za kielektroniki. |
| 10 | Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili | Taasisi hii haina mashine za kutolea stakabadhi za kielektroniki. |

| | | |
|----|--|---|
| 11 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Singida | Malipo kwa watoa huduma ambayo hayakuwa na stakabadhi za kielektroniki ya Sh. milioni 18.56 |
|----|--|---|

Kufanya malipo bila kudai stakabadhi za kielektroniki kunaweza kusababisha ukwepaji wa kodi hivyo, kuleta hasara ya mapato kwa Serikali.

Ninapendekeza Taasisi za Umma kufuata kanuni za Stakabadhi za Kielektroniki ya mwaka 2010 (na marekebisho yake ya 2012) kwa kudai stakabadhi za kielektroniki kwenye malipo ya manunuzi ya huduma na bidhaa.

19.7 Kutokutekelezwa kwa mradi wa KFW kwenye Mbuga ya Wanyama Serengeti

Tarehe 16 Desemba 2013, Tanzania kupitia Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), iliingia makubaliano ya kifedha na KFW na Frankfurt Zoology Society kwa ajili ya kuendeleza mazingira katika mbuga ya Serengeti na Ngorongoro. Gharama za mradi zilikadiriwa kuwa EUR za Ulaya milioni 24.12. KFW ilikubali kufadhili EUR za Ulaya milioni 20.5, wakati Frankfurt Zoological Society (FZS) ilikubali kufadhili EUR za Ulaya milioni 1, na zilizobaki EUR za Ulaya milioni 2.62 zifadhiliwe na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania. Muda wa mradi ulikadiriwa kuwa miaka mitano kutoka tarehe 11 Julai 2014.

Fedha hizi zilitarajia kujenga nyumba za watumishi, vituo vya watalii, mifereji ya maji, kuanzisha mpango wa matumizi ya ardhi vijijini, kurasimisha matumizi ya ardhi, kuanzisha mpango wa matumizi bora ya mali kwenye kanda, na kuanzisha jamii ya Wanyama pori na usimamizi bora wa misitu.

Pia, fedha hizo zilitarajia kujenga barabara za kimkakati za vijiji vya wilaya ya Serengeti na Ngorongoro, kusaidia mbuga ya Serengeti, programu ya kugawana faida na kusaidiwa jamii za vijijini, na kujenga miundombinu ya kiuchumi na kijamii.

Walikubaliana kuwa kodi zote za serikali na tozo zingine zitagharamiwa na Serikali au Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania, na KFW ina haki ya kukataa kutoa fedha baada ya 30 Juni 2018 kama ilivyoonyeshwa kwenye vipengele 1.3 na 3.2 vya makubaliano.

Mpaka kufikia Januari 2019, miaka minne baadaye toka kuanza kwa mkataba tarehe 11 Julai 2014 hamna kilichofanyika. Sababu za kuchelewa ni kwamba vitu vya ujenzi vilitakiwa visamehewe kodi wakati wa kuviingiza nchini kutoka nje. Hata hivyo, mpaka wakati wa ukaguzi Januari 2019, msamaha wa kodi ulikuwa haujakamilika.

Ninapendekeza kuwa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania na Mamlaka ya Mapato Tanzania kumaliza suala la msamaha wa kodi ili kusaidia utekelezaji wa mradi.

Kiambatisho Na. I: Mwenendo wa Hati zilizotolewa

| Na | Maelezo | Hati |
|----|---|--------------------|
| 1 | Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere | Hati inayoridhisha |
| 2 | Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya | Hati inayoridhisha |
| 3 | Chuo Kikuu cha Teknolojia (DIT) | Hati inayoridhisha |
| 4 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bukoba | Hati inayoridhisha |
| 5 | Baraza la Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTE) | Hati inayoridhisha |
| 6 | Baraza la Mazingira Tanzania (NEMC) | Hati inayoridhisha |
| 7 | Baraza la Michezo Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 8 | Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) | Hati inayoridhisha |
| 9 | Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) | Hati inayoridhisha |
| 10 | Baraza la Ushindani (FCT) | Hati inayoridhisha |
| 11 | Baraza la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) | Hati inayoridhisha |
| 12 | Benki ya Biashara ya TIB | Hati inayoridhisha |
| 13 | Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) | Hati inayoridhisha |
| 14 | Benki ya Maendeleo ya TIB | Hati inayoridhisha |
| 15 | Benki ya Posta Tanzania (TPB) | Hati inayoridhisha |
| 16 | Benki ya Wanawake Tanzania | Hati isiyoridhisha |
| 17 | Bodi ya Michezo ya Bahati Nasibu Tanzania (TGB) | Hati inayoridhisha |
| 18 | Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) | Hati inayoridhisha |
| 19 | Bodi ya Pamba Tanzania (TCB) | Hati inayoridhisha |
| 20 | Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (CRB) | Hati inayoridhisha |
| 21 | Bodi ya Usanifu na Upimaji (AQSRB) | Hati isiyoridhisha |
| 22 | Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi Tanzania (NBAA) | Hati inayoridhisha |
| 23 | Bohari ya Dawa (MSD) | Hati inayoridhisha |
| 24 | CDTF - (Cotton Board) | Hati inayoridhisha |
| 25 | Chuo cha Afya na Teknolojia Muhimbili (MUHAS) | Hati inayoridhisha |
| 26 | Chuo cha kidiplomasia (CFR) | Hati inayoridhisha |
| 27 | Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini (IRDPI) | Hati inayoridhisha |
| 28 | Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam (DMI) | Hati inayoridhisha |
| 29 | Chuo cha Ufundi Arusha (ATC) | Hati inayoridhisha |
| 30 | Chuo cha Usafirishaji (NIT) | Hati inayoridhisha |
| 31 | Chuo cha Wanyama pori Afika (MWEKA) | Hati inayoridhisha |
| 32 | Chuo Huria cha Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 33 | Chuo Kikuu cha Ardhi | Hati inayoridhisha |
| 34 | Chuo Kikuu cha Biashara Moshi (MUCO) | Hati inayoridhisha |
| 35 | Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam (UDSM) | Hati inayoridhisha |

| | | |
|----|--|--------------------|
| 36 | Chuo Kikuu cha Dodoma | Hati inayoridhisha |
| 37 | Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) | Hati inayoridhisha |
| 38 | Chuo kikuu cha Mkwawa (MUCE) | Hati inayoridhisha |
| 39 | Chuo Kikuu cha Mzumbe | Hati inayoridhisha |
| 40 | Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE) | Hati inayoridhisha |
| 41 | Co-operative and Audit Supervision Corporation (COASCO) | Hati inayoridhisha |
| 42 | Hospitali ya Taifa ya Muhimbili | Hati inayoridhisha |
| 43 | Kampuni Hodhi ya Kusimamia Rasilimali za Shirika la Reli (RAHCO) | Hati inayoridhisha |
| 44 | Kampuni ya Umeme Tanzania (TANESCO) | Hati inayoridhisha |
| 45 | Kituo cha Chakula na Lishe Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 46 | Kituo cha Elimu Kibaha (KEC) | Hati inayoridhisha |
| 47 | Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) | Hati inayoridhisha |
| 48 | Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) | Hati inayoridhisha |
| 49 | Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) | Hati inayoridhisha |
| 50 | Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) | Hati inayoridhisha |
| 51 | Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCCA) | Hati inayoridhisha |
| 52 | Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (TANAPA) | Hati inayoridhisha |
| 53 | Mamlaka ya kesi za Manunuzi ya Rufaa (PPAA) | Hati inayoridhisha |
| 54 | Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi ya Umma (PPRA) | Hati inayoridhisha |
| 55 | Mamlaka ya Kudhibiti Petroli Mkondo wa Juu (PURA) | Hati inayoridhisha |
| 56 | Mamlaka ya Maji Safi Masasi Nachingwea | Hati inayoridhisha |
| 57 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Songea | Hati inayoridhisha |
| 58 | Mamlaka ya Maji Safi Dar es Salaam (DAWASA) | Hati inayoridhisha |
| 59 | Mamlaka ya Maji Safi Kahama Shinyanga | Hati inayoridhisha |
| 60 | Mamlaka ya Maji Safi Lindi | Hati inayoridhisha |
| 61 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Arusha | Hati inayoridhisha |
| 62 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Babati | Hati inayoridhisha |
| 63 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira 'Chalinze (CHAUWASA) | Hati inayoridhisha |
| 64 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dodoma | Hati inayoridhisha |
| 65 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Iringa | Hati inayoridhisha |
| 66 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kahama | Hati inayoridhisha |

| | | |
|----|---|--------------------|
| 67 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya | Hati inayoridhisha |
| 68 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Morogoro | Hati inayoridhisha |
| 69 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Moshi | Hati inayoridhisha |
| 70 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara | Hati inayoridhisha |
| 71 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Musoma | Hati inayoridhisha |
| 72 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza | Hati inayoridhisha |
| 73 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Namtumbo | Hati inayoridhisha |
| 74 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Njombe | Hati inayoridhisha |
| 75 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Rukwa | Hati inayoridhisha |
| 76 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga | Hati inayoridhisha |
| 77 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Singida | Hati inayoridhisha |
| 78 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tabora | Hati inayoridhisha |
| 79 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tanga | Hati inayoridhisha |
| 80 | Mamlaka ya Udhhibiti wa Bima Tanzania (TIRA) | Hati inayoridhisha |
| 81 | Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) | Hati inayoridhisha |
| 82 | Mamlaka ya Udhhibiti wa Soko la Mtaji (CMSA) | Hati inayoridhisha |
| 83 | Mamlaka ya Usimamizi ea Maji na Nishati (EWURA) | Hati inayoridhisha |
| 84 | Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) | Hati inayoridhisha |
| 85 | Mfuko wa Bima ya Afya Tanzania (NHIF) | Hati inayoridhisha |
| 86 | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (GEPF) | Hati inayoridhisha |
| 87 | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (PPF) | Hati inayoridhisha |
| 88 | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (PSPF) | Hati inayoridhisha |
| 89 | Mfuko wa Pensheni wa LAPF | Hati inayoridhisha |
| 90 | Ocean Road Cancer Institute (ORCI) | Hati inayoridhisha |
| 91 | Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS) | Hati inayoridhisha |
| 92 | Bodi ya Wataalam wa Manunuzi na Ugavi (PSPTB) | Hati inayoridhisha |
| 93 | Shirika la Bima la Taifa (NIC) | Hati inayoridhisha |
| 94 | Shirika la Maendeleo Tanzania (NDC) | Hati isiyoridhisha |
| 95 | Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC). | Hati inayoridhisha |
| 96 | Shirika la Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASCO) | Hati inayoridhisha |
| 97 | Shirika la Masoko la Kariakoo (KMC) | Hati inayoridhisha |

| | | |
|-----|--|--------------------|
| 98 | Shirika la Simu Tanzania (TTCL) | Hati inayoridhisha |
| 99 | Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) | Hati inayoridhisha |
| 100 | Shirika la Viwango Tanzania (TBS) | Hati inayoridhisha |
| 101 | Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE) | Hati inayoridhisha |
| 102 | Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) | Hati inayoridhisha |
| 103 | Taasisi ya Uhasibu Arusha- IAA | Hati inayoridhisha |
| 104 | Taasisi ya Ustawi wa Jamii (ISW) | Hati inayoridhisha |
| 105 | Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) | Hati inayoridhisha |
| 106 | Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi Tanzania (TAFIRI) | Hati inayoridhisha |
| 107 | Tax Revenue Appeals Board | Hati inayoridhisha |
| 108 | Tax Revenue Appeals Tribunal | Hati inayoridhisha |
| 109 | TIB RASILIMALI | Hati inayoridhisha |
| 110 | Tume ya Ushindani (FCC) | Hati inayoridhisha |
| 111 | Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) | Hati inayoridhisha |
| 112 | Ubungo Plaza Company Ltd (UPL) | Hati inayoridhisha |
| 113 | Bodi ya Katani Tanzania (TSB) | Hati inayoridhisha |
| 114 | Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) | Hati inayoridhisha |
| 115 | Taasisi ya Utafiti wa Wanyama Pori (TAWIRI) | Hati inayoridhisha |
| 116 | Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Madawa (TPRI) | Hati inayoridhisha |
| 117 | Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) | Hati inayoridhisha |
| 118 | Kampuni ya Nyumba za Watumishi (WHC) | Hati inayoridhisha |
| 119 | Chuo cha Elimu na Ufundi Stadi (VETA) | Hati inayoridhisha |
| 120 | Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) | Hati inayoridhisha |
| 121 | Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Tanzania (COSTECH) | Hati inayoridhisha |
| 122 | Kampuni ya TTCL Pesa | Hati inayoridhisha |

Kiambatisho Na.II: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi wa Miaka iliyopita

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|--|--|---|---------------------|
| 1 | 2012/13 | Benki ya Azania ilitakiwa kuwa chini ya udhibiti wa Msajili wa Hazina na kuwasilisha taarifa zake za fedha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu cha 9(a)(iii) na (iv) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 | Wizara imeomba ushauri kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) ili kupata ufafanuzi katika suala hili. Mwanasheria Mkuu ameshauri Kifungu cha 3 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Ukurasa wa 418 kifanyiwe mabadiliko ili kumpa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua taasisi zilizoanzishwa na Sheria ya Makampuni. Hivyo, maana ya “Taasisi za Umma” ibadilishwe ili iongeze Taasisi zilizoanzishwa chini ya Sheria ya Makampuni kama sehemu kubwa ya hisa zinashikiliwa na wanahisa kutoka Serikalini, yatatakiwa kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. | Ni matarajio yangu kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ataanzisha mchakato wa kubadili Sheria ya Ukaguzi wa Umma kujumuisha Taasisi zote za Umma yakiwemo makampuni ambayo Serikali ndiye mwanahisa mkuu. Hivi sasa Benki ya Azania inamilikiwa kwa asilimia 62.7 na mfuko wa PSSF. | Hayajat ekelezwa. |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|--|--|--|---------------------|
| 2 | 2015/16 | Menejimenti ya NHIF inashauriwa kuwa na makubaliano ya kimaandishi na mkopaji na kupata dhamana ya Serikali. Pia hapo baadaye, NHIF inashauriwa kuhakikisha kuwapo kwa makubaliano ya kisheria kabla ya kutoa mkopo. | Mfuko ulipokea barua kutoka Wizara ya Fedha na Mipango tarehe 15 Desemba 2015 yenye Kumbukumbu na. CJA.452/479/01 inayoonesha kuubadili mkopo kwenye hati fungani isiyo ya fedha inayotarajiwa kufuta madeni yote ya Serikali katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. | Nilibaini kuwa Mfuko umeendelea kutoa mkopo kwa Serikali bila ya kuwa na makubaliano ya kisheria; na mikopo iliyopita haijabadilis hwa kuwa hati fungani isiyo ya fedha kama ilivyoelekezwa na barua yenye kumbukumbu na. CJA.452/479/01 | Hayajat ekelezwa |
| 3 | 2015/16 | Menejimenti ya Shirika la Posta inashauriwa kufuata matakwa ya kisheria na kiudhibiti kwa kulipa madai ya Mrahaba na Ada za mwaka kiasi cha Sh. bilioni 1.38 kwa TCRA | Menejimenti imeiomba Serikali kufuta madai ya Sh. bilioni 1.38 kwa TCRA kupitia kiasi cha Sh. bilioni 3.87 ambacho Shirika la Posta limetumia kulipa pensheni kwa wastaafu waliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki | Hakuna ushahidi ambao menejimenti ya Shirika la Posta imeleta kwa ajili ya uhakiki ili kuthibitisha kuwa menejimenti ya Shirika la Posta iliomba Serikali kufuta madai hayo. | Hayajat ekelezwa |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|--|--|---|----------------------------------|
| 4 | 2015/16 | Hasara iliyopatikana kutokana na LAPF kuvunja mkataba Sh. milioni 473.76 | Kituo kimeandika maombi kwa wawekezaji wa maduka makubwa (shopping mall) kuonesha nia katika mradi wa maduka makubwa. Pia Kituo kimeendelea kutafuta wawekezaji wengine watakaovutiwa katika Utaratibu wa Ushirika wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. | Ninakubali juhudi zinazofanywa na menejimenti, lakini ninasubiri utekelezaji wa maoni ya ukaguzi. | Yapo kwenye hatua za utekelezaji |
| 5 | 2015/16 | Kukosekana kwa maendeleo katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya ADS-B Sh. bilioni 3.4 (Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania) 'Naishauri menejimenti kufanya utafiti mpya na wa kina wa Kampuni juu ya uwezo wa kifedha na uendeshaji wa COMSOFT GmbH. Hii inaweza kuhitaji kuuhusisha Ubalozi wa Tanzania nchini Ujerumani kwa maelezo ya kuaminika. Menejimenti inashauriwa kufanya tathmini ya changamoto za utekelezaji wa mradi na kuchukua hatua sahihi ili kuboresha shughuli za uhibitaji wa anga. | Sehemu muhimu ya kukamilisha mradi inatarajiwa kufungwa (installed) sambamba na rada mpya ya uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere ili kuunganisha taarifa za rada na taarifa za ADS-B kwenye kidhibiti cha taarifa (monitor) ili kutumiwa na Mdhhibiti wa anga (Air Traffic Controller). | Ipo katika hatua za utekelezaji , nitaendelea kufuatilia utekelezaji kamili | Yapo kwenye hatua za utekelezaji |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|--|---|--|---|
| 6 | 2015/16 | <p>Usimamizi wa Kampuni Binafsi za Uzalishaji Umeme na Gharama zake</p> <p>Ili kulihusha Shirika la TANESCO na kulifanya lipate ufanisi, nina mapendekezo yafuatayo;</p> <p>Bei za umeme zinazopitishwa na EWURA zizingatie gharama halisi zinazotumiwa na TANESCO kuzalisha umeme au kununua toka kwa makampuni binafsi ya uzalishaji umeme.</p> <p>Vilevile, bei itakayopitishwa izingatie gharama za uendeshaji wa shirika na uwezo wa kufanya uwekezaji kwenye miundombinu ili huduma ya umeme iendelee kuwa ya uhakika.</p> <p>'Manunuzi ya umeme toka kwenye makampuni binafsi ya uzalishaji umeme yafanywe kwa uwazi na ushindani kama inavyotakiwa na sheria ya manunuzi ili kuwezesha TANESCO kupata bei nafuu.</p> <p>Serikali iwezeshe TANESCO kifedha ili iweze kuwekeza kwenye uzalishaji umeme wa bei nafuu,</p> | <p>i. Ongezeko la bei kutokana na matumizi ya EPPs na IPPs litasababisha athari tofauti kwa uchumi wa Nchi. Badala yake, Serikali imetoa ruzuku kwenye umeme ili kuwezesha kufikia majukumu yake ya kifedha na kutoa huduma zinazohitajika kwa wateja wake;</p> <p>ii. Serikali tayari imeelekeza chini ya GN No.292 ya tarehe 21/10/2016 kwa IPPs zote zishiriki katika zabuni za ushindani. Hata hivyo, Serikali imetoa msisitizo juu ya maendeleo ya mradi wa uzalishaji umeme.</p> <p>iii. TANESCO imekuwa ikihusishwa katika mchakato wa manunuzi, majadiliano na utoaji zabuni.</p> | <p>Majibu ya Menejimen ti nimeyapok ea kwa ajili ya ufuatiliaji wa utekelezaji .</p> | <p>Yapo kwenye hatua za utekelezaji</p> |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|-------|--|------------------|------------------|---------------------|
| | | hivyo kusaidia kuepukana na utaratibu wa kununua toka vyanzo vyenye gharama kubwa. | | | |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|---|---|---|-----------------------------|
| 7 | 2015/16 | <p>Ujenzi wa mradi wa maji Songwe 'i) Nashauri Serikali kuidhinisha mkataba wa kuanzishwa kwa Tume ya Bonde la Mto Songwe ili kuwezesha mradi kuanza.</p> <p>'ii) Aidha, Serikali inapaswa kuhusisha TANESCO katika mchakato wa Ujenzi wa Bwawa la Chini na katika ujenzi wa mtambo wa kuzalisha umeme kwa kutumia Maji ili kutoa ushauri wa kiufundi wakati unapohitajika.</p> | <p>Ushiriki wa TANESCO katika shughuli za uwekezaji kwenye shughuli za kuzalisha na kusambaza nishati ya umeme, hasa katika kuhamasisha ukusanyaji wa rasilimali za utekelezaji wa mradi na kutoa msaada wa kiufundi.</p> <p>'Tunachukua ushauri pamoja na wazo la TANESCO kushiriki katika ujenzi wa bwawa dogo na mtambo wa uzalishaji umeme kwa kutumia maji na kutoa ushauri wa kiufundi wakati unapohitajika</p> | Jibu limenukuli wa na tutafuatilia utekelezaji wake kwenye Ukaguzi ujao | Katika hatua za utekelezaji |
| 8 | 2015/16 | <p>Manufaa ya ushuru wa umeme kwa TANESCO</p> <p>'Ninapendekeza kwamba EWURA inapaswa kuchunguza kwa kiasi kikubwa ushuru wa umeme ili kuingiza gharama zote zinazohusiana na uzalishaji wa umeme na kuweza kurudisha faida, huku ikiruhusu uwekezaji wa kiuchumi na kuboresha utoaji wa huduma za TANESCO kwa ufanisi zaidi.</p> | TANESCO itaendelea kufuatilia kwa karibu, ili kuhakikisha kwamba EWURA inapitia marekebisho hayo ya mara kwa mara katika kila robo mwaka kadri inapohitajika. | Jibu limenukuli wa na tutafuatilia utekelezaji wake | Katika hatua za utekelezaji |
| 9 | 2015/16 | <p>Kutokulipwa kwa Kodi Wizara ya Nishati na Madini Sh. bilioni 1.12.</p> <p>'Uongozi wa TANESCO unashauriwa kuweka</p> | | Serikali haikutoa majibu kwa ushauri huu | Haijatekeleza |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|--|--|--|-----------------------------|
| | | juhudi zaidi katika Wizara ya Nishati na Madini ili kuhakikisha kuwa Wizara inalipa kodi yao wanayodaiwa. Kwa upande mwingine, kwa Wizarakuwa wizara Mama ya TANESCO inapaswa kuhakikisha kuwa inapunguza changamoto za kifedha zinazokabiliwa na Kampuni. | | | |
| 10 | 2015/16 | Kuchelewa kwa utekelezaji na kukamilika kwa miradi midogo ya Mlimani city 'Uongozi wa UDSM unashauriwa kuzingatia upya mkataba na kampuni hodhi ya Mlimani City ili kufuatilia kasi ya kukamilika kwa miradi iliyochelewa. | Tarehe ya kukamilisha sio iliyopangwa tarehe 1 Septemba, 2006 kwa kuwa tarehe ya awali ilisogezwa mbele kupitia Mkataba wa Utendaji ambao umeainisha tarehe ya kumalizika kuwa tarehe 31 Desemba, 2019. 'Wakati wa mkutano wa pamoja uliofanyika tarehe 20 Aprili, 2017 kati ya UDSM, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mlimani Holdings Ltd (MHL). MHL alisema kuwa wana nia ya kuweka bustani ya mimea kabla ya mwisho wa kipindi cha mkataba lakini hapakuwa na mipango ya kujenga hoteli ya nyota 4. 'Hata hivyo, UDSM na TIC walimwomba | Utekelezaji bado unaendelea , nitaendelea kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yangu. | Katika hatua za utekelezaji |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|---|---|--|-----------------------------|
| | | | MHL kutafakari upya suala la hoteli kulingana na mkataba uliopo na MHL aliahidi kufanya hivyo. 'UDSM tayari imeanzisha mchakato wa kurekebisha mkataba wa kukodisha ardhi. | | |
| 11 | 2015/16 | Uvunjaji wa Malipo ya Kodi kwa UDSM. (i) Ninashauri menejimenti ya Chuo Kikuu kuwa: (i) ikokotoe upya sehemu yake ya asilimia 10 kama inavyotakiwa na mkataba na tofauti idaiwe kutoka kwa mpangaji, (ii) kushauriana na mpangaji na kufikiria kuingiza vifungu vyote muhimu kama vile kuruhusu idara ya ukaguzi wa ndani wa UDSM kufanya ukaguzi | Hatua zinazofaa zinaendelea ikiwa ni pamoja na kulipa fidia ya ada zilizolipwa kwa upungufu, zikifuatiwa na ripoti inayoonesha tofauti kati ya kiasi cha jumla na kiasi cha mkopo kinachotakiwa kulipwa kwa UDSM. 'Wakati huo huo, UDSM inatafuta mambo mengine yanayohusiana na MHL kuanzisha njia bora ambayo itakuwa na manufaa | Utekelezaji bado unaendelea , nitaendelea kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yangu. | Katika hatua za utekelezaji |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkatuzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|---|---|--|-----------------------------|
| | | wa mapato na gharama za uendeshaji. | ya pamoja na ya kiwango cha juu zaidi kitakachokubalika na kuingizwa katika mkataba ambao itakua na mionogozo kwa pande zote mbili kuhusiana na mradi wa Mlimani City. | | |
| 12 | 2015/16 | Ufuatiliaji na usimamizi usiojitosheleza kwa makusanyo ya Mapato kutoka kwa wapangaji 'Uongozi wa UDSM unashauriwa kufuata vigezo na masharti ya makubaliano ya kukodisha, ikiwa ni pamoja na kifungu cha 11.2 (l) cha Makubaliano ya Mkataba ambao unahitaji UDSM kupitisha ukodishwaji wa mpangaji mdogo kutoka kwa mpangaji mkuu. | Hivi sasa, UDSM inapaswa kuidhinisha wapangaji kabla ya makubaliano rasmi ya kukodisha kusainiwa, na hivyo kuongeza uwazi juu ya makubaliano ya mkataba. UDSM, pia inapaswa kupitisha mikopo kwa wapangaji. Hadi sasa, UDSM imeimarisha mahitaji haya ya kiutaratibu. | Utekelezaji bado unaendelea , nitaendelea kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yangu. | Katika hatua za utekelezaji |
| 13 | 2015/16 | Ukosefu wa Haki ya kuangalia shuguli za MHL 'UDSM inashauriwa kuwasiliana na MHL kwa mtazamo wa kupata haki ya kuangalia shuguli za MHL kwa maslahi bora ya pande zote mbili na kwamba wakati wa mchakato huo, UDSM iruhusiwe kujua shughuli za mpangaji. | Afisa wa Uhusiano wa UDSM anaendelea kuthibitisha kumbukumbu zote hizo na hadi sasa, hakukuwa na kizuizi chochote kutoka kwa MHL. | Utekelezaji bado unaendelea , nitaendelea kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yangu. | Katika hatua za utekelezaji |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|---|--|---|-----------------------------|
| 14 | 2015/16 | Utekelezaji usiofaa wa miradi ya maendeleo TPA. TPA inashauriwa kuharakisha utekelezaji wa miradi yote iliyopangwa ili kuhakikisha kuwa malengo ya kimkakati yaliyopangwa yanafikiwa. | | Serikali haikutoa majibu kwa ushauri huu | Haijatekelezwa |
| 15 | 2015/16 | Tathmini ya randama ya makubaliano kwenye ukusanyaji wa ushuru wa maegesho ya meli bandarini kati ya TPA na TRA. 'Ninashauri uongozi wa TPA kuwasiliana na TRA 'Kuhusiana na vigezo na masharti ya randama ya makubaliano ili kuhakikisha kwamba pande zote mbili zinatimiza mahitaji ya makubaliano ili kuhakikisha kuwa ufanisi wa uendeshaji wa TPA hauathiriwi kwa njia mpya ya ukusanyaji wa ushuru wa maegesho ya meli bandarini wa TRA. | | Serikali haikutoa majibu kwa ushauri huu | Haijatekelezwa |
| 16 | 2016/17 | Kushuka kwa mwenendo wa kifedha wa TANESCO 'Ninaishauri TANESCO kutafuta njia ya kuboresha ukuaji wake wa kifedha ili kuweza kusaidia maendeleo ya kitaifa kupitia maendeleo ya viwanda | TANESCO imechukua hatua mbalimbali za lengo la kuboresha utendaji wa kifedha wa kampuni kwa ajili ya usaidizi endelevu wa mabadiliko ya kitaifa ya uchumi kwa njia ya viwanda. Hatua zilizochukuliwa hadi | Jibu limenukuliwa hata hivyo tunangoja ukamilishwaji wa mradi | Katika hatua za utekelezaji |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|-------|------------------------|---|------------------|---------------------|
| | | | <p>sasa ni hizi zifuatazo;</p> <p>Kwanza, kupunguza gharama za uzalishaji kupitia miradi kuu ya uwekezaji katika vyanzo vya bei nafuu vya uzalishaji cha nguvu za umeme (Kinyerezi II na Stigler Gorge)</p> <p>'Pili, kuendelea na mradi wa upanuzi kwa ajili ya ugani wa Gridi ya taifa (Makambako - Songea, Kaskazini-Magharibi ya gridi ya taifa) kuunganisha matawi yaliyotengwa ambayo hutumia mafuta ya gharama kubwa kwenye uzalishaji,</p> <p>'Tatu, kuboresha miundombinu ya usambazaji ili kupunguza vikwazo vya umeme na kuongeza idadi ya uunganishwaji wa wateja wapya kutoka wateja 250,000 hadi 290,000 kwa mwaka ili kuongeza mapato,</p> <p>'Nne, kuboresha kiwango cha kukusanya kutoka asilimia 94 hadi asilimia 98 kutoka</p> | | |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|---|--|---|--|
| | | | <p>kwa wateja wanaolipa baada ya huduma kuja kwenye matumizi ya LUKU na kwa kupitia kampeni ya 'KA-TA' kwa walioshindwa kulipa madeni.</p> <p>'Kadhalika hatua za kupunguza gharama zimeanzishwa ili kuruhusu shughuli muhimu tu zinazofadhiliwa.</p> | | |
| 17 | 2016/17 | <p>Riba inayopaswa kulipwa kwa Pan African Energy Dola za Kimarekani milioni 10.43.</p> <p>'TANESCO inashauriwa kutafuta njia za kutatua migogoro ili kuepuka kukusanya kiasi kikubwa cha ankara zisizolipwa.</p> | <p>TANESCO imeendelea kuimarisha dhima ya kulipa deni la PAET</p> <p>'Kuanzia Julai 2016 hadi tarehe 31 Machi, 2018 jumla ya Sh. Bilioni 161.84 kutoka Sh. bilioni 350.63 imekwishalipwa.</p> <p>Hivi sasa, deni lililobaki ni Sh. Bilioni 188.79 ambayo TANESCO imedhamiria kulipa Sh. Bilioni 2 kila wiki.</p> | <p>Jibu limenukuliwa, hata hivyo tunaendelea kusisitiza menejimen ti ya TANESCO kuongeza jitihada za kumaliza deni lililoko mbele yao</p> | <p>Ipo katika hatua za utekelezaji</p> |
| 18 | 2016/17 | <p>Kodi ambayo haijalipwa na Hospitali ya Tumaini Dola za Kimarekani milioni 9.4.</p> <p>'Nahimiza uongozi wa TANESCO kuhakikisha kwamba amri ya mahakama inatekelezwa bila kuchelewa zaidi.</p> | <p>Hukumu ilitolewa kwa upande wa TANESCO. Hivi sasa, TANESCO imefungua Maombi ya Utekelezaji wa hukumu ya Mahakama Kisheria baada ya kuondolewa kwa maombi ya awali ambayo ilionesha</p> | <p>Jibu limenukuliwa, litahakikiwa zaidi mwaka ujao wa ukaguzi</p> | <p>Katika hatua za utekelezaji</p> |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|---|--|--|-----------------------------|
| | | | Hospitali ya Tumaini kama Mchukuaaji wa Hukumu "Judgement debtor". | | |
| 19 | 2016/17 | Deni tarajiwa baina ya SCBHK na TANESCO Dola za Kimarekani milioni 148. 'TANESCO inashauriwa kuandaa chanzo mbadala cha fedha ili kuweza kulipa deni ikitokea kesi hii ikiamuliwa kwa upande wa SCBHK. | TANESCO kwa kushirikiana na Serikali iko katika mchakato wa kutekeleza Hati ya Usalama "Deed of indemnity" iliyotumiwa na ndugu Habinda Singh Sethi kwa niaba ya IPTL na Benki ya Tanzania kwa ajili ya Serikali ya Tanzania kutatua madai yanayotarajiwa na SCB HK ikiwa TANESCO itashindwa. | Jibu la uongozi limenukuliwa kwa ufuatiliaji kwenye ukaguzi wa mwakani | Katika hatua za utekelezaji |
| 20 | 2016/17 | Kuchelewa katika Kuhamisha Wateja katika viwango vyao sahihi vya ushuru. 'TANESCO inashauriwa kuhakikisha kwamba ufanisi wa hatua za udhibiti unawekwa, 'Pia, katika kufuatilia uhamisho wa watumiaji katika viwango sahihi vya ushuru sahihi kulingana na matumizi yao. Aidha, mfumo wa kiteknolojia unaweza kutumika katika kutekeleza mabadiliko | TANESCO imekuwa ikiamisha wateja wake kutoka kwenye mfumo mmoja ya ushuru hadi mwingine kila mwezi hasa kutoka D1 kwenda T1. Hata hivyo, ili kuhakikisha kwamba hii limefanikiwa kwa ufanisi, katika mwaka wa fedha wa 2018/19 kampuni imepanga kuhamisha mchakato huu katika mfumo wake kama vile wateja watahamishwa | Jibu limenukuliwa, litahakikiwa zaidi mwaka ujao wa ukaguzi | Katika hatua za utekelezaji |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|--|--|--|-----------------------------|
| | | ya haraka ya ushuru ili kupunguza makosa ya kibinadamu. | kutoka kwenye kundi moja ya ushuru hadi kundi jingine bila mwiingiliano wowote | | |
| 22 | 2016/17 | MWAUWASA kufanya malipo kwa Mkandarasi bila hati ya uthibitisho Sh. milioni 420.10 'MWAUWASA inashauriwa kuhakikisha kuwa Sh. milioni 420.10 'zinarejeshwa kwa mamlaka ya MWAUWASA bila kuchelewa zaidi | Kwa kuwa mkandarasi bado yupo kwenye kazi, na kuna malipo ambayo hayakuingizwa katika hesabu za mkandarasi, hivyo kiasi hicho cha fedha kitajumuishwa katika hesabu za mkandarasi ya cheti cha mwisho cha akaunti. Hadi sasa, kiasi hicho tajwa kimewasilishwa kwa mkandarasi kwa majumuisho. | Majibu wa uongozi yamenukuliwa, hata hivyo, vyeti vinavyoithibitishwa hayo havikuwasilishwa kwa uhakiki wa ukaguzi ili kuthibitisha malipo yaliyotajwa | Katika hatua za utekelezaji |
| 23 | 2016/17 | Kuchelewa katika Kukamilika kwa Mradi MWAUWASA Sh. 6.66 Bilioni. 'Nilipendekeza kwamba MWAUWASA wahakikishe mradi huo unakamilika bila kuchelewa zaidi. | MWAUWASA imechukua hatua ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa sehemu ya maji ambayo iko katika kiwango cha asilimia 90 ya kukamilika, kimekamilika. Kwa sehemu ya usafi wa mazingira MWAUWASA pamoja na Wizara ya Maji na Umwagiliaji wapo katika maandalizi ya kusitisha mkataba na kuleta mwaliko kwa Mkandarasi mpya Kupitia uzabuni wa wasambazaji maalum ili kuhakikisha kuwa Ujenzi | Jibu limenukuliwa. | Katika hatua za utekelezaji |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|--|--|---|-----------------------------|
| | | | unakamilishwa kabla ya dirisha la mfadhili (AfDB) halijafungwa ambayo litafungwa Septemba 2018. | | |
| 24 | 2016/17 | Ongezeko kubwa la deni na Jitihada zisizotosheleza Katika Ukusanyaji Madeni katika Hospitali ya Muhimbili 'Hospitali inahitaji kubuni njia na kuwekeza jitihada zaidi katika kukusanya madeni yake | Kufikia mwaka wa fedha 2017/18 kiasi cha Sh. bilioni 54.59 kilikua kiko tayari kupokelewa na kiasi cha Sh. bilioni 46.63 zilikusanywa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018. Hivyo kufanya makusanyo kufikia asilimia 85.4. 'Jumla ya wadaiwa ilikuwa Sh. Bilioni 18.16 kufikia tarehe 30 Juni, 2018, kati ya hizo Sh. Bilioni 7.96 tayari ilishapelekewa ankara yake, Sh. Bilioni 9.63i ankara bado haijatolewa kwa NHIF na Sh. bilioni 0.56 ankara haikutolewa kwa makampuni mengine yanayodaiwa. | Uboreshaji mkubwa umefanyika . Madeni yamepungu a kutoka Sh. Bilioni 30.8 hadi kufikia Sh. Bilioni 18.16 kufikia tarehe 30 Juni, 2018. Ninasisitiza Uongozi wa Muhimbili kuongeza juhudi zaidi za kupata salio lililobakia. | Katika hatua za utekelezaji |
| 25 | 2016/17 | Ankara ya Bima ya Afya kukataliwa Sh. 1.86 bilioni kwa Hospitali ya Muhimbili (MNH). 'Ninashauri MNH kuchunguza bili zilizokataliwa kwa lengo la kutafuta sababu za kukataliwa na kuchukua hatua zinazofaa. 'Pia, MNH inapaswa kuchunguza mchakato | Hospitali imeboresha kwa kiasi kikubwa uthibitisho wa madai ya bima. 'Asilimia ya madai iliyokataliwa imepungua kutoka asilimia 6 mwaka 2016/17 hadi kufikia asilimia 3 mwaka 2017/18. 'Mnamo mwaka wa 2016/17 Hospitali | Kukataliwa kwa malipo kumepungu a kutoka Sh. Bilioni 1.855 hadi kufikia Sh. bilioni 1 kwa mwaka 2017/2018. 'Ninapendekeza Menejimenti ya | Katika hatua za utekelezaji |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|--|--|---|-----------------------------|
| | | wa kulipa ili kutambua mapungufu ya kutosha ambayo yanaweza kusababisha malipo ya udanganyifu. | ilitoa Ankara ya Sh. 31.7 bilioni na kulipwa Sh. 29.8 bilioni ambapo mwaka 2017/18 jumla ya malipo kutoka Julai, 2017 hadi Machi, 2018 ilikuwa Sh. Bilioni 29.45 na kiasi kilicholipwa ilikuwa Sh. Bilioni 28.45. | Muhimbili iimarisha zaidi usimamizi na kuimarisha mchakato wa kulipa kwa lengo la kupunguza ankara zitakazokat aliwa. | |
| 26 | 2016/17 | Kuchelewa katika kukamilisha kazi Sh. Bilioni 1.18 UWASSA Moshi 'Mamlaka inashauriwa kufuatilia Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa utekelezaji wa mradi wa awamu ya pili. | Mradi huu ulianzishwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji chini ya mwavuli wa WSDP na ulikuwa unafadhiliwa na Benki ya Dunia na itakuwa na awamu 2, ikiwa ni pamoja na uandaaji wa kina na matayarisho ya nyaraka za matengenezo na ujenzi. | Jibu limenukuliwa, litahakikiwa zaidi mwaka ujao wa Ukaguzi. | Katika hatua za utekelezaji |
| 27 | 2016/17 | Ukinzani kati ya Sheria ya TCAA na Katiba ya URT 'Ninapendekeza kuwa, TCAA - CCC kufanana na kifungu 52 (4) cha Sheria ya TCAA (2006) na kwa masharti ya Kifungu na 143 cha Katiba. | TCAA CC limewasilisha jambo hilo kwa vyombo vya serikali husika, ikiwa ni pamoja na Wizara ya Mama, Wizara ya Mambo ya sheria na Katiba, Ofisi ya AG, CAG, na TCAA kupitia barua yenye kumbukumbu namba. TCAA CCC / 06/181 tarehe 31 Januari, 2018. Aidha, tumeungana na TCAA kurekebisha Sheria ya Aviation Civil, Cap 80 ili | Jibu limenukuliwa, tunangojea utekelezaji utakaohaki kiwa mwaka ujao wa Ukaguzi. | Katika hatua za utekelezaji |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|---|---|--|-----------------------------|
| | | | kuendana na Kifungu 143 (2) (c) cha Katiba. | | |
| 28 | 2016/17 | Nyumba imenunuliwa na BAKITA lakini haijakabidhiwa Sh. Milioni 180 'Uongozi wa BAKITA unapaswa kufuatilia na kutafuta hitimisho la jambo hilo. | Halmashauri kupitia watetezi wake (Mwanasheria Mshirika wa G&S) ameongeza gharama katika kesi ya 175/55 kulazimisha NIC kulipa fidia kwa gharama zote za mahakama pamoja na fidia (mesac profit) kwa kutumia viwanja vyake vinne. | Jibu limenukuliwa, tunangojea utekelezaji utakaohaki kiwa mwaka ujao wa Ukaguzi. | Katika hatua za utekelezaji |
| 29 | 2016/17 | Tofauti katika Mapato yaliyoripotiwa Sh. Milioni 607 katika TPC 'TPC inahitaji kuunganisha ofisi zote kwenye mfumo wa mapato, kufanya upatanisho wa mapato kutoka ofisi zisizo na uhusiano na kuchunguza uasilia wa tofauti zinazojitokeza 'Hata hivyo, TPC iko katika mchakato wa kuunganisha mifumo yake ya mapato kupita mfumo wa malipo wa serikali wa "Government electronic payment gateway" | Uongozi unaboresha mfumo wake wa kudhibiti juu ya mapato yake kwa kutumia mifumo ambayo itaingiliana na Post Global Netsmart. | Jibu limenukuliwa, tunangojea utekelezaji utakaohaki kiwa mwaka ujao wa Ukaguzi. | Katika hatua za utekelezaji |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|---|--|--|------------------------------------|
| 30 | 2016/17 | <p>Kutokufanyika kwa usuluhisho wa vitabu vya fedha Sh. Bilioni 12.52.</p> <p>'TPC inapaswa kuhakikisha kwamba upatanisho wa Benki unafanyika vizuri.</p> | <p>Serikali kupitia uongozi wa TPC inaendelea kusuluhisha mahesabu ya muda mrefu ambavyo hayajasuluhishwa.</p> <p>'Kuanzia tarehe 30 Juni, 2017, salio la vitu ambavyo havijatambulishwa ni Sh. Bilioni 3.95, mpango huo ni kuwaondoa wote kufikia tarehe 30 Juni, 2018.</p> <p>Zoezi la upatanisho litakamilika tarehe 30 Juni, 2018.</p> | <p>Jibu limenukuliwa, tunangojea utekelezaji utakaohaiki wa mwaka ujao wa Ukaguzi.</p> | <p>Katika hatua za utekelezaji</p> |
| 31 | 2016/17 | <p>Madeni yasiyosuluhishwa ya TTCL Sh. milioni 922.05.</p> <p>'TBC inashauriwa kufuatilia kwa karibu na TTCL ili kutatua tofauti na kurekodi salio lililobakia linalofaa kutokana na vitabu husika.</p> | <p>Menejimenti imepokea mapendekezo ya Mkaguzi Mkuu.</p> <p>'Mnamo tarehe 14 Desemba, 2017, TTCL imeitaarifu Menejimenti kupitia barua pepe kuwa ipo katika mchakato wa kuondoa kiasi chenye mgogoro.</p> | <p>Jibu limenukuliwa, tunangojea utekelezaji utakaohaiki wa mwaka ujao wa Ukaguzi.</p> | <p>Katika hatua za utekelezaji</p> |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|--|--|---|--|
| 32 | 2016/17 | <p>Kushuka thamani kwa miradi isiyokamilika Sh. Bilioni 1.61</p> <p>'Nashauri kampuni ya RAHCO ifanye uchunguzi wa aina ya miradi na kufanya uamuzi sahihi kuhakikisha miradi inamalizika au kuwachukulia hatua viongozi wote waliohusika kuisababishia hasara kampuni hiyo.</p> | <p>Ujenzi wa miradi kama huu wa standard gauge unategemea zaidi kutengwa kwa fedha za bajeti kutoka Serikali Kuu kupitia mapato ya ndani, mikopo au kwa wahisani wa nje; na si kutokana na fedha zipatikanazo na mapato ya biashara za ndani.</p> <p>'Miradi hii yote ni lazima ipitie kwenye hatua zote tatu ambazo ni upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na ujenzi wa mradi.</p> <p>'RAHCO na sasa TRC ni wakala wa mradi katika usimamizi wa eneo la utaalim na usimamizi wa makubaliano ya malipo.</p> <p>Kwa msingi huo, usimamizi na upatikanaji wa fedha hufanywa na Serikali kupitia Wizara ya Fedha.</p> <p>'Katika ngazi ya upembuzi yakinifu ndipo hapo tutakapofahamu kama mradi una manufaa au laa. Tunaenda kwenye hatua ya ujenzi iwapo tuu</p> | <p>Majibu ya Menejimenti yamezingatiwa. Hata hivyo, nasisitiza Menejimenti ya RAHCO iwasiliane na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kuhakikisha fedha za kugharamia miradi inatolewa kwa wakati.</p> | <p>Ipo kwenye hatua za utekelezaji</p> |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|-------|------------------------|---|------------------|---------------------|
| | | | <p>tutajiridhisha kuwa mradi una faida na pesa ipo. Pia, upembuzi yakinifu ni waraka muhimu kwa ajili ya kuwaaminisha wahisani au wawekezaji namna umuhimu wa mradi na faida yake kwa miradi mikubwa na muhimu kama hii.</p> <p>'Mwisho, iwapo Serikali ikitaka kutekeleza mradi kwa kutumia fedha za ndani, usanifu wa kina ni moja ya waraka muhimu ambayo inahitajika kuidhinishwa kwa ujenzi. Kwa bahati sana miradi hii ni ya matrilioni ya Sh. hivyo upembuzi wa kina umetumia mabilioni ya Sh. Hata hivyo, kwa baadaye RAHCO/TRC tutaboresha na kufanya kazi kwa karibu na MOWTC kwa ajili ya kufanyia kazi mapendekezo.</p> | | |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|--|--|---|--|
| 33 | 2016/17 | <p>Udanganyifu Ulioleta Hasara ya Sh. Milioni 130.6</p> <p>'Nashauri Taasisi ya Moyo ya Jakaya kuendelea kuufatilia kesi hii ili kuhakikisha maamuzi ya mwisho yanapatikana ili waliouhusika wachukuliwe hatua inayostahili. Pia, Taasisi iongeze uhabiti wa mifumo ya ndani itakayopunguza uwezekano wa ubadhirifu kwa kugawanya majukumu ya watumishi, kuhamisha watumishi mara kwa mara, na kufanya mapitio ya mara kwa mara ndani ya Taasisi.</p> | <p>Hatua mbalimbali zimechukuliwa na Menejimenti kwa ajili ya kuboresha uhabiti wa ndani ikiwemo:</p> <p>'a) Mgawanyo wa majukumu</p> <p>'Sasa hivi shughuli mbalimbali zinazohusiana ba masuala ya uhasibu, ikiwamo mapokezi ya pesa, kuweka benki, na usuluhishi wa kibenki hufanywa na watu tofauti.</p> <p>'Taasisi imeanza utekelezaji wa mbadilishano wa kazi kama sehemu ya uhabiti wa ndani.</p> <p>'b) Mbadilishano wa majukumu</p> <p>'c) Uandalizi wa ndani kwa ajili ya kuimarisha uhabiti kwa mifumo ya ndani taasisi ilichukua hatua zifuatazo:</p> <p>'i) Uwekaji pesa Benki (NMB) umeongezwa muda kutoka siku tano za awali mpaka siku sita (Jumatatu-Jumamosi) Yalifanyika makubaliano maalum kati ya NMB na Taasisi kwa ajili</p> | <p>Majibu ya Menejimenti yamezingatiwa kwa umuhimu mkubwa na kupongeza juhudi zilizofanywa ili kuboresha uhabiti wa ndani. Hata hivyo, nitaendelea kuangalia mwenendo wa kesi katika vipindi vijavyo vya ukaguzi.</p> | <p>Ipo kwenye hatua za utekelezaji</p> |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|---|--|--|--|
| | | | <p>ya kuongeza muda wa kufunga kutoka saa 04:30 mpaka 10:00 pm</p> <p>'ii) Usuluhishi na usahihi unafanyika kila siku kati ya pesa inayokusanywa na ile inayopelekwa Benki</p> <p>'iii) Huduma za Kibenki kwa njia ya Mtandao</p> <p>'Taasisi imepata haki za kutumuia mtandao kwa ajili ya huduma za kibenki ambapo itarahisisha upatikanaji, mchakato na hata kuziona ripoti zote za usuluhishi kutoka Benki na zile ripoti za ndani .</p> | | |
| 34 | 2016/17 | <p>Chuo cha Mabaharia Dar es Salaam (DMI)</p> <p>'Ubadhirifu katika Malipo ya Dola za Kimarekani 26,356.65 na Euro 2,500;</p> <p>'Nashauri Chuo kufuatilia kwa umakini mwenendo wa ubadhirifu huo kwa kitengo cha Makosa ya Mtandao cha Jeshi la Polisi ili kujua hatua iliyofikiwa ili kufanikisha upatikanaji wa fedha hizo. Pia, nashauri chuo kihakikishe mifumo ya ndani inawezesha upitiaji wa usahihi wa nyaraka za malipo ili</p> | <p>Jeshi la Polisi Tanzania kwa kushirikiana na wenzao wa Interpol wanaendelea kufanya uchunguzi wa kina lakini wameungana kwa ajili kulipa kiasi kiasi hicho cha fedha.</p> | <p>Nakubaliana na majibu ya Menejimenti, lakini ufuatiliaji wa hoja hii unaendelea na nitafanya ufuatiliaji wa muendeleo kwenye utekelezaji wake</p> | <p>Ipo kwenye hatua za utekelezaji</p> |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|-------|---|------------------|------------------|---------------------|
| | | kuhakikisha fedha zote zinalipwa kwenye akaunti halali. | | | |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|---|--|---|--|
| 35 | 2016/17 | <p>Chama cha Hati miliki Tanzania (COSOTA)</p> <p>'Madeni ya Mirabaha ya Sh. milioni 987.86 kwa vituo vya Televisheni na Redio</p> <p>'Chama cha Hati Miliki kinashauriwa kuongeza jitihada kwa kuvikumbusha vituo vya televisheni na redio kuwa vina wajibu wa kulipa mirabaha hiyo.</p> | <p>Menejimenti inaendelea kufanya jitihada ya ufuatiliaji kwa wamiliki kulipa madeni yao kulingana na ankara ya malipo tulizowatumia. Tumepanga kituo cha taarifa na COSOTA kufanya kazi kwa pamoja kwa ajili ya utoaji wa ankara, usimamizi, ukusanyaji, usambazaji na usisitizaji wa tozo za mirahaba baada ya kituo cha uwekaji wa kumbukumbu kukamilisha Mfumo wa usimamizi wa vituo vya utangazaji.</p> <p>'Kwa sasa COSOTA wamejiunga na mfumo wa malipo wa Serikali (GePG) kwa ajili ya kurahisisha ukusanyaji wa maduhuli ya ada. Mifumo hiyo miwili itasaidia ukusanyaji wa mapato ikiwemo mirahaba isiyolipwa.</p> | <p>Majibu ya Menejimenti yamezingatiwa. Nasisitiza bado COSOTA iongeze nguvu kwenye ukusanyaji wa mrahaba kwa vituo vya redio na televisheni Sh. milioni 927.86</p> | <p>Ipo kwenye hatua za utekelezaji</p> |
| 36 | 2016/17 | <p>Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA)</p> <p>'Mapungufu Katika Kuripoti Uwekezaji katika Mfuko wa Kulinda Uhifadhi (NPF)</p> <p>'Naushauri uongozi wa mamlaka kufuatilia na kupata nyaraka zinazothibitisha umiliki wa Mfuko wa Uhifadhi</p> | | <p>Hakuna majibu kutoka kwa Serikali kutoka kwenye mapendekezo haya.</p> | <p>Haijatekielezwa</p> |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|--|--|---|----------------------------------|
| | | kwa kuainisha uhusiano uliopo baina ya Mamlaka na Mfuko huo. Kufanya hivyo kutarahisisha kujua ni kwa namna gani uwekezaji wa kwenye Mfuko unaweza kuonekana kwenye hesabu za mamlaka. | | | |
| 37 | 2016/17 | Malipo kwa manunuzi ya Ardhi yaliyo kinyume na Utaratibu. 'Mamlaka ya Bandari Tanzania inashauriwa kufuata taratibu zilizowekwa na sheria ya Manunuzi ya Umma, ikiwemo kuhakikisha inapata idhini ya Bodi pamoja na kuhakikisha ardhi hiyo tajwa inatathiminiwa kabla ya kulipa gharama zilizobaki. | Ardhi itapimwa kabla ya kufanyika kwa malipo. | Nakubalina na majibu ya Menejimenti lakini ufuatiliaji wa hoja hii unendelea na nitafanya ufuatiliaji wa muendeleo kwenye utekelezaji wake. | Ipo kwenye hatua za utekelezaji |
| 38 | 2016/17 | Utata wa Umiliki wa Kituo cha Mafuta cha COPEC Kilichopo Eneo la Makumira 'TPDC inashauriwa kufuatilia umiliki wake katika makampuni hayo mawili ili kujua hali ya uwekezaji wake na kuchukua hatua zinazofaa. | Serikali imepokea mapendekezo ya Mkaguzi na itayafanyia kazi mara moja. | Hakuna Utekelezaji uliofanyika mpaka sasa. | Haijatekelezwa. |
| 39 | 2016/17 | Upungufu wa Kamera za CCTV katika kiwanja cha ndege cha Kilimanjaro Naishauri Menejimenti ya KIA iharakishe mchakato wa zabuni na kumpata mshindani | Makubaliano kati ya KADCO na Agreneb Consult yaliingiwa kwa ajili ya michoro na kufanya maandalizi ya makabrasha kwa ajili ya zabuni ya ufungaji wa CCTV. Kwa wale | Nakubaliana na jitihada zinazofanywa na uongozi katika kushughulikia jambo | Ipo kwenye hatua za utekelezaji. |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|---|--|--|---------------------------------|
| | | halisi kwa ajili ya kutekeleza majukumu hayo. | washindani, makabrasha yapo tayari kwa ajili ya mradi wa ufungaji wa CCTV Camera. | hili. Hata hivyo, utekelezaji wa mapendekezo haya tutayafuatilia kwenye kipindi kijacho cha ukaguzi. | |
| 40 | 2016/17 | Kutofanyika kwa marekebisho ya Mazingira katika Mgodhi wa Buhemba 'Nashauri STAMICO wawasiliane na Wizara ya Nishati kwa ajili ya kupata suluhisho la kurekebisha mazingira ya mgodi huo. | | Hakuna majibu kutoka kwa Serikali kutoka kwenye mapendekezo haya. | Haijatekelezwa. |
| 41 | 2016/17 | Viwanja visivyo na Hati miliki vyenye Thamani ya Sh. bilioni 5.44 'Inashauriwa NBS kuchukua hatua zinazofaa ili kuhakikisha maeneo yote inayoyamiliki yanakua na hati miliki zake na Pia kufanya majadiliano na BOT ilikuweza kupata umiliki wa kiwanja cha Arusha | NBS iliandika barua kwenda kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma yenye kumb.namba NBS/A.30/6/11 ya tarehe 8 mwezi wa Februari 2018 kwa ajili ya kuielekeza Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma kuipatia ofisi ya NBS hati miliki kwa jina la NBS. 'Barua nyingine iliandikwa kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Arusha ikimtaka atoe hati miliki yenye jina la NBS kwa kiwanja namba 565 kilichopo Kibla Makao Mapya | Majibu ya Serikali yamezingatiwa, hata hivyo nasubiri upatikanaji wa hati zilizotajwa pamoja na ya Dar es salaam ambayo haijaletwa kwa ajili ya uhakiki. | Ipo kwenye hatua za utekelezaji |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|---|--|--|--|
| 42 | 2016/17 | <p>Mapato Yanayokosekana kutokana na kutotekelezwa Vifungu vya Mkataba.</p> <p>'Kwa kuwa kipindi cha miaka 10 ya mkataba kinakaribia kufika mwisho, ninashauri mkataba kurekebishwa ili kuweza kubadili vifungu vya mkataba vinavyoelekeza kuwa kodi ya pango itafidiwa na huduma za mtandao. Hii itawezesha kupata malipo ya kodi badala ya utaratibu wa mwanzo.</p> | <p>Mapendekezo yamechukuliwa. Kabla ya kuisha mwezi Machi mwaka 2018 timu ya Chuo Kikuu itakuwa tayari imeshakutana kwa ajili ya marekebisho ya Mkataba. Pia, hati miliki kwa kiwanja cha Dar es Salaam kilichopo Magogoni tayari hati yake yenye namba 87784 kiwanja namba 86 imeshapatikana. Ufuatiliaji wa karibu utaenelea kufanyika kwa Manispaa ya Kigoma na Arusha kwa ajili ya kupatiwa hati .</p> | <p>Majibu ya Menejimenti yanazingatiwa. Nasubiri utekelezaji wa mapendekezo niliyoyatoa.</p> | <p>Ipo kwenye hatua za utekelezaji.</p> |
| 43 | 2016/17 | <p>Kutolewa kwa mikopo zaidi ya kiasi cha Mkataba Sh. Bilioni 6.18</p> <p>'NSSF inashauriwa kuchunguza sababu za malipo zaidi kwa Taasisi hizo nne na kuhakikisha kunafanyika majadiliano juu ya urejeshwaji wa fedha hizo. Pia, Mfuko katika siku zijazo, uhakikishe hakuna malipo ya ziada yanayofanywa kinyume na mikataba.</p> | | <p>Hakuna majibu kutoka kwa Serikali kwenye mapendekezo haya.</p> | <p>Haijatekelezwa.</p> |
| 44 | 2016/17 | <p>Kukosekana kwa Mkakati na Mpango wa Kuhuisha Tafiti na Kutowekea mkazo Makubaliano</p> <p>'Chuo kinashauriwa kuwa na mkakati na</p> | <p>Chuo Kikuu kimeanzisha kitengo maalum cha ubunifu kinachohusiana na haki miliki ambapo moja ya majukumu yake ni kusajili bunifu zote.</p> | <p>Majibu ya Menejimenti yamezingatiwa, Ufuatiliaji wa utekelezaji</p> | <p>Ipo kwenye hatua za utekelezaji .</p> |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|-------|--|---|--------------------------------|---------------------|
| | | mpango madhubuti wa kuhuisha na kuboresha tafiti zake. Pia, kuingia makubaliano na wapokea leseni ili kutoa msaada wa kiutaalamu. Zaidi, Chuo kinatakiwa kikusanye kodi ya kukimu ya mwaka pamoja na mirabaha ambayo haijalipwa. | Teknolojia mbili zenye haki miliki zilichapishwa kwenye jarida la mambo ya Sayansi. Kwa mujibu wa miongozo ya biashara taratibu hizi zinakubalika kukiwa na ukweli kwamba hata haki miliki ni machapisho ya kisayansi kwa ajili ya matumizi kwa Umma, na inatakiwa ipatikane kwa uwazi. Zaidi ya hapo, mhariri wa jarida haruhusiwi kuchapisha haki miliki, ambayo tayari ipo wazi kwa ajili ya matumizi ya jamii. Mwisho wa machapisho yote yanayohusianana haki miliki, mchapishaji lazima aeleze kipya kilichopo kwenye teknolojia. Sera ambayo inatumika inahusisha uhitaji wa kuandaa mbinu ambazo zitawezesha kuweka vitu vyote hivi kibiashara na kuwapa nafuu wawekezaji kama namna ya kuwaongezea ari. | utafanyika kwenye kaguzi ujao. | |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|--|---|---|--|
| 45 | 2016/17 | <p>Gawio la Fedha lisilotosheleza Kwa Shughuli za Bohari Kuu</p> <p>'Ninashauri Bohari Kuu washirikiane na Serikali kuhakikisha kuwa inalipa deni lake ili kuimarisha mtaji wa Bohari, hivyo kuongeza ufanisi.</p> | <p>Menejimenti ilishaiandikia mara kadhaa Wizara ya ya Fedha kupitia Wizara ya Afya kueleza hali mbaya kifedha iliyopo na kuwaomba walipe deni lao.</p> | <p>Naendelea kusisitiza kuwa Menejimenti ya Bodi ya Dawa iendeleo kuwasiliana na wizara ili deni liweze kulipwa</p> | <p>Ipo kwenye hatua za utekelezaji</p> |
| 46 | 2016/17 | <p>Kutofanya kazi kwa Baadhi Vituo vya Mafuta na Kuisha kwa Mikataba baina ya TPDC na Watoa Huduma ya Mafuta</p> <p>'TPDC inashauriwa kuingia katika makubaliano mapya ya ukodishaji na wapangaji wake, kurekebisha majengo yaliyo chakaa, na kupangisha majengo yasiyotumika kwa sasa ili kunufaika kiuchumi kama ilivyokusudiwa.</p> | <p>Serikali imeyachukua mapendekezo ya Mkguzi wa nje.</p> | <p>Nasubiri hatua za utekelezaji wa mapendekezo ziweze kuchukuliwa.</p> | <p>Haijatekelezwa.</p> |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|--|------------------|--|---------------------|
| 47 | 2016/17 | <p>Ukomo wa wigo wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali katika sekta ya Madini, Gesi na Mafuta</p> <p>'Kutokana na umuhimu wa kuwapo kwa uwazi katika sekta ya madini, gesi na mafuta, kuna ulazima wa kurekebisha sheria mama za madini na mafuta ili ziweze kumtaja na kumpa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mamlaka ya wazi ya kupata taarifa zilizo na zisizo za kihasibu za makampuni ili kuboresha uwajibikaji wa kampuni hizi juu ya maliasili walizopewa kuziendeleza.</p> | | Hakuna majibu ya Serikali juu ya mapendekezo haya. | Haijatekelezwa |
| 48 | 2016/17 | <p>Kutokuwapo kwa kanuni za kuelezea sheria za Maliasili na Rasilimali</p> <p>'Serikali, kupitia Wizara ya Madini, inashauriwa kutunga kanuni zitakazoongoza na kusimamia utekelezaji wa sheria za Rasilimali na Maliasili.</p> | | Hakuna majibu ya Serikali juu ya mapendekezo haya. | Haijatekelezwa |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|--|------------------|--|---------------------|
| 49 | 2016/17 | <p>Kutofanyika kwa uhakiki wa gharama za uwekezaji wa migodi</p> <p>'Serikali, kupitia Tume ya Madini, inashauriwa kufanya uhakiki wa usahihi wa gharama za awali na muendelezo wa uwekezaji katika migodi kuthibitisha usahihi wa taarifa za uwekezaji zilizotolewa na makampuni ya migodi ili kuiwezesha serikali kukusanya mapato stahiki kupitia mrabaha na kodi.</p> | | Hakuna majibu ya Serikali juu ya mapendekezo haya. | Haijatekelezwa. |
| 50 | 2016/17 | <p>Ucheleweshwaji wa kuendeleza vitalu Namba 4/1B/1C</p> <p>'Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na Wizara ya Nishati wanashauriwa:</p> <p>'a) Kutunga na kusaini makubaliano yatakayoongoza shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta katika vitalu husika,</p> <p>'b) Kuhakikisha leseni ya utafutaji wa mafuta inatolewa kwa Shirika la Mafuta ili kufanikisha uendelevu wa vitalu, na</p> <p>'c) Kuwasiliana na Serikali pamoja na washirika wengine kuweza kupata fedha za kuendesha na kufanikisha mradi husika.</p> | | Hakuna majibu ya Serikali juu ya mapendekezo haya. | Haijatekelezwa |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|--|------------------|--|---------------------|
| 51 | 2016/17 | <p>Kutokuendelezwa kwa Vitalu saba vya Mafuta kwenye kina kirefu cha Ziwa na Kitalu Kimoja katika Ziwa Tanganyika.</p> <p>'Shirika la Maendeleo ya Mafuta Tanzania linashauriwa kuielekeza Serikali umuhimu wa kupitia vifungu vya mfano wa mkataba wa uzalishaji gesi (MPSA) wa mwaka 2013 ili kuhamasisha uwekezaji katika vitalu.</p> | | Hakuna majibu ya Serikali juu ya mapendekezo haya. | Hajiatekelezwa. |
| 52 | 2016/17 | <p>Matumizi ya Mitambo ya Gesi chini ya Uwezo wake</p> <p>'Shirika la maendeleo ya mafuta Tanzania linashauriwa kutafuta wateja wapya watakaooongeza matumizi ya mitambo, ambapo itasababisha kuongezeka kwa faida ya jumla kwa shirika</p> | | Hakuna majibu ya Serikali juu ya mapendekezo haya. | Hajiatekelezwa. |
| 53 | 2016/17 | <p>Mrabaha kulipwa Kutoka kwenye Faida ya Serikali</p> <p>'Kupitia mamlaka iliyopewa kwenye kifungu namba 4 cha Sheria ya Mikataba ya Maliasili na Rasilimali, Serikali inashuriwa kupitia na kubadilisha vifungu vya mkataba wa Songosongo ili kuwezesha mrabaha kuweza kulipwa na mmiliki wa leseni au mkandarasi kama</p> | | Hakuna majibu ya Serikali juu ya mapendekezo haya. | Hajiatekelezwa. |

| Na . | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|------|---------|--|------------------|--|---------------------|
| | | ilivyoelekezwa kwenye sheria ya petroli ya mwaka 2015 | | | |
| 54 | 2016/17 | <p>Kutokulipwa kwa Ankara za Mauzo ya Gesi Asilia kutoka TANESCO Kwenda TPDC kiasi cha Sh. billioni 248</p> <p>'Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Wizara ya Nishati inashauriwa kuisadia TANESCO kuweza kufanikisha kulipa deni lake wanalodaiwa na TPDC ili kuliokoa shirika lisiweze kupokonya haki zake na benki ya Exim-China.</p> | | Hakuna majibu ya Serikali juu ya mapendekezo haya. | Haijatekelezwa |

Kiambatisho Na. III: Viwanja vya Ndege Kutokuwa na Leseni Halali

| Viwanja Vya Ndege | Tarehe za Leseni Kuisha Muda Wake | Maoni |
|-------------------|-----------------------------------|-------------------|
| Songea | 31 Desemba, 2016 | Hazijafanywa upya |
| Lesingita | 30 Juni, 2016 | Hazijafanywa upya |
| Loolblin | 30 Agosti, 2015 | Hazijafanywa upya |
| Kilombero | 30 Desemba, 2017 | Hazijafanywa upya |
| Lemguru | 30 Agosti, 2017 | Hazijafanywa upya |
| Dodoma | Hakuna rekodi | Hakuna Leseni |

Kiambatisho Na. IV: Viwango ambavyo haviko sambamba na vitabu vya ushuru wa forodha

| Shehena za kuhifadhi Mizigo | | | Bandari | Maelezo | Kiwango kilicho tumika | Kiwango cha forodha | Tofauti |
|-------------------------------|-------------------|--------------|---------|-------------------------------|------------------------|---------------------|----------------------------|
| 15-Sep-17 | STV/24230/09/2017 | IN Indonesia | DSM | 20'F.C.L (Local) | 71 | 100 | Dola za kimar ekani 23,989 |
| | | | | 20' F.C.L DANGEROUS (LOCAL) | 85.2 | 120 | |
| | | | | 20'F.C.L (Transit) | 80 | 100 | |
| | | | | 20'L.C.L (Transit) | 160 | 170 | |
| | | | | 20'OVER DIMENSION () | 92.3 | 130 | |
| | | | | 40' F.C.L (LOCAL) | 107 | 150 | |
| | | | | 40' EMPTIES (LOCAL) | 80 | 70 | |
| | | | | 40' F.C.L (Transit) | 120 | 150 | |
| 15-May-18 | STV/729/05/2018 | KOTA MAKMUR | DSM | 20'F.C.L (Local) | 71 | 100 | Dola zakim arekani 19,834 |
| | | | | 20'L.C.L (Local) | 142 | 170 | |
| | | | | 20' F.C.L DANGEROUS (LOCAL) | 85.2 | 120 | |
| | | | | 20'F.C.L (Transit) | 80 | 100 | |
| | | | | 20'L.C.L (Transit) | 160 | 170 | |
| | | | | 40' F.C.L (LOCAL) | 107 | 150 | |
| | | | | 40' EMPTIES (LOCAL) | 80 | 70 | |
| | | | | 40' F.C.L DANGEROUS (Local) | 128 | 180 | |
| | | | | 40' F.C.L (Transit) | 120 | 150 | |
| 40' F.C.L DANGEROUS (Transit) | 144 | 180 | | | | | |
| 28-Feb-18 | STV/9198/02/2018 | KOTA GEMAR | DSM | 20'F.C.L (Local) | 71 | 100 | Dola za Kimar ekani 28,166 |
| | | | | 20'F.C.L (Transit) | 80 | 100 | |
| | | | | 40' F.C.L (LOCAL) | 107 | 150 | |
| | | | | 40' EMPTIES (LOCAL) | 80 | 70 | |
| | | | | 40' F.C.L DANGEROUS (LOCAL) | 128 | 180 | |
| | | | | 40' F.C.L (Transit) | 120 | 150 | |
| | | | | 40'OVER DIMENSION () | 139.1 | 195 | |
| 26-Jun-18 | STV/4226/06/2018 | SONGA HYDN | DSM | 20' F.C.L DANGEROUS (Transit) | 204 | 120 | Dola za kimar ekani 534 |
| | | | | 40'OVER DIMENSION () | 225 | 195 | |

Kiambatisho Na. v: Orodha ya wadaiwa wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TEA)

| MAJINA YA TAASISI ZINAZODAIWA | Madai ya Taasisi 'Sh. | Madai yaliyolipwa kwa mwaka Sh. |
|--------------------------------------|------------------------------|--|
| Shule ya sekondari Wazo Hill | 66,381,759 | |
| Shule ya Msingi St Moses | 20,000,000 | |
| Chuo kikuu cha St Augustine-Mwanza | 204,677,782 | |
| Shule ya Sekondari Winning Spirit I | 46,286,580 | |
| Chuo Kikuu cha Sebastian Kolowa | 58,349,621 | |
| Chuo Kikuu cha St Augustine- Tabora | 796,065,053 | |
| Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima | 172,235,429 | 47,702,372 |
| Chuo Kikuu cha Mzumbe | 500,000,000 | |
| Chuo Kikuu cha Ardhi | 263,122,083 | |
| Ailanga Juniour Seminary | 9,072,903 | |
| Chuo Kikuu cha Theofilo Kisanji | 500,000,000 | 0 |
| Chuo Kikuu cha kilimo Sokoine | 337,132,931 | 0 |
| Libermann Pre-Primary | 53,676,540 | 0 |
| Shule ya Sekondari Mbogamo | 29,811,000 | 0 |
| Kisukuru Regent | 22,905,665 | 22,905,665 |
| Shule ya Sekondari Mzinga | 100,053,055 | 0 |
| Shule ya Msingi Daystar | 34,000,000 | 34,000,000 |
| Shule ya Sekondari Loamo | 38,000,000 | 38,000,000 |
| Shule ya Genius King | 54,687,313 | 54,687,313 |
| Shule ya Sekondari Charles Totera | 95,261,819 | 0 |
| Shule ya Sekondari TEJ | 43,038,325 | 0 |
| Shule ya Sekondari ya Pemier | 65,577,440 | 0 |
| Shule ya Sekondari ya Agape | 39,177,559 | 0 |
| Chuo cha Elimu cha Biashara (CBE) | 162,785,029 | 0 |
| Chuo Kikuu cha Tumanini Iringa | 81,073,127 | 0 |
| Chuo Kikuu Huria cha Tanzania | 374,494,777 | 0 |
| JUMLA | 4,167,865,790 | 197,295,350 |